

# Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA NNE

Kikao cha Hamsini na Tano – Tarehe 25 Agosti, 2011

(Mkutano Ulianaza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, napenda kutoa taarifa kwamba, ujumbe uliokwenda kushiriki maziko kwa ndugu yetu mpendwa sana, Mheshimiwa Silima, tulikwenda kwa usalama na mwenzetu amelazwa vizuri, kwa amani na upendo mkubwa sana. Watu wa kule wamefurahi kwamba, tumeweza kushirikiana nao vizuri. Kwa hiyo, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge, kwa kufanya maombolezo kwa ajili ya ndugu yetu. Roho yake ipumzike mahala pema peponi; *Amin.*

## HATI ZILIWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. GREGORY G. TEU):** Taarifa ya Mwaka na Hesabu za *The National Board of Accountants and Auditors – Tanzania* kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 (*The Annual Report and Accounts of the National Board of Accountants and Auditors – Tanzania for the Financial year 2009/2010*).

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI:** Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Fedha kwa Mwaka 2010/2011 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA):** Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani juu ya Wizara ya Fedha kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

## MASWALI KWA WAZIRI MKUU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, leo ni Siku ya Maswali kwa Waziri Mkuu; naomba maswali yaye yale ya kisera na siyo maswali ambayo yanakuwa siyo eneo lake hasa Waziri Mkuu. Kwa kuwa tunaye Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, yeye siku zote anaanza. Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Mbewe.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE – KIONGOZI WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza ya kumwuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa sababu kauli iliyotolewa na Katibu Mkuu Kiongozi kuhusiana na sakata la Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini limeleta utata mkubwa katika Taifa; na kwa sababu Bunge lako jana lilitidhia umuhimu wa kuunda Kamati ambayo itachunguza undani wa jambo hili; na kwa sababu Katibu Mkuu Kiongozi alimrudisha ofisini Ndugu Jairo; je, Serikali

haioni kuna umuhimu wa Bwana Jairo aendelee na likizo wakati Kamati Teule ya Bunge inafanya kazi yake? (*Makofî*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kulifarifu Bunge lako Tukufu kwamba, hatua hiyo tayari imeshachukuliwa na Rais. Ninachoweza kuliahidi Bunge lako ni kwamba, kwa sababu jambo hili limeundwa kwa mujibu wa utaratibu, Serikali itatoa ushirikiano wa kutosha ili tuweze kubaini mazingira na mambo yote yanayoendana na yaliyojitekeza. (*Makofî*)

**MHE. FREEMAN A. MBOWE – KIONGOZI WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, pamoja na majibu mazuri sana ambayo nakupongeza kwa kauli hiyo, ningependa tu kukumbusha kwamba, wakati Katibu Mkuu Kiongozi anatoa kauli ile, alizungumza jambo lingine ambalo nalo vilevile ni zito na lenye utata mkubwa; aliposema kwamba ni utamaduni wa kawaida wa Serikali kufanya hivyo; na wakati huo huo, kwa faida ya Bunge na Watanzania kwa ujumla, Wizara ya Waziri Mkuu ambayo ilikuwa na bajeti kubwa ambayo ilijadiliwa kwa siku tano, ilitumia jumla ya shilingi 174,545,000 kuwezesha bajeti kupita, wakati Wizara ya Nishati na Madini ilitumia shilingi 578,000,000; je, pamoja na kwamba Bunge litachunguza; Serikali itakuwa tayari kuwachukulia hatua za kinidhamu wale wote watakaokuwa wamehusika na ubadhifuru wa fedha za umma? Je, itatangazwa rasmi kwamba siyo Sera ya Serikali au tuchukue kauli ya Katibu Mkuu Kiongozi kwamba hiyo ni Sera na utaratibu wa kawaida wa Serikali? (*Makofî*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, mimi nafikiri Mheshimiwa Mbewe, mengine haya tuiachie Kamati Teule, kwa sababu naamini kabisa katika eneo hili, wataweza pengine kugundua mambo mengine mengi ambayo yote yanaweza kuwa ni kwa maslahi ya nchi. Kwamba, ule ndio utaratibu, *well*, anaweza kuwa alikuwa ni sahihi kwa upande mmoja, lakini inawezekana vilevile siyo sahihi sana, inategemea zile fedha mmezitumia kwa ajili ya jambo gani. Kwa hiyo, kama zipo sababu ambazo zinaweza kuhalalishwa kwa maana kwamba, zimetumika kwa jambo ambalo wote tunaweza tukaona ni sawa, hakuna tatizo. Hofu hapa ni kwamba, inawezekana fedha hizo hazitumiki kwa nia njema, ndio maana kidogo linaleta hisia ambazo ni lazima kwa kweli wote turidhiane.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwa kuwa biashara ya dawa za kulevyia ni biashara ambayo inaliathiri Taifa letu sana; na kwa kuwa Mheshimiwa Rais ameliona hilo na akaunda Kikosi Kazi ambacho nafikiri Wabunge wote tunakubali kwamba kimefanya kazi nzuri sana; je, Mheshimiwa Waziri Mkuu, haoni kwamba kuna umuhimu sasa wa kuchukua hatua ya dharura ya kuwatafatutia Kikosi Kazi kile jengo la kuhifadhi zile dawa za kulevyia wanazokamata kuliko ambavyo sasa zimerundikana ofisini kwao na wakati mwingine zinapotea na wao kukosa ushahidi?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nakubaliana na Mheshimiwa Anne Kilango kwamba, ile *Task Force* inafanya kazi nzuri sana. Hiyo ni dhahiri kabisa na Serikali inaridhika na kazi wanayoifanya. Vilevile ni kwamba, kikundi hiki kinakabiliwa na changamoto nyingi tu za kiutendaji ambazo ni dhahiri kabisa kwamba, kama Serikali lazima tukubali kutafuta suluhu ya matatizo yao. Kwa hiyo, hilo ulilolisema Mheshimiwa Mama Anne Kilango ni eneo moja kwa maana ya kuona ni namna gani tunaweza tukawasaidia kuwa na jengo la uhakika, hasa kwa sababu ya hifadhi ya zile *exhibits* ambazo wakati mwingine zinaleta utata kutokana na mlundikano uliopo pale.

Mheshimiwa Spika, sisi tumekwishaanza kuliangalia na kimsingi ni kwa sababu lipo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa hiyo, kazi hiyo tumeshaanza kuifanya na Katibu Mkuu, kuona namna ya kuwasaidia katika eneo hilo.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninashukuru kwamba, changamoto mmeshaziona. Changamoto kubwa ni kwamba; Kikosi Kazi kile kinafanya kazi eneo kubwa ambalo ni Tanzania nzima, lakini kina magari mawili tu na hakina mgawo maalum, hakina bajeti; je, Ofisi yako Mheshimiwa Waziri Mkuu haiwezi kutoa gari moja kutoka kwenye *poo*/pamoja na Ofisi ya Rais ikatoa gari moja, wakaongezewa japo magari mawili ili wafanye kazi kwa urahisi zaidi?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, Kikosi Kazi kile ni kikundi kidogo sana, lakini makini sana. Kwa hiyo, Serikali tunajitahidi sana kukiwezesha kiweze kufanya kazi zake vizuri; ni Kikosi Kazi lakini kipo chini ya Tume ya Kudhibiti Dawa za Kulevyia.

Kama nilivyosema, Rais alipoamua jambo hili ni kwa sababu alitaka sasa tuwe na kikundi ambacho kitajikita zaidi katika eneo hili ili tuweze kupambana vizuri zaidi, badala ya kuliacha liwe jambo la jumla. Kwa hiyo, nakubaliana kabisa na rai yako na ushauri wako; sisi tutafanya kila litakalowezekana kuhakikisha Kikosi Kazi hiki kinatimiza majukumu yake vizuri, ikiwa ni pamoja na kukipatia nyenzo hizo. Nadhani katika hili, hata Waheshimiwa Wabunge, hawatagombana na mimi na viposhoposh o vya kuhakikisha wanafanya kazi yao vizuri. (*Makof*)

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Wakulima wa Tanzania na mimi nikiwa mmojawapo, ninaomba kumwuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Serikali imepiga marufuku kuza mazao nje ya nchi; na wakulima kwa sasa hivi wanateseka kwa sababu wameshindwa kuza mazao yao kwa vile wanunuzi wameacha kununua mazao na wale wanaonunua wanunua kwa bei ya chini sana kwa mfano; mbaazi, choroko, dengu, ngwala; ni mazao ambayo yote sasa hivi hayanunuliwi; sasa tunaomba Serikali itoe tamko kwamba inakuwaje kuhusu hayo mazao? Kama hairuhusi kuuzwa nje, je, Serikali ipo tayari kununua hayo mazao ili hao wakulima waweze kujandaa kwa msimu ujao ambaa umekwishafika? (*Makof*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, Tangazo la Serikali ambalo ndilo liliipiga marufuku uuzaaji wa mazao nje ya nchi, halihusiani hata kidogo na mbaazi wala jamii ya mikunde ya namna yoyote. Ili kuondoa utata huu na sijui umetokana na nini, nadhani ni kwa sababu tu labda lile tangazo wengi hawajui linasema nini; tutaiagiza ofisi yetu, lile tangazo litoke kwenye gazeti ili watu wajue. Tulichokuwa tunalenga zaidi pale ilikuwa ni Zao la Mahindi. Kama inabidi tuongeze orodha zaidi, ni lazima lile tangazo tulirekebishe ili tuweze kuongeza mazao mengine. Vinginevyo, hauwezi ukakataza zao nje ya yale ambayo yamewekwa kwenye Tangazo la Serikali. (*Makof*)

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali kwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa udini na ukabila ni vitu hatari sana katika jamii kwa wakati huu ambavyo kwa namna moja au nyingine vinaweza kutuharibia umoja wetu, mshikamano wetu na amani na utulivu uliokuwepo katika Taifa hili. Kwa muda mrefu sasa jamii ya watu wenye imani ya Uislam wanatoa kauli zao hadharani katika vyombo vya habari na katika machapisho mbalimbali kwamba ndani ya Mfumo wa Utawala kwa sasa kuna udini dhidi yao; je, Serikali inasema nini juu ya hoja hiyo?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nataka nikubaliane kabisa na Mheshimiwa Barwany kwamba, sisi kama Taifa, Katiba inatuasa kama Wananchi wa Tanzania tusiwe na tabia au mwelekeo wowote ule wa kubaguana ama kwa misingi ya dini au makabila yetu au rangi zetu au jinsia au namna nyingine yoyote. Hivyo ndivyo Katiba inavyosema. Kwa hiyo, kwa mtu yeoyote ambaye anafanya jambo lolote kinyume na matakwa ya Katiba hii, maana yake anavunja Katiba.

Mheshimiwa Spika, sasa Mheshimiwa Barwany anasema, zimekuwa zikisikika kauli na maneno yanayoashiria kwamba, kuna kundi moja mionganii mwetu, ambalo linaonekana pengine linabaguliwa kutokana na imani yake. Mimi nasema, tuendelee wote kama Watanzania kukemea jambo hilo kwa nguvu zetu zote. Kwa sababu hakuna eneo ambalo wakati mwingine linaweza likatufanya tukagombana kwa urahisi kama dini. Dini ni suala la imani na kila mtu lazima awe na uhuru wa kuamini kile anachoamini yeye kwamba, ndiyo kitakachomsaidia kufika peponi. Sasa, kupigana vijembe kwenye eneo hili, hakuwezi kukubalika hata kidogo. Kwa hiyo, nadhani kikubwa ni sisi Watanzania wote kulitambua na tuendelee kulisema na hasa sisi Viongozi, tusiruhusu mwelekeo wa namna yoyote ya ubaguzi wowote ule achilia mbali huu wa kidini.

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Ahsante kwa majibu mazuri. Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa sura ambayo ipo sasa hivi Waislam wanaamini hilo kwa asilimia kubwa; kama Kiongozi wa Serikali

katika Bunge hili na sisi ni wawakilishi wa jamii yote ya Watanzania; je, hatua gani ambazo Serikali inaweza kuchukua ili kuliridhisha kundi hili ambalo tayari linaona hali ni mbaya kwao?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, siyo rahisi sana, ukiondoa hili nililolisema, kuweza kupata maneno mengine ya namna ya kujibu swali la Mheshimiwa Barwany. Ingaliwa pengine hoja imejengwa kwamba, dai linasema tunabaguliwa kwa sababu hii, ningeweza basi nikajikita kwenye jambo hilo, tukaona namna ya kulizungumza na kulipatia ufumbuzi. Kwa ujumla, mimi niseme tu Mheshimiwa Barwany, kama Watanzania ni lazima wote tutambue hilo na tujitahidi kujiepusha na ubaguzi wa namna yoyote kwa dhati kabisa. Tukiingia huko ni hatari sana kwa Taifa letu.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Naomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkoo, kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Mkoa wa Kagera umevamiwa na wahamiaji haramu wenye mifugo kutoka nchi jirani ya Rwanda pamoja na wao wenyewe; na kwa kuwa wameingia Mkoa wa Kagera wameharibu mazingira ya nchi yetu; lakini pia wameua watu wetu, Watanzania sita wameuwawa katika Wilaya ya Ngara; na kwa sisi Wabunge wa Mkoa wa Kagera tumekuwa tukikullilia kuusaidia Mkoa wetu; je, unawaambia nini Wananchi wa Mkoa wa Kagera kuhusu uvamizi wa Raia wa Rwanda? (*Makof!*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, uhamiaji haramu wa aina yoyote ile haukulaliki hapa nchini na tutaendelea sisi kuchukua hatua stahiki kila tutakopobaini kwamba, upo uingiaji katika nchi yetu, ambao ni kinyume cha sheria. Sasa ninazo taarifa za kutosha juu ya hali ya Mkoa wa Kagera na tayari tulishazungumza na Mheshimiwa Nahodha, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kuhusu nini tufanye ili kukabiliana na hilo tatizo.

Ningeweza nikasema tunachowaza ni nini lakini pengine haitatusaidia sana. Itshe tu kusema, tumeshachukua maamuzi ambayo katika muda ujao, tutajaribu kuhakikisha kwamba tunakabiliana na hilo tatizo.

**MHE. ANGELAH J. M. KAIRUKI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi, nami niweze kumwuliza Waziri Mkoo swali la msingi.

Katika Chuo cha Ustawi wa Jamii Dar es Salaam pamekuwa na mgogoro mkubwa ambao umekuwa ukiigubika Menejimenti ya Chuo kile na imepelekeea wafanyakazi zaidi ya 27 kufukuzwa kazi bila kupata haki ya kusikilizwa, jambo ambalo pia limepelekeea Menejimenti hii kutokuwa na sifa ambazo zinastahili kwa viongozi hao kwa mujibu wa *NACTE*; je, Serikali kwanza ipo tayari kuwarejesha wafanyakazi hawa waliofukuzwa kazini bila ya masharti yoyote na kutangaza nafasi hizi za Menejimenti upya ili watu wenye sifa waweze kuomba? Ahsante.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kuitaka Serikali iwarejeshe wale wahadhiri kwa namna ambavyo Mheshimiwa Kairuki angependa, Serikali inasema hapana hatutafanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, nasema hatutafanya hivyo kwa sababu unajua nchi hii inazo taratibu zake za kisheria, ndiyo maana mfumo ulivyo umeweka kila aina ya *safe guard* katika sheria zetu. Yupo mmoja atachukua hatua hii, lakini inakupa fursa wewe ya kwenda mbele kipinga hatua iliyo chukuliwa na huyo mwingine. Sasa hawa Wahadhiri, kwanza, walikuwa watano tu, ambao Serikali iliamua kwamba, waondolewe katika Chuo na kwa sababu nilizopewa mimi kwa maelezo, niliona ni sababu nzuri kwa sababu zili kuwa zinagusa zaidi utumishi wao. Matokeo yake ni kwamba, Walimu zaidi wakasema hapana na sisi tunaungana tunagoma, kwa hiyo, kundi likawa kubwa.

Mheshimiwa Spika, tumefanya jitihada za kuwapelekeea barua kundi moja ili waweze kujieleza wamekataa; sasa kama Serikali mnafika mahali mnasema hatuwezi kuendesha Chuo namna hii. Kwa hiyo, ndiyo maana ule uamuzi ukafanyika na mimi bado nasema kama wanaona wameonewa taratibu za kukata rufaa zipo.

Mheshimiwa Spika, nataka nishukuru sana, tayari tumeshapata wahadhiri wengine wa muda kumi na nane, wameshaanza kufundisha na wanafunzi sasa wanaendelea na masomo kama kawaida.

Kwa hiyo, rai yangu ni kwamba; Watanzania wenzangu, hii tabia ya kukimbilia migomo na mambo kama haya badala ya kufuata taratibu, wakati mwingine haina tija. Nataka nimwombe sana Mheshimiwa Kairuki, tusaidie kwa sababu wewe umetokana na eneo hilo; hebu jaribu kuwaambia wahadhiri hawa ni wasomi na ni waelewa; wafuate taratibu na sheria. Hakuna mgogoro hata kidogo, kama sheria itasema wote warudi kesho, tutawarudisha wote.

**MHE. ANGELA J. M. KAIRUKI:** Mheshimiwa Spika ahsante. Kwanza kabisa, wafanyakazi hawa hawakugoma, mwezi Machi mwaka huu, *NACTE* walifuta ithibati ya Chuo cha Ustawi wa Jamii. Sasa je, wahadhiri hawa watafundishaje wakati hakuna ithibati?

Pia wafanyakazi hawa walikuwa wazalendo, walikwenda katika Tume ya *CMA* wakaandikisha mgogoro wao wa kikazi lakini Menejimenti hii imeitwa zaidi ya mara mbili na imekaidi na hajahudhuria. Je, Serikali inasemaje kuunda Tume kwa sababu suala hili limefikia utata sana na limechukua muda mrefu? (*Makof*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, mimi sitaki nionekane nabishana na dada yangu Kairuki hata kidogo, wala siyo busara nzuri. Ninachosema, kama wana hoja ya kisheria, turudi tukae tufuate sheria, kama unalolisema hilo ndilo lilitangulia mimi nitalisimamia; lakini kama unalolisema ni jambo lilloluja baada ya mgomo na mimi nasema ni lazima turudi tukae tufuate taratibu, tukilifanya hili halina tatizo hata kidogo. (*Makof*)

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuweza kunipatia fursa hii nami nimwulize Waziri Mkuu swali.

Tarehe 23 Agosti, majira ya saa nne katika Shule ya Msingi Nyabigina, Polisi walipiga mabomu Nyamongo ...

**SPIKA:** Mwaka huu?

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Nyabigina.

**SPIKA:** Nasema ni mwaka gani? (*Kicheko*)

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, mwaka huu tarehe 23 Agosti, 2011, majira ya saa nne, katika Shule ya Msingi ya Nyabigina, Polisi walipiga mabomu katika Shule ya Msingi ile, ambapo yalijeruhi wanafunzi tena wa chekechea, yakawapiga yakawang'oa wengine meno, kuna wanawake wajawazito pia walikuwa katika shughuli zao wakaathirika na kulazwa hospitali.

Kwa kawaida, ninavyoju maeneo ya shule ni ya utulivu sana, kwa sababu wanafunzi wanatakiwa wapate utulivu wa kutosha ili waweze kufuatilia masomo yao.

Nataka kujua je, hii ni Sera ya Serikali kuwapiga wanafunzi amba hawana hatia na ni watoto wadogo sana na kama siyo Sera ya Serikali hawa walioathirika watalipwa fidia kiasi gani na lin?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, juzi Mheshimiwa Matiko alikuja kuniona kwa jambo tofauti kidogo, angekuwa amenidokeza jambo hili ningekuwa nimeshamfanyia kazi nzuri sana na ningempa majibu mazuri sana. Kwa hiyo, ninachowea kusema kwa sasa ni kwamba, nashukuru kwa taarifa yako, acha niifanyie kazi halafu kwa wakati mwafaka nitakupa maelezo ambayo pengine ni mazuri zaidi.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Naomba nimwulize swali Waziri Mkuu.

Kwa kuzingatia *Doctrine ya Separation of Powers* kati ya Bunge kama Mhimili mwengine na Serikali kama Mhimili mwengine, Katibu Mkuu David Jairo, alitoa pesa na si kwa kutumia hati moja tu ambayo iliwasilishwa hapa kwa ajili ya kuwezesha kuitisha Bajeti ya Wizara yake, kuna hati nyingine ambazo baadaye nitaomba kuziwasilisha Mezani; kuna ya milioni ishirini na mbili na kuna ya milioni 5.8. Ningependa kujua kama ni utaratibu wa kawaida wa Serikali kwamba; Makatibu Wakuu wanawenza wakakusanya pesa kwa ajili ya ku-facilitate upitishwaji wa bajeti ikiwa pesa hizo hazijapitishwa na Bunge Tukufu? Je, huu ni utaratibu wa kawaida?

**SPIKA:** Hata kama Kiongozi wa Kambi ya Upinzani aliuliza swali linalofanana na hilo, lakini Waziri Mkuu labda ujibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ndiyo maana nilimjibu Mheshimiwa Mbewe kwamba, maadam tumeshafikia hatua hii ya kuwa na Kamati Teule, yapo mambo mengi ndani humu, ambayo pengine yatajitekeza na mimi ningemba hilo unalolisema linaweza kuwa vilevile ni sehemu ya jambo ambalo linaweza likatazamwa na hiyo timu ili tuweze kuona hatimaye tunakubalina nini kama Taifa.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika ahsante. Kwa kuwa Wabunge wa Majimbo ndiyo wenye Mifuko ya Jimbo; na kwa kuwa Wabunge wa Viti Maalum hawana Mfuko wa Jimbo na hawapo kwenye Kamati ya kugawa hizo fedha za Mfuko wa Jimbo; na kwa kuwa Wabunge wa Viti Maalum ni wadau wakubwa wa kuchangia Miradi ya Maendeleo pamoja na kuhimiza shughuli za maendeleo; je, Serikali haioni kwamba Wabunge wa Viti Maalum kutokuingia kwenye Kamati ya kugawa fedha za Jimbo ni kutokuwatendea haki pamoja na Wanawake wanaowawakilisha?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwa muundo au mfumo wa sheria ile ulivyo, anachokisema Mheshimiwa Diana Chilolo, ndivyo ilivyo. Mfuko ule ultengenezwa kwa ajili ya kuwa wezesha Wabunge wenye Majimbo, waweze kuendesha shughuli zao vizuri na mtakumbuka suala hili lillleta mjadala mkubwa, lakini tukaishia kutunga sheria kwa mfumo huo.

Mhehsimiwa Spika, nakubalina naye kabisa kwamba, Wabunge wa Viti Maalum wanao mchango mkubwa sana katika maendeleo ya maeneo yao. Kwa kuwa Wabunge wa Majimbo ninavyojuu hawana uchoyo, hawana ubaguzi na wanashirikiana vizuri sana na Wabunge wa Viti Maalum; nataka nitoe rai kwa Wabunge wote kwamba, endeleeni na moyo huo na mimi Jimboni kwangu nimekuwa namchukua Mbunge wa Viti Maalum, namfanya ni Mjumbe kwenye Kamati yangu; wala halinipi tatizo hata kidogo.

Ninatoa rai kwa Wabunge wengine, wakaribisheni ama wawekeni kwa utaratibu huo, wawe ni Wajumbe kwenye zile Kamati kwa sababu zile fedha chini ya Mfuko, siyo fedha ambazo Mbunge anatembea nazo, ni fedha kwa ajili ya kuchangia au kuchajisha shughuli za maendeleo katika Jimbo. Kwa hiyo, kinachofanywa ni maeneo yote hata yale ambayo Mbunge wa Viti Maalum anasema na ye ye ana sehemu ya kuchangia, kote huko tunachangia kuitia Mfuko huo huo. Kwa hiyo, akiwepo pale itasaidia tu kuimarisha ushirikiano na upendo mlongoni mwao na mimi nadhani sheria haikuka vibaya ila kama kutakuwa na hoja kubwa ya kutaka hili liwekwe bayana kwenye Sheria kwamba ni lazima awe Mbunge kwenye ile Kamati, sioni tatizo hata kidogo kwa sababu ni Mjumbe tu wa ile Kamati.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mhehsimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa Waziri Mkuu amejibu swali hili vizuri sana; na kwa kuwa wakati wa mchakato wa kuanzisha Mfuko huu Serikali iliahidi kwamba italeta sheria ili kuifanyia marekebisho Wabunge wa Viti Maalum na wao waweze kupata haki zao za msingi kuitia Mfuko huu wa Jimbo ...

**WAZIRI MKUU:** Sikumpata vizuri hapo mwishoni maana makofi yalizidi.

**SPIKA:** Hebu rudia kidogo pale mwishoni.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mhehsimiwa Spika, kwa kuwa Serikali wakati tukiwa kwenye mchakato wa kuanzisha Mfuko wa Jimbo iliahidi kuleta sheria hii ili iweze kufanyiwa marekebisho

na Wabunge wa Viti Maalum waweze kupata fungu na haki zingine katika Mfuko huu wa Jimbo; je; ni lini sasa Sheria hii italetwa hapa Bungeni tuweze kuijadili na sisi Wabunge wa Viti Maalum tuweze kupata haki zetu za msingi? (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, mimi binafsi sikumbuki ahadi hiyo, lakini tutakachofanya, tutajaribu kutumia *Hansard* kuona tuliahidi nini, kama ni hili analolisema Mheshimiwa Diana Chilolo basi tutaliangalia.

Mheshimiwa Spika, lakini nataka niseme kwamba, tunaweza tukavutana sana hapa juu ya Viti Maalum lazima wawe na Mfuko wao, tulibishana sana sisi kwenye *cabinet* lakini hata wakati wa kupitisha ile sheria. *Constituency* ya Viti Maalum ni Mkoa mzima, mambo yote yanayohusiana na maendeleo katika Mkoa ule ni yale ambayo unayakuta yanatekelezwa katika ngazi ya Jimbo; iwe ujenzi wa shule, ujenzi wa kituo cha afya, kuchimba visima au mradi wa kusaidia kutengeneza barabara, bado itakuwa katika eneo la Jimbo. Ndiyo maana unaona dhana iliyojengwa katika Mfuko ule ni kwamba ni lazima Mfuko huu uendelee kuwa wa Jimbo kutokana na sababu hiyo.

Mheshimiwa Spika, ninaloona ni jambo la busara ni hii rai kwamba, hawa nao wawe ni sehemu ya Kamati inayopitia maeneo yale ili kama ana eneo ambalo angependa likumbukwe nalo liingizwe katika ule utaratibu. Mimi nadhani hilo linaweza kuwa ni jema zaidi. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri Mkuu, muda umekwisha, tunakushukuru sana kwa majibu na pia nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa maswali. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Katibu hatua inayofuata.

#### **MASWALI NA MAJIBU**

Na. 485

#### **Kuwakwamua Kiuchumi Wavuvi Wanaoishi Kanda ya Mwambao - Nkasi Kusini**

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA** aliuliza:-

Jiografia ya Jimbo la Nkasi Kusini liliogawanyika katika Kanda mbili imeleta tofauti kubwa ya shughuli za kiuchumi zinazofanywa na wakazi hao ambapo Wananchi wa Kanda ya Ufipa Juu hutegemea zaidi kilimo na wale wa Mwambao hutegemea uvuvi na biashara ndogondogo; Serikali imeonesha nia nzuri ya kuwasaidia Wananchi wa Kanda ya Ufipa Juu kwa mpango wake wa Kilimo Kwanza ambao umeleta tofauti ya hali ya kimaisha katika Jimbo hilo:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kuwanusuru kiuchumi Wananchi wa Kata za Wampembe, Kala na Ninde ambao ni maskini kwa sababu ya kutumia zana duni za usafiri na uvuvi?

(b) Je, Serikali inakubaliana na ushauri kuwa Wananchi hawa wasaidiwe kwa kuwauzia vyombo vya uvuvi kwa bei nafuu katika vikundi vyao vya uvuvi kama njia mojawapo ya kunusuru tatizo hili?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Desderius John Mipata, Mbunge wa Nkasi Kusini, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kuptitia Mradi wa Uwiano wa Usimamizi wa Mazingira ya Bonde la Ziwa Tanganyika chini ya uratibu wa Ofisi ya Makamu wa Rais, ina mpango wa kuwawezesha wavuvi katika Mikoa ya Rukwa na Kigoma. Katika kipindi cha mwaka 2010/2011, kiasi cha Euro 480,000 kimetengwa ili kuanzisha Miradi midogo midogo ikiwemo ya uvuvi na utunzaji wa mazingira. Vilevile kuptitia mipango ya kuendeleza Sekta ya Kilimo ya Wilaya (*DADPs*),

Halmashauri zimeshauriwa kutumia fedha za *DADPs* kuhamasisha jamii za wavuvi kuunda vikundi vya ufugaji wa samaki pamoja na uvuvi ili waweze kujiongezea kipato na hivyo kuboresha maisha yao. Katika mwaka 2011/2012, kiasi cha shilingi 1,268,362,000.00 zimetengwa kwa ajili ya *DADPs* katika Halmashauri ya Nkasi. Kati ya fedha hizo, shilingi 57,700,000.00 ni kwa ajili ya kuendeleza vikundi vya wavuvi na wafugaji wa samaki.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imeondoa ushuru wa zana za uvuvi, vifaa vinavyotumika kutengeneza nyavu (*accessories*), injini za kupachika pamoja na vifungashio vya mazao ya uvuvi, zinazoingizwa nchini ili kupunguza bei ya vifaa hivyo na hivyo kuwapa wavuvi unafuu wa bei. Kwa upande wa vyombo vya uvuvi, utengenezaji wake kwa sehemu kubwa, unafanywa na Sekta Binafsi, ambapo bei hutegemea hali ya soko. Wizara inawashauri wavuvi wajunge katika vikundi vya uzalishaji mali, ikiwa ni pamoja na utengenezaji wa vyombo vya uvuvi na hivyo kuvipata kwa bei nafuu. Aidha, kuititia vikundi vyao, wanaweza kuomba mikopo kutoka kwenye taasisi za fedha kwa ajili ya kununulia vyombo vya uvuvi pamoja na zana zake.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa biashara ya samaki wabichi inalamikiwa sana kwa sababu inavunja sheria, inawanyima Wananchi kitoweo na inawanyima akina mama ajira kwa sababu hufanyika majini moja kwa moja bila kufika kwenye ufukwe. Je, Serikali inasema nini juu ya biashara hii?

(b) Kwa kuwa suala la samaki wabichi kwenda Zambia ni kufuata soko; je, ni lini Serikali itawezesha kupatikana kwa soko la samaki katika maeneo ya eneo la uvuvi ikiwa ni pamoja na kujenga kiwanda cha usindikaji wa samaki wabichi katika eneo la Wampembe? (*Makofii*)

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, Sheria yetu ya Uvuvi Namba 22 ya Mwaka 2003 pamoja na Kanuni zake za Mwaka 2009, zimeweka wazi kwamba, taratibu za kuvua lakini pia biashara inayohusiana na mazao ya samaki, siyo ruhusa kufanya biashara wanapokuwa wabichi. Hata hivyo, taratibu zinaweza zikawekwa na Mamlaka ya Halmashauri husika ili kile kinachofanyika, kifanyike kwa mujibu na taratibu za sheria; na hivyo ningelishauri tu kwamba, kama kuna haya yanayofanyika, labda sheria hiyo itumike katika ngazi ya Halmashauri husika na nina uhakika kwamba, ufumbuzi utapatikana.

Mheshimiwa Spika, sheria nilizozitaja zipo wazi pamoja na Kanuni zake, zinakataza kabisa uuzaaji wa mazao ya samaki wanapokuwa wabichi kwenye nchi za nje. Hii imekusudia kuwapa Watanzania uwezo wa kuvua na kuchakata na kuza mazao nje yakiwa yameongezewa thamani; na hivyo kama hili linafanyika, ningeliomba kwa kuititia Bunge lako Tukufu, niwaelekeze wahusika kwamba, hili lisifanyike kwa sababu ni kinyume cha sheria na sheria itachukua mkondo wake kuhakikisha kwamba halitokei.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, umeulizwa Kiwanda; kwa nini msijenge kiwanda huko?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru; kwa upande wa kiwanda ningependa tu kujibu kwamba, Serikali inaandaa mazingira wezeshi, haijengi viwanda kwa sababu ni sehemu ya biashara, lakini yale mazingira wezeshi yanapokuwa yameandaliwa, tunatarajia kwamba kwa kuhamasisha Sekta Binafsi, watatokea wawekezaji watakaojenga kiwanda na Mradi niliousema ambao unatekelezwa kule ni sehemu ya kuandaa haya mazingira wezeshi.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa uvuvi ni sehemu ya Kilimo Kwanza; je, Serikali ipo tayari kuwasaidia wavuvi kuwapatia boti za kisasa (*fibre boats*) ili waweze kutumia wakati wa kuvua kwa kutumia ruzuku kama wanavyowasaidia wakulima kwa kuwapatia pembejeo na matrekti? (*Makofii*)

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, utaratibu kama huu umeshafanyika kuititia Mradi wa *MANCEP*, kwa upande wa Ukanda wa Bahari ya Hindi, lakini

kwa Miradi iliyopo kando kando ya Ziwa Tanganyika, kwa sasa hatujafikia kule. Ninaloweza kusema ni kumwomba Mheshimiwa Mbunge kwamba, tushirkiane kuwahamasisha wavuvi wadogo wadogo ili wajunge katika vikundi nya uzalishaji, kwa njia hii ama kwa kwenda kwenye taasisi za fedha, tuone uwezekano wa wao kuweza pia kupata mikopo kwa ajili ya kupata boti hizi anazoongelea ambazo ni bora na labda zitawawezesha kuzalisha zaidi.

Na. 486

#### **Mahitaji ya Umeme**

**MHE. ZAYNABU M. VULLU** aliuliza:-

Mwaka 2007 Serikali ilipitisha laini ya umeme kutoka Bunju hadi Bagamoyo na Wananchi wa Vijiji vyote vilivyoko kandokando ya barabara wamenufaika na huduma hiyo:-

Je, Serikali itaongeza mtandao huo ili Wananchi wasiokuwa kandokando na njia hiyo ya umeme kama vile Vijiji nya Mapinga, Kerege, Kiromo na Kitopeni, waweze kuvuta umeme kwa gharama nafuu?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zaynab Vullu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, njia ya umeme ya msongo wa Kv 33 kutoka Tegeta kuititia Bunju hadi Bagamoyo, ilianza kujengwa mwaka 2004 na kukamilika mwaka 2008. Njia hii ya umeme imesaidia wakazi wa kandokando ya Barabra ya Bagamoyo, kunufaika na huduma ya umeme kutoka kwenye njia hiyo. Vijiji alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge, havikuwa sehemu ya Mradi wa Ujenzi wa njia ya umeme kwenda Bagamoyo. Umbali kutoka njia hii ya umeme hadi vilipo vijiji hivi ni kama ifuatavyo: Mpaka kijiji cha Mapinga Mpiji ni kilomita nne, Kijiji cha Kitopeni ni kilomita mbili, Kijiji cha Kiromo ni kilomita mbili na hadi Kijiji cha Amani Kerege ni kilomita tatu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa maombi ya ya upelekaji wa umeme katika vijiji hivi yamepokelewa na Shirika la Umeme (*TANESCO*), Wizara yangu imeelelekeza *TANESCO* kufanya tathmini ya mahitaji ya umeme, kazi zitakazofanyika na gharama za kupeleka umeme katika maeneo yote ambayo yapo kandokando ya barabara iendayo Bagamoyo. Baada ya tathmini hiyo kukamilika, Serikali itaangalia uwezekano wa Miradi hiyo kufadhiliwa na *TANESCO* au *REA*, kulingana na ukubwa wa gharama za Miradi hiyo.

**MHE. ZAYNABU M. VULLU:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amebainisha katika majibu yake kwamba umbali wa vijiji hivyo kutoka kwenye nguzo za umeme hadi Kijiji cha Mpiji ni kilomita nne na Kijiji cha Kitopeni kilomita mbili, Kijiji cha Kiromo pia kilomita mbili na Kijiji cha Amani Kerege kilomita tatu:-

(a) Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kutuambia kazi hiyo ya tathmini itakamilika lini na ni lini watarajie kupata huo umeme na gharama zitakuwa nafuu? (*Makofî*)

(b) Kwa kuwa Sera ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni kuwapatia Wananchi wa Vijiji huduma ya umeme; na kwa kuwa nguzo za umeme zimepita katika Kijiji cha Boma kwenye Kata ya Kiromo na Kijiji cha Kondo kwenye Kata ya Zinga na Kijiji cha Mataya kwenye Kata ya Kiromo pia vijiji hivyo vyote havihitaji kufanyiwa tathmini; je, ni lini Serikali itawapatia umeme Wananchi wa Vijiji hivyo na wao waweze kuhamasika katika kuendeleza maisha yao? (*Makofî*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, niseme kwamba, huu utaratibu wa kushusha umeme kwenda kwenye vijiji ambavyo laini inapita ni wa kawaida isipokuwa tu kwamba, utaratibu huu unafanyika pale ambapo laini ya msongo wa KV 33 inapita; lakini kuna vigezo ambavyo inabidi watu waviangalie ili kushusha umeme.

Mheshimiwa Spika, swali la pili la Vijiji vya Kiromo na Boma, inawezekana ukaona nguzo inapita juu lakini haikidhi vigezo. Inawezekana kushusha umeme pale ukawa ni gharama kubwa sana, ambapo hailingani na maendeleo ya pale. Kwa hiyo, tunaangalia vigezo vingi; shughuli za kiuchumi, huduma za kijamii na kadhalika ili kufikia maamuzi ya kushusha umeme. Mara nyinyi ni kweli inakuwa rahisi ikiwa na KV 33 lakini ikiwa na msongo wa juu zaidi kwa maana ya *high tension transmission lines* inakuwa ni jambo ambalo haliwezekani, kwa sababu linataka utaratibu wa gharama kubwa zaidi wa kushusha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi niseme hivi; kwa haya maeneo tumeyapokea tutakwenda kuwapa *TANESCO*. Hata hizi ambazo anasema nguzo zinapita juu labda isitakiwe kazi ya kufanya tathmini, bado kuna kazi ya tathmini inatakiwa kufanywa. Kwa hiyo, namhakikishia tu kwamba, nimepokea na nitawakabidhi *TANESCO* walifanye kazi hii halafu baada ya hapo ndiyo tutajua kulingana na gharama, kazi hiyo itafanywa na *REA* au itafanywa na *TANESCO* wenyewe.

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MINYAA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali ilikubali na ikakili kwamba gharama za kuunganisha umeme majumbani ni kubwa na Wananchi wengi hawamudu; na Serikali ikatoa kauli hapa Bungeni katika Kauli za Mawaziri kwamba, itatayarisha Mpango utakaowawezesha hata Wananchi wenyewe nyumba za nyasi waweweze kutumia umeme huo; je, mpango huo mpaka leo uko wapi kwani mpaka leo Serikali hajatekeleza; Serikali inasema nini?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, Serikali ilikiri kwamba, gharama za kuunganisha umeme ni kubwa. Tulisema yapo maeneo ambayo tunaamini kwamba, *TANESCO* inaweza kuweka utaratibu wa kushusha gharama hizo; kwa mfano, kwenye nguzo ambazo zinazalishwa humu humu ndani na kadhalika.

Inapohusu bidhaa ambazo zinatoka nje ya nchi, ambapo gharama zinakosekana na mambo mengine mengi, inakuwa ngumu kushusha bei hiyo. Kwa hiyo, tulichosema ni kwamba, tunakwenda kufanya tathmini ya kuangalia namna ya kushusha gharama za umeme na pale ambapo haitawezekana, tutaangalia namna ya kuleta utaratibu wa kuunganisha kwa awamu ili kuondoa mzigo kwa wateja hawa.

Mheshimiwa Spika, sasa hili la pili la kusema tuunganishe umeme kwenye nyumba za nyasi, kweli ni utaratibu ambao tulikuja nao tukasema *TANESCO* waufanyie kazi kuangalia namna itakavyokuwa na tutaangalia namna itakavyowezekana. Kimsingi, nadhani ni vyema zaidi tuhimizane Watanzania walio wengi waunganishe umeme kwenye nyumba zao. Sote tunapenda Watanzania waishi kwenye nyumba ambazo zina usalama zaidi kuliko nyumba za nyasi.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa umeme umefika Mji Mdogo wa Longido, lakini haujasambazwa katika nyumba za Wananchi kutokana na kutokuwa na nguzo pamoja na nyaya. Je, Waziri ataniambiaje kuhusu usambazaji huu ambao unatakiwa kwa sasa Mji Mdogo wa Longido? (*Makofii*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, tatizo la Longido ni sawa na tatizo la Kasulu, ni sawa na tatizo Kibondo, kwa sababu haya majenereta yaliingia pamoja. Kweli majenereta haya yalipopelekwa pale, kazi kubwa ilikuwa ya kufikisha umeme pale na kuwashaa majenereta, lakini kwa sasa hivi tulikuwa na tatizo la vifaa vya usambazaji; kwanza, iliusu nguzo; kweli tatizo hilo limefanyiwa kazi, nguzo zimeingia na sasa hivi ni matatizo ya nyaya. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Lekule Laizer kwamba, kama ambavyo tunataraja kukamilisha tatizo la Kasulu na Kibondo kwa pamoja, ningependa pia kuoanisha tatizo hili la Longido na kulifanyia kazi limalizike mara moja.

Na. 487

**Serikali Kuwajali Wafanyabiashara Ndogondogo**

**MHE. DAVID E. SILINDE** aliuliza:-

Biashara ndogondogo kama mama ntilie na wamachinga inawawezesha Wananchi kujajiri na kupata vipato vinavyowawezesha kukabiliana na ugumu wa maisha:-

(a) Je, ni kwa nini Serikali inatumia nguvu kubwa kupertia Mgambo kuwaondoa maeneo wanayofanyia biashara?

(b) Je, kwa nini Serikali isiwajengnee wafanyabiashara hao maeneo ya kufanya biashara ili kuondoa kero na usumbufu?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Mbozi Magharibi, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Kwanza, ninaomba nihitilafiane na mwuliza swali kuwa, Serikali inatumia nguvu kubwa kupertia mgambo, kuwaondoa wamachinga na mama ntilie maeneo wanayofanyia biashara. Kinachofanyika ni:-

- (i) Kusimamia Kanuni za Serikali za Mitaa za Mwaka 2008, Tangazo la Serikali Na. 242 la 2008, sehemu ya sita ya Kanuni hizi inakataza mtu ye yote kufanya biashara katika maeneo yasiyoruhusiwa.
- (ii) Kusimamia Sheria ya Leseni za Biashara Na. 25 ya 1972 kama ilivyorekebishwa, ambayo inaruhusu mfanyabiashara ye yote kufanya biashara mahali panaporuhusiwa.
- (iii) Kuondokana msongamano usio wa lazima ambao pia unaweza kusababisha ajali za barabarani kwa watembea kwa miguu, uchafuzi wa mazingira kwa shughuli wanazozifanya, kukosekana takwimu sahihi ya nguvu kazi hiyo, ukosefu wa kodi kwa Serikali na kutoweza kupatiwa huduma muhimu za kijamii kama vile maji, umeme, vyoo na kadhalika.

Kwa kuzingatia hali hiyo, Serikali hutumia rasilimali kujenga na kuweka miundombinu kwa ajili ya wafanyabiashara hao, lakini kwa kuwa wafanyabiashara ndogo ndogo wamekuwa wakiendoka katika maeneo waliyopangiwa na kwenda kufanya biashara katika bakaa za barabara, kitendo ambacho ni uvunjifu wa sheria; hivyo, mgambo hutumika kuwakamata na kuwaelekeza warudi katika maeneo waliyopangiwa.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikisha Halmashauri za Miji, Manispaa na Maji nchini kote, imeendelea kutenga maeneo maalum ya kufanya biashara kwa wafanyabiashara ndogondogo. Kwa mfano, Jengo la *Machinga Complex* na maeneo mengine ambayo nimeyataja.

Natoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge, ambao ndiyo mnakaa kwenye Vikao vya Madiwani kusaidia kulipatia ufumbuzi suala hili kwa kuhakikisha Mamlaka za Serikali za Mitaa zinawatengea wafanyabiashara hawa maeneo maalum ya kufanya biashara. (*Makoti*)

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri katika majibu yake ya msingi amekiri wazi kwamba huwa wanatumia mgambo kuwakamata na kuelekeza warudi katika maeneo waliyopangiwa; lakini kiukweli hali inakuwa tofauti, hivi sasa kumekuwepo na mgambo ambao wamekuwa na tabia ya kukamata mitaji na bidhaa za Wamachinga pamoja na vifaa vya mama ntilie:-

(a) Je, ni kwa nini mgambo wanakamata mitaji badala ya kuwaelekeza? Katika hilo tunahitaji kauli ya Serikali; inawaelekeza nini Mgambo juu ya kukamata mali za Wamachinga?

(b) Kwa nini tunapoelekea Uchaguzi Mkuu hali ya Wamachinga na Mama Ntilie kibashara inakuwa imetulia lakini baada ya uchaguzi hali inakuwa ni tofauti? Serikali naomba itupe sababu ni kwa nini? (*Makofii*)

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, mgambo hawa wanatakiwa watekeleze sheria tu. Nadhani kitu ambacho naweza nikasema kwa maana ya kauli ni kwamba; ni muhimu hawa askari mgambo kwenye Majiji waelekezwe kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu bila manyanyaso na dhuluma wakati wanapotekeleza majukumu yao ya kuwaondoa wafanyabiashara katika maeneo yasiyorhusiwa. Hawajapewa amri ya kuchukua bidhaa. Kwa hiyo, hilo ni kosa na mimi ningependa nitoe wito wasifanye hivyo.

Hili la pili kwamba, kuelekea uchaguzi ndiyo akina Mama Ntilie wanatulia. Mimi nadhani ni mtazamo wake tu, lakini ukweli ni kwamba, sheria zinaendelea kutekelezwa miezi yote 12 na miaka yote bila kuwa na wakati wowote. Kwa kuwa hata sisi wanasiasa wakati wa kuelekea uchaguzi tunakuwa na *pressure*, tunaweza tukaona hivyo lakini siyo kweli. (*Makofii*)

Na. 488

#### **Kushuka kwa Kiwango cha Elimu Nchini**

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA** aliuliza:-

Ripoti ya Utekelezaji wa MKUKUTA Awamu ya Kwanza ya Mwaka 2009/2010 inaonesha kwamba ubora wa elimu ya sekondari unashuka mwaka hadi mwaka:-

- (a) Je, Serikali imefanya utafiti kubaini chanzo cha mwelekeo huo?
- (b) Katika Awamu ya Pili ya MKUKUTA Serikali imejipanga vipi na itachukua hatua gani kurekebisha hali hiyo?

#### **NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Christowaja Mtinda, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ubora wa elimu ni dhana pana ambayo inahusisha mchakato mzima wa utoaji wa elimu bora kama vile uwepo wa walimu wa kutosha na wenye sifa, mitaala inayokidhi haja, vifaa vya kufundishia na kujifunzia, maabara, maktaba pamoja na miundombinu stahiki kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum.

(a) Ufaulu hasa katika Mitihani ya Kidato cha Nne umekuwa unashuka. Hata hivyo, matokeo ya Mitihani ya Kidato cha Sita kwa kipindi cha miaka minne kuanzia mwaka 2007 – 2010, kinaonesha kuwa, ufaulu unapanda na ni kwa wastani wa asilimia 92, ambacho ni kiwango kizuri.

(b) Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na kushuka kwa ufaulu wa Kidato cha Nne, Awamu ya Pili ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES II), umejikita kuongeza ubora wa Elimu ya Sekondari kwa kufanya yafuatayo:-

- Kukamilisha majengo katika shule 1,200 ili kuzifanya shule hizo kuwa bora na hivyo kufanya mazingira ya kujifunzia kuwa bora na toshelevu kwa nyumba na maabara.

- Kuongeza idadi ya walimu ili shule zote zipate walimu wa kutosha wenye ujuzi wa juu wa kufundisha masomo yao. Kila mwaka kuanzia sasa, tunatarajia kupata walimu wasiopungua 13,000 wanaohitimu mafunzo yao ya shahada na stashahada. Aidha, mafunzo kazini yataimarishwa kwa walimu walioko shulenii.

- Fedha ya ruzuku ya kununulia vifaa vya kufundishia na kujifunzia nayo imeongezwa kutoka shilingi 20,000 kufikia shilingi 25,000 kwa mwanafunzi kwa mwaka.
- Maabara 264 zinatarajiwa kujengwa katika Halmashauri zote kwa kipindi cha mwaka 2010 – 2015, maabara mbili katika kila Halmashauri.
- Kuboresha Menejimenti za Shule kwa kuweka mifumo mizuri ya menejimenti na uongozi bora wa shule utakaochangia katika kuleta uwajibikaji na matumizi sahihi ya rasilimali zote zilizopo kama vile fedha, watu na muda ili kuongeza ubora wa elimu nchini.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kumwuliza Naibu Waziri, maswali mawili ya nyongeza:-

(a) Kwa kuwa katika jibu la msingi Naibu Waziri amekiri kwamba ufaulu wa wanafunzi wa Kidato cha Nne umekuwa ukishuka mara kwa mara na ule wa Kidato cha Sita ukiwa mzuri; je, ni kwa nini au ni sababu zippi zinazopelekeea kushuka kwa kiwango cha ufaulu kwa Kidato cha Nne na ule wa Kidato cha Sita kuwa mzuri wakati Mfuko wa Elimu ni ule ule mmoja katika Tanzania?

(b) Katika majibu ya msingi Naibu Waziri amesema kwamba katika kipindi cha mwaka 2010/2015 maabara 264 zitajengwa katika Halmashauri zote nchi nzima kwa maana ya kwamba maabara mbili katika kila Halmashauri; je, katika Mkoa wa Singida ni shule zippi ambazo zitajengewa maabara hizo? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Christowaja Mtinda, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba, ufaulu wa Kidato cha Nne unashuka, lakini ufaulu wa Kidato cha Sita umeongezeka katika mfululizo wa miaka hii minne. Labda tu sababu zinazopelekeea hivyo, nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwanza, Kidato cha Sita maana yake vijana wale wanakuwa wameshakuwa *screened*, wamechujwa kutoka kwenye mitihani yao ya Taifa ya Baraza la Mitihani na vilevile ni wachache na tayari wanakuwa wanasoma pale kufuatana na *combinations* zao. Kwa hiyo, kama kijana anakuwa anachukuwa *PCB*, maana yake anasoma masomo ya *physics, chemistry* na *biology*, anakuwa ame-specialise kwa hiyo ni rahisi sana kijana yule kufaulu.

Sababu za msingi kama nilivyosema; vijana wanakuwa wametoka kwenye mchakato wa Kidato cha Nne, kwa hiyo wanakuwa wamechujwa; ni tofauti labda na Kidato cha Nne ambapo vijana wale wanaokuwa wamemaliza darasa la saba wanakwenda sekondari, wanasoma *form one, two, three* na *form four* ndipo wanaukuta ule mtihani mkubwa wa Taifa. Vilevile vijana wale ni wengi sana na kama nilivyosoma kwenye changamoto zangu kwamba, tunayo changamoto ya maabara, upungufu wa walimu, majengo na nyumba za walimu na kadhilika, ambapo Serikali sasa imeyaona hayo na imejikita kuboresha kama nilivyosoma kwenye Mipango ya MMES kwamba; hata mwaka huu tunatarajia kuajiri walimu zaidi ya 13,000 waweze ku-cover yale mazingira ya upungufu. Pia kama nilivyosema, maabara 264 zitajengwa; mbili kila Halmashauri.

Katika swali lako la pili umependa kujua katika Mkoa wa Singida ni shule zippi zingeweza kujengewa maabara na nyumba za walimu au shule zile za mfano. Napenda kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge wote kama wanapenda kujua kwenye Halmashauri zao ni shule zippi zile mbili tutajenga, basi wanaweza wakanifuata nikawapatia. Kwa Mkoa wa Singida ninayo nakala hapa, katika Wilaya ya Manyoni ni Shule ya Itigi Sekondari na Mwanzi; Singida Vijiji ni Puma Sekondari na Ikanoda; Singida Mjini ni Dokta Salmini na Mwenge; na Iramba ni Igunduno na Lulumba. Hizo ndizo Shule za Mkoa wa Singida zitakazojengewa maabara.

**SPIKA:** Hakuna swali lingine; si mnaona lilivyokuwa refu?

## **Soko na Bei ya Zao la Kahawa**

**MHE. ASSUMPTER N. MSHANA** aliuliza:-

Mkoa wa Kagera unategemea Kahawa kama Zao la Biashara, lakini bei ya Kahawa imeshuka kiasi cha kuwakatisha tamaa wakulima wasilime zao hilo na kusababisha umaskini kwa Wananchi wa Kagera;

Je, Serikali haoni kuwa ni vyema ikatafuta soko na kuongeza bei kwa ajili ya zao hili ambalo dunia nzima hutumia Kahawa kama kiburudisho/kinywaji ili pia kuinua ari ya wakulima kuendeleza zao hilo?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Assumpter Nshunju Mshama, Mbunge wa Nkenge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kahawa ni Zao la Biashara Mkoani Kagera, linalotegemewa na wakulima wengi wa Mkoa huo. Kwa taarifa tulizonazo, bei ya Kahawa aina ya Robusta inayolimwa Mkoani Kagera, imekuwa ikipanda na kushuka siku hadi siku. Hata hivyo, bei ya Kahawa imekuwa iklongezeka kwa wastani wa kutoka shilingi 500 kwa kilo mwaka 2006/2007 hadi shilingi 950 kwa kilo mwaka 2010/2011. Pamoja na ongezeko hilo la bei, gharama za uzalishaji nazo zimekuwa ziklongezeka na hivyo kupunguza faida aipatayo mkulima.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa, mkulima wa Kahawa anapata beti nzuri, Serikali imeanza kutekeleza mkakati wa kuanzisha matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Maghala kwa Zao la Kahawa Mkoani Kagera. Faida ya matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi Ghalani ni: Wakulima kupata bei nzuri zaidi ili kushawishi mabenki kutoa fedha zaidi za kununulia mazao; kuongezeka kwa ubora wa mazao; na kupunguza gharama za ununuzi na uuzaji wa mazao na hivyo bei kwa mkulima kuongezeka. Aidha, mfumo huu unaruhusu wanunuzi kushindana katika mnada mmoja badala ya kununua mazao kiholela majumbani kwa wakulima bila kuzingatia vipimo rasi na ubora unaotakiwa.

Mheshimiwa Spika, hatua nyininge zinazochukuliwa ni pamoja na kuhamasisha usindikaji wa Kahawa kabla ya kuuza, kuanzisha masoko ya mipakani yatakayowawezesha kuuza Kahawa yao nchi jirani, kuhamasisha Wananchi kunywa Kahawa iliyozalishwa hapa nchini na kuendeleza Mradi wa Kutengeneza Kiashiria Ubora wa Bidhaa (*branding*), utakaosaidia kuongeza thamani ya Kahawa inayozalishwa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, mwisho, Serikali inampongeza Mheshimiwa Assumpter Mshama, kwa jitihada anazofanya kuwasaidia Wakulima wa Kahawa katika Jimbo la Nkenge na Mkoa mzima. Aidha, nachukua nafasi hii, kuwashimiza Wananchi kote nchini, kujunga katika Vikundi vya Vyama vya Ushirika ili jitihada zinazofanya na Serikali ziweze kuzaa matunda.

**MHE. ASSUMPTER N. MSHANA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza, napenda kuipongeza Wizara kwa jitihada inazochukua ili kuongeza thamani ya Kahawa. Naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Waziri haoni kwamba hiyo bei ya kilo moja shilingi 950 ni hela ndogo sana tukizingtaa nguvu nyangi wanayoweka Wananchi na maisha yamepanda sana kutokana na mafuta ya petroli kuwa juu sana; huoni kwamba ni vyema kuongeza bei kidogo ili Mwananchi apate kufaidika?

(b) Mheshimiwa Spika, wakati wa mtikisiko wa uchumi duniani, Wanankenge au Wanakagera kwa ujumla, walikuwa wameahidiwa kufidiwa milioni 700 kwa ajili ya kupunguza hasara waliyoipata; na kwa kuwa waliandikiwa barua kutoka Wizara ya Fedha kwamba watapewa milioni 700, lakini mpaka leo hawajapewa ukizingatia wakulima wengine wa pamba wameweza kupewa; naomba Serikali inieleze ni lini watapewa fidia hiyo? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyo sema katika swali langu la msingi, bei ya Kahawa imepanda kutoka shilingi 500 hadi 950 na sisi katika Wizara ya Viwanda na Biashara, tunakubaliana sana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, bei hii bado ni ndogo kulingana na gharama za uzalishaji. Serikali itaendeleza jitihada zote za kuongeza wigo wa sisi kuwa na uwezo wa kuingia katika masoko makubwa, kwa kupitia mchakato tuliouanzisha wa stakabadhi za maghala katika nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Serikali imejenga maghala 31, ambayo yanaingia moja kwa moja katika mtindo huu wa kuhakikisha kwamba, Zao hili la Kahawa linauzwa kwa utaratibu wa stakabadhi ya maghala na bei itakuwa nzuri kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, la pili, kuhusu fidia ya shilingi milioni 700 na kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge, kama Wizara Wizara ya Fedha ilishatoa barua utekelezaji wake ni bayana.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda umekwisha sana, naomba tuendelee, leo tuna siku fupi. Tunao wageni waliofika Bungeni kwa ajili ya mafunzo nao ni wanafunzi 50 kutoka Shule ya Sekondari ya Viwandani Dodoma; sijui wako wapi wasimame na walimu wao kama wapo. Wapo kule nyuma, ahsante karibuni sana.

Tuna wanafunzi 26 wa Kidato cha Nne kutoka Shule ya *Star Evening Class Program* Dodoma. Hawa nao wako wapi wasimame? Kwa hiyo, ni *evening classes*; haya karibuni sana mkazane kusoma.

Tuna wanafunzi 55 wa Shule ya Msingi Jenerali Msuguli Dodoma na wao wasimame walipo, aha! Ndiyo hawa, ahsante karibuni sana msome kama Jenerali Msuguli mwenyewe.

Tuna Viongozi 15 wa Kata ya Sasajila kutoka Manyoni; hawa Viongozi wako wapi? Ahsante sana, hawakuniambia ni Viongozi wa kitu gani, lakini labda wa Serikali, karibuni sana.

Tuna Watendaji kumi wa Vijiji kutoka Jimbo la Magu; hawa nao wako wapi? Karibuni sana mjifunze mambo ya Serikali huku ndani.

Kuna Makatibu Kata kumi kutoka Jimbo la Mtwara Mjini nao wasimame walipo; ahsante sana karibuni. Poleni kwa safari ndefu na mjifunze yaliyopo hapa.

Kuna wageni wengine nitawataja mchana saa hizi hawahusiani na mambo ya humu ndani.

Shughuli za kazi: Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Jenista Mhagama, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo saa saba na nusu mchana, watakuwa na kikao katika Ukumbi Namba 231.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Margaret Sitta, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo hii saa saba na robo, wakutane katika Ukumbi wa *Basement* hapo chini.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Edward Lowassa, anaomba niwaarifu Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo saa saba na robo, watakuana katika Ukumbi wa Pius Msekwa B.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Sheria Ndogo, Mheshimiwa George Simbachawene, yeye anaomba Wajumbe wa Kamati wakutane saa saba na robo katika Chumba Namba 219.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa, anaomba Wajumbe wa Kamati yake, wakutane saa saba na robo katika Chumba Namba 227.

Mwenyekiti wa Kamati ya TAPAC, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, anaomba niwatangazie wale Wajumbe wapya wote na wa zamani kwamba, kutakuwa na kikao leo tarehe 25, Agosti, 2011 kuanzia saa saba na robo katika Ukumbi wa Msekwa.

Mheshimiwa Magdalena Sakaya, yeze ni Katibu wa Wabunge wa CUF, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wa CUF kuwa, leo tarehe 25 Agosti, 2011, saa tisa alasiri, kutakuwa na kikao muhimu kwenye Ukumbi wa Basement.

Mheshimiwa John Mnyika, yeze ni Katibu wa Wabunge wa CHADEMA, anaomba niwatangazie Wabunge wa CHADEMA kwamba, saa saba na robo kutakuwa na kikao ghorofa ya pili katika Jengo la Utawala. Hii ni katika Ofisi ya Kiongozi wa Kambi ya Upinzani; wao ni saa saba na robo pia.

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo matangazo kuhusiana na kazi, halafu washabiki bado wanaendelea kuniambia kwamba, Simba wapo njiani watafika Ukumbini wakati wowote. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na shughuli inayofuata. Leo muda hautoshi, naomba mniache kabisa, tutakuwa na watu wawili tu kuchangia. Katibu, hatua inayofuata.

#### **MISWADA YA SHERIA ZA SERIKALI**

(*Kusomwa Mara ya Kwanza*)

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Biashara wa Mwaka 2011 (*The Business Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2011*)**

(*Muswada uliotajwa hapo juu ulisomwa Bungeni Mara ya Kwanza*)

#### **HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2011/2012  
Wizara ya Katiba na Sheria**

(*Majadiliano yanaendelea*)

**SPIKA:** Wheshimiwa Wabunge, kama mtakavyoona, siku zinamalizika na kutokana na mabadiliko kidogo ya ratiba tuliyoyafanya juzi kutokana na matatizo ya msiba, tumekuwa na mabadiliko mengi tu, kwa sababu lazima tumalize Bunge kesho. Kwa hiyo, leo hii watakaochangia katika hoja iliyobakia ni wale amba wamechangia mara moja na watakuwa wanenye tu. Ndivyo itakavyokuwa sasa na mpo wengi, lazima saa saba tuimalize Wizara hii. Kwa hiyo, watakaoanza kuchangia ni Mheshimiwa Muhammad Chomboh, Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, Mheshimiwa Raya Ibrahim Khamis na Mheshimiwa Sadifa Juma Khamis; hawa tu ndiyo watakaochangia.

**MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwangi wa Rehema, kwa kunipa uwezo wa kusimama mbele yako au mbele ya Bunge hili na mimi kuchangia katika Hotuba ya Waziri wa Katiba na Sheria. Kama waliviyotangulia kuchangia wenzangu, Bajeti ya Wizara hii haitoshi kulingana na matakwa na haja kubwa iliyokuwepo katika kufanikisha azma au malengo mazuri ya Wizara au Mahakama zetu kwa ujumla.

Leo nataka kuchangia zaidi kwenye rasimu ambayo tunaitegemea ya Katiba Mpya, lakini zaidi nataka kuzungumzia Hotuba au maoni ya Kambi ya Upinzani, yaliyowasilishwa na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani jana.

Msemaji wa Kambi ya Upinzani, katika maelezo mengi aliyoyazungumza, alitoa mapendekezo yake kuhusiana na rasimu inayotegemewa kuletwa kwa ajili ya Katiba Mpya. Katika mapendekezo yake alisema; naomba kunukuu:-

"Pili, Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya Rasimu ya Muswada hayakubaliki kwa sababu yanaweka mchakato wa Katiba Mpya kwenye huruma na au fadhila ya Rais wa Zanzibar na siasa za Zanzibar kwa ujumla." Hakusita hapo, alisema tena kwamba: "Mustakabali wa Taifa letu hauwezi kuwekwa tena rehani kwa siasa za Zanzibar na kwenye matakwa ya Wanzibari kwa kiasi hicho. Namwona Mheshimiwa wa Kambi ya Upinzani, anapiga makofi kwa msisitizo kwamba, anayaamini ninayoyazungumza." (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, haya maneno aliyoyazungumza kwa sisi Wazanzibari na mimi nikiwa ni mtu ambaye nimekuja hapa kuiwakilisha Zanzibar na nimechaguliwa kwa kura na Wananchi kuiwakilisha Zanzibar; hii ni dharau na kejeli na ufedhuli. Sasa basi nataka kumfahamisha Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Tundu Lissu, ye ye pamoja na wengi waliokuwepo humu ndani, wenge mawazo mgando kama ye ye na waliokuwepo nje ya Jumba hili; Zanzibar siyo koloni la Tanganyika na haitakuwa hata siku moja koloni la Tanganyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Tundu Lissu, tarehe 7 mwezi wa nane, alizungumza kuhusiana na mambo ya Muungano wakati wa kuchangia Hotuba ya Muungano. Alijaribu kuwataja Viongozi ambao aliwatajaa ye ye kwamba ni *victim* wa Muungano, ambapo ni mwongo na ni mnafiki. (*Makofi*)

Hawa watu aliowazungumza mimi niliwaona, kwa sababu Muungano wakati ukiundwa mimi nilikuwa hai na akili zangu. Bahati mbaya, Mheshimiwa Waziri alisema kwamba, hakuwaona na hawakuhusika kabisa na suala la Muungano. Kwa hiyo, nataka kumfahamisha kuwa, Wazanzibari hawatakubaliana na mpuuzi ye yote au upuuzi wowote unaozungumzwa kwa minajili ya kutugombanisha sisi. (*Makofi*)

## KUHUSU UTARATIBU

**MBUNGE FULANI:** Kuhusu utaratibu.

**SPIKA:** Mnakaa chini halafu nitawaita mmoja moja. Kwanza, Mheshimiwa nakuomba unapochangia toa mawazo yako, kwa sababu mkianza kutupiana madongo namna hii, mwisho wake hatutakuwa tumelewa tulikuwa tunasema nini. Hoja inakuwa haipo. Toeni hoja nzito, halafu zitajadiliwa na wanaowasilikisha. Nawaombeni hivyo. Kwa hiyo, Mheshimiwa toa hoja nzito halafu zitajibiwa. Mkianza kutukanana na kufanya nini, hiyo siyo nafasi ya Bunge. (*Kicheko/Makofi*)

**MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH:** Ahsante Mheshimiwa Spika.

**SPIKA:** Toeni hoja nzito zitajibiwa. Tunaendelea. Toa hoja nzito.

**MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH:** Ahsante Mheshimiwa Spika. Kwa taarifa tu ni kwamba, sisi Zanzibar sisi tuna uzoefu sana wa Siasa ya Vyama Vingi na Chaguzi za Vyama Vingi; ilianza toka miaka ya 1950 na tumepiga hatua ambayo ni mfano kwa Afrika. Hatukuanza leo, tumepita kwenye Vyama Vingi, Chaguzi za Vyama Vingi na tumefika hadi hayo Mapinduzi mnayoyaona sasa duniani, sisi Zanzibar tulipindua mwaka 1964. (*Makofi*)

Kwa hiyo basi, tumekaa na tumeyaona na tukasema sasa basi. Sasa chokochoko zote ambazo zinakuwa zinakuja kwa maslahi au kwa maana ya kutugombanisha, sisi hatukubaliani nazo. Zanzibar ni nchi ambayo ilikuwa ina haki yake kamili katika Umoja wa Mataifa na tukakubaliana na wenzetu wa Tanganyika kwa maslahi yetu sote tuungane na tuna imani hiyo na tunakubaliana hivyo. Sasa kwa maoni yako wewe au maoni ya mtu mwingine ye yote atakayesema ye ye kwamba, Zanzibar, Rais wa Zanzibar iletewe tu ushauri; haukulaliki ikiwa hakuna hata siku moja ambayo Zanzibar itashirikishwa kwenye mchakato wowote unaohusiana na masuala ya Muungano kuanzia chini mpaka juu.

Sisi Wazanzibari tuna msemo na msemo huo aliusema Rais wa Kwanza, Mheshimiwa Sheikh Abeid Aman Karume kuwa, Mwisho Chumbe. (*Makofi*)

Wazanzibari wanalelewa hili. Mwisho Chumbe. Sasa basi, wa leo inakuwa hawajui mwisho wa ujumbe, nawafahamisha sasa. Ukienda Zanzibar kwa kuitia baharini, kuna kisiwa kimoja kinaitwa Chumbe. Kwa hiyo, upuuzi wote, upumbavu wote unaotoka kwingine, usitokee Zanzibar, hautafika pale tunausimamisha Chumbe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ...

#### KUHUSU UTARATIBU

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu.

**SPIKA:** Naomba aendelee kujadili. Waheshimiwa Wabunge, kila mtu awe na uvumilivu. (*Kicheko/Makofi*)

**MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH:** Mheshimiwa Spika, mimi nataka kuwaambia Wazanzibari kokote kule wanakotusikiliza, sisi Viongozi wenu mliotuchagua tupo imara, tutaitetea Zanzibar mpaka tone la mwisho. Tu hakikisha kwamba, haki zetu zote za Muungano zinapatikana na tuna imani ya Muungano asilimia mia kwa mia. Kwa hiyo basi, tunataka kuwafahamisha Watanzania wenzetu kuwa, Wazanzibari nia yetu ni Muungano. Isitokee udogo wetu mkaudharau kwa sababu tu ya maslahi ya kikundi fulani au watu Fulani; hatukubaliani nao. (*Makofi*)

Wazanzibari wanakwambieni aliyetamka maneno haya ni Mheshimiwa anaitwa Tundu Lissu. Ninyi Wazanzibari mnafahamu maana ya maneno haya; Tundu Lissu mnafahamu. Kwa hiyo, hamna sababu ya *ku-panic*; ni wajibu wenu kutilia maanani tu aaah kumbe Tundu Lissu tumefahamiana. Wazanzibari tulieni, viongozi wenu tuko madhubuti na tutaitetea nchini yetu mpaka tone la mwisho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, Mungu ibariki Tanzania. Naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

**SPIKA:** Washa moja.

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Kwanza, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu. Pili, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii leo na mimi niweze kuchangia. Leo nitajikita katika mambo matatu; jambo la kwanza ni Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Kivuli wa Katiba na Sheria, ukurasa wa 29. Jambo la pili ni utoaji wa haki na jambo la tatu ni kuhusu Katiba yenewe.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nimpongeze Mheshimiwa Chomboh, amefafanua kwa kina na namwunga mkono mia kwa mia. Nitanukuu maelezo ya Mheshimiwa Waziri Kivuli wa Katiba na Sheria kama ifuatavyo; naomba uniruhusu: "Mustakabali kwa Taifa letu hauwezi kuwekwa tena rehani kwenye siasa za Zanzibar na kwenye matakwa ya Wazanzibari kwa kiasi hicho. Kambi ya Upinzani inapendekeza kwamba, Rais wa Zanzibar ahusishwe tu katika mambo ya Kikatiba ambayo ni ya Muungano tu. Nje ya masuala hayo, Rais wa Zanzibar hana sababu yoyote kuhuishwa na mchakato wa Katiba kuhusu mambo ya Tanzania Bara." (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Kivuli wa Katiba na Sheria, nadhani haelewi nini maana ya Taifa. Amesema mustakabali wa Taifa letu hauwezi tena kuwekwa rehani; mustakabali wa Taifa. Kwa hiyo, Mheshimiwa huyu haelewi nini maana ya Taifa. Nadhani haelewi nini maana ya historia ya Zanzibar. Kwa maana hiyo basi, mwelekeo wa Kambi ya Upinzani umepotea njia. (*Makofi*)

Nadhani haya ni maoni yake. Unaposema Rais wa Zanzibar atolewe katika mambo ambayo si ya Muungano una maana gani? Je, kuna Serikali ngapi hapa? Kuna Serikali ya Tanganyika? Ipo Serikali ya Tanzania ambayo ni ya kujadili mambo ya Tanganyika; iko wapi? (*Makofi*)

Huyu ni msomi, sijui huyu ni Wakili, atawawakilisha hao wateja wake. Mheshimiwa Waziri, unapomtaja Rais wa Zanzibar kumwondoza kwenye Katiba unaiondoa Serikali ya Zanzibar; Serikali nyingine ipo wapi hapa? Kesho huyu atasema Wazanzibari tokeni kwenye Bunge wakati wa kujadili mambo ya Tanganyika. Mambo yako wapi?

Iko wapi Bajeti ya Tanganyika hapa? Unazungumza nini? Ana mwelekeo gani huyu? Anawagawa Wazanzibari na Watanganyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nazungumza hili kwa uchungu kabisa, msomi lakini sijui amehitimu vipi usomi wake. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa tusianze malumbano hapa, uvumilivu ndiyo unahitajika humu ndani. (*Kicheko/Makofi*)

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, nasema kwamba, Zanzibar ina madaraka kamili ya kushiriki masuala yote ya Muungano na yasiyokuwa ya Muungano kwa mujibu wa Katiba. Jambo la msingi ni kuimarisha Taifa letu liwe na nguvu, lenye utawala bora, lenye utawala wa haki na misingi ya uwajibikaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mawazo haya ya Mheshimiwa Waziri Kivuli wa Katiba na Sheria ni mawazo finyu, yamepitwa na wakati na hayatapewa nafasi. Mataifa yenye nguvu ni mataifa yenye kuungana. Hivi sasa Jumuiya ya Afrika Mashariki inaendelea vizuri na kipindi kifupi tutakuwa na sarafu moja. Leo Mheshimiwa unaturudisha tugawanyike Wazanzibari na Watanganyika. Nadhani haya ni mawazo yake si mawazo ya Kambi ya Upinzani na infaa awaombe radhi Wazanzibari. (*Makofi*)

Hii ni aibu na fedheha. Nasema hivi lakini siupingi Upinzani. Lazima Kambi ya Upinzani ioneshe mipango mizuri, kujenga Taifa letu na ili kushindana na mipango na Chama cha Mapinduzi iwe bora na siyo kuleta mgawanyiko ndani ya Bunge hili. Baada ya kusema haya, naendelea na hoja yangu ya pili ya utoaji wa haki.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la msingi kwa kila jamii; jamii inayokosa haki ndani yake kutatokea migogoro. Nasema hivi kwa sababu Jamii ya Waislamu wa Tanzania Bara, wanapoteza haki zao kila siku. Nasema hivi kwa sababu katika Tanzania Bara hakuna Mahakama wala chombo chochote kinachosimamia haki za Waislamu. Waislamu wana Sheria zao za ndoa, wana Sheria zao za Mirathi na wana Sheria zao za huduma za watoto. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mahakama hii ya Kadhi ipo Uingereza, Uganda, Kenya, Afrika Kusini, ipo Zanzibar na Tanganyika ilikuweko hadi mwaka 1963. Suala gani liliofanya Waislamu wakose haki zao za msingi kabisa? *Law of Marriage Act* ya Mwaka 1971 ndiyo inayowafanya Waislamu wapoteze haki zao katika hali hii. Nasema kifungu cha 13 kina mgogoro na Sheria ya Kiislamu; kifungu hiki kinasema umri wa mtu kuoaa usipungue miaka 18 na kuolewa kusipungue miaka 15.

Sheria ya Kiislamu inasema kwamba, mwanamke akivunja ungo na mwanamume akibalehe wanaweza kuoana. Siyo Sheria hii. Kuhusu talaka, imekuwa na mgogoro mkubwa sana, mume hawezikutoa talaka kwa mujibu wa Sheria hii. Kuna kesi moja ya Abdallah Saidi dhidi ya Mwanamkuu Yussuf ya mwaka 1978, *Tanzania Law Report* Nambari 43. Mwanamume hapa alitoa talaka tatu kwa pamoja kumwacha mke wake, lakini Mahakama kupitia Kaimu Jaji Samata aliikataa; alisema lazima kuwe na mambo matatu muhimu: Jambo la kwanza wale wameoana kwa utaratibu wa Kiislamu. Jambo la pili, waende katika Tume ya Usuluhishi na wahakikishe kuwa wameshindwa kutaka kusuluhisha. Tatu, kuwe na jambo au kuwe na kitu kinachovunja ndoa. Kwa hiyo, Sheria hii haizingatii uvunjaji wa ndoa. Inazingatia kipi na jambo

lipi? Uwe mwenda wazimu, umefungwa muda mrefu, ni mkatili na mambo mengine. Hayo ndiyo yanavunja ndoa. Hii siyo Sheria ya Kiislamu.

Mheshimiwa Spika, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, atakuwa anawajibika kuhusu haki zote za Waislamu zinazopotea na atajibu kesho kwa Mwenyezi Mungu. Ili kumsaidia Mheshimiwa Rais, tunamwomba Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Katiba, aje atupe kauli rasmi ya Mahakama ya Kadhi Tanzania Bara. Kama hakutoa jibu rasmi, kipindi kijacho natoa ahadi kwa *Lailaha ilallah Muhamadan Rasulullah* kwamba, nitaandamana na Waislamu wote mnisikie hivyo; tunataka Mahakama ya Kadhi isimame kwa sababu hakuna sababu kwa nini Waislamu wapoteze haki zao kila siku. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, watu wanazini chini ya Sheria hii. Kifungu cha 160 kinasema kwamba; mtu yoyote amekaa mke na mume ikifika miaka miwili na zaidi wanaonekana hawa ni mke na mume. Sasa Sheria hii inasemaje? Mnawafunza nini Waislamu; wazinishwe bure? Sheria hii inasema kwamba, itatoka talaka kama Mahakama haijathibitisha, basi talaka inaendelea; ni kusema kwamba, hawa watu wanaendelea kuzini na kuzaa watoto ambao siyo halali. Masuala yote haya atayabeba Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tumwondoleeni mzigo huu, hatujui atakufa lini. (*Makofii*)

Huyu ni binadamu, hakikisheni jamii hii inapata haki zake na kama haikupata Tanzania hapatakalika, nasema hivyo. Imefika mwisho sasa hatustahmili tena; lazima Waislamu wapewe chombo cha kusimamia haki zao na kulinda haki zao za mirathi, ndoa na kutunza watoto.

Mheshimiwa Spika, baada ya haya, siungi mkono hoja. (*Makofii*)

**MHE. RAYA IBRAHIM KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia katika hotuba ya bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria. Kwanza kabisa, katika mchango wangu nitakuwa na mambo machache ambayo nahisi yatakuwa na uzito mkubwa katika bajeti yetu na katika Wizara yetu.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti hii ama tunasema kwamba, kama ilivyo katika Katiba ina mapungufu, ni kama vile vile ambavyo tunaona katika Sheria zetu nazo zina mapungufu yake. Mfano, katika *Civil Procedure Code*, katika *Order Number One (1)*, kuna Kipengele kinachomtaka mtu katika Mahakama ya Mwanzo kwamba, hatakuwa na Wakili ye yeyote ambaye *ata-appear* kumsimamia ama kusimama kumsemea kwa niaba yake. Kama ilivyo, tunaona Watanzania wengi ambao wana kesi wanashindwa kupata haki zao, wanashindwa kujua ni nini ambacho wanatakiwa wapate kwa kutokujua Sheria na hakuna msaada wowote ambao unatolewa na Wizara hii kwa wananchi ambao hawajui Sheria, katika kuwasaidia kupata haki zao ama kutambua ni nini ambacho wanatakiwa wakipate. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, cha kusikitisha zaidi ni kwamba, katika Mahakama za Mwanzo, kumekuwa na mrundikano mkubwa sana wa kesi. Kumekuwa na mambo mengi ambayo yangetafutiwa ufumbuzi ama Mawakili wangkuwa wanawakilisha *ma-client* wao katika zile Mahakama, nadhani kusingkuwa na mrundikano wa kesi, kusingkuwa na dhuluma katika kutafuta haki za Watanzania wenzetu. Vile vile hili suala pia Waziri Mkuu, nashukuru kwamba aliliona na katika Mkutano uliokuwepo Arusha, alilizungumzia akasema kwamba, kuna haja ya kufanywa *amendment* katika Kipengele hiki ili kuwe na Mawakili ambao watasimamia watu katika kesi zao. Kwa hiyo, kama ni hivyo tunataka Serikali ifanye haraka kusaidia hivyo ili wananchi nao wawe wanapata haki zao kwa kuwekewa Mawakili katika Mahakama za Mwanzo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vile vile ningependa nichangie katika suala zima la Mgombea Binafsi. Kama tunavyojua kulikuwa na kesi ya Mtikila *versus Republic*, ilikuwa inahusiana na suala zima la Mgombea Binafsi; suala hili ni kwamba, limewaweka watu katika mikinzano ya hapa na pale kwa kutokujua kwamba, ni haki ipi, ni kitu gani ambacho kinavunjwa. Kama tunavyoona sasa tunaelekea katika mchakato wa kutengeneza Katiba Mpya, kuweka Katiba Mpya, sasa tulikuwa tunataka hili suala nalo la Mgombea Binafsi lishughulikiwe, ni vipi litashughulikiwa? Kwamba, katika *issue* ya Mgombea Binafsi, kumezungumziwa suala la kwamba, hii kesi iko katika Mahakama ya Rufaa, walichokisema ni kwamba, katika Katiba inasema kwamba, mgombea ye yote wa Urais

Iazima awe na chama. Kwa hiyo, kutokana na hivyo wakasema kwamba, hili suala watakuwa wamekwendwa kinyume na Katiba ya nchi. Na kwamba, wameenda kinyume na Katiba na sasa tunaelekea katika mchakato wa Katiba, tunaomba hili suala liingizwe na liangaliwe, kwa sababu sio wote watakuwa wanagombea watakuwa na vyama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vile vile katika suala hili la Mgombea Binafsi ni kwamba, walivyotoa katika *Court of Appeal* wakasema kwamba, hili suala tunaliachia liende Bungeni; kama kawaida hapa Bungeni kunakuja Miswada mingi, kunakuja mambo mengi, aidha yawasilishwe na Mbunge, yaletwe na Kamati ama yaletwe na Serikali. Lakini kwa tulivyozowea ni kwamba, mambo mengi yanaletwa kutoka Serikalini. Kama ni hivyo basi, tunataka Serikali ione umuhimu sasa wa kulifanya hili suala uharaka zaidi ili liingizwe katika Serikali, liletwe hapa Bungeni, tulijadili na kumpa Mtanzania haki ya kugombea bila ya kuwa na chama. Kwa sababu, katika Katiba hiyo hiyo ambayo inasema kwamba, mtu anatakiwa awe na chama ndiyo agombee; vile vile Katiba hiyo hiyo inatamka kila mtu ana haki ya kupigiwa kura na haki ya kuwa kiongozi. Kwa hiyo, tunaona kwamba, tutakopompa haki hii, unamnyima hii. Kwa hiyo, marekebisho ya Katiba yashughulikiwe yafanywe haraka ili kuliwezesha hili suala na Watanzania kwa ujumla. Wengi wanataka kuingia kwenye siasa, wengi wanataka na wao kuwa wagombea bila ya kuwa na chama, lakini tunaona kwamba, hicho kipengele kinawanyima hiyo haki ya kutaka kuwa na chama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vile vile ningependa nzungumzie suala zima la *Legal Aid*. Katika Mahakama zetu ama katika *Civil Procedure Code* hiyo hiyo, inazungumzia kwamba suala la *suit by a poor person*, kwamba mtu maskini anaendesha mashtaka yake katika Mahakama, kuna taratibu ambazo Serikali ama Mahakama inatakiwa ifuate ama mtu anatakiwa afuate, ambaye ni maskini anataka kuendesha mashtaka yake, anataka kupata haki yake katika Mahakama na yeze ni maskini, hana pesa ya kusimamiwa na mtu na ya kumlipa. Kwa hiyo, kuna taratibu ambazo inapaswa mtu azifahamu katika kupata haki zake kuititia suala la kushtaki, lakini cha kusikitisha ni kwamba, katika hizo Sheria zetu, zipo katika masuala mazima ya *Criminal Matters*, ambapo katika hizo *Criminal Matters* ni zote ambazo zina *Capital Punishment*, ndio ambayo yanawekewa mtu kuwa na Wakili ambaye atalipiwa na Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vilevile kuna Watanzania ambaeo leo hii wanashindwa kujua haki zao, wanashindwa kutambua ni nini wanahitaji kwa kukosa kujua ni *process* gani, ni *procedure* gani wanatakiwa wazifuate, yaani wao ni maskini na wanataka wapate haki zao! Lakini tunaona kwamba, hili suala linafichwa, hii nafasi inatumiwa na watu wachache ambaeo wanazijua Sheria, ambaeo wanazijua haki, wanakuwa wachoyo kuwaambia Watanzania wenzao ni vidi mtu maskini anatakiwa aendeshe mashtaka yake, aendeshe kesi yake bila ya kulalamika kwamba, hana pesa wakati Serikali ipo na ina Sheria ambayo inataka Serikali itoe kiasi fulani kwa mtu.

Mheshimiwa Spika, mfano mzuri, Marekani wenzetu katika Sheria zao, hili suala wameliingiza pia katika *Civil Matters*, lakini kwetu tunaona kwamba lipo katika *Criminal Matters* peke yake, kwa hiyo, tunataka kwamba, Waziri mhusika katika Sheria zetu, katika mambo ya kufanyiwa *amendment* na hili nalo tunataka liingizwe lifanyiwe *amendment* katika masuala ya *Civil Matters*, Serikali nayo ione umuhimu wa kuwasapoti hawa watu masikini. Kama ilivyowekwa katika *Criminal Procedure Code* kwamba, mtu maskini Serikali inatakiwa imsapot i katika kuendesha kesi yake, kwa hiyo, tunataka tuone Serikali inakuwa *active*, tunataka kuona Waziri, hii Sheria inafanyiwa *amendment* kuwasaidia Watanzania wote ambaeo ni maskini, wanashindwa kupata haki zao, wapate haki zao kwa kusaidiwa na msaada kutoka kwa Mawakili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vile vile, ningependa nzungumzie suala zima la bajeti katika Wizara hii. Wizara hii tunaona kwamba, bajeti yake, yaani Mahakama kama Mahakama, tunaona kuna matatizo mengi, kuna mambo mengi. Mfano mzuri, kuna kesi ambayo toka *decision* imetoka, *judgement* imetoka, huu ni mwezi wa nne! Mtuhumiwa yupo ndani, wanasubiri ile *judgement* wakakate rufaa, wanashindwa kukata rufaa! *Judgement* imeshatoka, upande umeshinda, basi watoe ile hukumu ili Wakili wa ule upande wa pili afuate *procedure*, afuate *process* zote za kumtoa huyu mtu ndani. Huyu mtu anaendelea kuwa ndani ya kifungo wakati *decision* imeshatoka, Mahakama inachelewesa kutoa hukumu yake! Ni kwa nini, inachelewesa kutoa hukumu? Kutokana na bajeti nzima kuwa finyu; unakwenda leo unaambiwa hakuna umeme, unakwenda unaambiwa hakuna karatasi! Bajeti ni mbovu, bajeti ambayo inapelekea kwa mfano,

katika Mahakama ili ijendeshe inahitaji bilioni 52, lakini katika bajeti yetu tunaona kwamba kuna bilioni tisa peke yake ambazo hazitatosha katika Mahakama kufuatilia shughuli zake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama tunavyosema tunatakiwa tuwe tuna haki, tunatakiwa tuwe na viongozi ambao ni wazuri, tutoe haki kwa watu wetu na sio mambo mengine zaidi ya kutoa haki, mbali na kuongeza bajeti katika kusaidia suala zima la watu waendeshe kesi zao vizuri na wapate hukumu zao kwa wakati. Kwa sababu, tunaona kwamba hukumu zinachelewa, watu wanachelewa kupata hukumu zao kwa wakati na wanaendelea kuteseka. Pia katika suala hilo hilo kwamba, *security* kwa Mahakimu katika bajeti, kama ingekuwa ya kutosha basi hawa Mahakimu wetu wangekuwa na *security* ya kutosha! Kwamba, wanakosa *security* nzuri kwa sababu bajeti haitoshi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo hii unakwenda Mahakamani unahukumiwa, labda ndugu yako akakae jela miaka kadhaa; ndugu yako anahukumiwa kifo, ndugu yako anahukumiwa chochote; Jaji yule unaishi naye jirani, ambapo mazingira hayamuweki katika ulinzi wa aina yoyote yule Jaji, Jaji huyo hana tuseme labda posho au kitu chochote ama tuseme mshahara wake uboreshwe mishahara ya Mahakimu wetu. Mishahara yao haiwatoshelezi, wanaishi katika mazingira magumu, kazi wanazofanya ni nzito, ambazo wao katika mazingira magumu wangekuwa na *security* nzuri, wasingegekuwa na maisha ya kuhofia, mtu unafanya kwa hiyo *sometimes* inamlazimu Hakimu kuchukua rushwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunalalamika rushwa, lakini kwa upande mwagine sisi ndio chanzo ama bajeti ni chanzo kwa Mahakimu wetu kuchukua rushwa. Kwa hiyo, wanachukua rushwa, sio kwamba wanapenda, mazingira ambayo wanakaa ni magumu, kazi wanafanya katika mazingira magumu, mazingira hatarishi ambayo yanawahatarishia maisha yao na familia zao. Mtu hana *means* inabidi afanye vile ambavyo anaona itakidhi. *Sometimes* anakuwa anaangalia huyu ni jirani yangu ama ni ndugu yangu, kwa hiyo, anakuwa na *bias* katika kufanya maamuzi katika kesi, ambavyo si Sheria na haki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo ningependa niligusie ni suala zima la *Clawback Clause*. Yaani inakuwa kwamba, unapewa haki na mkono wa kulia, inanyang'anywa na mkono wa kushoto! Kama tunavyojuu kuna mapungufu mengi katika Katiba, kuna mapungufu mengi pia katika Sheria zetu, mfano, kwenye Katiba, Ibara ya 14, inakwambia kila mtu anayo haki ya kuishi, hapo hapo unaambiwa kwamba mtu anapokuwa Mahakamani kuna Sheria ambayo inampa mtu *death penalty*, kwa maana hiyo huku unapewa haki ya kuishi *at the same time* ile haki inapokonywa katika Sheria. Kwa hiyo, tunataka hili suala liangaliwe zaidi ili kusiwe na mambo ya kinafiki, kusiwe na mambo ambayo hayaeleweki. Tunajitahidi, tunasema kwamba, Katiba yetu inamtetea Mtanzania, kila Mtanzania ana haki ya kuishi, kila Mtanzania ana haki ya kufanya hivi! Wakati huo huo tulijisahau kwamba, zile Sheria tulifanya *copy and paste*, kutoka kwa wenzetu ambao wanaendana na Katiba zao na sisi kwetu inakuwa tofauti. Kwa hiyo, zaidi tulikuwa tunataka hilo liliwe mkazo na kufanyiwa kazi zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika kutilia mkazo zaidi narudi tena katika lile suala nililosema, nilikuwa nakimbizia muda, sikutoa maelezo ya kutosha, kuhusu suala zima la *Criminal Matters*, kwamba Serikali inakosa kutoa mtu wa kumsimamia mtu maskini katika kesi zake; tunajikuta kwamba, Serikali inapokuwa katika *Criminal Matter* ambayo ina *Capital Punishment*, inatolewa kutoka *Tanganyika Law Society* na *Legal and Human Rights Centre*, ndio ambao wanakuwa wanasmamia. Lakini kwa upande mwagine Serikali inakusanya kodi! Kwa nini isisimamie masuala haya katika *Civil Matters* na kujitoa na kuwaachia *Tanzania Law Society* na...

(*Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji*)

**SPIKA:** Ahsante, muda umekwisha. Mheshimiwa Sadifa Khamis.

**MHE. SADIFA JUMA KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Nami niungane na wenzangu kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhana Wataallah*, kwa kutuwezesha kuweza kufika hapa na kujadili mambo yetu kwa namna ambavyo tunaweza.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimpongeze Wazira wa Wizara hii na watendaji wake kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya, kwa kutekeleza majukumu ambayo wamepewa. Kwa upande wangu nitajikita katika *issue* ya *School of Law*, mchakato wa Katiba na kuna mtu alisema hapa Urais wa Kifalme, namna ambavyo unaathiri uhuru wa Mahakama na nyine nyinginezo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, lakini nikianza na *issue* ya *School of Law*, nataka niseme kwamba, Wizara ingeangalia tena namna gani ambavyo itaweza kuwaendeleza hawa wanafunzi ambao wanasoma Sheria. Kwa hivi sasa sisi ambao tumesoma Sheria, wengine tumesoma kwa muda wa miaka minne, wengine mitatu, bila ya msaada wowote! Kuna wengine wanasoma sasa hivi *School of Law* pale, hawana msaada wowote! Kwa hiyo, nipongeze Serikali kwa kuanzisha hii *School of Law*, lakini kwa upande mwingine, hebu tuangalie ni namna gani ambavyo tutawasaidia hawa. Kama tungeweka, kwa mfano, mfumo mmoja labda kwa vyuo vyote, kama ni wale ambao wanasoma miaka mitatu na wale ambao wanasoma miaka minne, ikawa ni mfumo mmoja, labda ni miaka minne lakini sasa wale wakawa wote kwa mfano ule mwaka wa mwisho basi ndio *School of Law* yenye! Basi nahisi ingekuwa nzuri, chini ya udhamini au usaidizi wa hii Bodi ya mkopo. Kwa maana hiyo, Bodi ya Mikopo sasa ile Sheria tulite hapa Bungeni ili tuifanyie kazi ili na wao hawa waweze kusaidiwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nije katika *issue* nyine hii ya mchakato wa Katiba Mpya, kutokana na muda itabidi nizungumze kidogo. Ukweli ni kwamba, naipongeza Serikali, nampongeza sana Mheshimiwa Rais, kwa kuwa msikivu, kuwasikiliza wananchi wa Tanzania ni nini ambacho wanakihitaji, kwa hilo, naipongeza sana Serikali. Lakini kwa upande mwingine tuangalie sasa namna gani ambavyo wale wananchi wengine hasa wanaoishi vijiji na wao *at least* wapate taaluma ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, ukienda vijiji huko mwananchi ukimwambia kuhusiana na Katiba, yaani sijui anajua ni kitu gani! Hajui chochote kuhusiana na *issue* ya Katiba! Kwa hiyo, Wizara tungeangalia ni namna gani ambavyo tutaweza kuwasaidia hawa wananchi wetu ili waweze kupata taaluma. Katiba inauzwa 5,000/=, sifirkii kama mwananchi wa kijiji huko atatoa 5,000/= aende akanunue Katiba badala ya kwenda kununua mchele akala na watoto wake. Hebu tuangalie namna ambavyo tutawasaidia ikiwemo kupunguza bei, hata hizi Katiba zenyewe kwa sababu, sasa tuko katika *transition period*.

Mheshimiwa Spika, nije pia kwa upande mwingine, suala zima la ushirikishwaji wa wananchi wa Zanzibar. Kuna Mheshimiwa mmoja hapa, ambaye jana alizungumza, ukweli ni kwamba nataka kusema amevunja hata hii Katiba yenye. Kwa sababu, ukiangalia Ibara ya 8 na ya 9, cha Katiba hii ya Serikali ya Jamhuri ya Tanzania, basi inamtaka mwananchi ashiriki ipasavyo katika kutoa maamuzi mazito yanayohusu nchi hii ya Tanzania. Sasa ukiniambia mimi Mbunge, ambaye natokea Zanzibar, nisishiriki ipasavyo katika maamuzi mazito ya nchi, nasema hukunitendea haki! (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninachotaka kusema hapa, ni lazima tuwatendee haki wananchi, *regardless* kwamba, huyu anatoka Zanzibar ama anatoka wapi. Tukumbuke kwamba, mfumo wetu wa sasa hivi huu tulionao wa Serikali mbili, ni mfumo wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais huyu, ni Rais wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa maana hiyo, anatutumikia sote! Kama kungekuwa na Serikali ya Tanganyika, nadhani hata Mheshimiwa Tundu Lissu, kama kuna uwezekano basi angefanya hivyo; sisi tusingeingilia na mimi sina haja ya kuingilia mambo ya Tanganyika! Ukimwambia kwa mfano, Rais wa Zanzibar, asishirikishwe ipasavyo katika hili! Rais wa Zanzibar, hana sababu ya kusema kwamba, labda awaingilie katika mambo ya Tanganyika! Nasema tuwatendee haki, sisi tumeungana, tumekubaliana, lazima tukubaliane na lazima tuwe wavumilivu katika kujenga Taifa letu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, tulipoungana hatukuangalia ukubwa ama udogo wa Zanzibar! Hatukuangalia ukubwa wa Tanganyika ama kwa sasa hivi tunaita Tanzania Bara. Hii naifananisha na kusema kwamba, mtu anapooa mke huwa anaangalia tu huyu mtu ana sifa ninazozitaka! Haangalii kwamba huyu, samahani sana, ana makalio makubwa ama ana makalio madogo! Haangalii kwamba, huyu ni mrefu au ni mfupi! Anaangalia vigezo vyake anavyovihitaji, naomba

sana kama tumekubaliana basi tukubaliane na tuvumiliane; isifikie mahali sasa sisi wengine ambaa tumekaa kimya hapa tukaanza kuchokonolewa kidogo kidogo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tunawaheshimu sana na naheshimu maamuzi ambayo huwa yanatolewa hapa. Nasema umefika wakati sasa wengine tuzungumze, Mheshimiwa Tundu Lissu, nimekuwa nikimfuatilia sana katika hizi *speech* zake; nasema Wazanzibari tumechoka kupumbazwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie *issue* nyininge. Jana alizungumza Urais wa Kifalme na Uhuru wa Mahakama. Nadhani Mheshimiwa Tundu Lissu, haelewi maana ya ufalme, nini maana ya ufalme haelewi! Rais wa Tanzania, anapatikana kwa mujibu wa Katiba. Ufalme unapatikana kwa kurithishana ukoo! Rais wa Tanzania, anachaguliwa, sisi tunafanya uchaguzi kila miaka mitano hapa! Au kuna ufalme humu ndani? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Rais anamchagua Jaji kwa mujibu wa Ibara ya 109 ya Katiba; anamchagua Jaji baada ya kufanya *consultation with Judicial Service Commission*. Halafu pia vile vili baada ya hiyo anazingatia sifa maalum, kuna sifa, hebu mwambieni Mheshimiwa angalie Katiba na asome vizuri, kuna vipengele pale vimeweka sifa wazi kwamba huyu anastahiki kuwa Jaji au anastahiki kuwa Hakimu. Kwa mfano, Mheshimiwa Kikwete mtoto wake yule Ridhiwani Kikwete ni Mwanasheria mbona hakumteua kuwa Mwanasheria Mkuu hapa, Mwanasheria Mkuu ni Jaji Werema, yule pale anatokea Tarime. Lakini nataka kusema kwamba suala la ufalme, katika nchi yetu sisi halipo, kama lipo basi inawezekana kuna taasisi yake binafsi anayioilewa yeye. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ukiangalia utawala wa kifalme hauwezi kuweka utaratibu wa kumwondoaa Rais, lakini sisi hapa ukiangalia Article 46(a) tumeweka pale mfumo mzima Rais wetu namna gani ambavyo anaweza kuondoshwa, sasa mfalme gani atakayeondoka yeye mwenyewe. Sifikiri kwamba, naona hili neno basi angeliondoa aweke neno lililokuwa sahihi na haiwezekani Mheshimiwa Rais kumtoa mtu kama alivyosema hapa, nje ya vigezo vy a sheria hata kama halazimiki kufuata ushauri wa mtu ye yote lakini *he is duty bound* kuchagua mtu mwenye sifa, *degree* ya sheria, siyo vingine vinginevyo. Kwa hiyo, kama linatumika hili ni katika taasisi nyininge huko, ambazo ni za kwake binafsi asituletee hapa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niongezee suala la elimu kwa Majaji na Mahakimu. Ni ukweli usiopingika kwamba Majaji wetu, Mahakimu wetu wanahitaji kuendelezwa. Niwashukuru na niwapongeze Serikali, wameliweka hili sasa isiwe kimaneno na kimaandishi, vitendo ndiyo tunavyohitaji. Vijana wetu wanataka kusoma ili Taifa letu lifikie pale ambapo tunapopahitaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niongezee suala lingine, suala la mishahara na posho. Ni ukweli usiopingika kusema kwamba Majaji wetu na Mahakimu wetu wanateseka sana, ukiangalia tathmini ya hawa Majaji wetu wale pale wote utawaona wana kibiongo, hivi wameinama kwa kusoma sana kuangalia namna gani watawatendea haki wananchi. Wengine ukiwaangalia miguu yao myembamba huku chini, kwa jinsi namna gani wanavyoteseka, lakini ukiangalia malipo yao ni kidogo kweli. Mishahara, posho ni kidogo kweli yaani nataka kusema kwamba, hana ile *certainty* ya maisha yake. Nawapongeza kwa namna ambavyo tunavyowasaidia, lakini naomba tuliangalia tena kwa jicho la huruma, tuangalia na wao ili wapate *morality* ya kufanya kazi. Ukiangalia posho kwa mfano, wana posho mbili, posho ya mavazi, lile koti akiwa Mahakamani lakini posho ya nyumba, nazo pia ni kidogo.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuwapa lakini sasa tuwaongezee ili ifikie kile ambacho tunachokizungumza, maana utasema Jaji anakula rushwa, sijui Hakimu anakula rushwa, lazima ale rushwa, ukimwangalia Mheshimiwa Jaji wa sasa kwa mfano, mimi Mbunge ambaye nimeingia juzi nina afadhali, lakini yeye hata uwezo wa kumuoa mtoto wa Kizungu hana. Eeh! Kwa hiyo hebu tuwawezeshe, wanaweza, tukiwawezesha. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, niongezee suala lingine la haki za binadamu. Suala la haki za binadamu ninalotaka kulizungumza hapa, hususan wafungwa kule gerezani, naona sheria zetu hizi

sasa zimefikia wakati tuzilete hapa tuzibadilishe, zile ambazo zinastahiki tuzifanyie kazi ili nao wajisikie kuwa ni binadamu. Kwa mfano, ukiangalia katika ile Katiba, *bill of right*, mahabusu ama mfungwa tunaambiwa kwamba ile *right to life*, lakini kule magereza ni kinyume na hiki ninachokizungumza. Mfungwa ama mahabusu anakula mlo mmoja nasema, asubuhi anakunywa uji mchana ugali, lakini lingine analala saa tisa. Yule ni binadamu, kwa nini asilale saa moja halafu akaamka kesho kama kawaida hii pia kidogo itakuwa imewasaidia, kuliko mtu kusema kwamba eti alale saa tisa, binadamu gani huyo! Nadhani imefikia wakati sasa hivi sheria zilizopitwa na wakati tuzifanyie kazi *at least* kila mwanadamu ajisikie kwamba na yeze kweli ni binadamu na kweli haki zake anazipata.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Naona kengele yako ya pili.

**MHE. SADIFA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

#### **MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema inayoniwezesha kutekeleza majukumu yangu ya Kibunge.

Mheshimiwa Spika, naanza kuwapongeza Mawaziri, Katibu Mkuu, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na watendaji wote wa Wizara hii nyeti kwa kutekeleza majukumu yao vizuri, hali iliyopelekea uandaaji wa hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kuishukuru sana Wizara kwa kukamilisha ujenzi wa Mahakama za Mwanzo za Msoga – Lugoba, Bagamoyo ambazo zimeboresha utoaji wa haki katika Wilaya ya Bagamoyo.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kuitia programu ya maboresho ya sekta ya sheria na miradi ya maendeleo kwa ujenzi wa Majengo ya taasisi ya mafunzo ya uanasheria kwa vitendo (*The Law School of Tanzania*). Naipongeza Wizara hii kwa kutambua baadhi ya wanafunzi kugharamia mafunzo hayo. Kuitia bodi ya uendeshaji ya taasisi hiyo, Serikali imekuwa ikitoa mikopo kwa wanafunzi hao. Je, utaratibu wa marejesho hayo ukoje? Kwa kuwa wahitimu wengi wa fani hii ya sheria hawana ajira, je watarejeshaje mikopo hiyo kwa wakati ili kuwezesha wanafunzi wengine kukopeshwa?

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada hizi za Serikali, bado wahitaji wa mikopo hii kwa wahitimu wa shahada ya sheria ni wengi sana ambao hawana uwezo kabisa na wapo tu majumbani. Je, nini hatima yao katika suala zima la ajira kwa wanaokosa uwezo wa kujunga na taasisi ya mafunzo ya uanasheria kwa vitendo?

Mheshimiwa Spika, naiomba Wzara iharakishe rasimu ya mabadiliko ya sheria zote kandamizi zinazohusiana na haki za wanawake na watoto kuitia Tume ya Kurekebisha Sheria, mfano, Sheria ya Mirathi, Ndoa na Talaka zinatakiwa kufanyiwa marekebisho kuhusisha mabadiliko ya kimazingira.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. NYAMBARI C.M. NYANGINE:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kutoa shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Celina Ompeshi Kombani, Waziri wa Katiba na Sheria kwa kuwasilisha bajeti ya Wizara yake kwa makini. Pia nawapongeza watendaji wa Wizara hii kwa kuiandaa na kuikamilisha kwa makini bajeti iliyowasilishwa.

Mheshimiwa Spika, katika kuichangia hoja hii napenda kumwuliza Waziri maswali yafuatayo:-

Je, Mheshimiwa Waziri ana taarifa na habari kuwa rushwa imekithiri katika Mahakama zetu toka ngazi ya chini hadi ngazi ya juu?

Je, Mheshimiwa Waziri unafahamu kuwa rushwa katika Mahakama ya Wilaya ya Kinondoni hutolewa au kuombwa mchana kweupe?

Kwa nini kuna suala la ubambikizaji wa kesi katika Wilaya ya Tarime?

Je, bajeti ya Wizara hii kwa mwaka 2011/2012 inajitosheleza? Kama hajitoshelezi huoni kuwa itatoa mwanya wa rushwa kwa watendaji wa Wizara yako?

Rushwa katika Mahakama zetu za Mwanzo hususan katika Wilaya yangu ya Tarime. Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo ya Sirari huchukua rushwa na akiulizwa hutoa majibu kuwa Mbunge hakumwajiri na wala Mbunge si TAKUKURU! Je, Hakimu kama huyo achukuliwe hatua zipi?

Je, Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo ya Nyamwaga anawatendea haki wananchi wake? Kwa nini asisimamishwe kazi mara moja kwa kuwanyanyasa wananchi wa Tarafa ya Ingwe?

Majengo ya Mahakama zetu hasa zile za mwanzo yamechakaa sana. Halikadhalika Majengo ya Mahakama za Wilaya nayo yana hali mbaya. Je, ni lini Serikali itajenga, au itakarabati majengo haya? Je, Serikali haioni kuwa kuendelea kutumia majengo yaliyochakaa sana na wakati fulani hayana hata fanicha ni ukiukaji wa haki za binadamu?

Serikali inasema nini juu ya uhaba wa Mahakimu katika Mahakama zetu za Mwanzo?

Suala la Serikali kuanzisha Mahakama za Mwanzo kwa kila Taraifa katika nchi yetu si baya. Lakini Mahakama hizi ziko mbali sana kwa baadhi ya vijiji hasa katika Wilaya yangu ya Tarime! Je, Serikali haioni kuwa ni muda muafaka kwa sasa kuainisha Mahakama Za Mwanzo kwa kila Kata?

Kwa kuwa Wilaya ya Tarime inakabiliwa na migogoro ya kila aina; wizi wa mifugo, mapigano ya ukoo, magendo, kunyang'anyana ardhi na kadhalika. Je, Serikali haioni kuwa ni muda muafaka kuhalalisha sheria za kimila ili kupunguza uhalifu na ukiukwaji wa haki za binadamu Wilayani Tarime?

Kwa nini Serikali inaendelea kutambua Sheria za Kimila za Ndoa katika kipindi hiki cha maendeleo ya sayansi na teknolojia. Je, Serikali haioni kuwa Sheria za Ndoa za Kimila bado zinaendelea kumdhaliilisha mtoto wa kike kwa kumfanya kitegea uchumi cha Taifa?

Lugha rasmi ya Taifa ni Kiswahili, ambacho kinazungumzwa na kila Mtanzania. Lugha nyingine ni Kiingereza ambacho kinazungumzwa na Watanzania wachache! Je, ni kwa nini Mahakama zetu zinatumia Kiingereza badala ya Kiswahili? Je, ni kwa nini sheria zetu zinaandikwa kwa lugha ya kigeni? Ni lini Mahakama zetu zote zinatumia lugha ya Kiswahili?

Wananchi wangu wa Wilaya ya Tarime wanauelewa duni juu ya Sheria. Hali hii inapelekeu uonevu, unyanyasaji, udhulumaji, ukosefu wa haki na usawa pia udhallishaji, uvunjifu wa sheria, uhalifu na kadhalika. Je, ni lini Wizara itafika Wilayani Tarime kwa malengo mahsus ya kuuelimisha umma wa wana Tarime juu ya uelewa wa Sheria?

Je, ni lini Wizara itatoa elimu juu ya Sheria ya Hakimiliki na Haki Shirikishi ili kila Mtanzania na hasa wasanii na waandishi wa vitabu waelewe juu ya sheria hizo?

Watanzania wengi hasa wafanyabiashara, wasanii na hata watanzi wa vitabu pia wahakiki wa vitabu hawafahamu juu ya sheria ya *Fair competition*. Je, ni lini Wizara hii itachukua jukumu la kuuelimisha Watanzania juu ya sheria hii?

Kwa nini kuna ukiukwaji wa haki za binadamu katika baadhi ya sehemu za nchi yetu huku kuna vyombo vya dola? Je, vyombo hivi vya dola vimeshindwa kutekeleza majukumu na wajibu wanaovihu?

Lipi ni suluhisho la migogoro ya ardhi Wilayani Tarime?

Mrundikano wa kesi hasa kesi za jinai katika Mahakama zetu unatia shaka. Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya suala hili? Kesi hizo za jinai mara nyingi husimamiwa na Serikali na uchunguzi wake huchukua muda mrefu. Je, kuchelewa kutolewa hukumu kwa kesi hizo inadhihirisha kuwa Serikali imeshindwa kazi?

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Katiba mpya. Napenda kuchukua hatua za dhati za kuanzisha mchakato wa kutafuta maoni juu ya uundwaji wa Katiba mpya katika nchi yetu! Suala hili ni jema na zuri ila tahadhari ninayoitoa kwa Serikali ni kuwa macho na vibaraka wanaodandia hoja za Serikali na kuzigeuza kwa ulaghai kwa lengo la kuwadanganya Watanzania! Wanawadanganya Watanzania kwa nia mbaya ya kuwafanya wananchi wetu waichukie Serikali ya CCM iliyoko madarakani! Hivyo udanganyifu huu usitumie katika mchakato mzima wa Katiba Mpya.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kwamba, napendekeza kuwa umri wa mgombea urais upunguzwe toka miaka 40 hadi miaka 35, (thelathini na tano) tu ili kuweza kutoa nafasi kwa vijana kushiriki kikamilifu katika uongozi wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, mwisho wa yote, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.hawana uwezo wa

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri na watendaji wake wote kwa kutayarisha hotuba nzuri inayolenga kuwepo utawala wa sheria.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni muhimu sana kwa kuleta utengamano, haki na uadilifu nchini na kinyume chake haki isipokuwepo matokeo yake ni vurugu na fujo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu tatizo la kuchelewesha kesi. Wataalam wa sheria wanasesma: "*The right delayed is the right denied*"; hivyo ucheleweshaji wa kesi ni tatizo kubwa katika suala zima la utoaji haki. Je, Serikali ina mpango gani wa kuondoa kabisa suala la ucheleweshaji kesi hapa nchini?

Mheshimiwa Spika, kuhusu majengo ya Mahakana na nyumba za Mahakimu. Ni jambo la kusikitisha sana kuwa hata baada ya miaka hamsini ya Uhuru majengo ya Mahakama ni chakavu sana na hayalingani na heshima ya taasisi hiyo. Lakini pia Mahakimu wengi hawana nyumba za kuishi karibu na majengo ya Mahakama, hivyo, hulazimika kusafiri masafa marefu na mara nyingine husafiri kwa baiskeli. Hii ni hatari sana hata kwa usalama wa Mahakimu wetu.

Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itatoa kipaumbele kwa Mahakimu kujenga ofisi zenye hadhi na kuwajengea nyumba bora Mahakimu wetu.

Mheshimiwa Spika, rushwa katika Mahakama. Kuna ukweli usiopingika kuwa Mahakama inatajwa kuwa imegubikwa na rushwa jambo linalonyima haki isitendeke popote penye rushwa. Ni wale tu wenye uwezo wa kutoa rushwa ndio watakaokuwa na haki. Hivyo, tukififikia mahali haki inanunuliwa, hatuvezi kuwa na utawala wa sheria. Naomba Serikali iongeze vipato vya Mahakimu na Majaji na watendaji wote wa Mahakama ili wasiweze kushawishiwa kwa hongo ndogo ndogo. Naoimba Serikali iongeze bajeti ya Wizara hii ambayo miaka mingi imekuwa finyu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu katiba mpya, napongeza Serikali kuwa na mchakato wa kuandaa Katiba mpya. Ni muhimu kuwashirkisha wananchi tokea ngazi ya chini ili kupata muafaka wa makundi yote nchini. Ni muhimu pia kuangalia sana nguvu ya Rais katika Katiba mpya zisije zikawa ni kikwazo kwa maendeleo ya nchi.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu mchakato wa Katiba Mpya. Naomba niungane na Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwamba sheria inayoweka utaratibu wa kupatikana kwa Katiba mpya ni muhimu na utaratibu unaotakiwa ni ule wa kidemokrasia unaoshirikisha watu wote wa nchi hii kwani Katiba ni mali yao. Lakini ili kuwe na ushirikishi imara ni lazima watu wote waelimishwe na kuifahamu kwanza Katiba yao ya sasa ili kwa pamoja waweze kuyafahamu matatizo na kasoro zilizopo katika Katiba na wao wawe na uhuru na uelewa mpana wa kuchangia na kutoa maoni katika mchakato wa kuelekea kutengeneza Katiba mpya.

Mheshimiwa Spika, hali iliyopo kwa sasa ni kwamba Katiba iliyopo haifahamiki kwa karibu asilimia themanini ya Watanzania na hivyo hawajui kilichomo na kama hawajui ni kwa vipi wataweza kutoa maoni yao ili Katiba wanayoitaka iwe bora zaidi na iweze kutatua matatizo yao ya msingi? Ni busara kwa Wizara hii kutoa elimu kwa wananchi wote ili waielewe Katiba iliyopo na mapungufu yake na mwisho wawe na nafasi ya kutoa maoni yao katika mchakato wa Katiba mpya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sheria kandamizi na zilizopitwa na wakati. Kwa kuwa nchi yetu inajiaanda kuleta Muswada wa mchakato wa Katiba mpya, nina imani kwamba, sheria zile ambazo ni kandamizi na zilizopitwa na wakati zitaangaliwa upya. Lakini kwa wakati huu ambapo bado nchi yetu hajawa na Katiba mpya ni muhimu kwa Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 ikiangaliwa upya, hususan kwa kile kiwango cha matunzo kwa watoto pindi ndoa inapovunjika au mtoto anapozaliwa nje ya ndoa. Kiwango kinachowekwa Kikatiba ni kidogo sana na hakitoshelezi kwa hali ya maisha ya sana na matokeo yake ni watoto kushindwa kupata mahitaji yao ya msingi ikiwepo elimu na kuishia kuwa watoto wa mitaani.

Mheshimiwa Spika, kuna sheria zingine ambazo ni kandamizi zinazokandamiza wanawake na watoto wa kike. Sheria za urithi zinawabagua wanawake na watoto wa kike kurithi mali kama ilivyo kwa watoto wa kiume. Sheria zingine haziko wazi, mfano za unyanyasaji wa kijinsia. Inapotoka msichana amebakwa au mtoto wa kiume kunajisiwa hapo ndipo sheria inapochukua mkondo wake lakini kuna matukio mengine ya unyanyasaji mfano watoto wa kike kushikwa katika sehemu za siri, matiti na sehemu nyingine nyeti za mwili, lakini sheria haikuwa wazi na haitoi mashtaka au adhabu kwa makosa hayo. Wizara hii ni lazima iangalie ni kwa jinsi gani sheria itawekwa ili kuonesha adhabu kwa makosa haya.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo kubwa sana la wananchi walio wengi kutokujua haki zao hata pale ambapo wanatakiwa kupata haki hizo. Mfano, mtu anapokamatwa kwa tuhuma fulani, hatakiwi kukaa mahabusu kwa zaidi ya masaa 48 kabla ya kufikishwa Mahakamani. Hili halieleweki kwa wananchi walio wengi na matokeo yake kuna mahabusu wasiokaa hata zaidi ya wiki nzima au hata mwezi bila kufikishwa Mahakamani, hasa wale maskini wengi walio vijijini. Hili ni tatizo kubwa ambalo linahitaji elimu ya kutosha kwa raia ili waweze kuzidai haki zao za msingi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR:** Mheshimiwa Spika, kwanza ni ubovu wa majengo ya Mahakama. Majengo ya Mahakama mengi ni mabovu na yamechakaa na yamekuwa hayaendani na hadhi ya chombo hicho kikubwa na muhimu katika nchi hii. Naishauri Serikali kuongeza bajeti kwa Wizara hii ili iweze kujipanga zaidi katika shughuli zake. Pamoja na vitendea kazi kuwa finyu, wakati mwngine hata karatasi hakuna na mtuhumiwa anaambibiwa akanunue karatasi au akatoe photocopy jambo ambalo ikifikia hatua hii hata haki haitendeki tena.

Mheshimiwa Spika, pili, ni suala la rushwa. Kumekuwa na rushwa katika Mahakama zetu na sasa hata madalali wapo katika Mahakama, jambo ambalo linatia doa katika Taifa letu. Leo ukifika Mahakamani tu utazungukwa na watu wakikuuliza una shida gani ili waweze kukusaidia. Jambo hili linatia aibu Taifa letu, kwani linawakosesa watu haki zao hasa wale wanyonge. Kwa hiyo, naishauri Serikali iwaondoe watu wanaojazana nje ya maeneo ya Mahakama ambao hawana shughuli za kufanya zaidi ya udalali na imefikia watu wa aina hiyo kuwachukulia

dhamana hata watu ambao hawajui lakini kwa makubaliano ya kiasi cha fedha, jambo hili ni hatari na hatua zichukuliwe haraka.

Mheshimiwa Spika, tatu ni kuhusu masuala ya Katiba. Bado masuala ya Katiba baadhi ya utekelezaji wake haujafikiwa, mambo mengi ni yale ya uchaguzi tu ndio yanapewa kipaumbele, lakini katika maeneo mengine utendaji wake ni mdogo, kwa mfano, Tume ya Mipango ya Pamoja ya Fedha ya Muungano na *Account* ya Fedha ya Muungano vitu hivi viwili ni mambo yaliyomo katika Katiba lakini mpaka hii leo bado hayajatekelezwa. Je, Mheshimiwa huoni ni kuidharau Katiba? Je, kuna jambo gani ambalo linakwamisha utekelezaji wake? Je, mbona mambo mengine hufanywa haraka haraka na hili linapuuza? Namwomba Mheshimiwa Waziri atakapotoa majumuisho anipe ufanuzi wa kuniridhisha.

Mheshimiwa Spika, nne, ni kuhusu haki za binadamu. Uendelezwaji wa haki za binadamu ni bado, kwa hiyo, naishauri Wizara ijipange tena upya kuhusu suala la haki za binadamu. Watu wamekuwa hawajui haki zao za msingi lakini uvunjwaji wa haki zao umekuwa mkubwa hasa kuititia Jeshi la Polisi na Taasisi nydingine za usalama, kwa hili Serikali ni lazima ichukue tena juhudzi ya kutoa elimu kwa umma ili watu wajue haki zao. Polisi na usalama ambao kimaumbile ni watu wa usalama lakini kiutendaji wao ni watu wa mabavu na mtu anaogopa hata kufika sehemu zao kusikiliza shida za jamaa zao na ndugu zao. Kwa hiyo Wizara haina budi kuweka mfumo zaidi wa Polisi Jamii na kuondoa Polisi *Force*. Naelewa kuwa Polisi wako kwenye Wizara nydingine lakini kazi zao zifanyike chini ya sheria za nchi.

Mheshimiwa Spika, tano, ni kuhusu utawala bora. Panapokosekana utawala bora huwa hakuna haki. Kwa kuwa haki huanza kwenye uchaguzi lazima kuwe na mazingira mazuri katika uchaguzi pamoja na kuwa na sheria nzuri za uchaguzi lakini siyo zinazotumika. Wakati wa uchaguzi Polisi huwa wanatumia mabavu na hii ni kipinda haki na mfumo huu huwa haufanikiwi utawala bora. Kwa hiyo, naishauri Serikali isiwatumie Polisi kulinda vituo yya kupiga kura au kuranda na magari ya kivita wakati wa uchaguzi, kwani huwatia watu hofu na kuwanyima haki zao za msingi.

**MHE. HAMAD ALI HAMAD:** Mheshimiwa Spika, kumeundwa chombo na Mheshimiwa Rais cha kusimamia haki za wananchi kisheria ambapo Mheshimiwa Jaji Kisanga yeye ameteuliwa kuwa Mwenyekiti na pale Zanzibar wanayo ofisi yao.

Mheshimiwa Spika, napata shida kwamba Kamati hii inaposema kwamba, wao hawatahusika na yeoyote ambaye mashauri yake yameshaamuliwa na Mahakama au chombo chochote kinachofanana na Mahakama.

Mheshimiwa Spika, mwananchi hawezi kujua kwamba hakutendewa haki mpaka pale ambapo Mahakama imeamua, hivyo basi, baada ya maamuzi hayo ya Mahakama ndipo ambapo mwananchi anaweza kupima kwamba hakutendewa haki, sasa Tume hii hapa ndipo ambapo naiona kwamba, haipo kwa kuisaidia jamii. Naishauri Serikali kwamba Tume hii kwa kuzingatia kwamba Hakimu ni binadamu na anaweza kutoa hukumu kimakosa, sasa ni vema Tume hii isijivue katika kuwatetea wale wote ambao hawakutendewa sawa na Mahakama na ndio maana kunakuwa na Mahakama za Rufaa kuthibitisha kwamba Hakimu ni binadamu na anaweza kufanya makosa.

Mheshimiwa Spika, Mahakama zetu hapa nchini zimekuwa zikipewa lawama nydingi na Watanzania kwa kukosa uadilifu na hii inaleta dhana kwamba Mahakama ni mahali ambapo panauzwa haki lakini pia panabatilishwa sheria kwa wenye fedha. Mfano, Askari wa kikosi kazi ambao kazi yao ni kushughulika na wale wauza madawa ya kulevyta.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya kazi ya kizalendo wanayoifanya askari wa kikosi hiki, askari wamewakamata wauza madawa ambapo mionganii mwao walikuwemo wageni lakini pia Watanzania, cha kushangaza ni kwamba wale wageni (*Waasia*) waliachiwa na wale Watanzania hadi leo wako ndani na inasemekana kwamba Waasia hao wameshaondoka nchini hapa. Inasikitisha sana na hii inaonesha wazi kwamba Mahakimu hawa wamenyooshewa mkono na wahalifu hawa.

Mheshimiwa Spika, wananchi wanyonge nao tuwatendeeni haki na isiwe kwamba haki zinauzwa na Mahakama, hii sio haki na ni udhalilishaji mkubwa kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, kuhusu hoja ya Serikali moja. Baada ya Muungano mwaka 1964, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alisema: "Huu ni mwanzo kuelekea Serikali moja maana kwa wakati huu tuna Serikali mbili." Je, ni kwa nini sasa miaka 47 tangu Muungano tuwe na nchi mbili badala ya moja kama Waasisi wa Taifa hili walivyotaka? Je, Serikali inaweza kuliangalia hili upya ili liweze kuondoa mgogoro uliopo sasa? Maana kwa upande wa Zanzibar wao wanaamini kuwa ni nchi kamili na yenye Serikali yake. Ilighali upande wa Tanganyika tunaamini katika Serikali ya Muungano huku tukiadhimisha miaka 50 ya Uhuru. Je, miaka hiyo (50) hamsini ya uhuru ni ya nani na miaka 47 ya Uhuru wa Zanzibar ni ya nani? Nini ni Muungano katika Uhuru wa nchi hizi mbili? Hata historia za uhuru wa nchi mbili ni tofauti, maana sisi Tanganyika tumepata uhuru kwa njia ya amani, ilighali upande wa Zanzibar ni kwa njia ya Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, hivyo hoja ya kupigiwa kura kama tunataka Serikali moja ama Muungano ni la muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri ambayo inajitosheleza.

Mheshimiwa Spika, tatizo la bajeti yake ni kwamba, fedha aliyoomba ni ndogo na inaweza kukwamisha kazi za Mahakama. Maadam Serikali imeanzisha Mfuko wa Mahakama, nashauri Mfuko huu uongezewe ili kazi za Mahakama zisikwame na wananchi wapate haki zao katika wakati unaofaa.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu Waislamu wamekuwa wakidai Mahakama ya Kadhi ili kushughulikia masuala muhimu ambayo ni sehemu ya Ibada kwa Waislamu. Masuala hayo ni pamoa na:-

- (a) Ndoa na Talaka;
- (b) Mirathi;
- (c) Wosia/Wasia;
- (d) *Waqfu* na mali ya amana;
- (e) Hiba;
- (f) Malezi ya Watoto; na
- (g) Usuluhishi wa migogoro ya Kiislamu.

Mheshimiwa Spika, haya ni mambo ambayo yanahitaji kushughulikiwa kwa utaalam wa Kiislamu. Je, nini hatma ya Mahakama ya Kadhi? Waislamu wamesubiri sana sasa mnataka Waislamu wafanye maandamano ndio muwasikilize. Kwa nini mambo au masuala ya Waislamu hayapewi umuhimu unaostahili kama dini zingine? Vinginevyo tutaabmini usemi kuwa mnyonge hatapi haki yake mpaka mwenye nguvu apende.

Mheshimiwa Spika, naomba kujua suala la *OIC* limefikia wapi na tatizo ni nini? Nchi kadhaa zenye Wakristo wengi zimeingia *OIC* kwa nini Tanzania kuna kigugumizi? Basi Wazanzibari waruhusiwe wajunge kama huku Bara hatutaki.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu tumeomba sheria zote zinazomkandamiza mwanamke ziweze kufanyiwa marekebisho. Sheria hizi ni pamoja na Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 na Sheria ya Mirathi. Sheria hizi zimepitwa na wakati na zinaendelea kumnyanyasa mwanamke. Napenda kuelewa ni lini sheria hasa ya Ndoa italetwa hapa ili iweze kufanyiwa marekebisho na kuwaondolea unyanyasaji wanawake?

Mheshimiwa Spika, napongeza Serikali kwa kutafsiri baadhi ya sheria katika lugha ya Kiswahili ikiwemo Sheria ya Mtoto na Sheria ya Kuzuia Maambukizi ya Virusi vya UKIMWI. Nashauri sheria hizo zisambazwe vijijini kwa kila Serikali ya Kijiji kuwa na nakala ili kuelewa vizuri sheria hizi na ziweze kueleweka vijijini.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni moja ya nchi chache duniani zenye Sheria ya UKIMWI lakini pamoja na kuwa Sheria hii Kifungu cha 47 kinapingana na haki za binadamu kwa vile tumetunga sheria na kuweka kipengele hiki kinachotoa adhabu kwa watu wanaowaambukiza Virusi vya UKIMWI kwa makusudi. Hii imefanya watu waishio na virusi wasiweze kujitokeza, hivyo, kupunguza jitihada za mapambano haya. Nashauri Serikali ilete marekebisho ya sheria ili kipengele hiki kiweze kuondolewa ili kuongeza mapambano dhidi ya watu waishio na Virusi vya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, Wizara isaidie kufundisha watoa sheria ya msingi vijijini (*paralegals*).

Mheshimiwa Spika, Mahakama za Mwanzo ziongezwe na zipewe wataalam.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja ya Wizara tajwa hapo juu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, awali tulielezwa kuwa ofisi ya Mwanasheria Mkuu ndiyo itakayokuwa inaendesha kesi Mahakamani badala ya Polisi. Cha kusikitisha, Wilaya yangu ya Tunduru bado Polisi ndiyo wanaoendesha kesi kwenye Mahakama zetu. Je, ni lini agizo hili la Serikali litatekelezwa kwa Tunduru na maeneo mengine?

Mheshimiwa Spika, pili, nchi yetu inaongozwa kwa misingi ya sheria na demokrasi. Tunafanya chaguzi mbalimbali na kupata viongozi wa ngazi mbalimbali wakiwa na mipaka yao ya utekelezaji wa majukumu yao. Je, Serikali inasema nini pale Mbunge wa Jimbo anaingia kwenye Jimbo la Mbunge mwngine na kutangaza hadharani kuwa, Mbunge wenu hawawakilishi vema Bungeni, hivyo nipeni kero zenu nikawasemee huko Bungeni:-

- (a) Serikali inatoa tamko gani juu ya tabia kama hizi?
- (b) Mbunge huyu anafuata utawala wa Sheria?
- (c) Ikitokea wananchi wanaomuunga mkono Mbunge aliyeingiliwa Jimboni kwake kuleta upinzani wa wazi dhidi ya Mbunge Mvamizi hapatatokea uvunjifu wa amani?

Mheshimiwa Spika, naomba ufanuzi wa maswala haya.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuipongeza Wizara kwa kazi nzuri inayofanywa na vyombo vyake muhimu kama Mahakama katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Spika, kwanza Bajeti ya Sh.135,723,956,600/= ni kidogo sana ukizingatia majukumu ya chombo muhimu kama Mahakama.

Mheshimiwa Spika, jukumu la kutoa haki siyo kazi rahisi katika nchi kubwa kama Tanzania. Mahakama na Majaji wanafanya kazi katika mazingira magumu. Mahakimu na Mawakili maslahi

yao ni duni na makazi yao hayaeleweki vizuri. Mapendekezo ya Tume ya Ntukamazina ya mwaka 2006 kuhusu uboreshaji wa mishahara ya wataalam kama hawa hayajatekelezwa na Serikali kutokana na ufinyu wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, pili, Serikali inatakiwa itatue tatizo la umeme linaloathiri uzalishaji viwandani na *TRA* ifanye kazi yake ya ukusanyaji wa mapato kwa makini zaidi na kuwabana walipa kodi wakubwa ili tuweze kuboresha maslahi ya Mahakimu, Mawakili na Majaji.

Mheshimiwa Spika, tatu, naomba Wizara ijpange vizuri zaidi katika kupambana na rushwa iliyokithiri katika Mahakama. Ni aibu kwa chombo muhimu ambacho ni kati ya mihimili mitatu ya dola kuendelea kulea rushwa kwa watumishi wake.

Mheshimiwa Spika, nne, kumejitokeza tabia mbaya kwa watumishi wa Serikali wa ngazi za juu kulumbana hadharani kwa kutumia vyombo vya habari wakati Serikali ni moja. Huko ni kukosa *ethics* za utumishi wa umma. Malumbano kati ya *DPP* na Bosi wa *TAKUKURU* hayana tija na ni aibu kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, tano, kwa kuwa Rais ni kiongozi wa mihimili mmoja yaani Serikali kati ya mihimili mitatu, Bunge na Mahakama na Serikali ni vema uteuzi wa Jaji Mkuu pamoja na Majaji wengine uthibitishwe na wawakilishi wa wananchi yaani Bunge katika kuimarisha *the Doctrine* ya *separation of powers* na *the independence of the Judiciary*. Bila hivyo itaonekana kwamba kwa kuwa Rais amewateua Majaji basi anaweza kuwa na *influence* kwenye hukumu zinazotolewa na Mahakama.

Mheshimiwa Spika, sita, nimewahi kushiriki katika *Interview ya Panel* ya kumwajiri *Registrar* wa Mahakama ya Afrika ya *Human and Peoples Right* iliyoko Arusha, Watanzania walioomba nafasi ya *Registrar* walikosa kazi hiyo kwa sababu ya kukosa sifa ya *Law School*.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kwa Wizara kwa kutumia *Loans Board* vijana wengi zaidi wanaohitimu mafunzo ya sheria walipiwe karo ya kuhudhuria masomo ya *Law School* ili wawe Mahakimu na *Advocates* wazuri.

Mheshimiwa Spika, saba, ni muhimu Wizarani kuwe na utaratibu wa kudumu wa kuhakikisha wananchi wote wanaielewa vizuri Katiba ya nchi kama Sheria kuu ili wajue ni jinsi gani haki zao zinalindwa na katiba.

Mheshimiwa Spika, nane na mwisho, tutakapoanza kuunda Katiba mpya suala la *separation of powers* ni muhimu sana kuliboresha kwa Serikali kuundwa nje ya Bunge, Mawaziri watoke nje ya Bunge, ndiyo Serikali itaweza kuwajibishwa ipasavyo.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Celina Kombani kwa kuiandaa na kuiwasilisha vyema hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Katibu Mkuu na maafisa wote walio chini yake katika Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu inaelekea kutimiza miaka 50 ya uhuru wetu, kuna mambo mengi tumeyapitia katika kulijenga Taifa letu, sheria nydingi zimetungwa na kubadilishwa za zamani. Lakini umefikia wakati Mheshimiwa Rais wetu Awamu ya Nne kuona ipo haja ya Serikali kukubaliana na maoni ya wananchi siyo ya kisheria ila kwa mwelekeo wa maneno ya walio wengi kuwa Katiba ya nchi yetu iangaliwe upya.

Mheshimiwa Spika, kwa muono wangu, Serikali lazima iangalie katika mapendekezo yake ili kutoonekana au kuipa nafasi upande wa Tanzania Bara ambao una watu wengi kuonekana kuimeza Tanzania Visiwani ambapo itaonesha kuimeza kimaamuzi hasa katika chaguzi.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu utakapofikia wakati, napenda kutoa ushauri wangu kabisa kwa sababu naweza kuwepo au kutokuwepo, ni amri ya Mungu! Hivyo moja ya ushauri

wangu ni kwamba, uchaguzi wa ugombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwe na kifungu kinachoelekeza kuwa Rais apatikane kwa ushindi usiopungua asilimia kadhaa kwa upande wa Zanzibar kati ya kura zote alizopata pande zote mbili. Hii itasaidia kuonesha Rais anachaguliwa na ushindi wa wananchi wa Tanzania Bara tu walio wengi, hii italeta uwiano na heshima ya Muungano na kuondoa mabezano kutoka upande mmoja wa Muungano.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

**MHE. PUDENCIANA KIKWEMBE:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika masuala yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, je, Serikali inasema nini kuhusu wananchi kuendelea kujichukulia sheria mkononi hasa kwenye masuala ya wizi unapotokea?

Mheshimiwa Spika, pili, kwa kuwa nchi hii inaendeshwa na Katiba na Sheria na kwa kuwa baadhi ya viongozi (wanasiasa) wamekuwa wakifanya maandamano na kutumia lugha za matusi kutukana viongozi wenzao. Je, Serikali inachukukua hatua zipi na inatoa kauli gani kuhusiana na hilo?

Mheshimiwa Spika, tatu, je, ni kwa nini baadhi ya watuhumiwa hujidhamini wenyewe wakiwa na kesi Mahakamani? Je, huo utaratibu upo na kama haupo je, ni utaratibu upi unaotakiwa kutumiwa pindi mtuhumiwa anapokuwa amekamatwa? Je, Serikali inatoa mwongozo na maelezo gani kuhusiana na hilo?

Mheshimiwa Spika, nne, ni kwa nini kunakuwa na ucheleweshaji wa kesi? Pia kwa nini baadhi ya Mahakimu wamekuwa wakishikilia baadhi ya kesi kwa makusudi na manufaa binafsi?

Mheshimiwa Spika, ahsante na naunga mkono hoja.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri kwa namna nzuri alivyowasilisha hotuba yenyewe.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uzuri wa hotuba yenyewe kuna hoja kwa Serikali kuongeza bajeti kwa ajili ya Wizara ya Katiba na Sheria kulingana na majukumu yanayoikabili.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu inatambua wazi kuwa nchi yoyote ulimwenguni inaudwa kwa misingi ya Sheria Mama ambayo ni Katiba na sheria zenyewe ambazo hazikinzani na sheria mama. Kwa Katiba mgawanyo wa Mamlaka mbalimbali ikiwemo mihimili ya dola ambayo ni Serikali (*Executive Legislature (Parliament)*) (Bunge) na Mahakama (*Judiciary*).

Mheshimiwa Spika, nchi yetu inakabiliwa na matatizo makubwa ya namna ambavyo usimamizi wa sheria unavyoendeshwa na kukabiliwa na ufinyu wa bajeti matokeo yake kunakuwa na misongamano ya mahabusu katika Magereza yetu nchini.

Mheshimiwa Spika, aidha upo udhaifu mkubwa kwa namna ambavyo uendeshaji wa mashauri mbalimbali hasa kwa upande wa upelelezi na ukamataji na ufikishaji watuhumiwa Mahakamani na uzuiliaji katika Magereza hali inayosababisha msongamano wa wafungwa na mahabusu na hivyo kuonekana wazi kuwa haki inacheleweshwa na kuonekana dhahiri kuwa haki imekataliwa.

Mheshimiwa Spika, mojawapo ya sababu zinazosababisha msongamano mkubwa wa mahabusu Magerezani ni pamoja na kucheleva kwa upelelezi na wakati mwininge ni ukosefu wa fedha za kuwalipia gharama mashahidi wakati mashauri yanapokuwa yamepangwa kusilikizwa.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kupitia Wizara ya Sheria na Katiba iharakishe utaratibu wa kuondoa ukiritimba uliopo sasa wa Jeshi la Polisi kufanya kazi zote za upelelezi, ukamataji na kuandaa mashtaka kwa ajili ya kuwapeleka washtakiwa Mahamakani hali ambayo kwa hakika imesababisha kwa kiwango kikubwa Jeshi la Polisi kujilingiza katika rushwa za wazi wazi na

kulazimika kuyafikisha Mahakamani mashauri yale tu ya wakosefu wanaposhindwa kutoa rushwa ndio wanaofikisha Mahakamani, ipo sababu ya kuharakisha mpango wa kuhamishia masuala haya katika Ofisi ya Mwanasheria wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, yapo pia malalamiko ya wazee wa Mahakana katika Mahakama za Mwanzo kuwa hawalipwi kwa wakati malipo au posho zao ni kidogo sana na hazilingani na kupanda kwa gharama za maisha. Niambie Serikali ifanye haraka kuwalipa malimbikizo ya posho zao.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mchakato wa kupata Katiba mpya au marekebisho ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977, naishauri Serikali kuhakikisha elimu ya uraia ya kutosha inatolewa kwa Watanzania walio wengi ambaao kimsingi hawaifahamu hata hiyo Katiba ya sasa ambapo hawajui uzuri wala ubaya wa Katiba yenye.

Mheshimiwa Spika, kimsingi Watanzania walio wengi wanahitaji kuelekezwa na kwa bahati nzuri ni wepesi wa kuelewa, hata hivyo wasipoleweshwa upata tafsiri mbaya mfano wakati waasisi wa Taifa hili chini ya uongozi wa Chama cha *TANU* walikuja na kauli mbiu ya "Uhuru ni Kazi ya TANU", Tanganyika ilipopata uhuru wananchi wengi walijisahau na kufikiria kwamba hawapaswi kufanya kazi na kwa mantiki hiyo *TANU* ndiyo ifanye kazi na wao wapumzike hali iliyopelekea kubadili kaulimbiu kuwa "Uhuru na Kazi".

Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hiyo hivi sasa wapo Watanzania wanaodhani kuna Katiba mpya ikija maisha yao yatabadilika na kupata nafuu ya maisha bila kufanya kazi, upotoshaji unatumiwa na wanasiasa kupotosha wananchi.

Mheshimiwa Spika, rai yangu, ni kuiomba Serikali ifanye juu chini kutoa elimu ya uraia kabla ya kuingia kwenye mchakato wa Katiba mpya.

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kazi kubwa inayofanya katika eneo zima la sheria na Katiba. Naiomba Serikali ifanye yafuatayo:-

- (a) limarishe maslahi ya Mahakimu.
- (b) Iboreshe Mahakama zetu.
- (c) Iboreshe maslahi ya Wazee wa Baraza, itenye kiwango cha mishahara badala ya kutegemea posho kwa kesi kwa Wazee wa Baraza.
- (d) Usafiri kwa Mahakimu wetu ni jambo muhimu sana kwani Mahakimu wengi Vijijini wamekuwa wakihukumu kesi, halafu wanapanda pikipiki. Ni hatari sana.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. SALOME D. MWAMBU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naipongeza Wizara ya Katiba na Sheria kwa hotuba nzuri ya Waziri pamoja na mapungufu waliyonayo.

Mheshimiwa Spika, natoa ushauri kwa ajili ya kuboresha Wizara hii. Serikali itoe fedha kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama za Wilaya hata Magereza ya Wilaya. Pia nyumba za Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo. Si vizuri Hakimu kupanga mitaani kuchanganyika na wanakijiji, hivyo atashindwa kutenda haki.

Mheshimiwa Spika, nashauri kesi zishughulikiwe mapema ili tusiwe na mrundikano. Madhara ni:-

- (a) Kujenga uhasama kati ya watuhumiwa na ndugu wa mshtaki.
- (b) Huondoa amani katika jamii.

(c) Wananchi kujichukulia sheria mkononi hadi kupelekea mauti, kuchomeana nyumba na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali inunue magari Mahakama za Mwanzo na Wilaya ili kuwe na *mobile* Mahakama.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia bajeti ya Waziri na nitangulize kuunga mkono hoja. Katiba ndio mwongozo wa haki na kulinda sheria, haki za binaadamu na kulinda ardhi ya wananchi wote. Kuweka utaratibu wa kuweka mihimili yote mitatu, Mahakama, Serikali na Bunge. Pamoja na kuweka utaratibu wa kuwapata viongozi wote kuanzia viongozi wa kisiasa na viongozi wengi wa mihimili yote mitatu.

Mheshimiwa Spika, Katiba ndio chombo kinacholinda haki ya watu wa hali ya chini ili waweze kutendewa haki. Sheria hutokana na Katiba, kupatikana madaraka ya Rais, Madaraka ya Mahakama na Madaraka ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hali ya Mahakama zetu. Hiki ni chombo cha kutoa haki, kwa hiyo, ni muhimu Serikali ikatoa kipaumbele katika majengo kama yalivyo ya mihimili mingine. Serikali inapenda kujenga majengo ya Serikali na kupuza Mahakama, huku unakuta wananchi hufuata Mahakama mbali kwenye Wilaya zingine. Chombo hiki ni muhimu kiwepo katika kila Tarafa, Wilaya na Mikoa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuelezea hali ya matatizo yanayozikumba Wilaya ambazo hazina Mahakama. Wilaya ya Longido ni Wilaya Mpya. Tangu zamani Longido ikiwa chini ya Wilaya ya Monduli. Hakukuwa na Mahakama ya Mwanzo na baada ya kuwa Wilaya bado hakuna Mahakama Longido. Kutokuwa na Mahakama wananchi wanakosa haki mpaka wakawa wanaamua katika mashauri yao kutumia mila, jambo ambalo wananchi hawapewi haki kwani mila ina upendeleo wakati mwininge hasa kila mara mdogo hapewi haki. Wananchi wa Longido wanategemea Mahakama ya Wilaya ya Monduli ambayo iko mbali, kilometra 160 kufuata Mahakama. Wakati mashahidi wakitakiwa, walalamikiwa wanasafirisha mashahidi. Jambo ambalo kwa wakati mwininge wanafuata nani kampa nauli, chakula na kupoteza haki ya mtu. Naomba Serikali wajenge Mahakama ya Wilaya ya Longido pamoja na Mahakama za Mwanzo za Tarafa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ajira kwa watumishi wa Mahakama. Napenda kuelezea kwamba ukosefu huo unapelekea maeneo yenye ukosefu wa watumishi kuanzia Mahakama za Mwanzo na Wilaya kesi hizo kukosa mahali pa kuendeshewa. Kesi katika Wilaya ya Longido hazisikilizwi kutokana na kutokuwepo na Mahakama.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hali ya TAKUKURU. Kwenye maeneo mengi hawahangaiki na rushwa za aina nyingine isipokuwa kwenye uchaguzi, jambo ambalo wananchi wanashangaa sana kwamba wako kimya katika maeneo mengi.

Mheshimiwa Spika, hali ya maeneo mengi ambayo hayana Mahakama wala Hakimu ni kwamba hakuna sheria ambayo inafuatwa. Naomba Serikali wajenge Mahakama kwenye Wilaya ya Longido.

Mheshimiwa Spika, kama haki na sheria zinahitajika kuwe na Mahakimu pamoja na nyumba za Mahakimu kuishi.

**MHE. DKT. FENELLA E. MUKANGARA:** Mheshimiwa Spika, nina maoni katika Muswada wa kutunga au kurekebisha Katiba, kwamba, kauli ya Kambi ya Upinzani sio ya busara. Ni mkakati au kauli mbovu ya kuendeleza chuki haitusaidii. Kwa maoni yangu *statements* zake nyingi zisingeingia katika *records*. Kwanza, anazungumzia Muswada ambao haujaletwa kujadiliwa na anasema kwa kejeli kuwa wameupata kwa njia zao wenywewe na wanataka iende na hisia zao moja kwa moja kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa vile inajitokeza wazi nakala ya Muswada ambao bado unafanyiwa kazi upo katika mikono ya watu wasiowajibika moja kwa moja kwa wananchi na wanaendelea kupandikiza hisia mbalimbali, nashauri, tunapoendelea kutekeleza uboreshaji wa huu Muswada, tupate picha kamili ya mambo muhimu yaliyojitokeza kama upungufu katika Muswada ulioletwa kwanza. Ili kutuwezesha matokeo ya *public forums* kubeba uhalali katika macho ya jamii na kuepusha mijadala ya hisia ya watu mbalimbali ikiwepo mingine isyo ya busara wala tija.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu mjipange vizuri kuelezea kwa nini huu mchakato wa Muswada umeanza na Rais na kuishia na Rais. Hii ni *social political process* na mwenye dhamana ni Rais na Sheria au Muswada unatusaidia kuiweka sawa chini ya uongozi wa Rais. Dhana inayoletwa na *self appointed spokes persons* au *representative* wa wananchi wasiowajibika kwa yeote, ni muhimu ilelezwe na ielewewe vizuri hiyo ya kuwasemea wananchi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. AZZA HILLAL HAMAD:** Mheshimiwa Spika, kwanza nishukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia kwa maandishi katika Wizara hii. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, kuna mambo machache, naomba nishauri sana Mahakama za Mwanzo zitazamwe kwa kiasi kikubwa kwani Mahakimu hawatoshi, vitendea kazi pia hakuna. Majengo yako katika hali mbaya isiyoridhisha. Suala hili linapelekea ucheleweshaji wa kesi na kusababisha rushwa kwa kiasi kikubwa. Chonde chonde naomba sana suala hili militazame, bajeti ijayo iongezwe ili tuweze kuondokana na matatizo haya.

Mheshimiwa Spika, pia suala lingine naomba sana mahabusu za watoto ziwepo ikiwezekana kila Mkoa kuliko kuwachanganya na watu wazima.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuipongeza Wizara ya Katiba na Sheria kwa hotuba ya Waziri kwa mipango mizuri ya kuendeleza Mahakama zetu na kudumisha haki.

Mheshimiwa Spika, naamini Wizara hii inazo changamoto kubwa, lakini Watanzania wanaamini kuwa Serikali yao itawatendea haki. Lakini haki haipatikani kama ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kuna mengi yameongelewa, lakini, Jimbo la Nkenge tuna tatizo la Mahakama ya Mwanzo, tunayo Mahakama ya Mwanzo Tarafa nzima ya Kiziba wakati Kiziba ni kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Mahakama ya Mwanzo ya Buyango, Tarafa ya Kiziba irudishwe, ili kupunguza gherama za usafiri inayofanya wananchi kushindwa. Tarafa ya Kiziba ni kubwa sana ina Kata kumi na Kata ya Gera ni mbali sana na Kata ya Luzinga na Buyango. Kata ya Buyango majengo yapo yanahitaji ukarabati tu.

Mheshimiwa Spika, ni ombi letu kubwa na hili linafanya wananchi kuichuklia Serikali yao. Matokeo wananchi huchukua madaraka mkononi na kusababisha magomvi kati ya jamii.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. SOLEIMAN NASSIB OMAR:** Mheshimiwa Spika, (1) Rushwa katika Mahakama. Kuna rushwa kubwa katika kutoa haki katika ngazi za Mahakama. Mahakimu wengi si waaminifu wanachukua fedha kwa watuhumiwa na kufanya hukumu zisizo na haki.

Mheshimiwa Spika, mfano mzuri, watuhumiwa wa madawa ya kulevyta kutoka Pakistan ambao wamekamatwa na madawa mengi ya kulevyta. Watuhumiwa hao hivi sasa wako nje kwa dhamana, ingawa Kisheria watuhumiwa hawa hawastahiki kupata dhamana na kuwako nje.

Mheshimiwa Spika, hii inaonesha wazi kuwa Mahakimu wanachukua chochote kutoka kwa watuhumiwa na kutoa maamuzi ambayo hayana maslahi kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, tunapendekeza kuwa sheria ziwe ngumu zaidi kwa Mahakimu kukubali dhamana kwa mashtaka mazito kama ya madawa ya kulevyu, ujambazi, mauaji na kadhalika.

**MHE. JEROME D. BWANAUSI:** Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, kwanza, ni kuhusu Mahakama. Napenda kutoa masikitiko yangu kuhusu mwenendo wa huduma za Mahabusu hadi anapohukumiwa hasa katika Jimbo la Lulindi. Hali ilivyo sasa ni kwamba mtendewa kosa, mtuhumiwa akiwa mahabusu na kumsafirisha kipindi chote cha kesi yake na hata pale anapohukumiwa na kwenda gerezani bado anatakiwa atoe fedha ili apelekwe akitumikie kifungo chake na iwapo mshtaki akiwa hana fedha mtuhumiwa huachwa huru. Naomba wakati wa majumuisho Mheshimiwa Waziri anieleze ni hatua gani Wizara yake itachukua ili kuwaondolea kero hii wananchi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuridhishwa na majibu ndiyo nitaunga mkono. Ahsante.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Spika, kuna mrundikano mkubwa wa mahabusu katika Magereza yetu na inatokana na sehemu kubwa ya mwenendo mdogo wa kesi Mahakamani. Hali hiyo inaleta adha kubwa kwa Mahabusu hao. Je, Wizara ina mkakati gani wa ziada wa kuhakikisha hali hiyo inarekebishiwa.

Mheshimiwa Spika, imezuka tabia kwa Polisi baadhi yao katika utendaji wa kazi zao hasa wanapowakamata watuhumiwa wakati mwingine hufungwa bila ya sababu ya msingi. Je, Serikali inajua hivyo na imechukua hatua gani katika kuwaelimisha Askari Polisi ili watende kazi zao kwa mujibu wa sheria?

Mheshimiwa Spika, ipo haja kwa Wizara ya kuzitupia macho Halmashauri za Wilaya katika Kitengo cha Sheria. Mwanasheria aliyeko kwenye Halmashauri haonekani kuwa mtu muhimu; hana kasma, hana usafiri kwa kazi zake na hususan anapokwenda kwenye kesi zilizoshtakiwa kwa Halmashauri na zilizoshtaki. Katika hali hiyo Mwanasheria aliyeko kwenye Halmashauri anajiona yatima wakati kama si umahiri wa Mwanasheria kwenye baadhi ya kesi zinazoshtakiwa Halmashauri zingewajibika kulipa fedha nyngi kwa yule aliyeshtaki. Wathaminiwe na wawezeshwe ili waweze kufanya kazi zao kwa upendo.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2010/2011, walipatikana Mahakimu sita na hudhaniwa kuwa wamekiuka maadili ya kazi yao na wanapelekwa mbele ya Tume ya Utumishi wa Mahakama. Naona hizo taratibu za kuwapata wavunja maadili zitiliwe mkazo kwani idadi ya walioamatwa hao sita hailingani kabisa na malalamiko yaliyoenea nchini juu ya utendaji wa Mahakimu wetu.

Mheshimiwa Spika, kwa kupitia vyombo vyoma habari kuna taarifa kuwa jengo la Mahakama ya Rufaa, aidha, limeshauzwa au litauzwa. Naomba Waziri alithibitishie Bunge hili ukweli ukoje. Kwa maoni yangu itakuwa si vizuri kuliiza jengo hilo kwa kupisha Kilimanjaro Kempinski itanuliwe! Jengo hilo lina historia kubwa au niseme ni la kumbukumbu.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Serikali kila Wilaya pawepo na Ofisi za Mwendesha Mashtaka wa Serikali, ili kusaidia kuharakisha kesi kupelekwa Mahakamani na ili Mahabusu wapungue.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuishauri Serikali itafute mfumo mwingine wa kusikiliza kesi katika Mahakama za Mwanzo na Mahakama za Wilaya ili kupunguza msongamano wa wafungwa Magerezani. Mfano, kesi ya Strauss Kahn ilianza mwaka huu na tayari hukumu imetoka.

Mheshimiwa Spika, iko mifano mingine tunaona katika *program* za dunia nyingine ambazo ziko *fast truck* mfano, Judge Judy Penny (ya USA) inaonesha kuwa inawezekana Mahakama zetu zikafanya kazi kwa mtindo huo na msongamano ukapungua kwa Mahabusu na wafungwa. Kuna tatizo gani mbona ni ngumu kuiga utendaji kazi wa Mahakama za nchi nyingine zinazofanya kazi kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kuja na wazo la kutunga Katiba Mpya. Nashauri zoezi hili lifanyike kwa makini ili kuondoa manung'uniko katika jamii. Naomba Serikali izingatie ratiba ya Katiba kupatikana *by 2014*.

Mheshimiwa Spika, liko tatizo kubwa la sheria kutokufahamika kwa wananchi. Hii ni kwa sababu Bunge likishatunga sheria na Mheshimiwa Rais akathibitisha, sheria hizi zinakaa katika Ofisi za Wakuu wa Wilaya tu, Wakuu wa Wilaya na Makatibu Tawala hawaelekezwi kuzipeleka sheria hizi kwa wananchi. Mkuu wa Wilaya atazitumia tu pale anapoihitaji.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali sheria zitafsiriwe kwa lugha ya Kiswahili, lakini pia Halmashauri ya Wilaya na Makatibu Tawala wa Wilaya wazipeleke kwa wananchi ili wazifahamu.

Mheshimiwa Spika, bado wananchi hawafahamu sheria ya kutokuvuta sigara katika maeneo yenye watu wengi katika mabasi, mikutano na kadhalika. Watu wanavuta sigara mbele ya wananchi wengine jambo ambalo ni hatari sana kwa afya zao kwa sababu ugonjwa wa kansa unaosababishwa na uvutaji wa sigara unaelekeea kuongezeka.

Mheshimiwa Spika, ziko sheria nyingi za wakati wa mkoloni ambazo zinahitaji kurekebishiwa ili ziendane na hali halisi. Mfano, Sheria ya Ndoa, Sheria ya Matunzo ya Mtoto aliyezaliwa na wazazi wasiokuwa na ndoa, (kuna haja pawe na sheria ya *child support*).

Mheshimiwa Spika, sheria ya umri wa mtoto wa kike kuolewa (miaka 15 bado ni mdogo sana), sheria ya kumlinda mwanamke aliyeishi na mwanaume *under one roof* kwa zaidi ya miaka miwili, sheria ya *Parole* ni kwa kiasi gani inasaidia kupunguza wafungwa Magerezani na kadhalika?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Spika, nakupongeza Mheshimiwa Celina Kombani na Ofisi yako kwa kazi kubwa mnazozifanya za ushauri wa kisheria nchini. Pamoja na pongezi hizo nina machache ya kuchangia:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu mchakato wa Katiba mpya. Watanzania walio wengi hawaijui Katiba inayotumika sasa na kwa kupata uhakika wa jambo hili Wizara ijaribu kuititia katika Vyuo vya Elimu ya Juu, *secondary schools* na hata shule za msingi Wizara ifanye uchunguzi katika Ofisi za Serikali na Mashirika ya Umma. Mtagundua kuna watu wanapiga kelele kudai Katiba mpya lakini kilichomo ndani ya Katiba iliyopo sasa haifahamiki kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, nimetembelea baadhi ya Vyuo vya Elimu ya Juu hapa nchini na kugundua hili. Ni vizuri wananchi wakapata elimu kwanza bila kuwa na haraka ya mabadiliko ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, Mahakama zetu za Mwanzo zinasikitisha kwa kuwa na majengo yaliyochakaa kuptita kiasi. Serikali itenye fedha kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama zetu. Ni aibu kwa Mahakama hazina hata *Stationery* za kufanya kazi. Je, ni kweli Serikali inashindwa kutoa fedha za *stationery* kwa Mahakama zetu?

Mheshimiwa Spika, pamoja na majengo machakavu ya Mahakama, Mahakimu ni watu wanaofanya kazi nyeti lakini hawana nyumba za kuishi. Serikali ina mpango gani wa kuwajengea Mahakimu nyumba?

Mheshimiwa Spika, Mahakama zetu za Mwanzo Mahakimu hawatoshelezi. Kadhalika na Mahakama za Wilaya. Serikali iwaajiri Mahakimu na Mawakili wa kutosha ili wananchi waweze kupata haki zao katika Mahakama zetu kwa muda muafaka.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja ilioletwa mbele yetu na Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuunga mkono hoja, naomba nami nichangie hoja kama ifuatavyo:-

Utoaji wa haki kwa Wananchi wa Tanzania kwa Mikoa na Wilaya zote; inasikitisha sana kwamba, katika Wilaya yote Mpya ya Kalambo na Jimbo la Kalambo, lenye jumla ya Kata 17, hakuna Mahakama hata moja inayofanya kazi.

Mheshimiwa Spika, siku za nyuma kulikuwa na Mahakama katika Kata na Vijiji vifuatavyo; Mwimbi, Mwazye, Matai na Kasanga. Mahakama hizi za Mwanzo zilikuwa zikifanya kazi zikiwa na Hakimu mmoja kila Mahakama.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya sana, hata Mahakimu waliokuwa katika Mahakama tajwa, hakuna hata mmoja ambaye yupo na hivyo hakuna huduma ya utoaji haki kwa Wilaya Mpya yote ya Kalambo, lenye Kata 17.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kutambua upungufu wa watumishi katika Kanda hii, haivumilliki Wilaya nzima kutokana na huduma hii muhimu kwa Wananchi na hasa ukizingatia kwamba, kuna uwezekano mkubwa wa kutumia Mahakimu wa kutoka Sumbawanga Mjini walau mara mbili kwa wiki kabla ya kuwahamisha kwenye vituo hivi.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, naomba niipongeze Hotuba ya Waziri na pia utendaji kazi wa Watumishi katika Wizara hii, tukianza na Waziri na wengine wote.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe mchango wangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri anisaidie kuiuliza Serikali ni lini itaongeza fungu la Bajeti ya Wizara hii ili kukidhi haja ya matumizi ya Wizara hii; kwani hata ukiangalia mahali pengi pa kazi wanapofanya kazi Mahakimu wetu na Majaji si pa heshima kama hadhi walizo nazo. Mahakama nydingi zipo hoi, zimekwisha, miaka hamsini ya Uhuru bado Mahakama zetu (majengo) ni aibu hata kusema. Je, ni lini Serikali itaondoa aibu hiyo ya uchakavu wa Mahakama nydingi hasa ukianzia Mkoa wa Singida mfano Mahakama ya Igugumo na kadhalika?

Mheshimiwa Spika, pamoja na ubovu wa majengo ya Mahakama, nyumba wanazoishi Mahakimu wetu ni aibu! Jamani, mtu anatoa hukumu kubwa na bado anakwenda kuishi kwenye nyumba ya kupanga tena ya ajabu! Kwa nini tusitumie Shirika la Nyumba lijenge nyumba za watumishi hawa nchi nzima na Mahakama aidha mpange au mnunue kwa kudhaminiwa na Benki?

Mheshimiwa Spika, pia wapatieni Mahakimu usafiri wa uhakika hata kwa kuwakopesha; ni hatari kwao kushirikiana usafiri na watu ambao ndiyo kwanza ametoka kumhukumu ndugu yao.

Mheshimiwa Spika, je, kuna nini juu ya Jengo la Mahakama ya Rufaa kwani nasikia linapigwa mnada; kulikoni? Kwanza, naomba nitoe ushauri wangu; hayo yote ni sawa na ninajua Wizara ya Ujenzi ndiyo yenye dhamana na jengo lile; hivyo, kama linauzwa ama haliuzwi sidhani kama watu wa Mahakama ya Rufaa wanahuusika. Cha msingi, nashauri wao wapatiwe jengo lao, tena jipya na lenye hadhi illi kuwaondolea adha hii. Je, Serikali inatoa neno au tamko gani juu ya hili yaani jengo jipya la Mahakama ya Rufaa?

Mheshimiwa Spika, tatizo la ucheleweshwaji wa kesi za mirathi ni kubwa na linaumiza watoto walioachwa na wazazi wao. Je, Serikali ina mkakati gani wa kututua jambo hili? Je, Serikali itakubaliana nami kwamba kama aliyeua anawekewa wakili na Serikali; kwa nini kusiwe na

Mahakama pekee inayoshughulikia kesi za mirathi tu na talaka au kuwe na Wakili pekee anayetetea mali za marehemu kwa faida ya watoto?

Mheshimiwa Spika, kwa nini makosa ya jinai yanawekewa masharti magumu ya dhamana na kesi kuchukua muda mrefu? Mfano, kuna mtu mmoja anaitwa Donat Labila, amekaa mahabusu kwa miaka minne bila kupewa dhamana na alipewa masharti magumu kwamba, wadhamini wawe na nyumba Mkoani Iringa alipo mshtakiwa na kosa lake ni kwamba, aliingiza sukari kwa ajili ya watoto yatima lakini alikamatwa kwa kuuza kinyume na malengo ya *NGO* yake. Sasa kesi haisikilizwi inatajwa tu; kwa nini asihukumiwe kama ana hatia? Familia yake inaumia imesambaratika na hata kama ataonekana hana hatia; je, huo muda wote wa miaka minne ni miteso ya bure tu aliyoyapata; Serikali haioni kwamba kuna Watanzania wengi wanaoteseka kama huyu? Aliwekwa ndani tangu tarehe 13 Julai, 2007 hadi sasa jamani!

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye Wizara yetu ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, pili, nampongeza Waziri, Mheshimiwa Celina Kombani, (Mb), kwa Hotuba yake na hasa kwa kuteuliwa kuiongoza Wizara hii ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Katiba ni Wizara *unique* na nyeti tofauti na Wizara nyingine zote. Ninasema hivyo kwa sababu ni Wizara inayosimamia mhimili mwengine wa Dola, yaani Mahakama. Waziri Kombani, anasimamia Wizara Ilyosheheni Wanasheria, Majaji na Mawakili. Wanasheria wa Taasisi mbalimbali kama vile Tume ya Kurekebisha Sheria, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, *DPP, RITA*, Tume ya Haki za Binadamu, Utawala Bora, Mahakama yenyewe na Divisheni zake, wakati yeche si Mwanasheria. Mheshimiwa Kombani hongera sana kwa kutekeleza majukumu yako vyema.

Mheshimiwa Spika, kuiongoza Wizara hii ni sawa na kuiongoza Taasisi iliyosheheni Maprofesa wakati wewe si Profesa. Lipo kabila moja hapa nchini ambalo wana msemu wao ambaou husema *nshomile until no class ahead*.

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, sasa ninaomba nijielekeze kwenye hoja iliyo mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utajikita kwenye maeneo ambayo ni ya jumla sana (*issue of general nature*), ambayo Mheshimiwa Waziri halazimiki kunijibu mbele ya Bunge lako, ila ni changamoto ambazo Taasisi za Wizara yake zinaweza kuyafanya kazi siku za usoni. Moja, suala zima la Taasisi za Serikali kushindana na kumbana kwenye vyombo vya habari.

Mheshimiwa Spika, vyombo vya habari vimeduwa vikiandika kuhusu kauli tofauti zinazotolewa na Mawaziri wa Serikali hii hii moja, chini ya Rais huyu huyu anayetawala na huyu huyu anayeongoza Baraza la Mawaziri. Jambo hili halina tija hata kidogo, Wananchi wanashindwa kuelewa hali hii kwa nini inatokea.

Mheshimiwa Spika, mimi nina uelewa mdogo kuhusu masuala yahusuyo *ministerial responsibility*, kwa maana kwamba, kama Waziri hakubaliani na Baraza la Mawaziri, anatakiwa ama ajuzulu ili ayaeleze kwa Umma yale ambayo hakubaliani na Baraza la Mawaziri au anyamaze kwa sababu ya utaratibu wa *ministerial responsibility*.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu ni Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni, awaeleze Mawaziri hali hiyo haipendezi hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, nililolieleza linawahusu wanasiasa ambaou ni Mawaziri, lakini pia suala zima la kulumbana kati ya Viongozi lipo pia kwa baadhi ya Watendaji Wakuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukisikia malumbano kama hayo kati ya DPP na Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU kuhusu mafaili ya mashauri ya washtakiwa wa makosa mbalimbali. Wakati Mkuu wa TAKUKURU anavieleza Vyombo vya Habari kuwa faili fulani la shauri fulani lipo kwa DPP, siku inayofuata vyombo vya habari vinaleza kwamba, faili husika halipo kwake.

Mheshimiwa Spika, sasa swalii ni nani kati ya Watendaji hao anaeleza ukweli; DPP au TAKUKURU? Nawasihi sana Viongozi wa Serikali, epukeni kufanya kazi za Serikali na Vyombo vya Habari.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ninataka kulieleza ni hilli; yapo mashauri ambayo yalipelekwa Mahakamani hasa Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani kusikilizwa ama na Jaji mmoja au Majaji watatu katika mashauri yanayohitaji kusikilizwa na kuamuliwa na Jaji mmoja hakuna tatizo, lakini shauri linalohitaji kusikilizwa au kuamuliwa na Majaji watatu hapo lipo tatizo kubwa kweli; kwa sababu inapotokea kuwa si rahisi kuwapata Majaji wote watatu kwa wakati mmoja, shauri husika haliwezi kusikilizwa kila linapotajwa asilani. Matokeo yake inapangiwa tarehe ya kusikilizwa kila linapotajwa ili kuwezesha kupatikana kwa Majaji wote watatu.

Mheshimiwa Spika, utafiti wangu mdogo unaonesha kuwa, mashauri ya Tume hiyo hayafiki mwisho wake kwa wakati unaotarajiwa na Wanasheria wenyewe wanasema *Justice Delayed is Justice Denied*.

Mheshimiwa Spika, katika hili nawashauri kwamba, hali hiyo inayosababishwa na sheria iliyotungwa na Bunge hili; Mheshimiwa Waziri letu Muswada wa Kurekebisha Sheria hiyo ya Majaji watatu ili awe Jaji mmoja kama suala hilo ni la Sheria Ndogo (*Subsidiary Legislation*) zinazotungwa na wewe Mheshimiwa Waziri. Nenda kazibadilishe sheria ndogo hizo, kama suala husika lipo chini ya Jaji Mkuu, basi Mheshimiwa Jaji Mkuu alifanyie kazi ili mashauri husika yasikae muda mrefu yawe yanafikia mwisho katika muda uliopangwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ninaomba nizungumzie suala linalohusu *no objection*, ambayo hutolewa na *World Bank*. Nijuavyo mimi kuhusu eneo hili ni kwamba, Serikali hupata *donor funding* ya Miradi fulani hapa nchini. Fedha hizo zikishapatikana, Serikali huingia makubaliano kati yake na *World Bank* na kwamba, fedha hizo haziwezi kutumika kwa kazi fulani mpaka kwanza hiyo *no objection* ipatikane; na kupatikana kwake ni tatizo la ama kuchelewa kutolewa na *World Bank* au haitolewi kabisa na hivyo kuchelewa kwa Miradi iliyotarajiwa kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili ipo mifano kadhaa ambayo ilikuwa inafadhiliwa chini ya *Legal Section Reform Programme (LSRP)* ama *Business Section Reform Programme (BEST)*, ilichelewa kukamilika au haikutekelezwa kabisa kutokana na kukosekana au kutolewa *no objection* na *World Bank*. Mifano hiyo ni pamoja na kutokamilika kwa ujenzi wa Mahakama za Mwanzo, Mradi ambaa umechukua muda mrefu sana, ambaa ujenzi wake haujaanza mpaka sasa.

Mheshimiwa Spika, tatizo ni nini hapa; ni masharti magumu yanayotolewa na *World Bank* au Sheria ya Ununuzi imeweka mlolongo mrefu katika utekelezaji au uzembe wa baadhi ya Watendaji wetu? Hali hiyo huweza kusababisha kutokutumika kwa fedha zilizotengwa na kazi au huduma zilizotakiwa kufanywa hazifanyiki kabisa.

Mheshimiwa Spika, kama masharti yanayowekwa na *World Bank* ndiyo yanayochangia kutokpatikana kwa *no objection*, basi maswala hayo yafanyiwe kazi; tatizo ni sheria yetu ya ununuzi basi leteni Muswada wa kuiomba vifungu vilivyochangia tatizo hilo, Bunge letu Tukufu litavifuta mara moja; na kama tatizo ni uzembe wa baadhi ya Watendaji, basi eneo hilo nalo lifanyiwe kazi na wahusika.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, naomba Mheshimiwa Waziri atueleze ni kwa nini sheria nyingi zilizopitwa na wakati haziletwi Bungeni ili zirekebishiwe? Kutorekebishiwa kwa sheria hizo kunasababisha unyanyashaji mkubwa hasa kwa akina mama na watoto kufanyiwa ukatili mkubwa na kunyanyasika.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha wanawake wengi wanafanyiwa vitendo vy a unyanyasaji lakini wanakosa msaada wa kisheria na hasa akina mama wa vijijini.

Mheshimiwa Spika, Wananchi wengi sana wanatenda makosa kwa kukosa uelewa wa sheria tunazozitunga. Sasa nini mkakati wa Serikali kuhusu kuwapatia elimu Wananchi hawa kwa kuwa mara nyingi zinatungwa kwa Lugha ya Kiingereza na zinachapishwa katika magazeti ambayo siyo rahisi Mwananchi wa Kijiji kuzipata kwa sababu kuna wengine hata kusoma na kuandika hawajui?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Spika, nimewahi kumweleza Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Katiba kuhusu uadilifu wa Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo Nguruka. Hakimu huyu ni tazito kimaadili; ana matatizo makubwa ya ulevi wa pombe na kuna habari kuwa ni mvutaji bangi. Mazingira haya yanababisha pengine tabia zingine mbovu za kutembea na wake za watu na unyanyasaji wa raia katika maeneo ya Kata za Nguruka, Mtego na Mganza.

Niliwasiliana na Hakimu Mkazi, Mheshimiwa Mrangu, Hakimu wa Wilaya, Mheshimiwa Daud na wote walikubaliana hoja ya kumhamisha atoke Nguruka ili aende Mahakama ya Mwanzo Mjini, ambapo ni karibu na Viongozi wake kama njia ya kupunguza matatizo yake kwani atahofu Viongozi wake. Hii ni kwa kuwa tuna uhaba wa Mahakimu. Naomba kurudia kusitiza kuwa, Hakimu huyu aondolewe pale kwa heshima ya Mahakama na hata usalama wake, kwani wiki chache tu amechomewa nyumba. Tujenge heshima ya Mahakama.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa Jimbo la Kigoma Kusini, ambalo ni Wilaya Mpya ya Uvinza, kuna majengo manne ya Mahakama za Mwanzo, ambayo hayana Hakimu. Majengo haya yapo Kata ya Uvinza, Ilagula, Simbo na Kalya. Kote huko hakuna Hakimu. Mimi kama Mbunge, nipo tayari kutumia Mfuko wa Jimbo kusafisha majengo ya Kata za Simbo na Kalya. Ninaomba kwenye mgawanyo wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo, Mahakama hizi zikumbukwe. Aidha, katika kipindi cha mpito, naomba bajeti ya mafuta na usafiri pale Mahakama ya Hakimu Mkazi longezwe ili baadhi ya Mahakimu wapate nafasi ya kwenda kutoa huduma katika Mahakama hizi hususan maeneo ya Kalya, ambako usafiri pekee ni wa *boat*. Naomba sana muiwezeshe Ofisi hii ya Hakimu Mkazi ili katika kipindi cha mpito, Mahakama hizi zipate huduma.

Mheshimiwa Spika, nashauri kuwa, kutohana na mazingira ya kijirofia ya Mkoa wa Kigoma, upate Mahakama Kuu; umbali kutoka Kigoma mpaka Tabora ni mkubwa mno. Kwa kuwa bajeti bado ni ndogo, nashauri ule utaratibu unaotumika wa Mahakama ya Hakimu Mkazi kushirikiana na Mahakama Kuu ya Kazi, unaweza kutusaidia kipindi cha mpito.

Mheshimiwa Spika, bado kiasi cha bajeti kwa watu hawa ni kidogo mno. Naomba mzingatie katika bajeti zijazo.

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naipongeza Serikali kwa kuona shida ya Wananchi wa Karatu, kufuata huduma ya Mahakama ya Wilaya mpaka Monduli na kujenga Mahakama ya Wilaya Karatu. La ajabu na kushangaza ni kwamba, Mahakama ya Wilaya Karatu ilipangiwa Hakimu ambaye alikaa hapo na hatimaye kuambiwa kuwa amestaafu bila ya huduma ya Mahakama ya Wilaya kutolewa.

Mheshimiwa Spika, amepangwa Hakimu mwingine tena lakini bado huduma haitolewi hapo. Mheshimiwa Waziri atakumbuka kwamba, nilimshirikisha tazito hilo. Kisingizio ikiwa ni samani, akaahidi kufuatilia na shilingi milioni thelathini zimetumwa Kanda ya Kaskazini.

Je, ni lini Mahakama ya Wilaya ya Karatu itaanza kufanya kazi ili kuwaondolea adha Wananchi wa Karatu? Naomba jibu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, ili haki iweze kutendeka, napenda Wananchi wapewe nafasi ya kuwa na watu wa kuwasaidia kisheria (mawakili) wa Serikali na vituo vyake ili kuwasaidia kisheria maana

si Wananchi wote wenye uwezo wa kufahamu sheria. Pia hili litaondoa mlundikano wa kesi Mahakama ya Wilaya. Naomba hili lifanyiwe kazi na Serikali.

**MHE. JOSEPHINE TABITHA CHAGULLA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijali afya njema, kuweza kupata nafasi ya kuchangia kwa maandishi Hotuba hii iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, aidha, naomba nimpongeze sana Waziri wa Sheria, kwa Hotuba yake nzuri aliyoivasilisha leo hii. Pia ninawapongeza sana Watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, katika kuchangia kwangu, nitajikita zaidi upande wa Mahakama ya Mwanzo.

Mheshimiwa Spika, Mahakama za Mwanzo zinasikitisha sana, kutokana na kuwa na hali ya chini sana hasa majengo yake.

Mheshimiwa Spika, hali ya Mahakama zetu inatisha; majengo yamebomoka; hawana *furniture* na Mahakimu ndiyo usiseme hali zao siyo nzuri kabisa.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iboreshe ofisi hizo za Mahakama ya Mwanzo. Pia Mahakimu waongezewe mishahara yao pamoja na posho ili waweze kufanya kazi katika mazingira mazuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo: Changamoto katika Jimbo la Bukombe; suala la Katiba; na matumizi ya Kiswahili katika Sheria.

Mheshimiwa Spika, changamoto katika Jimbo la Bukombe: Katika Jimbo la Bukombe kama ilivyo katika maeneo mengine nchini, kuna matatizo yafuatayo ambayo yanaonesha kuwa, haki za binadamu na misingi ya Utawala Bora havizingatiwi: Polisi kuwabambikizia kesi Wananchi na kutozingatia taratibu na kanuni zinazohusu namna ya kumtendea mahabusu.

Mheshimiwa Spika, tatizo la kwanza linalojitokeza kwa baadhi ya Polisi linachangiwa kwa kiasi fulani na utaratibu uliopo wa Polisi kuandika maeleo ya mtuhumiwa badala ya mtuhumiwa kujandikia maeleo. Tatizo la pili linatokana na utamaduni wa Polisi hasa walio katika maeneo ya pembezoni, kutozingatia haki za mahabusu. Mahabusu huteswa na kunyanyaswa kwa njia mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, matatizo hayo ambayo pia yapo katika sehemu nyingine nchini, yanapaswa kushughulikiwa kwa Programu Kabambe ya Elimu kwa Wananchi ili wafahamu haki zao na wajibu wao na namna ya kutetea haki zao. Kadhalika, Programu Kabambe ya kuwafunza Polisi nchini kote misingi ya Utawala Bora na haki za raia inapaswa kuendeshwa. Bila kufanya hivyo, haki za raia zitaendelea kupuuzwa.

Mheshimiwa Spika, swal kwa Waziri; katika Kitabu cha Hotuba, ukurasa wa 37 – 38, Waziri anataja mafunzo yanayozingatia haki za binadamu kwa Maafisa na Askari wakati wakitekeleza majukumu yao, ambayo yameendeshwa katika kipindi cha 2010/11. Kwa bahati mbaya, mafunzo hayo yalifanyika kwa Maafisa 260 tu. Je, Maafisa waliobaki watapata mafunzo lini ili kuboresha uzingatiaji wa haki za binadamu? Je, mafunzo kwa Wananchi kuhusu haki zao za kiraia (wakiwa huru au mahabusu) yatafanyika lini?

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine ni uadilifu wa Mahakama hasa Mahakama za Mwanzo Bukombe na mlundikano wa kesi zinazopigwa tarehe mara kwa mara. Suala la uadilifu wa Mahakimu ni gumu na limeendelea kuwasumbua sana Wananchi. Jinsi kesi zinavyoendelea kupigwa tarehe, ndivyo Wananchi wanavyozidi kukata tamaa kuhusu kupata haki yao.

Mheshimiwa Spika, je, kuna mkakati gani wa kuboresha uadilifu wa Mahakama na kuondoa tatizo la mlundikano wa kesi?

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine ni ujenzi na ukarabati wa majengo ya Mahakama ya Mwanzo. Majengo yaliyopo Ushirombo na Runzewe, yanahitaji kukarabitiwa kwani ni ya kale mno. Jambo la mwisho ni majengo kwa ajili ya Watumishi wa Mahakama.

Mheshimiwa Spika, Serikali inapaswa kuwa makini sana katika kuandaa Muswada wa Sheria itakayoongoza uandaaji wa Katiba Mpya. Marekebisho yanayoonekana katika nakala iliyosambazwa hivi karibuni, hayakugusa masuala muhimu yaliyojadiliwa na wadau mbalimbali katika Mikutano ya Dar es Salaam, Zanzibar na Dodoma. Masuala ambayo lazima yazingatiwe na ambayo yalisisitizwa katika mijadala ni pamoja na madaraka ya Rais katika mchakato ni makubwa mno; asasi za kisiasa zishiriki kikamilifu; na Watumishi Serikalini wasishiriki.

Mheshimiwa Spika, maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu masuala hayo yazingatiwe.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwisha shauri katika michango yangu mingine, hakuna sababu kwa nini yafuatayo yaendelee kutumia Lugha ya Kiingereza; Rekodi za shughuli za Mahakama, kuanzia Mahakama ya Wilaya hadi Mahakama ya Rufaa; na Miswada ya Sheria inayoletwa Bungeni. Wizara ijpange vizuri ili mambo hayo yaanze kuandikwa kwa Kiswahili. Kadhalika, sheria zote zinazotumika nchini zitafsiriwe kwa Kiswahili mapema iwezekanavyo.

Je, Wizara itaanza lini kutumia Kiswahili katika kurekodi shughuli za Mahakama zote na Miswada inayoletwa Bunjeni? Je, Sheria zote za Tanzania zitatafsiriwa lini kwa Kiswahili?

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Wizara ya Katiba na Sheria ni roho ya nchi katika kuleta usawa, kutoa haki na maelewano katika nchi. Kwa muda mrefu sasa, Watanzania walio wengi hasa waishio vijiji wanashindwa kupata haki zao kwa kutokujua sheria ama kukosa utetezi mara wanapopatwa na mashtaka kutokana na uwezo wao mdogo wa kifedha kuweza kulipa mawakili wa utetezi wa kesi zinazowakabili.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Wizara hii iwe na mpango wa kudumu wa kutoa elimu ya Katiba. Pia ninalomba Wizara ya Elimu iweke somo la Katiba katika shule zetu litakaloeleza na kufundisha Sheria za Nchi kuanzia shule za msingi hadi vyuoni ili kuwezesha kila mtoto, raia wa Tanzania kujua sheria za nchi.

Mheshimiwa Spika, uvunjaji wa haki za binadamu unaendelea kwa kiasi kikubwa katika jamii hasa vijijini; hii inatokana na watu wengi kutojua sheria ama mila na desturi ambazo jamii inayopatwa na mikasa hiyo, huona ni aibu kusema au mila haziruhusu. Kibaya zaidi, kundi kubwa linalovunjwa haki hizo ni watoto wadogo; hivyo basi, upo umuhimu mkubwa wa elimu kutolewa mashulenji hasa shule za msingi. Ninaomba Waziri aje na mkakati wa kukomesha hayo.

Mheshimiwa Spika, Katiba Mpya kwa sasa haiepukiki; na kwa kuwa Serikali imeanzisha mchakato wa kuandika Katiba Mpya ya nchi; ninashauri kuwa, rasimu ya Katiba hiyo iandikwe na makundi ya jamii katika nchi na si kama ilivyo sasa kuwa Rais ndiyo atue Tume akishauriana na Rais wa Zanzibar. Ikumbukwe Katiba ni mkataba wa mtawala na watawaliwa. Hivyo, Wananchi ndiyo wenyewe mamlaka ya mwisho katika kuamua ni vipi wanependa kuongozwa.

Mheshimiwa Spika, Wananchi ndiyo wenyewe kutoa ajira na ndiyo walipa kodi na wamekosa kwa miaka mingi kupata Katiba. Imedhihirika kuwa Katiba iliyopo sasa Wananchi wengi hawalelewi kwa kuwa hawakushiriki kuiandika na kupelekea kutoijua na kuivunja kila kukicha. Sasa wakati umefika wa kuwashirikisha, kuwaacha waamue wenyewe, waiandike, waielewe na waitekeleze.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nampongezo Waziri kwa Hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia Hotuba hii kwa kuuliza maswali:-

(i) Kwa nini hukumu zinapotolewa Mahakamani nakala za hukumu huchulewa kutolewa kwa watuhumiwa hivyo kukosa fursa za kukata rufaa inapobidi; na je, Serikali inasema nini ili wananchi wasikie?

(ii) Kwa nini mfungwa hupata adhabu ya kufungwa na kufanyishwa kazi nzito zisizo na ujira; na je, Serikali itabadi lini sheria ili wafungwa wanapofanya kazi waweze kulipwa na hatimaye anapomaliza kifungo chake awe na kipato cha kuanzia maisha?

(iii) Je, lini wataajiriwa Mahakimu wa kutosha pia kuwapa nyenzo za kutekeleza majukumu yao kama usafiri na nyumba hasa ngazi ya Wilaya/Kata?

(iv) Rai yangu Wizara iimarishe kusimamia sheria mbalimbali za sekta mtambuka, kwani sheria zinapuuzwa nchi hii na kupoteza maana nzima. Ninaomba Wizara ikemee na kuelimisha Wananchi juu ya sheria mbalimbali.

(v) Kero kubwa ni kesi kutosikilizwa; naomba Wizara ioneshe kumaliza kesi zilizorundikana na watu wapo rumande.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii, kutoa mchango wangu kuhusu Hotuba ya Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Celina Ompeshi Kombani (Mb), aliyoiwasilisha Bungeni ya Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, watoto wengi waliopo katika Mahabusu ya Watoto Upanga, Dar es Salaam, wamefika pale kwa kusingiziwa. Baadhi ya watoto walipohojwa walisema nini kilichosababisha wao kufika katika gereza hilo la watoto; walijibu kwamba, wanaishi na mama wa kambo na mama huyo alihonga Polisi kwa visingizio kwamba watoto hao wameiba nyumbani.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya watoto walioko katika mahabusu hiyo wana umri wa kwenda shule. Mazingira ya mahabusu siyo rafiki kwa watoto, chakula wanachokula siyo chenyе virutubisho vyote vinavyohitajika katika mwili wa mtoto ili aendelee kukua vizuri, watoto wanaendelea kuathirika kisaikolojia.

Mheshimiwa Spika, ningependa kumwuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria; watoto wanatakiwa kukaa mahabusu kwa muda gani? Kwa nini Serikali haisikilizi mashauri hayo ya watoto mapema warudi nyumbani na waweze kuendelea na masomo na maisha yao ya kawaida?

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache, naomba kuwasilisha.

**MHE. JUMA SURURU JUMA:** Mheshimiwa Spika, natoa pongezi na naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, imekuwa ni mazoea kuyaona Majengo ya Mahakama kuwa mabovu sana na ya kizamani, hususan katika Wilaya mbalimbali hapa Tanzania. Aidha, Majengo ya Mahakama ya Kigamboni ni mabovu, magofu na madogo, yaani hayana hadhi tena kuitwa Majengo ya Mahakama. Hivyo, nashauri Wizara ichukue hatua za makusudi za kuyatengeneza Majengo ya Kigamboni.

Mheshimiwa Spika, naishauri Wizara iwaongezee posho maalum Mahakimu wa Vijijini, kwani wamekuwa wakidhalilika kwa kukosa huduma muhimu za maisha yao.

**MHE. CYNTHIA HILDA NGOYE:** Mheshimiwa Spika, naomba kumpongeza Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote, kwa kuandaa Hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mahakama za Mwanzo ni eneo la chini katika ngazi ya Kata au Kijiji na ambacho huchukua jukumu la utoaji haki kwa Wananchi; lakini hizo zimechakaa sana na wala hazifanyiwi matengenezo; je, Wizara imejipanga vipi katika kurekebisha hali hii?

Jambo lingine ni mazingira ya kufanya kazi kwa Mahakamu wa Mahakama za Mwanzo. Serikali iangalie sasa eneo hilo, ikiwa ni pamoja na kuangalia upya malipo ya Wazee wa Mahakama, ambao viwango vya posho yao ni kidogo sana, jambo ambalo linaweza kuathiri utendaji wa kazi na kujenga ushawishi wa kupokea au kudai rushwa.

Mheshimiwa Spika, kuna sheria nyingi za nchi hii zinahitaji usimamizi katika utekelezaji; kwa mfano, Sheria ya Parole, ambayo tulipitisha hapa Bungeni, ililenga kusaidia kupunguza msongamano wa wafungwa Magerezani, lakini hatuoni utekelezaji wake ukifanyika kwa uwazi. Sheria hii ni nzuri na lazima utekelezaji wake uwe wa wazi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi, kuwapongeza Waziri wa Sheria na Katiba, Mheshimiwa Celina Ompeshi Kombani, (Mb); Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Jaji Frederick Mwita Werema (Mb); Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii nzuri na imewasilishwa vyema.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Jaji Fatma Masengi, kwa kazi kubwa aliyofanya ya kujenga Mahakama za Mwanzo ikiwemo Mahakama ya Mwanzo ya Utetmini iliyopo Singida Mjini wakati alipokuwa Mkurugenzi Mkuu wa Mahakama za Mwanzo Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa, Mahakama hii ya Mwanzo ya Utetmini ambayo ni miaka mitatu sasa tangu ilipokamilika ujenzi, ikiwa ni pamoja na nyumba ya Hakimu na ya Karani; napenda Mheshimiwa Celina Kombani, Waziri mwenye dhamana anieleze sababu za msingi ambazo zinafanya Mahakama hii iliyotumia fedha nyingi isifunguliwe ukizingatia Manispaa ya Singida inazo kesi nyingi sana ambazo zinasubiri kusikilizwa. Vilevile anieleze na Wananchi wasikie ni lini itaanza kufanya kazi?

Mheshimiwa Spika, napenda kuitaarifu Serikali kuwa ni zaidi ya miaka minne sasa tangu Serikali ilipotoa ahadi ya kujenga Mahakama Kuu Singida. Jambo linalowashangaza Wananchi wa Singida ni Serikali kukaa kimya, ingawa kila mwaka imekuwa ikitoa ahadi.

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Serikali isiwakatishe tamaa Wananchi wa Singida, kwani walikuwa tayari kuchangia nguvu zao katika ujenzi huu kwa kupeleka mawe, mchanga, kokoto pamoja na mashine za kufyatulia matofali ya kisasa. Ninamwomba Mheshimiwa Celina Kombani, Waziri wa Sheria na Katiba, anieleze mimi na Wananchi wa Mkoa wa Singida kuwa lini ujenzi huu wa Mahakama Kuu ya Singida utaanza ili kuwapunguzia Wananchi wa Singida kutumia gharama kubwa kuja Dodoma kwenye kesi ilipo Mahakama Kuu?

Mheshimiwa Spika, kama sijakosea tuliwahi kupitisha Sheria ya Kutunza Maslahi ya Majaji hapa Bungeni. Napenda kuitaarifu Serikali kuwa, Sheria hii haijatekelezwa ipasavyo kwani mpaka sasa Majaji wanastahili kupatiwa Nyumba za Daraja la A lakini hawapewi na nimeongea nao. Vilevile Majaji wanapaswa kupatiwa watumishi wa ndani lakini hadi leo hawajapewa.

Mheshimiwa Spika, hata suala la matibabu bado halijawa na utaratibu mzuri, kwani wanatibiwa kwa fedha zao ndipo wanakwenda kudai ili Serikali iwarudishie. Je, endapo Mheshimiwa Jaji wakati anaumwa atakuwa hana fedha ukizingatia matibabu mengine yanakuwa na gharama kubwa atafanyaje?

Mheshimiwa Spika, Wananchi walifurahia sana kasi ya Serikali ya kujenga Mahakama za Mwanzo nchini, kwani ilikuwa inaondoa adha ya Kata nyingi ambazo zilikuwa hazina Mahakama za Mwanzo pamoja na kukarabati Mahakama za Mwanzo ambazo majengo yake yalichakaa sana.

Mheshimiwa Spika, napenda kufahamu kwa nini kasi hii imepungua kabisa na Serikali sasa ipo kimya? Tatizo la Mahakama kuwa chache bado lipo pale pale; hivyo, sioni sababu ya kasi hii kupungua na bado zipo Mahakama zingine ambazo zimechakaa sana na majengo kutishia maisha ya watumiaji.

Mheshimiwa Spika, napenda kujua sababu ya kasi ya ujenzi wa Mahakama za Mwanzo kupungua na vilevile ni lini kasi hii inaanza ili kuendelea kuondoa kero ya upungufu wa Mahakama za Mwanzo pamoja na kukarabati zile ambazo zimechakaa kabisa? Mheshimiwa Waziri atoe maelezo wakati wa majumuisho hapo kesho.

Mheshimiwa Spika, kila mwaka nimekuwa nikichangia nikiikumbusha Serikali kuwa, Wilaya ya Iramba haina majengo bali huwa imejibanza kwenye Mahakama ya Mwanzo ya Kiomboi Bomani.

Mheshimiwa Spika, napenda kujua ni lini Serikali itasikia kilio cha Wananchi wa Wilaya ya Iramba ili Hakimu wa Mahakama ya Wilaya aweze kuondoka kwenye Jengo la Mahakama ya Mwanzo na aweze kufanya kazi vizuri na kwa moyo mkunjufu. Ninasubiri maelezo ya Serikali kutoka kwa Waziri mwenye dhamana.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo la Wazee wa Mahakama kulimbikiziwa posho zao, kwani hadi sasa wanadai malimbikizo ya posho zao, utaratibu huu unaweza ukawa chanzo cha rushwa. Ninaomba Serikali iache utaratibu wa kuwakopa Wazee wa Mahakama. Hii itasaidia kuwatia moyo pamoja na kuondoa mianya ya rushwa. Ninaomba Serikali itoe majibu ili Wazee wa Mahakama wapate nguvu mpya ya kazi.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiofichika kuwa, Sheria nyingi zinazolinda maslahi ya wanawake wanapofiya au kuachika au kuzaa nje ya ndoa, zimepitwa na wakati. Ninaomba Serikali ipitie upya Sheria zinazowanyima haki na kuwakandamiza wanawake, watoto na vijana wa kike na wa kiume ili wanawake na watoto wapate haki zao ikiwemo matunzo ya watoto. Vilevile vijana hugandamizwa kwa mambo mengi, ikiwemo kuolewa kwa nguvu na wazee au vijana wa kiume kuolewa na wanaume wenzao. Napenda kujua sheria hizi ni lini zitaanza kufanya kazi na zile ambazo hazijarekebishwa ziletwe Bungeni kurekebishwa?

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kutamka kuwa ninaunga mkono hoja hii, ninategemea nitapewa ufanuzi wa mchango wangu.

**MHE. ANGELAH J. KAIRUKI:** Mheshimiwa Spika, zipo habari kwamba, Jengo la Mahakama ya Rufani linatarajiwu kuvunjwa ili kuwa Maegesho ya Hoteli ya Kempinski. Ningependa Mheshimiwa Waziri atoe maelezo kuhusu ukweli wa jambo hili, kwani Jengo hili lina historia kubwa katika utoaji wa haki nchini na lipo karibu na Mahakama Kuu pamoja na Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako lilipitisha Sheria ya Huduma za Mashtaka Nchini (*NPS*) kwa ajili ya kuwezesha kutenganisha jukumu la upendelesi na mashtaka. Hivi sasa, Mawakili wa Serikali wameanza kuendesha mashauri ya jinai katika ngazi za Mahakama za Wilaya na za Hakimu Wakazi.

Mheshimiwa Spika, ili kutekelezwa kwa Sheria hii, ilipaswa kuwa ni Mamlaka au Taasisi inayojitegemea ya usimamizi wa mashtaka yenye rasilimali watu ya kutosha. Wenzetu wote wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wana mfumo unaofanana.

Mheshimiwa Spika, kukosekana kwa muundo huu, kunapelekea kuwa na upungufu mkubwa wa Mawakili wa Serikali, kwa kuwa ajira na uhamisho ndani ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali hufanya na mwajiri ambaye ni Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ambaye kimsingi, siyo Mkuu wa kazi za mashtaka. Hivi sasa, Wakili akiombwa kuhamia Idara nyingine, anakuwa hana uwezo wa kuzuia uhamisho unaofanywa na Mamlaka Ajiri. Vilevile muundo huu utamwezesha *DPP* kuwa na Naibu *DPP* kama inavyoainishwa kisheria kuliko hivi sasa ambapo kuna Naibu Mkurugenzi.

Mheshimiwa Spika, Serikali itenye fedha za kutosha kwa ajili ya uendeshaji kesi kama vile za *EPA*, Uchaguzi na nyinginezo, kwani zinahitaji mwendelezo na uratibu madhubuti.

Mheshimiwa Spika, uanzishwe Mfuko wa Uendeshaji Mashtaka, yaani *Prosecution Fund*.

Serikali iridhie mpango wa sehemu ya fedha itakayopatikana kwa mali ambayo ni mazalia ya jinai, kutumika kwenye operesheni za kuzuia uhalifu wa biashara haramu ya madawa ya kulevyu na utakasishaji wa fedha haramu kama inavyofanyika katika nchi nyingine zilizofaulu katika zoezi la kukamata mali haramu kama Afrika Kusini na nyinginezo.

Mheshimiwa Spika, Serikali itenye fungu maalumu ili kuwezesha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na Ofisi Pelelezi zingine ili kuhakiki kesi za jinai zilizoko Mahakamani kwa kutembelea Magereza. Hii itasaidia kupunguza idadi ya mahabusu.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, ninampongeza Mheshimiwa Waziri na Timu yake yote, kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, pili, naomba ufanuzi juu ya yafuatayo:-

(i) Mkakati gani umewekwa kumaliza kesi mbalimbali ambazo zina zaidi ya miaka kumi? Je, kesi hizo ni ngapi na kuchelewa kwa hali hii kumesababishwa na nini? Je, falsafa ya *Justice delayed is justice denied* kulikoni?

(ii) Je; ni hatua gani huchukuliwa Mahakimu ambao hutoa hukumu ambazo zinaonekana waziwazi kuwa na upungufu? Kwa mfano, katika kesi za talaka kuwaonea wanawake pale ambapo wananyimwa talaka kwa visingizio wakati wameonesha waume zao wanawaweka katika maisha hatarishi kwa kutokuwa waaminifu?

(iii) Jengo la Mahakama ya Mwanzo Kata ya Muleba lipo katika hali mbaya sana. Je, Wizara ina taratibu gani kutengeneza Jengo hili na mengine ambayo yapo katika hali hiyo inayokatisha tamaa na kuondoa imani? Haki itapatikana!

(iv) Umuhimu wa kumaliza mchakato wa Katiba Mpya ndani ya wakati uko wazi na dhahiri. Je, Wizara imejipanga vipi kuhusu changamoto hii?

**MHE. CHARLES J. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, kuitia maandishi, nachangia Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria, Sekta nyeti katika amani na utulivu wa nchi yetu. Sekta hii inalenga kutoa haki kwa wale ambao haki zao zinaporwa au zinaelekeea kuperwa. Bila haki hakuna amani, bila amani hakuna utulivu, hali ambayo inapelekea kutokuwepo maendeleo na ustawi wa Wananchi.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nikiri kuwa, huduma za Sekta hii zinahitajika sana, lakini bado zinapatikana chini ya kiwango kinachohitajika. Tuna upungufu wa Mahakama za aina zote, tuna upungufu wa Mahakimu, Wanasheria na Washauri wa Kisheria. Hali hii inadhoofisha jitihada za kuona kuwa, kila anayestahili kupata haki anakuwa hivyo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na upungufu huu wa jumla, nachangia kwa kuzungumzia maadili na uadilifu wa Watendaji wa Sekta hii. Sekta hii ambayo ni kimbillio la watu walio wengi, imekumbwa na tatizo la mtazamo hasi toka katika jamii.

Mheshimiwa Spika, Wananchi walio wengi wanaona au wanadhani haki haitendeki, haki inanunuliwa na mhimili wa kutoa haki hautekelezi jukumu lake ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, yamekuwepo mashauri ambayo maamuzi yake yamewaacha walioyakisika wasilelewe kilichotendeka. Wananchi wenye uwezo mdogo kiuchumi, wamekuwa na dhana ya kuwa, hali zao zinawafanya wapoteze haki Mahakamani. Hii inachochewa na matumizi ya wanasheria/mawakili wanaohitaji malipo makubwa huku wanyonge wakikosa msaada wa sheria walipohitaji. Hii ni dalili mbaya inayotuelekeza katika kuamini kuwa, rushwa inatumika kwa kiwango cha hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na upungufu huu makubwa, Serikali kwa upande wake imeonesha upungufu katika kuiweka sawa Sekta hii. Upungufu wa watendaji, nyumba za kuishi watendaji na vyombo vya usafiri ni kasoro kubwa. Udhibiti wa Sekta hii unaendana na matakwa ya kuwapatia Watumishi wa Sekta hii mahitaji hayo hapo juu achilia mbali mshahara mzuri.

Mheshimiwa Spika, pamoja na upungufu nilioutaja hapo juu, ucheleweshaji wa mashauri ni jambo linalotia doa bayaa kazi ya Sekta hii. Tatizo hapa ni yale mashauri ambayo hata wale wasio wasomi wa sheria, wanaona wazi kuwa ucheleweshaji na maamuzi hauna msingi. Tunashauri wadau wakuu wa Sekta katika kujisafisha mbele ya jamii, tatizo kama hili la kuchelewesha maamuzi pasipo sababu ya msingi, likemewe kwa nguvu.

Mheshimiwa Spika, suala lingine linalohitaji jicho la tatu ni Mabaraza ya Mahakama ya Ardhi. Sekta ya Ardhi imekuwa na migogoro inayoongezeka siku hadi siku. Mbali na sababu za ongezeko la mahitaji ya ardhi, maamuzi mabovu nayo yanaongeza chumvi kwenye kidonda. Pendekazo langu ni kuwa, Mabaraza na Mahakama ya Ardhi, viongezewe rasilimali. Hii ni pamoja na Wanasheria ambao taaluma zao na vyombo vinavyowasimamia, vitawafanya angalau watoe maamuzi ya haki.

**MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kutoa pole kwa Familia ya Marehemu Mussa Khamis Silima, aliyekuwa Mbunge wa Baraza la Wawakilishi. Naomba Mwenyezi Mungu, awape nguvu za kuupokea na kuvumilia msiba mkubwa huo. Aidha, namwombea kheri na apate nafuu ya haraka majeruhi huyo aliyepo hospitali, ambaye alikuwa mmojawapo katika mfasara huo.

Mheshimiwa Spika, mfumo wetu wa Sheria na jinsi ambavyo Mhimili wa Mahakama umekuwa ukifanya kazi, bado kuna upungufu mkubwa katika kutoa haki kwa Wananchi hususan wale wenye kipato cha chini. Katika Mhimili huu, kumekuwepo na tofauti ya wazi wazi kati ya walionacho na wasionacho.

Mheshimiwa Spika, katika hali isyo ya kawaida, kumekuwepo na ucheleweshaji wa kesi nydingi na mlundikano mwingi wa kesi hata zile zenye ushahidi wa moja kwa moja. Hii inapelekeea kutoa nafasi kwa mianya ya rushwa na uporwaji wa haki. Mfano wa dhahiri ni katika madai ya kesi za mirathi. Kuna kesi nydingi sana za mirathi na nydingi ni zile zinazohusu wafanyakazi waliokuwa katika sekta rasmi. La kushangaza ni mizunguko mirefu ya kurudisha mirathi hizo ili kupata haki na wakati mwingine utaambiwa baadhi ya nyaraka ni pungufu na hazipo. Inasikitisha kuona mtumishi huyu alikuwa anapata haki na stahili zote, lakini mara baada ya kifo chake, ndio hizo nyaraka au mafaili yanapotea; huyu mtumishi alikuwa ameajiriliwa na nani na mshahara ulikuwa unatoka wapi kama hakuna vielelezo vya kumfanya mtu huyu awe na haki anazopata?

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Serikali iliangularie suala hili kwa umakini sana ili kupunguza namba ya wategemezi na watoto wa mitaani au ombaomba.

Mheshimiwa Spika, aidha, suala la maslahi na marupurupu ya Wafanyakazi wa Idara ya Mahakama yaangaliwe upya. Inasikitisha kuona Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo hawana vyombo vya usafiri, nyumba bora na ofisi nzuri. Hali hii inapelekeea Mahakimu hawa wanapopanga mitaani, wapate vishawishi vya rushwa ili kuweza kukidhi mahitaji yao ya maisha ya kila siku. Hakimu anayeishi mbali na ofisi yake, hawezi kuhudhuria kazini, mathalani, kunapokuwepo hali ya mvua. Hali hii itapelekeea kuwepo kwa mlundikano wa kesi Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika Mahakama nydingi za Mwanzo, kumekuwepo na mpangilio usio mzuri wa majalada ya kesi na hii kupelekeea kupotea kwa kesi mbalimbali kwa kupoteza ushahidi. Napenda kuishauri Serikali kuona umuhimu wa kuwa na watu wenye taaluma za utunzaji wa kumbukumbu kwani bila hivyo, hatutafanikiwa kupunguza kero ya kesi nydingi.

Mheshimiwa Spika, mwisho ni kuhusu malipo ya Wazee wa Mahakama; kumekuwa na madai makubwa ya posho ya Wazee hawa, ambao Sheria inawatambua rasmi kwa kazi wanayoifanya. Wazee hawa wanalipwa posho ndogo sana na kimsingi hawana mshahara. Suala la kujiliza; wazee hawa kwa mtindo wa kulipwa posho ndogo na kwa kucheleweshewa; je, tutawakinga vipi na mdudu mchafu rushwa? Anatoka nyumbani ambako ana wategemezi hajaacha kitu, mtu huyu si malaika wa kuacha familia ikihangainka na asishawishike kuchukua rushwa kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya familia.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Serikali, aidha, wazee hawa wawe ndani ya mfumo rasmi wa utumishi, wapewe haki na stahili muhimu ili waweze kuona kuna Serikali inawathamini na kutambua mchango wao mkubwa katika kutoa uamuzi ambao ni wa haki bila kujali itikadi, jinsia na kipato cha mtu.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa kuiongoza vyema na kuishauri vyema Serikali katika maswala yanayohusu sheria katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, amani ya nchi yetu na ustawi wa watu wetu, inategemea sana uadilifu wa Mahakama ikirishikiana vyema na Jeshi la Polisi. Hata hivyo, katika utendaji wake, Jeshi la Polisi katika baadhi ya maeneo, limeigeuza Mahakama kama idara yake.

Mheshimiwa Spika, ninajenga hoja hii kwa sababu imekuwa jambo la kawaida kwa baadhi ya wapelelezi kutoka katika Jeshi la Polisi kuchelewa kufika Mahakamani na kwa sababu hiyo, kuwafanya Mahakimu kuwasubiri na hivyo kuchelewesha mashauri Mahakamani. Vilevile baadhi ya Polisi wamekuwa wakifanya majadiliano kuhusu dhamana ya watuhumiwa.

Mheshimiwa Spika, jambo hili linaonesha kwamba, kuna mtandao usio rasmi ambao unasihamiwa na baadhi ya wapelelezi na ambao baadhi ya Mahakimu wanafahamu katika kutoa dhamana.

Mheshimiwa Spika, dhamana ni haki ya watuhumiwa, ambao makosa yao hayawazui kupewa dhamana. Nashauri jambo hili lichunguzwe na hatua zichukuliwe.

Mheshimiwa Spika, Katiba yetu inatoa uhuru kwa kila raia hadi hapo sheria inapomtia hatiani. Hivi sasa umezuka mtindo wa Mahakimu kutoa masharti magumu sana ya dhamana. Masharti kama kuwa na wadhamini wawili ambao ni Watumishi wa Serikali na kuwa na hati ya nyumba; ni Wananchi wangapi wanaweza kumudu au ni mkakati tu wa kuwanyima dhamana baadhi ya Wananchi na hivyo kuzijaza mahabusu za nchi yetu bila sababu?

Mheshimiwa Spika, vilevile kuna tabia ya Mahakimu kuahirisha mashauri ya dhamana kwa wiki mbili au zaidi.

Mheshimiwa Spika, hakika huu ni mkakati mwengine wa kutafuta na kushinikiza rushwa, kwani siamini kama ipo sababu ya msingi kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo ningependa kuchangia ni uteuzi wa Majaji na Mahakimu. Kazi ya kutoa haki ni takatifu, inahitaji weledi wa hali ya juu, uadilifu na kadhalika. Nawapongeza sana Majaji na Mahakimu ambao wamekuwa wakitenda haki na kufanya kazi katika hali ngumu sana.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, wapo ambao siyo waadilifu kutokana na tabia zao mbalimbali kama rushwa, ulevi na ucheleweshaji wa mashauri. Mahakama imekuwa ikitipiwa lawama nydingi; nashauri uwazi na umakini uwepo na au uongezwe katika uteuzi wao.

Mheshimiwa Spika, maslahi ya Majaji na Mahakimu wetu kama vile mishahara, posho, nyumba na usafiri ni duni sana. Kwa mfano, Hakimu atapandaje usafiri wa pamoja na kuishi mitaani wakati usafiri huo na maeneo anayoishi anakutana na wale anaowahukumu! Ni vema wapewe usafiri na kujengewa makazi maalumu ili kuwapa ari ya kazi na usalama wao.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchangia kuhusu sheria, *Attorney General's Office (Discharge of Official Duties) Act*.

Mheshimiwa Spika, Sheria hii inawafanya Mawakili wa Serikali hata kama wameajiriwa baada ya kumaliza masomo, kuwa Senior kuliko Mawakili wa Kujitegemea waliodumu katika fani kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, hii siyo sahihi maana hao Mawakili kwa hakika wanaendelea kujifunza kutoka kwa waliovatangulia.

Mheshimiwa Spika, Wananchi wa Rombo, Serikali ya Wilaya na hata Polisi, wanaituhumu Mahakama kwa rushwa, kuwaachia huru watuhumiwa ambao ushahidi unatosheleza kupokea rushwa na kuwanyima watuhumiwa dhamana.

Mheshimiwa Spika, anayetuhumiwa zaidi ni Hakimu Mfawidhi, Mheshimiwa Aziza Temu.

Mheshimiwa Spika, hali hii sasa imewafanya Wananchi kufurika Mahakamani kama shinikizo dhidi ya Mahakama kama iliyotokea tarehe 22 Agosti, 2011 pale ambapo Wananchi zaidi ya 400 na Viongozi wao wa Dini, walipoizingira Mahakama wakidai shilingi milioni 15 zilichangwa ili Hakimu amwachie mtuhumiwa ambaye aliwaingilia watoto sita kinyume cha maumbile. Naomba uchunguzi ufanyike.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naanza kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Celina Kombani, kwa uwasilishaji wake makini na utendaji kazi wake ambao umetukuka. Pia kwa imani na upendo wake mionganoni mwetu kama Wabunge.

Mheshimiwa Spika, pamoja na umakini wa Hotuba hii, naomba nichangie japo kwa ufupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo kubwa sana la maadili kwa Watumishi wa Mahakama zetu hasa Mahakimu. Nadhani ipo haja sasa ya kuweka Sheria ili wafanyiwe *veting* kabla ya kuidhinishwa kufanya kazi hizi ambazo ndiyo msingi halisi wa kusimamia haki kwa Wananchi. Hakika wengine wengi wamekuwa ni mfano mbaya sana kwa jamii hasa kutohana na matendo yao. Naamini kabisa, utaratibu huu utasaidia sana kama ambavyo wenzetu katika nchi nyininge wanavyofanya kama Kenya, Malawi, Marekani na kwingineko.

Mheshimiwa Spika, ili kupunguza msongamano magerezani, ipo haja sasa kwa Serikali kuititia upya adhabu za vifungo na kutoa adhabu mbadala hasa kwa makosa madogo ambayo washtakiwa wanaweza wakatumikia.

Mheshimiwa Spika, pia lipo tatizo kubwa sana katika uendeshaji wa kesi hasa utunzaji na uangalizi wa vithibiti ambapo Wananchi wanapoteza sana thamani ya mali zao kwa kutohifadhiwa vizuri. Nashauri kabla ya shauri kusikilizwa ni vyema Mahakama zianze na kuangalia vithibiti na kuruhusu wahusika wachukue mali zao au la vithaminiwe, viuzwe ili ihifadhiwe fedha badala yake.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali iimarishe Mabaraza ya Ardhi kwa kushirikiana kati ya Wizara ya Sheria na Wizara ya Ardhi, maana chombo hiki ni muhimu sana katika kutoa haki kwa Wananchi hasa wa kima cha chini.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ardhi ipitiwe upya na kutotoa kabisa fursa kwa mgeni yeoyote kupewa ardhi kwa namna yoyote. Pia hata kama ni uwekezaji, basi uwe ni kwa kipindi chenye ukomo unaowiana na uwekezaji na si kwa kuwapa muda mrefu kama inavyofanyika sasa.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Kilwa Kaskazini kuna Mahakama moja ya Mwanzo Miteja na hali yake ni mbaya sana, watumishi pia wanaishi katika mazingira magumu mno kiasi kwamba inasikitisha mno. Umbali uliopo baina ya maeneo ya Jimbo na Mahakama ya Wilaya ni mkubwa mno, ukizingatia ukubwa wa Jimbo na Wilaya. Hivyo, naiomba Serikali sasa ifikirie kuweka japo Mahakama moja katika eneo la Chumo au Kipatimu kwa kushirikiana na Wananchi ambao wapo tayari.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. ABDULSALAAM S. AMER:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa Hotuba yake nzuri.

Mheshimiwa Spika, maoni yangu ni kuwezesha Mahakama za Mwanzo. Katika Jimbo langu kuna matatizo makubwa ya Mahakama za Mwanzo. Katika Kata ya Kisange kuna Mahakama ya Mwanzo inatakiwa kujengwa upya au kutumia gharama kubwa zaidi ili kukarabati, kwani inawagharimu sana Wananchi kama wana kesi.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Mheshimiwa Waziri alipe kipaumbele suala la Mahakama hiyo. Nauli ya kwenda Mikumi na kurudi shilingi 14,000, hapo bado chakula na gharama ya mtuhumiwa ambaye inabidi mlalamikaji alipe kama Polisi anavyotaka.

Mheshimiwa Spika, shukrani.

**MHE. DKT. WILLIAM A. MGIMWA:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, ye ye mwenyewe binafsi, kwa kazi nzuri anayofanya katika Wizara ya Sheria.

Mheshimiwa Spika, takwimu mbalimbali ndani ya Kitabu cha Hotuba chake zinaonesha kwamba, mashauri yaliyofunguliwa kila ngazi ya Mahakama yaliongezeka kuanzia mwaka 2008/2009. Kwa mfano, mwaka 2009/2010, mashauri yaliyofunguliwa katika Mahakama ya Mwanzo yalikuwa 140,095, ambapo mashauri yaliyofunguliwa mwaka 2010/2011 yalikuwa 303,032, ambayo ni nyongeza ya mashauri 162,937. Takwimu hizi ni mara mbili ya mashauri ya mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, tunatakiwa tupewe maelezo nini chanzo au sababu ya ongezeko kubwa namna hii? Nini athari zilizombele yetu na Wizara ina mikakati gani kulikabili tatizo hili?

Mheshimiwa Spika, Serikali inashauriwa kuongeza Bajeti ya Wizara ya Mahakama ili ifanye kazi zake inavyopasa bila kulazimika kuahirisha kesi na mashauri mbalimbali kwa tatizo la ufinyu wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie namna ya kuwakopesha wanafunzi wanaomaliza Chuo Kikuu na kuijunga na *Law School*. Tatizo hili lisipotatuliwa, linaleta hisia za ubaguzi na uonevu kwa wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, Wizara inashauriwa kulifanyia kazi tatizo hili.

**MHE. ZARINA S. MADABIDA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Kwanza, naamba nitoe paongezi kwa Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria na Watendaji wote kwa hotuba nzuri yenye kina na mipango mizuri. Nianze kwa kusema, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo, kumekuwa na mlundikano mkubwa sana wa kesi. Ikumbukwe kwamba *Justice delayed is justice denied*. Hivyo, Wizara ni lazima ifanyie kazi mipango yake ya kuajiri wanasheria wengi ili kuhakikisha kesi na hukumu inapatikana kwa haraka sana.

Mheshimiwa Spika, napongeza mpango wa ujenzi uliopangwa kujenga Mahakama na kuboresha hizi zilizopo. Hivi sasa hali ya Mahakama zetu ni mbaya sana kuanzia majengo, ambayo mengi ni mabovu na ina miundombinu isiyokidhi. Vyoo vya Mahakama ni vibovu sana na vichafu ambayo ni hatari kwa watumishi wa Mahakama hizo.

Mheshimiwa Spika, hizi ni karibu zote za Mkoa wa Dar es Salaam lakini zaidi ya yote ni Makahama ya Hakimu Mkazi Kisutu. Lakini hata vyumba vyaya kufanya kazi na kuhifadhi majalada ni finyu, hivyo kutoa mwanya wa majalada kupotea hovyo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mazingira duni ya Ofisi za Mahakama, lakini pia maslahi ya watumishi ikiwa pamoja na Waendesha Mashitaka na Mahakimu ni mbaya sana. Hii ni pamoja na

mishahara na marupurupu, hawana nyumba za kukaa na kulazimika kutafuta nyumba mitaani. Hivi ni vipi atatoa haki ikiwa mshitakiwa ni baba/mama mwenye nyumba wake? Lakini pia anafikika kirahisi, hivyo kumtia kwenye majoribu ya rushwa kwa kutaka kuboresha maisha yake au hata kulinda maslahi yake. Sambamba na hilo, ni vipi utategemea Hakimu akwee daladala na kuchanganyika na watuhumiwa wake? Siyo tu tunatoa mwanya wa rushwa, lakini pia tunahatarisha maisha ya watumishi hao muhimu.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kabisa kwamba ni lazima Serikali iwapatie watumishi wa Mahakama hususan Mahakimu na waendesha mashitaka nyumba na usafiri hata ikibidi kuwakopesha fedha za kununua magari na kuwalipa posho za mafuta. Kuwe na mkakati na kwa sababu ni suala linalohusu Wizara nyingine ya Ujenzi na Fedha, basi ni lazima kuwe na ukaribu kufanikisha hilo, kwani ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, lugha ya kisheria ni ngumu na inataka mwanasheria kuweza kuieleta vizuri. Hivyo basi, badala ya kuandika sheria kwa lugha ya Kiingereza ambazo hata wasanii wengine hatuelewi, sheria zote zitafsiriwe na kuandikwa kwa lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, kuna sheria nyingi zimepitwa na wakati na zinatakiwa kufanyiwa marekebisho mara kwa mara ili ziendane na wakati. Sheria ambazo zinahitaji kufanyiwa marekebisho ni pamoja na ile ya watoto, Sheria ya Ndoa na Sheria ya Mirathi. Sheria hizi zinaathiri sana haki za watoto na wanawake.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko mengi sana ya rushwa hasa katika Mahakama za chini. Mahakama hizi ndiyo zinazohusu sana wananchi wa kawaida na hivyo, sifa hiyo ya rushwa kuondoa sifa nzuri ya Tanzania kwani hao ni wengi sana au imejengeka kuwa kama huna hela, basi huwezi kupata haki, kwani hii ni potofu na ni hatari kwa usalama wa nchi. Tumeona wananchi wakichukua sheria mkononi na kuua vijana wadogo kwa kesi ndogo ndogo kama wizi wa kuku, simu na kadhalika. Hii ni matokeo ya kuchelewesha kesi na pia watu kudhani kuwa akienda Mahakamani atatoa rushwa na kuachiwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba tena nipongeze hotuba hii na naunga mkono hoja.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Spika, pongozi nyingi kwa Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu, Jaji Mkuu na watendaji wote katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshuru sana Ndugu J. Suzan - Mtendaji Mkuu wa Tume kwa kupeleka watu wake Mbanga na kufanya Semina ya kuelimisha Wanambinga.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa Mahakama za Mwanzo, vijiji vingi havina majengo ya Mahakama na hivyo wananchi wengi kulazimika kutembea mwendo mrefu kufuata huduma hiyo. Lakini hata pale panapokuwa na jengo kama katika Kijiji cha Ruanda, Hakimu hayupo.

Mheshimiwa Spika, kipindi hiki Kata kumi zimeongezeka katika Jimbo na Tarafa mpya tatu Ni wazi kwamba huduma hizi zitahitajika zaidi. Naiomba Serikali itambue maeneo hayo na kuweka mpango wa kujenga Mahakama hizo.

Mheshimiwa Spika, wapo vijana wengi wanehitimu sheria, lakini bado hawajapata ajira mpaka leo huku tukiwa na upungufu mkubwa wa watalaan katika Mahakama zetu.

Mheshimiwa Spika, nashauri kwamba Sheria zitungwe kwa lugha ya Kiswahili. Sheria zetu zinatungwa zikiwa kwenye lugha ya Kiingereza. Huu ni utaratibu mzuri tukizingatia kwamba wananchi wetu wengi hawajui lugha hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhuru *RITA*, napendekeza kubuni utaratibu mzuri wa kuandikisha vizazi na vifo. Kwa mfano, mama anaporudi na mtoto toka hospitali, arudi na cheti chake. Hamasa maalum itolewe kwa Wenyeviti wa Mitaa/Kijiji ili ahakikishe kuwa watoto wanaandikishwa na vifo vyote vinaandikishwa pia.

Mheshimiwa Spika, zipo taarifa kuwa watoto chini ya miaka 18 wamefungwa katika jela za wakubwa. Ni vyema Wizara iwe na mpango wa kupata taarifa za watu wanaofungwa kila wiki ili kubaini ukiukwaji huu ikiwa ni kufanya ukaguzi wa kushtukiza katika magereza mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhehebu ya dini mbalimbali yashirikishwe na yahamasishwe kutembelea majengo yote hasa ya watoto ili kutoa ushauri nasaha kwa watoto hao.

**MHE. FAKI HAJI MAKAME:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mungu kwa kutujaalia amani na salama kwa siku ya leo, mpaka tukaweza kuhudhuria kikao cha Bunge kinachoendelea.

Mheshimiwa Spika, ninayo maoni machache kuhusu Wizara ya Katiba na Sheria kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 30 wa hotuba hiyo, kumeelezwa habari ya Sheria ya Mirathi. Serikali imejitahidi kueleza namna inavyoshughulikia mirathi, Sheria inafafanua namna inavyolinda haki za wanawake na kuahidi kufanya mapitio ya Sheria ya Mirathi ili sheria hiyo iwe bora zaidi. Jitihada hizo zimeghafilika mno katika kuelewa dini za wananchi. Serikali yetu kupitia Katiba ya Jamhuri ya Muungano, inaruhusu wananchi wake kuamini dini wanazotaka kwa uhuru wao (Katiba Uk.24, ibara ya 19 (4). Kwa uhuru huu wa Kikatiba ni kosa kubwa wananchi wote kuwahukumu kwa Sheria za Mahakama zisizojali dini zao. Nashauri Serikali iruhusu Mahakama za Kadhi kwa wafuasi wa Dini ya Kisalamu na wale Wakristo na madhehebu mengine, nao waruhusiwe kuwa na Mahakama zinazolingana nao.

Mheshimiwa Spika, Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ukurasa 47, ibara ya 47 sehemu ya pili, inaeleza kuwepo kwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kazi zake (a) – (c). Kwa kuwa Jamhuri hii imeundwa kwa nchi mbili, Tanganyika na Zanzibar zilizokuwa huru. Ni uonevu mkubwa kutozingatia uasili huu kwa kufutwa kwa nafasi ya Makamu wa Rais ambaye ni Rais wa Zanzibar kama ilivyokuwa wakati wa awali wa Serikali hii kabla ya marekebisho yaliyoifuta nafasi hiyo.

Mheshimiwa Spika, ni vyema Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano akawa ni Rais wa Zanzibar, ambaye ni mchaguliwa na ni kauli ya wananchi wa Zanzibar. Sheria zetu hapa zimeleta utata unaodhoofisha utawala bora wa demokrasia.

Mheshimiwa Spika, baada ya maoni hayo kuzingatiwa na Mheshimiwa Waziri na kuchukuliwa hatua za kutayarisha Miswada ya Marekebisho, nitaunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, vile vile mapendeleko yangu wakati wa kupitisha sheria za nchi hii, theluthi mbili za idadi ya Watanganyika na theluthi mbili za Wazanzibar ni lazima zikubali au zikatae, ndipo maamuzi yafanyike. Hivyo, na kura yoyote ya maoni ni vyema kuzingatia theluthi mbili ya wapiga kura.

Mheshimiwa Spika, kama hoja hizi na mapendeleko hayo yatazingatiwa nitaunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. SALVATORY N. MACHEMLI:** Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kuongeza pesa kwenye Wizara ya Katiba na Sheria kwani ufinyu wa Bajeti ya Wizara husika unaifanya Wizara hasa Idara ya Mahakama kushindwa kutenda kazi kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, Rais aondolewe Madaraka hasa ya kuteua Majaji kwani unawafanya Watendaji hao kutokuwa huru katika maamuzi ya kiutendaji.

Mheshimiwa Spika, kuwaondoa Wakuu wa Mikoa na Wilaya kwenye Bodi za Mahakama kwa Watendaji hawa ni makada wa Chama na ni wawakilishi wa Rais katika maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, iboreshwe miundombinu ya Mahakama hasa Mahakama za Mwanzo ambazo zinafanya kazi katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Spika, Watendaji wa Mahakama hasa za Wilaya na za Mwanzo kuwezeshwa nyenzo za kufanya kazi kama vile pikipiki na magari.

Mheshimiwa Spika, Mahakimu wasikilize kesi kwa wakati ili kuondoa ghasia kwa mahabusu.

**MHE. HIGHNESS S. KIWIA:** Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali itenye fungu la kutosha katika kuboresha miundombinu ya Mahakama zetu, kwani hali ya miundombinu katika Mahakama hizo ni mbaya sana.

Mheshimiwa Spika, kutoptaka na ufinyu wa Bajeti ya Katiba na Sheria, naishauri Serikali ichukue shilingi bilioni 213 zilizo sawa kwenye fungu la *Special Road Construction Project* na kuiingiza katika Wizara ya Katiba na Sheria ili kunusuru hali ya Mahakama na huduma zake kwa ujumla.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hotuba hii kwa kuanzia na uanzishaji wa Katiba Mpya.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete kwa kutangaza uanzishwaji wa Katiba mpya.

Mheshimiwa Spika, kabla ya zoezi hili la uanzishwaji wa Katiba mpya ni vyema Serikali ikaaza kwanza na kutoa elimu kwa wananchi wote mjini na vijiji, kwanza kuilewa Katiba iliyopo sasa na kisha wananchi wabainishe ni kitu gani kinatakiwa kusahihishwa na ni kitu gani kiongezwe.

Mheshimiwa Spika, wananchi katika jambo hili wasishinikizwe juu ya jambo lolote kwa maslahi ya kikundi chochote wala Chama cha Siasa.

Mheshimiwa Spika, wakati tunaanzisha Katiba mpya, nchi yetu inatakiwa kulinda utamaduni wa mwafrika kwa maana ya utamaduni, mila na desturi zetu za kiafrika.

Mheshimiwa Spika, katika mchakato huu lazima tuwe waangalifu tusishinikizwe na matakwa ya Mataifa ya nje, maana nia yao wanataka kutuparaganyisha.

Mheshimiwa Spika, Serikali iongeze ajira kwa Mahakimu wa Mahakama za mwanzo kwani vituo vingi nya Mahakama havina Mahakimu, mfano Jimbo langu la Kwela halina Mahakimu katika Mahakama za Mwanzo katika vituo vifuatavyo: Muze, Illemba, Milepa, Kipeta na Kaengesa pia ni pamoja na makarani.

Mheshimiwa Spika, tunalo tatizo kubwa la ukosefu wa majengo ya Mahakama na nyumba za Watumishi jambo ambalo linafanya Mabaraza ya Mahakama kuendesha Mabaraza katika majengo ya Taasisi nyingine au nyumba za watu binafsi jambo ambalo linafanya Mahakimu wafanye kazi bila kuwa na uhuru ikiwa ni pamoja na kutokuwa na mahali imara pa kutunzia nyaraka za Serikali.

Mheshimiwa Spika, vile vile Mahakimu wanapanga nyumba za watu binafsi jambo ambalo ni hatari kwa maisha yao. Mfano ukosefu wa nyumba za Mahakimu katika vituo vifuatavyo: Mtowisa, Kipeta, Mpui, Laela na Mtowisa.

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo la Mahakimu kutokuwa na vyombo vyaa usafiri kama vile gari na pikipiki. Serikali iwapatie au kuwakopesha Mahakimu vyombo vyaa usafiri.

Mheshimiwa Spika, Sheria zote zilizopo kwa sasa zinaandikwa kwa lugha ya Kiingereza jambo ambalo linafanya wananchi walio wengi kushindwa kuzielewa sheria hizo, hivyo wakati umefika sasa sheria zote ziandikwe kwa lugha ya Kiswahili ili wananchi waweze kuzielewa vizuri.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali ili Mabaraza ya Kata yaweze kufanya kazi vizuri na kwa ufanisi ni vema Serikali ikatoa ajira. Maana makarani wamekuwa wakifanya kazi kwa upendeleo bila kufuata haki kwa kuogopa kuondolewa wakati wowote au kupewa rushwa na kupotosha sheria. Kwa vile hawajaajiriwa wanashindwa kuvumilia kwa kuwa wanakabiliana na kuendesha maisha yao kwa kubangaiza.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa mchango wangu katika hoja hii iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mungu kwa kuweza kunipa uwezo wa kusimama na kutoa mchango katika Bunge letu Tukufu.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana wanawake wa Tanzania kwa ushirikiano wanaonipatia katika utekelezaji wa majukumu yangu ndani ya Bunge na nje ya Bunge. Nawashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nampongeza sana Waziri wa Katiba na Sheria Mheshimiwa Celina Kombani, Katibu Mkuu na wote walioandaa bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Serikali kwa bajeti ya Wizara ambayo imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka toka mwaka 2005/2006 kutoka Sh. 49,929,600/= hadi Shilingi bilioni 138 mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi, naiomba Serikali kuendelea kuongeza fedha kwa sababu Wizara hii katika kipindi hiki cha kuelekea mwaka 2015 itakuwa na kazi kubwa ya kurekebisha Katiba, jukumu la kufanya matengenezo ya Mahakama zetu za mwanzo, kwani zinakabiliwa na tatizo kubwa la uchakavu, jukumu la ujenzi wa majengo ya Mahakama za Mwanzo na ujenzi wa nyumba za Wafanyakazi wa Mahakama.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali iongeze fedha kwa Wizara hii kwani wana majukumu makubwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri iliyofanywa na Serikali yetu chini ya Uongozi wa Rais wetu shupavu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kuhakikisha wanawake wanapata haki zao za msingi, bado zipo baadhi ya sheria ambazo bado zinawakandamiza na kuwabagua wanawake, mfano, Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971. Sheria hii imetoa mwanya kwa mtoto chini ya umri wa miaka 18 kuolewa.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kutambua umuhimu wa mtoto kupata haki zake za msingi ili akue katika maisha bora na kuwa tegemeo kwa Taifa. Mwaka 2009 Bunge lako likatunga Sheria ya Mtoto. Pamoja na kazi nzuri iliyofanywa na Serikali, bado lipo tatizo la kutoeleweka kwa Sheria hii hasa kwa Viongozi wa Vitongoji, Vijiji, Mitaa na Madiwani ambao kwa mujibu wa Sheria hiyo ndiyo wasimamizi wa utekelezaji wa Sheria na wazazi ambao ndio watekelezaji namba moja.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada za Serikali za kuongeza Mahakimu katika Mahakama ya Mwanzo, bado kuna tatizo la uhaba wa Mahakimu.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali ifanye kila linalowezekana ili kuhakikisha inaajiri na kupeleka Mahakimu katika Mahakama za Mwanzo kote nchini ili kuondoa tatizo la ucheleweshaji wa kesi na vile vile kuiingizia hasara Serikali kwa kugharamia Mahakimu wanaosafiri kutoka kituo kimoja kwenda kituo kingine.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Mahakimu sio waaminifu, hupokea rushwa na huchelewesha kesi, hasa kesi za wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Spika, katika mchakato wa Katiba Mpya, nashauri Serikali iandae mazingira yatakayowapa fursa wanawake kutoa maoni yao bila kuingiliwa na wanaume wenye mila na desturi za kutowaruhusu wanawake kuzungumza mbele ya wanaume.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa *RITA* ipeleke elimu na kuhamasisha wananchi kuandika wosia ili kuondoa adha wanayoipata wanawake wajane na watoto pale ambapo baba anakuwa ametangulia mbele ya haki.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ucheleweshaji wa kesi, hasa za miradi mbalimbali kama vile ya barabara, ardhi na mauaji. Serikali ifanye kila linalowezekana ili kuhakikisha, kesi za mirathi na aArdhi zinasikilizwa mapema ili kuondoa adha wanayoipata wanawake wajane na watoto yatima katika mchakato mzima wa usikilizaji wa kesi.

**MHE. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, uchangiaji wangu ni katika suala la Chuo cha Mahakama – Lushoto. Kwanza naipongeza Wizara kwa kazi nzuri ya kushirikiana na Mahakama Kuu katika juhudzi za kuimarisha Chuo cha Mahakama Lushoto.

Mheshimiwa Spika, mambo muhimu ya kuzingatiwa katika kuimarisha Chuo ni ukamilishaji wa ujenzi wa Hosteli. Vijana au wanafunzi wanahangaika sana, wanaishi katika maisha duni ya kupanga vyumba mitaani. Serikali itenye fedha za kumalizia *hostels* zinazojengwa na kuongeza ujenzi wa hosteli mpya zaidi. Ikiwezekana wanafunzi wote wakae chuoni. Chuo hiki ni muhimu sana katika uimarishaji wa haki nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mlundikano wa kesi na mahabusu katika Mahakama na Magereza ni tatizo sugu. Bado tatizo lipo. Serikali ijithidi kuendelea kuweka mikakati ya kurekebisha hali hiyo. Kuwepo na ushirikiano wa mamlaka zote husika kama vile Polisi, Mahakimu na Magereza, idadi ya Mahakimu, Majaji na Mawakili lazima iongezwe katika kumaliza tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, tatizo la rushwa lipo katika Taasisi nyingi nchini zikiwemo Taasisi zilizoko chini ya Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, nashauri Elimu na hatua kali zichukuliwe kwa watumishi wachache wanaoharibu sifa nzuri ya mhimili wa Mahakama.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. Tuchukie rushwa.

**MHE. BERNADETHA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri, Mwanasheria Mkuu, Katibu Mkuu na Wataalam wote kwa kuandaa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara yako kwa maandalizi yanayoendelea ya kuleta Muswada hapa Bungeni utakaoelekeza namna nzuri ya ukusanyaji maoni ya wananchi, nani atahusika na kwa kiwango gani. Ni mategemeo yangu kuwa kabla ya mwisho wa mwaka huu, Muswada huu utakuwa umeletwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kuna upungufu mkubwa sana wa Mahakimu. Hii inasababisha kesi nyingi kutoamuliwa mapema. Mnamo mwaka 2009 kulikuwa na kesi zilizochelewa kuamuliwa kwa miaka hadi miwili ni kesi zipatazo 16,714 Tanzania nzima. Huku ni kuchelewesha haki kutendeka. Ni lini kasi ya kuamua kesi itaongezeka ili haki itendeke kwa wakati?

Mheshimiwa Spika, majengo mengi ya Mahakama za Mwanzo ni mabovu, hayafanyiwi ukarabati. Napenda kujua kwa nini jengo la Mahakama lililo katika Kata ya Katoma, Bukoba Vijiji

halijakarabatiwa? Jengo hili liliangukiwa na mti wakati wa mvua za El-nino, ni miaka mingi imepita, watu na Mahakimu wanaotumia jengo hili maisha yao yako hatarini. Ni lini litakarabatiwa.

Mheshimiwa Spika, ziko Sheria nyingi zinazomnyanyasa mwanamke. Sheria ya Ndoa, Sheria za Mirathi, Sheria za Kimila; wanawake wengi, mashirika yasiyo ya kiserikali na Wabunge wengi wanawake wamekuwa wanauliza, ni lini zitaletwa Bungeni zikarekebishwa ili ziendane na wakati na viondolewe/kurekebishwa vipengele vinavyomnyanyasa/mbagua mwanamke na hasa ukizingatia kuwa sasa tunayo bahati Waziri wa Katiba na Sheria ni mwanamke?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Spika, Wizara ya Katiba na Sheria ndiyo Wizara inayohusika na usimamizi wa haki inayotolewa Mahakamani. Kwa muda mrefu kumekuwepo na kero kubwa sana kwa wananchi, hasa vijiji, kwa ajili ya rushwa katika Mahakama za Mwanzo. Mahakimu wa Mwanzo ni kero kubwa kweli! Wanadai rushwa bila uoga wala huruma. Inaelekea kila mtu mwenye kwenda katika Mahakama hizo anajua ya kuwa bila kutoa chochote, hupati haki na kama unashitakiwa lazima ushindwe kesi.

Mheshimiwa Spika, hata dhamana hupati kama hutoi fedha. Watu wanawekwa jela (rumande) kwa kesi za madai. Lazima Wizara ichukue hatua madhubuti na za haraka kuondoa kero hii. Ni rahisi kuchunguza na kubaini wala rushwa. Fanyeni hivyo na watakaopatikana na hatia wachukuliwe hatua kali.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Waziri wa Katiba na Sheria, Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Watendaji Wakuu wa Wizara na Ofisi ya mwanasheria Mkuu wa Serikali na Taasisi zote zinazosimamia utoaji wa haki.

Mheshimiwa Spika, napenda kufahamu, ni lini ujenzi wa Mahakama Kuu Mkoa wa Mtwara utafanyika? Kwani majengo wanayofanya kazi Mkoa wa Mtwara na Kanda ya Kusini hayana hadhi kabisa, au kwa kuwa Mkoa wa Mtwara ni pembezoni umepangwa kuwa wa mwisho kila kitu?

Mheshimiwa Spika, hali ya Watumishi katika Mahakama zetu kwa kweli ni mbaya sana. Kwa nini msiwapangie kazi moja kwa moja wahitimu wa Sheria kama tunavyofanya kwenye kada za walimu na Sekta ya Afya? Ni aibu kufunga Mahakama wakati Wahitimu wa fani ya Sheria wamejaa tele Mitaani.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Spika, Serikali iliamua itajenga Mahakama ya Mwanzo katika Kata ya Mkomazi toka mwaka 2009 hadi leo haijapata Mahakama.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Korogwe, Mahakama hazina hadhi. Ni lini Mahakama ya Mwanzo ya Korogwe imekuwa kama nyumba ya mtu? Mahakama ya Vugiri, Mahakama ya Bungu, Mahakama ya Mashewa, hakuna, zimefungwa. Ni lini Mahakama hizo zitaanza kazi?

Mheshimiwa Spika, naomba Mahakama ziongezwe Mahakamu katika Wilaya yangu. Hasa za Mahakama za Mwanzo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono kwa asilimia mia moja.

**MHE. VINCENT J. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mungu kwa yote anayokubali yatekelezeke katika nchi yetu, hasa yale yaliyo mema.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa michango yangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Vijana wengi katika nchi wamekuwa wakikamatwa kwa makosa ya uzembe na uzururaji. Hii siyo haki kwa vijana ambao kucha kutwa wanatembea kusaka ajira,

wanakamatwa na kupewa makosa ya uzembe na uzurulaji. Unawezaje kumtathmini mzembe wakati hujampa kazi ambayo amezembea na kumtuhumu mtu kwa kosa la uzembe na uzururaji. Ipo haja ya kuliangalia vizuri sana suala hili kwani vijana wengi wamekuwa na chuki na Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na madai makubwa ya kesi za kubambikwa, na pale inapobainika hakuna hatua yoyote inayochukuliwa na (Polisi) ambao wamekuwa lawamani kutokana na huo ubambikwaji, ningependa kupata majibu ya Serikali juu ya hatua ambazo Serikali imejipanga kuchukua kwa wale ambao wamekuwa na kawaida ya kubambika kesi.

Mheshimiwa Spika, kuna mahabusu wengi sana wanaojikuta wanakuwa Gerezani kwa muda mrefu sana. Ipo haja ya kufidia muda kwa mahabusu aliyekaa muda mrefu Gerezani bila kesi yake kuamuliwa. Pindi kesi yake itakapoamuliwa, basi waangalie muda alioCAA kama Mahabusu, afidiwe na muda wa hukumu ya kifungo.

Mheshimiwa Spika, mfano, kama Mahabusu amekaa miaka nane na siku ya hukumu ikawa ni miaka kumi, basi atumikie miaka miwili gerezani kwa kuwa tayari alikuwa amekaa Gerezani kwa miaka nane.

Mheshimiwa Spika, ikiwa Serikali itazingatia jambo hili, basi kuna uwezekano mkubwa sana wa mlundikano wa kesi mbalimbali kupungua na kesi nydingine kujifuta ikiwemo kupunguza mlundikano wa mahabusu Gerezani.

Mheshimiwa Spika, kupunguza mlundikano wa mahabusu na wafungwa kutapunguza matumizi yasiyo ya lazima ya Serikali kwa kuwa hatutakuwa na fedha nydingi zitumikazo kwa kuwashudumia wafungwa na fedha hizo zitasaidia sana kuongeza vikao vya Mahakama Kuu na Mahakama za chini na hali ya amani baina ya jamii.

Mheshimiwa Spika, napenda kujua ni lini angalau kila Mkoa utakuwa na *Judge* Mkazi kwa ajili ya kesi za Mahakama Kuu na hasa zile za mauaji, ili watu wengi wapewe haki zao au hukumu zao mapema? Ni vizuri kuongeza idadi ya Majaji kuliko kuongeza Mikoa na Wakuu wa Mikoa wakati mahitaji ya huduma za Mahakama Kuu zinahitajika kuliko huduma itolewayo na Wakuu wa Mikoa.

Mheshimiwa Spika, nategemea kupata majibu mapema ni namna gani Serikali imejipanga katika kuongeza majaji katika mwaka huu wa fedha na kama kuna wazo la kuwa na *Judge* mkazi katika kila Mkoa.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kujua, ni lini Katiba mpya itaanza kuchukua nafasi ya kutumika? Kwani kwa kweli hadi sasa sioni hatua zozote zinazoonekana kwa Serikali katika hatua za haraka za kuanza mchakato.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na mhemko wa Tanzania kutaka Katiba mpya mapema kwani hii iliyopo siyo tu imechakaa na haikidhi vigezo ila kwa kukua kwa uelewa wa Watanzania juu ya nchi yao. Sasa wanataka kila mtu ahusike na kuiendesha nchi yake kwa kuweka mchango wake kwa namna gani wangetaka nchi yao iendeshwe.

Mheshimiwa Spika, kuchelewa kwa Serikali kuandika Katiba mpya mapema kunapelekea kupunguza imani kwa wananchi dhidi ya Serikali, kwani kunaonyesha kuwa Katiba iliyopo inaipa mwanya mkubwa wa kutawala vibaya Serikali iliyopo madarakani.

Mheshimiwa Spika, nategemea hatua za Katiba mpya za haraka zitakazomhusisha kila Mtanzania, sasa zitaanza kuchukuliwa na Katiba mpya itaandikwa.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kwanza kabisa kumshukuru Mwenyezi Mungu na wananchi wa Jimbo la Babati Vijiji.

Pia napenda kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete na Mheshimiwa Mizengo K. P. Pinda, kwa kazi kubwa na jitihada ya kuboresha Wizara hii ya Katiba na Sheria. Pia kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kutangaza na kukubali kutunga au kuandaa Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii nyeti na muhimu. Ningependa kuchangia kwanza katika Wizara hii kwa kutoa ushauri kwa Serikali waongeze bajeti ya Wizara hii nyeti ili haki kwa wananchi ipatikane kwa muda muafaka. Pia Wizara iangalie namna ya kuboresha huduma na kuweka vifaa vya kisasa, yaani mtandao na kutumia kompyuta ili huduma bora ipatikane katika Mahakama zetu na ipatikane kwa wakati.

Pia Mahakimu zaidi wangeajiriwa ili huduma isogee Wilayani na katika Kata na Vijiji. Pia kuangalia namna ya kupata Mawakili wa kujitolea au kwa gharama nafuu kwa wananchi wa vijijini wenye uwezo mdogo.

Naomba Serikali kupitia Wizara iangalie namna ya kutupatia Mahakimu wa Mahakama ya mwanzo Babati Vijijini na kukarabati majengo yenye hali mbaya. Pia usafiri wa Mahakimu wetu vijijini na fedha ya kuendesha Mabaraza yetu ya mwanzo.

Pia naomba Serikali iangalie na kuweka mpango wa kujenga Mahakama ya Wilaya ya Babati na Mkoa wa Manyara. Jengo la sasa ni la Taasisi ya Jumuiya ya Vijana na siyo vizuri kuendelea kutumia jengo hilo na pia namna ya kukarabati unakuwa mgumu.

Mheshimiwa Spika, vifaa vya *computer, photocopy* na *printer* zingeongezwa hapo ili kuboresha huduma muhimu.

Mheshimia Spika, *Customer Charter* ya Wizara hii ingewekwa wazi na kutangazwa na wananchi wajulishwe haki zao. Pia nyenzo za kufanya kazi kwa Mahakimu na Watendaji wengine wapatiwe pamoja na usafiri.

Mheshimiwa Spika, nashauri suala la Katiba mpya liwekwe wazi na pasiwe na malalamiko. Wananchi waliokuwa wengi vijijini pia wapatiwe elimu ili waweze kuchangia vizuri na kupata fursa sawa na wengine. Pia naomba Waziri na *team* ya wataalam waje Babati na Mkoani Manyara ili kujiona hali halisi.

Mheshimiwa Spika, mwisho naendelea kuishauri Serikali kwamba Wizara hii ifanye kazi kwa karibu na Wizara ya Mambo ya Ndani na Ardhi ili wananchi wawe na imani zaidi katika kupata haki yao. Elimu bado ni muhimu itolewe kwa wanachi na makundi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, nashukuru na ninaunga mkono hoja.

**MHE. ATHUMAN R. MFUTAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, upungufu wa Mahakama za Mwanzo Jimboni Igalula na pia Mahakimu na ukosefu wa Mahakama za Wilaya ya Uyui. Jimbo la Igalula lina upungufu mkubwa wa Mahakama za Mwanzo na ukosefu wa Mahakimu wa kutosha Jimboni na hivyo haki kuchelewa. Wananchi kulalamika sana katika Kata kumi za Jimbo la Igalula. Hakimu wa Igalula pia anahudumia Kata nyingine tano. Vile vile Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo hawana usafiri.

(i) Wilaya ya Uyui haina Hakimu, anatumika wa Tabora Mjini. Washtakiwa inabidi kupelekwa Tabora Mjini. Nashauri kwamba Wilaya iwe na Gereza la Wilaya.

(ii) Majengo ya Mahakama ya Mwanzo yaliyopo yamechakaa, naomba yakarabatiwe na mapya kujengwa.

(iii) Mahakimu wanaishi uraiani na wengine kupanga nyumba za raia. Inawapa wakati mgumu katika kutoa haki. Wasaidiwe.

**MHE. MESHACK J. OPULUKWA:** Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kuharakisha ujenzi na ukamilishwaji wa Mahakama Kuu ya Shinyanga ili wananchi wapate huduma hii muhimu haraka na kwa gharama nafuu, maana kesi zote zinashughulikiwa Tabora na watu wanataabika sana.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na Katibu Mkuu kwa hotuba nzuri na yenyewe mwelekeo chanya.

Pamoja na pongezo hizo, napenda kuelezwaza ucheleweshaji wa kesi nyingi na kuchukua muda mrefu sana: Je, tatzizo ni nini? Hasa ikizingatiwa kwamba wahitimu wa fani ya sheria katika ngazi zote ni wengi sana. Yafaa kero hii ifanyiwe kazi na Wizara ili kuwatendea haki wananchi.

Wilaya ya Kilolo haina Mahakama ya Wilaya, hivyo kulazimu Mahakama ya Wilaya Iringa kuhudumia kesi za Kilolo. Je, ni lini sasa Mahakama ya Wilaya ya Kilolo itajengwa?

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Nkasi ina umri wa miaka zaidi ya 25, lakini haina Mahakama ya Wilaya wala jengo la Mahakama. Jengo liliopo ni bovu sana, halifai kabisa na Hakimu huwa anatoka Sumbawanga siku anayotaka. Huwa mfano anapanga tarehe 5/2 wananchi wote huwa wanakuja toka sehemu za mbali mfano toka *KLM* mpaka 150 wanakuja kwa shida kwa gharama zao. Cha ajabu, Hakimu hatokei kabisa na kuwa ni usumbufu mkubwa sana kwa wananchi wa Wilaya ya Nkasi. Naoma Wizara yako ifikirie sana Wilaya ya Nkasi kuwa na Hakimu wa Wilaya mwenye makazi yake Namanyere.

Mheshimiwa Spika, Namanyere ni Makao Makuu ya Wilaya, yupo DC Mkurugenzi na Watumishi wote wenye hadhi ya Wilaya ila Hakimu tu. Hii siyo kuwatendea haki. Wakazi wa Wilaya ya Nkasi wapatao 260,000 wanapata usumbufu isiyokuwa na kifani kutafuta haki zao. Leo tunaadhimisha miaka 50 ya Uhuru Wilaya ya Nkasi haina Hakimu wa Wilaya, mpaka atoke Sumbawanga. Wananchi wanapoteza muda wao, pesa zao na hata haki zao kwa kuogopa gharama ya kusumbuliwa.

Mheshimiwa Spika, tafadhali nataka jibu. Kwa hilo, waonee huruma wananchi wasio kuwa na hatia.

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nimpongeze Waziri, Katibu Mkuu, Wakuu wa Taasisi na Watendaji wote kwa kuandaa Bajeti nzuri na ya Kisayansi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa Wilaya Kondoa ni mionganoni mwa Wilaya za zamani sana, inasikitisha kuwa mpaka mwaka huu 2011 Wilaya haina majengo ya Mahakama. Majengo yanayotumiwa ni mali ya Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa. Matumizi ya majengo ya Halmashauri yanasaababisha Watendaji wa Halmashauri kusongamana katika Ofisi zao, matokeo yakiwa utendaji usio mzuri. Katika jedwali No. 14 – Ukurasa wa 85, inayohusu ujenzi/ukarabati wa Mahakama ambapo haikuonyesha muda/miaka ya utekelezaji, haikuonyesha mpango wa ujenzi wa Mahakama ya Kondoa.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri anapofanya majumuisho alieleze Bunge, Serikali ina mpango gani kuhusiana na ujenzi wa Mahakama hiyo ili majengo yanayotumiwa na Mahakama yarejeshwe Halmashauri ya Wilaya ambapo yanahitajika sana?

**MHE. DKT. SEIF S. RASHID:** Mheshimiwa Spika, naomba nichangie Wizara hii muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nianze kuanza kuhoji “utawala bora” na maamuzi yanayofanya kuthibitisha utawala bora. Tumekuwa tukishuhudia ongezeko kwa maeneo ya utawala na kuongeza mzigo wa uendeshaji wa Serikali na kuendelea kupunguza kasi ya maendeleo ya upatikanaji wa huduma za msingi kwa kila Mtanzania. Utawala unahusisha watu wenye dhamana hiyo na upana au wigo wa utendaji ikiwemo maeneo ya kiutawala kama Mkao, Wilaya, Kata hadi Vijiji. Sijaona taarifa ya manufaa chanya ya ongezeko kubwa linaloendelea la Mikao, Wilaya hadi Kata. Sioni kama ni busara kuendelea kuongeza Mikao na kuongeza mzigo usio na tija.

Mheshimiwa Spika, haki inayocheleweshwa ni sawa na kutokuwepo haki. Naiomba Serikali kuongeza idadi ya Mahakama na kuwezesha usikilizaji wa kesi katika Mahakama za Mwanzo ufanyike katika maeneo ya Kata. Nathibitisha kusema hali ni mbaya sana Wilaya ya Rufiji na ni mategemeo yangu kwamba Serikali, angalau kwa uchache wake itaongeza Hakimu ili wawe wawili ambaye yupo anachoka na anazidiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, suala la uandikishaji wa vizazi na vifo (*RITA*) pamoja na uwepo wake naomba wawe na wawakilishi Watendaji katika ngazi ya Kata ambao watakuwa wanatembelea vijiji kwa ratiba maalum ili waandikishe na kusajili matukio hayo muhimu ya wanaozaliwa na kufariki kwa usahihi zaidi. Wilaya yangu ya Rufiji bado tuna changamoto ya watu kusafiri kwenda Makao Makuu ya Wilaya, kazi ambayo wengi hawafanyi na hivyo kupoteza taarifa na haki ya msingi ya kuandikishwa.

Mheshimiwa Spika, hali ya majengo ya Mahakama ya Wilaya ya Rufiji ni mbaya sana, naiomba Serikali kuongeza juhudzi za kukarabati, kujenga, na kuboresha Mahakama zote zikiwemo zile za Tarafa na Kata.

Mheshimiwa Spika, katika juhudzi za kuanzisha mchakato wa mapitio na kuelekea kuwa na Katiba mpya, tuendelee na zoezi hili kwa makini zaidi na kusoma yote yanayoendelea nje ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kuongeza bajeti ya kuongeza kasi ya uboreshaji wa mhimili Mkuu wa nchi - Mahakama ili iweze kutimiza wajibu wake.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. AMOS G. MAKALLA:** Mheshimiwa Spika, naomba nichangia hoja ya Waziri wa Sheria na Katiba katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Mvomero ni Wilaya mpya na haina Mahakama ya Wilaya. Hivi sasa tumetumia Mahakama ya Hakimu Mkazi Morogoro Vijijini. Nataka kujua Serikali ina mpango gani wa kujenga Mahakama ya Wilaya Mvomero ili kurahisisha usikilizaji wa kesi na kupunguza gharama za wananchi kufuata Mahakama mbali, Morogoro Mjini.

Mheshimiwa Spika, Mahakama za Mwanzo Jimboni Mvomero zipo katika hali mbaya, hazina majengo na samani. Naomba Waziri aelekeze mkakati wa kuboresha Mahakama ya Mwanzo.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko ya ucheleweshaji wa posho za Wazee wa Baraza la Mahakama za Mwanzo na ngazi nyingine. Serikali itamaliza lini tatizo hill?

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. Naunga mkono hoja.

**MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO:** Mheshimiwa Spika, natoa hongera sana kwa Waziri wa Katiba na Sheria, pamoja na wataalam kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, nashauri Mahakama ijipange vizuri ili kwa kutumia fursa ya kusimamia mfuko wake wenyewe watoe kipaumbele kwenye kesi zenye maslahi ya umma. Kesi hizi zisikilizwe na kuamuliwa haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Maadili ya Mahakama ijiiamarishe, ipambane na Mahakimu na Majaji wasiofuta maadili ya kazi zao.

Mheshimiwa Spika, Mahakama iunde Tume yake ndogo yenye watu wataalam wa mipango. Tume hii ya Mipango isaidie Mahakama kupanga mipango yake ya muda mfupi, muda wa katи na mipango ya muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, pia nashauri *Tanzania Law Reform Commission* iwezeshwe ili kupitia sheria zote ambazo zimepitwa na wakati ili kuhuisha sheria hizo.

Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara ijipange kukarabati Mahakama za Mwanzo Kibaye na Dosidosi Wilayani Kiteto na kujenga Mahakama za Mwanzo Ndodo, Matui na Kiperera.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, kwa Wilaya ya Kongwa tunaomba mambo matatu:-

- (i) Idadi ya Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo ni ndogo mno, iongezwe.
- (ii) Mahakama ya mji mdogo Kibaigwa wametenga eneo la kujenga Mahakama ya Mwanzo Kibaigwa. Huu ni mji unaokua kwa haraka na hakuna huduma ya Mahakama na inahitajika mno.
- (iii) Mahakama za Mwanzo za Kongwa ni mbovu, chakavu, kwa hiyo, zinahitaji ukarabati mkubwa huko Kongwa, Mlali, Sagara, Pandambili, Mkoka na Zoissa. Pia zijengwe Mahakama za Mwanzo mpya.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa mchango wangu wa dhati na masikitiko makubwa kwenye hoja hii katika tabia inayofanywa na Jeshi la Polisi, aidha kwa maslahi binafsi au chuki binafsi au kwa kutumiwa na Wanasiasa ili kuwanyima haki Watanzania wanyonge.

Mheshimiwa Spika, kumekithiri tabia ndani ya Jeshi la Polisi kwa Askari Polisi kukamata na kufungulia wananchi kesi za uongo zinazohusu makosa makubwa ya jinai ambayo hayana dhamana kisheria. Kwa masikitiko makubwa, Mkurugenzi wa mashtaka ameshindwa kabisa kutetea na kukemea tabia hii ili kuhakikisha haki inatendeka ili kuweza kuboresha tabia hii inayofinya haki na uhuru wa wanyonge ambaa ni wananchi wengi nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa ripoti ya Tume za Haki za Binadamu ya toleo lililochapishwa Mei, 2005 limeainisha jinsi gani wananchi wa Wilaya za Serengeti Ranya na hasa Tarime wanavyonyanyaswa na Jeshi la Polisi. Cha kusikitisha ni hadi sasa Mkurugenzi wa Mashtaka hajachukua hatua zozote dhidi ya Watendaji wote wa Jeshi la Polisi katika Kanda Maalum ya Ranya na Tarime kwa kufanya unyanyasaji kwa wananchi wa Tarime. Mathalan hadi leo hii Diwani wa CHADEMA katika Kata ya Bumera anaendelea kuteseka Gerezani kwa kosa la kubambikiwa kesi ya mada - Mhe. Tengera Marwa licha ya *nolle prosequi* kadhaa za Mkurugenzi wa Mashtaka.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla wake Jeshi la Polisi limekuwa halitendi haki mathalan hivi majuzi baada ya kifo cha aliyekuwa Diwani wa Kata ya Susuni - Marehemu Felix Horombe. Polisi mara ya kwanza walisema au kukana kabisa tabia za Wanasiasa kutaka kumsakazia ndugu Nicholas Matiko Nkorouh ambaye alikuwa mgombea wa tiketi ya CHADEMA mwaka 2010 kwenye uchaguzi. Kuna hofu ya Chama cha Mapinduzi kuhofu kupoteza Kata ile kwani ni dhahiri wagombea ambaa ni *prominent leader* ni Marehemu Felix na Ndugu Matiko. Naomba kusema au kukiri kuwa Mzee Matiko ni baba yangu mzazi. Inasikitisha CCM walimtuma mtu ili mzee Nicholas Matiko asigombee. Hiyo ilikuwa ni Jumapili. Nami nikawajibu kwamba hiyo itabaki kuwa ni maamuzi ya baba mwenyewe na Katibu Mwenezi wa CCM, Kata ya Susuni, alisikika akisema kuwa CHADEMA hamtashinda ile Kata kwa kuwa mzee Matiko wameshamweka ndani.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha sana kuona haki zinatekwa kwa wananchi na hasa kama wanaweza kuteka haki hii kama baba wa Mbunge, hebu fikiria kwa mnyonge wa kijijini, si ndiyo basi tena! Hebu tutafakari na tuijulize, Tanzania ya leo tunaipeleka wapi? Iwapo Polisi hao hao leo baada ya kusikia Mzee Matiko kuombwa na wananchi kugombea na baada kiongozi wa CCM ndugu Zakaria ambaye ni Katibu Wilayani Tarime kunifuata Dodoma akiwa na mjomba wangu Christopher Mantogo ambaye ni Meya wa Mji mdogo wa Tarime (CCM). Baadaye kuna mzee alisema anachukua fomu usiku huo huo wa saa saba siku ya Jumatatu, Polisi wasiopungua 20 walimkamata baba nyumbani kwake Kijijini Nyabirongo na ni baada ya kumlazimisha mmoja kati ya mtuhumiwa ndugu Mgesi, baada ya kipigo kuwa aseme Mzee Matiko aliwapa fedha Sh.

6,000,000/= alizotoa benki. Cha kujuiliza, walishindwa kuona *statement* ya mzee? Je, walivyosema ana silaha: Je, walihakikisha kuwa mzee ana silaha? Kwani miaka yote mzee hajawahi kumiliki silaha wala kujihusisha na makosa yoyote ya jinai na ni kiongozi wa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mkurugenzi wa Mashitaka na Watendaji wote wanaosimamia haki watende haki mbele za Mungu. Halafu pia naomba sana haki itendeke kwa wale wote waliobambikiwa kesi za kisasa, ile ya Mheshimiwa Mama Tengera na sasa hii ya Mzee Nicholas Matiko Nkorouh, mzee mwenye umri wa zaidi ya miaka 67 na ambaye hana hatua. Pia wapo wengi katika Gereza la Tarime walioonewa, haki itendeke.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. VICK P. KAMATA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kupata nafasi ya kuchangia kwa maandishi katika hotuba hii ya bajeti ya Waziri wa Katiba na Sheria. Kwanza naipongeza sana Serikali kwa kazi nzuri inayofanya. Baada ya pongezi hizo naomba kutoa mchango wangu ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, Kesi za Mirathi zinachelewa sana kwisha kitu ambacho kinaleta mashaka na kukata tamaa kwa wananchi juu ya Serikail yao. Mfano, kuna mama mmoja, jina lake Grace Msekanae, alifiwa na mume wake mwaka 2008 na baada tu ya arobaini alifungua kesi ya mirathi. Amezungushwa Mahakamani muda zaidi ya miaka mitatu. Juzi amekwenda Mahakamani akakuta Jaji aliyekuwa akiendesha kesi yake amehama na sasa kuna Jaji mwininge ambaye anadai kesi hii inabidi ifunguliwe upya maana Jaji wa Mwanzo aliikosea.

Pili, kwa nini Jaji ashindwe kuelewa kile ambacho Jaji mwenzie amekifanya kwa zaidi ya miaka mitatu? Inaumiza sana. Sasa mama huyu amekata tama, hana tena pesa ya kumlipa Wakili na mali alizoachiwa na Marehemu mume wake zinazidi kuteketea kwa kukosa usimamizi wake.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kuchangia ni kuhusu mMawakili wa Serikali. Mimi naomba wapelekwe hadi Wilayani japo mmoja mmoja kila Wilaya ili haki itende na huko!

Mheshimiwa Spika, nashauri wasaidizi wa majaji waboreshewe maslahi yao, kwani ndio wanaofanya kazi kubwa pale Mahakamani na kitendo cha kutopewa mishahara na posho nzuri kinaweza kuendeleza mianya ya kuomba rushwa.

Mheshimiwa Spika, yangu ni hayo. Naunga hoja hii mkono. Ahsante.

**MHE. ABDUL R. MTEKETA:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumpa pongezi Waziri na Idara yake kwa kazi kubwa ya kujenga Taifa letu. Napenda kuchangia katika Wizara hi ya Katiba na Sheria kama ifuatavyo:-

Je, kuna Sheria yoyote ya wafungwa wakiwa gerezani akifanyishwa kazi kulipwa? Kama haipo: Je, unaonaje Wizara yako ikapendekeza kwa utungaji wa Sheria hiyo? Mfungwa anapofungwa muda mrefu na akifanya kazi za uzalishaji hapo gerezani awe analipwa kiasi fulani ili atokapo gerezani awe na pesa kiasi za kujikimu na kumfanya awe na shughuli za kufanya. Naona hayo yanafanya na nchi nyingine duniani.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa namshukuru Mungu aliensiwezesha kuwa hapa Bungeni, na kunipa nafasi ya kuchangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, natoa pongezi nyangi kwako, Naibu Spika, na Wenyeviti wote watatu kwa jinsi mnavyoendesha vikao kwa umakini hapa Bungeni. Natoa pongezi kwa Waziri wa Katiba na Sheria kwa kazi nzuri anayoifanya. Pia natoa pongezi kwa Katibu Mkuu, Watendaji wote wa Wizara kwa kazi wanazozifanya kufanikisha mazuri katika Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kuchangia kuhusu kesi za Mahakamani. Kesi zinachukua muda mrefu kusikilizwa na pia kutoa hukumu. Wafungwa wanapata shida sana, kukaa

magerezani bila kesi zao kusikilizwa. Namwomba Waziri, Mheshimiwa Celina Kombani, jambo hilo aliangalie. Watu wengine wanakaa miaka minge bila ya kusikilizwa na kumalizika kwa kesi zao. Jambo hili liangaliwe.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuhusu mahabusu. Muda unakuwa mrefu mpaka kusikiliza kesi zao angalau kwa mara ya kwanza. Mahabusu zimejaa sana, na pia ukichukulia na ongezeko la watu wa kutoka Somalia na Ethiopia, mara wanapokamatwa kwenye Mikoa yetu, hupelekwa kwenye mahabusu hizi.

Mheshimiwa Spika, nashauri Mheshimiwa Waziri akishirikiana na Wizara nyininge husika waliangalie vizuri, suala hili la Wasomali na Waethiopia, kupita kwenye mipaka na kuingia nchini kwetu, Wizara husika walifanyie kazi.

Mheshimiwa Spika, tatizo la wafungwa na mahabusu kukaa sana gerezani, ni kwa sababu kesi zao zinachukua muda mrefu kusikilizwa. Nashauri Waheshimiwa Majaji na Mahakimu waongeze kasi na kusikiliza kesi na kuzimaliza kwa wakati. Jambo hili, litapunguza mlundikano wa kesi na wafungwa magerezani/mahabusu.

Mheshimiwa Spika, pia ni vizuri kuziangalia magereza zetu, zile ambazo majengo yamechakaa yaweze kukarabatiwa. Ingawaje hili inaweza ikawa ni suala la Wizara ya Mambo ya Ndani, lakini wafungwa/mahabusu wanaolala kwenye gereza hizi wanatuhumiwa na kesi zinazohusu Wizara hii ya Katiba na Sheria. Kwa hiyo, naishauri Wizara kwamba washirikiane katika kutatua mambo mbalimbali yanayohusu Wizara hizi.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu kwa Serikali, kwani wahitimu wa Sheria hasa katika digrii ya Kwanza na ya pili wameanza kuwa wengi. Tatizo wanapomaliza hawapati kazi mara moja na mahakimu wanahitajika kwa wingi, kufuatana na fani zao. Ningeshauri, uwepo utaratibu maalum wa kuwezesha hawa wahitimu kufanya kazi ya uhakimu, kwani naamini wanawenza, sheria wamefundishwa na kuzifahamu.

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu wafanyakazi wa sheria hasa Majaji na Mahakimu hawatoshi, bado ni wachache na Mahakimu hawatoshi, bado ni wachache. Chuo cha Mahakimu Tanzania ni Chuo cha Lushoto tu. Wahitimu wanaweza kufanya kazi nydingine za kisheria, lakini hasa chuo hiki ni cha Mahakimu, yaani baadhi ya wahitimu wa cheti au stashahada wanakuwa Mahakimu. Chuo kimoja tu na wahitimu kutoka chuo hicho katika fani ya Uhakimu hawatoshi. Mahakama ni nyngi, wafanyakazi hawatoshi, kwa hiyo, mpango wa kuajiri wahitimu wa sheria kutoka vyuo vyetu hapa Tanzania ni muhimu.

Mheshimiwa Spika, Jaji, Hakimu, Wakili ni fani muhimu, Mheshimiwa Waziri naomba/nashauri Wizara ilione. Baadhi ya Mahakimu hawana nyumba, wanapanga. Ni vyema hili jambo liangaliwe kwa undani kusudi wapate/wajengewe nyumba nzuri. Waheshimiwa hawa, kazi wanazozifanya ni ngumu mno, kwa hiyo, ni vizuri kuangalia usalama wao, hasa majumbani kwao.

Mheshimiwa Spika, wakati mwingine kunajitokeza mwanya wa rushwa. Waheshimiwa hawa ni vizuri waangaliwe katika mafao yao, kuanzia mishahara yao wanayopata na mafao mengine kuwa mazuri, ili kupunguza au kukomesha mwanya wa rushwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria ni ndogo. Ingawaje ni tatizo kwa wote, lakini wakati mwingine ni vizuri kupandisha bajeti kidogo, bajeti ya Sh.138,723,956,000/= ni ndogo, haitoshi. Mahakama ni nyngi na wafanyakazi wanaongezeka kidogo kidogo.

Mheshimiwa Spika, nashauri mwaka ujao wa fedha bajeti ipande kukidhi mahitaji. Nashukuru kwa kupata muda wa kuchangia Wizara hii ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, nashukuru na ninaunga mkono hoja.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, watuhumiwa nchini wamekuwa wakiwekwa mahabusu kwa muda mrefu bila kesi zao kusikilizwa. Kumweka mahabusu kwa miaka akisubiria kupelekwa mahakamni ni kumnyima haki yake ya kupewa nafasi mapema ili ajitetee na hatimaye haki itendeke.

Mheshimiwa Spika, hivi ni kwa nini Serikali haichukulii umuhimu kumwezesha mwendesha mashtaka ili aweze kusikiliza kesi nyngi iwezekanavyo hatimaye tupunguze *case logs* yaani mrundikano wa mashauri (*cases*).

Mheshimiwa Spika, ingekuwa vema sasa Serikali izingatie kuwawezesha waendesha mashtaka ili tuwanusuru mahabusu kukaa mahabusu kwa muda mrefu. Naomba kuwasilisha.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu kumekuwa na malalamiko makubwa juu ya madeni wanayochukua mahakama na deni kubwa linatokana na malimbikizo ya deni la pango la Majaji na kufikia bilioni 1.2 hivyo kusababisha Majaji kufukuzwa na kudhalilishwa kwa kushindwa kulipa pango.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha inawapatia Majaji nyumba, ili kuwaondolea adha wanayoipata na kuwawezesha kufanya kazi zao bila kuwa na hofu ya kuondoshwa kwenye nyumba?

Je, Serikali lini itaboresha maslahi ya watumishi wa Mahakama na kuwawezesha kujikimu kimaisha na kuondokana na vishawishi vya rushwa na kuwafanya watimize wajibu wao kwa mujibu wa sheria?

Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kuwawezesha vyombo vya usafiri watumishi wa Mahakama?

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hotuba hii ya Katiba na Sheria nikianza na uhuru wa mahakama.

Katika Ibara ya 107 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaeleza namna gani Mahakama imekuwa ni chombo pekee ya utoaji haki, lakini kupitishwa kwa Sheria ya Utawala wa Mahakama (*The Judiciary Administration Act 2011*) kutasababisha Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa kuingilia shughuli za Mahakama kwani wao ni wanasiasa na ni sehemu ya Serikali (*Executive*) mfano katika kesi ya *R vs Idd Mtegule 1979 LRT* ni moja ya kesi ambazo Mkuu wa Wilaya alilingilia maamuzi ya Hakimu. Napenda kupata majibu kutoka Serikalini kwa nini Sheria hii isipitiwe upya?

Jambo la pili ni kuhusu Rais kuteua Jaji Mkuu, AG, Jaji Kiongozi bila kuhusisha Bunge inaweza kusababisha kutokuwa na uhuru wa mahakama.

Kuhusu elimu ya sheria na mafunzo kwa vitendo, pamoja na utoaji wa mikopo, napenda kupata majibu kutoka Serikalini ni lini wanafunzi wanaosoma sheria kwa vitendo (*School of Law*) wataanza kupatiwa mikopo ikiwa ni pamoja kutengeneza mfumo mmoja wa utoaji elimu yaani kuwa miaka mitatu na mwaka ule wa nne uwewe wa vitendo ili kuwa na uwiano wa masomo na mitaalaa inayowiana kwa nchi nzima?

Mheshimiwa Spika, kuhusu mchakato wa Katiba mpya, napenda kupata majibu kutoka kwa Waziri juu ya mambo yafuatayo; je, kwa nini mchakato huu umekua unalegalega kama vile Serikali haina uhakika na jambo inalolifanya? Pia napenda kupata majibu kwamba ili kupata Katiba nzuri, ni lini Serikali itatoa ratiba ya mchakato mzima kuliko kuendelea na mfumo na utaratibu huu unaolegalega?

Kuhusu Mahakama Maalumu ya Katiba, napenda kupata majibu, Ibara ya 126 ya Katiba inaeleza kwamba kutakuwa Mahakama Maalum ya Katiba yaani *Special Constitutional Court*. Napenda kupata majibu kwa nini mahakama hii haijaundwa tangu mwaka 1977 hadi leo. Je, mnaogopa nini wakati kuna mambo mengi yanayohitaji tafsiri mfano uwepo wa nchi ya Zanzibar,

uwepo na baadhi ya vifungu vya mkataba wa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar wa mwaka 1964.

Mheshimiwa Spika, upungufu wa Mahakama Kuu hasa Kigoma, napenda kupata majibu kutoka Serikalini ni lini kutakuwa na ujenzi wa Mahakama Kuu kwenye kila mkoa. Mfano kutoka Wilayani Kibondo hadi Tabora ni gharama kubwa na wanafanya watu wengi kushindwa kufika mahakamani (*access to justice*) hivyo napenda kujua ni lini Serikali itajenga lini Katiba mikoa yote Tanzania na hasa Kigoma?

Kuhusu Mahakama za Mwanzo na Wilaya, napenda kupata majibu kutoka kwa Serikali kwa kuwa kuna wahitimu wengi wa Sheria, napenda kupata majibu ni lini *Magistrate Court 1984 Act* itafanyiwa marekebisho ili wahitimu hawa waarajiwe Mahakama za Mwanzo ili kupunguza uhaba wa Mahakimu. Naomba kuwalisha.

**MHE. ANNAMARYSTELLA J. MALLAC:** Mheshimiwa Spika, inafahamika wazi kwamba nchi yetu inaongozwa kwa sheria, kanuni na miongozo mbalimbali. Lakini Katiba na Sheria za nchi inaonekana wazi kuwa mianya mingi ya upindishaji wa sheria na kwa sababu Sheria za Tanzania zimekuwa zikishikiliwa na chombo chenye dhamana ya sheria (Mahakama) na kwamba sheria zinaelekezwa kwa wananchi ambao wengi hawazjui sheria.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara kuandaa mpango angalau kwa wananchi waweze hata kufahamu baadhi ya sheria ndogo ndogo hasa za uraia na baadhi ya Sheria ya Manunuzi na Mikataba ya Kibiareshara, Ardhi na Sheria za Utawala.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ukweli wa Watanzania wengi kutokufahamu sheria, ni wazi kuwa kuna baadhi ya Mahakimu Wilayani wamekuwa chanzo cha uvunjaji na upindishwaji wa sheria na hii inatokana na ukithiri wa rushwa na ukiukwaji wa haki za binaadamu.

Naiomba Wizara, kuziagiza Mahakama na Mahakimu kwa ujumla kutupia macho Sheria ambazo daima zinawagusa wananchi moja kwa moja, Sheria za Ndoa na Mirathi, Sheria za Migogoro ya Ardhi na Sheria za Umilikkishwaji Mali. Sheria hizi zimekuwa zikivunjwa vunjwa kwa kuwakandamiza maskini, baadhi ya Mahakimu wamekuwa wa kwanza kupindisha sheria hizi za kuwakandamiza maskini na huwakumbatia wenye pesa, ili wajipatie pesa. Kwa mfano, Wilaya ya Mpanda.

Mheshimiwa Spika, kuna mzee mmoja anaitwa Hamisi Kapani kutoka kijiji cha Milala kilomita sita toka Mpanda Mjini. Mzee huyo na familia yake alikuwa na mashamba yake toka enzi za babu zake ambayo analima na kuyamiliki miaka yote. Lakini miaka mitano sasa anahangaika na kesi kwa shamba lake ambalo alinyang'anywa na kupewa mtu mwingine kwa sababu tu alitoa pesa kumzidi yule mwenye shamba ambaye ni maskini. Baada ya wanakijji wenzake kuja juu kwa kumtetea na kumtolea ushahidi juu ya shamba hilo, maskini mwenye shamba alishinda kesi. Baada ya kushinda kesi, muda mfupi alibambikizwa kesi kuwa amechoma nyumba ya aliyeokuwa anahitaji shamba lile na tayari alihukumiwa kifungo na mpaka sasa yupo gerezani ili asipate muda wa kuendelea kufuatilia shamba lake. Wananchi wamelaani sana kitendo hicho bila mafanikio.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iboreshe mishaahra ya Mahakimu ili ikidhi maisha yao na kwa kufanya hivyo, tutapunguza tamaa kwa hawa Mahakimu na hapo wataweza kutoa haki sawa. Pia naiomba Serikali ikarabati majengo ya Mahakama za Mwanzo ambazo zimechoka na ni za muda mrefu. Je, Serikali ipo tayari kufanya haya ili kupunguza tamaa kwa Mahakimu na wananchi wapate haki wanazostahili?

Kuhusu usimamiaji wa haki za binadamu na utawala bora, majeshi ya nchi yamekuwa ya kwanza kuvunja sheria ya haki za binadamu hususan jeshi la polisi ambalo limekuwa likisababisha mauaji kwa makusudi ya wananchi wasio na hatia kwa ajili ya kutetea tu Serikali, hata kama mahali imekosea. Huo si utawala bora, ni uonevu na utawala mbovu. Jeshi ni mali ya umma na si kazi yake kutetea uovu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu haki na utawala bora ni nguzo katika kuimarisha amani ya nchi. Katika Uchaguzi Mkuu, Tume ya Uchaguzi ilitangaza kuwa uchaguzi utakuwa wa huru na haki, lakini mpaka hivi leo Tume hiyo inayotenda haki hajamtangaza Diwani Viti Maalum Mpanda Mjini kutoka Chama cha CHADEMA, imewatangaza tu Madiwani Viti Maalum wa CCM. Je, ni nini kinachosababisha Diwani Viti Maalum CHADEMA asitangazwe? Ni mwaka sasa unakimbilia kuisha je, atajuaje majukumu yake?

Mheshimiwa Spika, mwisho huo ni utawala bora unaozingatia sheria na haki? Naomba jibu muhimu sana hilo kwa Mheshimwa Waziri. Ahsante sana.

**MHE. ROSWEETER F. KASIKILA:** Mheshimiwa Spika, nchi yetu ni ya utawala wa bora na utawala wa sheria, nchi yetu ina mihimili mitatu, Bunge linalotunga sheria kwa ajili ya wananchi, Mahakama inayotafsiri sheria kwa ajili ya wananchi na Serikali inayotekeleza sheria kwa ajili ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu elimu ya sheria kwa umma, sote tunafahamu kuwa kutokujua sheria siyo kinga (*the ignorance of law is not a defence*) Serikali inayo wajibu wa kuielimisha jamii kuhusu sheria katika ngazi zote za kiutawala Wilaya, Mkoa, Kata, Vijiji, Kitongoji, Mtaa hadi Kaya.

Mhehsimiwa Spika, ili kazi hii ifanyike Serikali iwaajiri Wanasheria hasa katika ngazi ya Kata ambao wataelimisha kwanza Wajumbe wa WDC lakini pia kwa kupitia Watendaji wa Vijiji wataomba kuwa na mikutano ya hadhara na wananchi, hapo sheria mbalimbali sera, haki za binadamu, haki za watoto na kadhalika zitafundishwa.

Mheshimiwa Spika, endapo Serikali itajiri Wanasheria na kuwapangia kazi kwenye Kata, wananchi watajua sheria, wahalifu watapungua, hapatakuwa na mrundikano wa kesi mahakamani, hapatakuwa na wafungwa kwenye magereza, hapatakuwa na Bajeti kubwa kwa Serikali kwa ajili ya dawa, chakula na huduma nyingine kwa wafungwa. Lakini pia ule Mfuko wa Mahakama unaotegemea kuanzishwa utafanya kazi zake vizuri na utafanya kazi kwa *quality assurance* na *cost effectively*.

Mheshimiwa Spika, zipo sheria kandamizi kwa wanawake na watoto. Ni kandamizi kwa sababu kwanza hawazijui na ni vipi wangeweza kudai haki zao wakati sheria hizi hazijulikani. Ni vema Wanasheria hao wa Kata wakawaelimisha wanawake kuhusu sheria hizo. Pia zipitiwe kwani zina mapungufu makubwa, sheria hizo ni kama zifuatazo:-

- (i) Sheria ya Ndoa ya 2002 hata baada ya kufanya mabadiliko ya mwaka 1971;
- (ii) Sheria ya Ardhi ya 1999 ;
- (iii) Sheria ya Ardhi ya Vijiji ya mwaka 1999;
- (iv) Sheria ya SOSPA ya mwaka 1998, unyanyasaji wa kijinsia;
- (v) Sheria ya *Anti-trafficking in person* ya mwaka 2008; na
- (vi) Sheria ya Kimila (*Cultural Policy*) na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kazi nzuri zinafanya kwenye Kata na Maafisa wa Maendeleo, Maafisa Afya, Afisa Kilimo, Afisa Mifugo. Vilevile elimu ya sheria kwa jamii ingetolewa na kusaidia pale wananchi wanapokuwa wanahitaji msaada wa kisheria lakini hawapati.

Mhehsimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA:** Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu sasa Mahakama zetu za Kasulu zimekuwa hazitendi haki ipasavyo kwa wananchi wa Kasulu hata masuala madogo yaliyowazi kama ya dhamana kwa watuhumiwa. Kuna watuhumiwa wengi waliochelewesewa na hata kinyimwa dhamana akiwemo Diwani wa Kata ya Heru Ushingo hali iliyopelekea kusota

mahabusu kwa zaidi ya siku 14 bila ulazima wowote. Hali inaonyesha wazi namna ambavyo Jeshi la Polisi linashirikiana na Mahakama kwa ukaribu zaidi ili kuwadhoofisha wananchi wa Kasulu lakini pia wanaandaa mazingira ya rushwa licha ya kwamba dhamana hutolewa bure na ni haki ya kila raia.

Namuomba Waziri atoe tamko sambamba na maelekezo kwa Jeshi la Polisi na Mahakama ili kukomesha tabia hii mbaya inayoonekana kuwa sugu ili hatimaye wananchi wapate unafuu katika nchi yao iliyo huru.

Mheshimiwa Spika, katika hali ya kutatanisha siku hizi Mahakama zinapoteza umakini katika utendaji wake Mkoani Kigoma. Hii ni kwa sababu kuna Mahakimu ambao bado wanafanya maamuzi kwa kushurutishwa na maslahi yao binafsi. Kuna Hakimu ambaye amehukumu kesi moja kwa kutoa hukumu mbili zinazopingana kufuatia ushawishi na maelekezo ya Mwanasheria wa Halmshauri yaliyopelekea kupindishwa kwa sheria kwani hukumu ya kwanza inampa ushindi raia dhidi ya Halmashauri na hukumu nyingine inamnyima ushindi raia kwa kesi hiyo hiyo moja na muda huo huo hali inayoleta walakini na maswali mengi. Namuomba Waziri atoe ufanuzi na atoe tamko juu ya hakimu huyu ili iwe fundisho kwa mahakimu wengine na turejeshe imani ya wananchi kwa mahakama zao.

Mheshimiwa Spika, imekuwa ikifahamika kwamba askari wanajukumu la kuhakikisha usalama wa raia na mali zao lakini pia polisi ni mahali pa usalama. Lakini hali hii ni kinyume kwa Wilaya ya Kasulu kwani watuhumiwa wengi wanapofikishwa Kituo cha Polisi bila uangalizi wowote huwa wanateswa na kuna taarifa kuwa wengine huwa wanakufa na mbaya zaidi wananchi wanagundua halafu hawaoni hatua zozote dhidi ya askari wanaosababisha ukatili huo.

Mheshimiwa Spika, namuomba Waziri atoe tamko juu ya ukiukwaji wa haki za binadamu na uvunjaji wa sheria unaoweza kuhatarisha amani ya nchi yetu hasa pale wananchi watakapoamua kulipiza kisasi na mimi kama Mbunge sipendi hali hii itokee, hivyo namuomba tena Waziri anieleze kama atakuwa tayari ye ye au watalaam wengine tuambatane nao kwa ushirikiano wa wananchi kubaini ukweli na hatimaye hatua za haraka zichukuliwe.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii. Naomba yafuatayo kwanza ni kuhusu Sheria ya Ndoa na Mirathi zifanyiwe mabadiliko ili kuweza kuwasaidia wanawake wengi ambao wanashindwa kupata haki zao katika masuala yanayohusu mirathi na ndoa. Sheria hizo ziletwe haraka na zifanyiwe mabadiliko.

Mheshimiwa Spika, pili, wazee/washauri wa Mahakama malipo yao ni kidogo sana, ni lini watapatiwa ongezeko la posho ili kuwawezesha kushiriki vizuri katika ushauri wao kwenye Mabaraza ya Kata na Mahakama za Mwanzo?

Mheshimiwa Spika, Mahakama nyingi ni mbovu na maeneo mengine hazijajengwa, tunaomba Bajeti iongezwe ili kusogea shughuli za haki karibu na wananchi.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, nawatakia kila lillio na kheri.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Spika, wafungwa ni watu, wanapewa adhabu mbili kwa kosa moja. Adhabu ya kwanza ni kufungwa au kunyimwa uhuru ya pili ni kazi ngumu Gerezani. Iletwe Sheria humu Bungeni ili wafungwa wapewe adhabu moja kufungwa tu, wakifanya kazi yoyote ngumu au ya kawaida walipwe na fedha hizi wawekewe ili siku wakitoka wapewe.

Mheshimiwa Spika, fedha hii itawawezesha kuacha uhalifu, wakitoka jela na kupata fedha zao huu utakuwa ni mtaji mzuri wa kuanzia maisha na hivyo kuacha uhalifu na kuwa raia wema. Hii hufanyika katika nchi nyingine duniani. Ahsante.

**MHE. ANGELAH J. KAIRUKI:** Mheshimiwa Spika, shukrani. Nashukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ili nami niweze kuchangia kwenye Bajeti ya Wizara hii. Awali ya yote, natoa pongezi kwa

Wizara hii, kwa kazi kubwa wanayoifanya ikiongozwa na Mheshimiwa Kombani, Jaji Mkuu, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wafanyakazi wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo kwa kweli niseme tu kwamba Bajeti iliyotengwa kwa Wizara ni ndogo sana, wana kazi kubwa sana. Huwezi kutenga shilingi 138,723,956,600 kwa ajili ya matumizi kwa kazi kubwa wanazozifanya.

Mheshimiwa Spika, upungufu huu mkubwa wa Bajeti kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, una athari zifuatazo:-

Kwanza, kufukuzwa katika majengo, kwani hivi sasa majengo yanayotumika kwa shughuli za kiofisi kama vile Benjamin Mkapa, *Sukari House, NSSF Bukoba, TTCL (Arusha) NHC* (Shinyanga na Mbeya) ni ya kukodisha na takribani shilingi 1,489,070,000/= katи ya 3,541,330,000/= zitalipia pango ni karibu nusu ya fedha zinazoidhiishwa kwa Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka. Hii itakwamisha shughuli na wananchi watashindwa kuhudumiwa ipasavyo.

Pili, kwa Bajeti hii, Mawakili wa Serikali watashindwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo na watashindwa kuhudhuria mahakamani na itakwamisha mfumo wa uendeshaji wa kesi.

Mheshimiwa Spika, tatu, kutakuwa na kuongezeka kwa mrundikano wa kesi mahakamani na msongamano wa mahabusu na hatimaye kuchelewesha upatikanaji wa haki nchini, nne, mpango wa kutenganisha shughuli za mashtka na upelelezi utakwama.

Tano, tutakuwa na matumizi mabaya ya rasilimali watu ambao watakuwa ofisini bila ya kufanya kazi, hii ni hatari sana na sita, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali itashindwa kuwasomesha watumishi katika maeneo mbalimbali yenye changamoto mpya kama vile uharamia baharini, utakasishaji wa fedha haramu, wizi kupitia mitandao ya kompyuta na maeneo mengine kama vile majadiliano ya mikataba, uandishi wa mikataba na uandishi wa sheria.

Mheshimiwa Spika, pia Bajeti hii iboreshwe. Mawakili wa Serikali, pamoja na kwamba waliongezewa mshahara na maslahi mengi, bado upo chini sana ikilinganishwa na taasisi zingine za upelelezi kama TAKUKURU na vyombo vingine. Mishahara midogo wanayopata inapelekeea wengi kuacha kazi na kuajiriwa na *private law firms* za nje, Serikali ina mpango gani wa *pay and incentive* ili *kuwa-retain?* Watumishi hawa wa AGC hawapati *communication allowance; risk allowance*; wala *non-practicing allowance* na hata posho ya kulipia kodi ya nyumba inayotolewa haikidhi mahitaji kabisa hasa ukizingatia kazi wanazozifanya. Wanafanya kazi nyeti, lakini kwa hela wanayopewa inaweza kupelekeea kuishi na kuchanganyika katika nyumba moja na wahalifu au ndugu wa karibu wa wahalifu hao, hivyo kuhatarisha maisha yao.

Pia kukosekana kwa posho ya mawasiliano kunapelekeea mawakili kutumia fedha zao ambazo ni ndogo kuwasiliana na vyombo vingine vya upelelezi, ifike hatua, mawakili hawa wapewe posho hii ya mawasiliano, posho ya mafuta kwa ajili ya vyombo vyao vya usafiri.

Mheshimiwa Spika, Wizara inakabiliwa na upungufu mkubwa wa usafiri ukilinganisha na idadi iliyopo ya mawakili.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali iimarishe Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake ya Kikatiba ili kupanua wigo wa uwajibikaji kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, mfumo uliopo hivi sasa unasababisha ofisi za mashtaka mikoani kufanya kazi za divisheni nyingine zilizopo Makao Makuu, mfumo huu unadumaza mpango wa huduma ya uendeshaji mashtaka nchini, utegemezi huu utatuliwe haraka.

Mheshimiwa Spika, ni vema pia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ikaweka mpango kabambe utakaoiwezesha kusimamia mikataba yote inayoingiwa na Serikali ngazi zote kwa karibu zaidi na kufanya utafiti wa kutosha na kuandika sheria kitalaam zaidi.

Mheshimiwa Spika, Serikali iajiri Mawakili wa Serikali, Mahakimu, Wapelelezi na watumishi wa kutosha kwenye vyombo vinavyohusika na utoaji wa haki.

Mheshimiwa Spika, mfano, *Sukari House* magari ni mawili hayatoshelezi kuwasafirisha watumishi kwenda Mahakamani. Haki nyingine za msingi kama likizo, wapo Mawakili hawaajaenda likizo zao kwa muda mrefu, huu ni ukiukwaji wa sheria na vilevile mtumishi hawezi kufanya kazi kwa ufanisi.

Kuhusu upandishwaji wa vyeo umefanyika, nipongeze lakini bado haitoshelezi kwani kuna ambao ukiangalia miaka na uzoefu wao kazini vyeo vyao haviendani, vipo chini!! Wizara ijithadi kusimamia zoezi hili kila anayestahili apate cheo anachostahili.

Kuhusu upungufu wa maktaba, ipo maktaba moja na ina upungufu mkubwa na vitabu tu. Imefika wakati Mawakili wanaenda Mahakamani bila kuwa na *statutes*, vitabu wala marejeo na *law reports*. Naiomba Wizara iliangalile hili na ihakikishe huduma za maktaba zinapatikana katika Ofisi za AG. Vilevile nakala za hukumu zisizoripotiwa za kesi zinatolewa kidogo sana. Ushauri kuwe na utaratibu mzuri wa usambazaji wa nakala hizi za hukumu ili kuwawezesha Mawakili kufahamu namna kesi mbalimbali zilivyoamuliwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mahakama, ili kupunguza mrundikano wa kesi mahakamani tumeelezwa hapa na Waziri kwamba Mfuko wa Mahakama umetengewa shilingi bilioni 20 ili kusikiliza kesi zilizokaa muda mrefu mahakamani, fedha hizi ni ndogo. Jamani, mhimili wa Bunge na Serikali wamekuwa wakitengewa fedha ambazo zinawawezesha kutekeleza majukumu yao. Hakuna safari za watendaji zilizosimama kwa kutokawa na fedha. Kwa kutokuwapatia mahakama fedha za kutosha, tunasababisha mrundikano wa kesi mahakamani na msongamano wa mahabusu.

Mheshimiwa Spika, ningependa kufahamu je, mpango wa kupunguza mrundikano wa kesi (*Case Backlog Programme II*) unaoainisha vigezo vinavyotumika kuainisha kesi iliyokaa muda mrefu ni iliyo kaa muda gani na katika ngazi ipi ya Mahakama? Kuanzia Mahakama za Mwanzo mpaka ngazi ya Mahakama ya Rufani? Kwani kuititia hotuba ya Waziri inaonyesha mashauri yaliyosikilizwa ni 28% tu, mashauri 789 kati ya 2,857, vilevile Wizara ilifanya tathmini ya msukumo wa kesi yaani *case flow analysis* ambayo ilikamilika Juni mwaka huu. Ningependa Mheshimiwa Waziri anapofanya majumuisho alieleze Bunge lako Tukufu ni hatua zipo muhimu za kwanza Wizara hii itachukua na Wizara itatekeleza mapendekezo yapi kama yalivyoainishwa na tathmini hiyo?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa nchini kwetu bado tuna idadi ndogo ya Mawakili wa Kujitegemea na kwa kuwa maeneo mbalimbali nchini hususan maeneo ya vijijini hawana huduma za Mawakili wa Kujitegemea, ni dhahiri wakati umefika sasa wa kuwa na kada ya Mawakili Jamii. Mheshimiwa Waziri anaweza kutueleza ni lini mchakato wa kutayarisha utaratibu maalum chini ya sheria ili kuanzisha kada hii maalum ya Mawakili Jamii?

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu na ugumu wa kazi zinazofanywa na Wazee wa Baraza, ningependa kufahamu Serikali ina mpango gani wa kuwaboreshea posho zao hususan kuwapandishia viwango vya posho zao kwani shilingi 5,000/= kwa kesi inayomalizika ni ndogo mno.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kumpongeza Waziri Celina Kombani kwa kuteuliwa kuwa Waziri katika Wizara hii nyeti na muhimu sana ikiwa ni mratibu wa moja ya mihimili ya nchi hii. Aidha, nampongeza kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mwanasheria Mkoo kwa uongozi wake wa kisheria humu ndani ya Bunge, Katibu Mkoo Mhaiki na watendaji wote wa Wizara yake. Kipekee nimpongeze Msajili wa Mahakama Jaji Mutungi kwa misaada, ushauri wa kueleweka na misaada ya kifedha kwa mustakabali wa Mahakama ndani ya Mkoo wa Tanga na Wilaya ya Kilindi.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mnyimi wa fadhila nisipomshukuru *His Worship Judge* Mussa Kipenka wa Tanga, wasaidizi wake na watendaji wake wote.

Aidha, nashukuru sana miongozo, mshikamano wa Hakimu Mfawidhi aliyepo Handeni na wasaidizi wake wote na Mahakimu wa Mahakama ya Mwanza Wilayani Kilindi.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu kwanza ni kuhusu Wilaya ya Kilindi, tangu ianzishwe ni takriban miaka tisa sasa. Inasikitisha kuona hadi leo hatuna Mahakama ya Wilaya. Tuna mahakama tatu za Mwanza katika Wilaya nzima. Mahakama ya Wilaya ipo Handeni kilomita 130 toka Makao Makuu ya Kilindi, jambo ambalo kwanza ni gharama sana na pili haki haitendeki ipasavyo kwani kama anayeshitaki hana hela ya kutoa mshitakiwa apelekwe mahakamani, basi ile kesi inasikilizwa aidha, upande mmoja au isisikilizwe. Tuna uwanja mkubwa uliotengwa kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama pamoja na mahabusu na uliwekewa jiwe la msingi na Jaji Kiongozi mwaka 2007 hadi leo hakuna kilichoendelea.

Mheshimiwa Spika, pili, Mahakama za Mwanza zilizopo zimechakaa kupita maelezo, ilibidi mimi Mbunge nichangie kufanya ukarabati. Je, nitaweza kukarabati zote?

Tatu, nyumba za Mahakimu hakuna, wanapanga uraiani nyumba ambazo hazina hadhi kabisa kwani kwa zile nzuri chache za watu binafsi zilizopo gharama ni kubwa na hawana hiso pesa. Kwa *style* hii haki itatendeka?

Mheshimiwa Spika, kuhusu usafiri, hatuna gari hata moja kwa sababu hatuna Mahakama ya Wilaya wala akaunti ya Mahakama, kwa kweli tunaweza kuendesha haki. *Documents sensitive* za ushahidi zinabebwa kwenye basi la abiria la kawaida. Gari ikiharibika anakaa hapo na *documents* hiso nyeti hata siku tatu. Tuna pipipiki mbili ambazo zimekuwa chakavu kutokana na matumizi makubwa. Tunaomba tutazamwe, tusaidiwe kama ilivyo katika Wilaya nyingine.

Mheshimiwa Spika, Wazee wa Mahakama watazamwe, wanafanya kazi ambayo kwa kweli saa nyingine wanatumia busara bila kuchanganya na elimu, wawezeshwe kwa semina za mara kwa mara. Pili maslahi yaani posho zao ziangaliwe, hata mavazi. Wengine wanavaa nguo chakavu, kandambili na kwa vile hawana pesa, nahisi kuna nyakati wakiwezeshwa pengine haki inaweza kuyumba, naomba watazamwe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. EUSTACE O. KATAGIRA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri na timu yake kwa kuandaa na kuwasilisha Bajeti nzuri na nawapongeza kwa uendeshaji.

Mheshimiwa Spika, majengo mengi ya Mahakama ni mazee hasa ya Mahakama za Mwanza na Wilaya yaboreshwe na kwingine yajengwe mapya, majengo ya kupangisha ni ya ghali tujitahidi kujenga.

Mheshimiwa Spika, kuhusu masurufu, watumishi waongezewe masurufu na hasa Mawakili wa Serikali wapewe hela za kuwawezesha kufanya kazi zao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *Law School*, mpango na utaratibu wa kuwapa mikopo ya masomo uwekwe vizuri tofauti na utaratibu wa sasa ambaa ni wa muda na haujawekwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, naomba nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Katiba kwa kazi nzuri anayofanya. Pia nampongeza Mwanasheria Mkuu, Naibu Mwanasheria Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii. Pongezi nyingine ni kwa watendaji wote wa Idara ya Mahakama kwa kazi yao nzuri ya kutoa haki. Pamoja na pongezi hiso ninayo machache ya kuchangia.

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kuhusu lugha ya Kiswahili, usemi wa kisheria usemao kutojua sheria si kinga (*ignorance of the law is not a defence*), unamtaka kila mtu ajue sheria za nchi ili pale atakapoivunja asitoe visingizio kuwa hakujuwa kuwa tendo hilo ni kinyume cha sheria. Sheria zetu nyingi hazijulikani kwa mwananchi wa kawaida. Sababu mojawapo ni kwamba zimeandikwa

katika lugha ya Kiingereza ambayo si lugha inayotumiwa na wengi. Lugha yetu ya Taifa ni Kiswahili. Nashauri sheria zetu zitungwe katika lugha ya Kiswahili ili na wananchi wasiojua Kiingereza waweze kuzisoma na kuzielewa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *Law School* (Shule ya Sheria ya Vitendo) Serikali ilianzisha *Law School* kwa lengo la kuwapatia wahitimu wa Digrii ya Sheria elimu ya vitendo ili baadaye wapate kusajiliwa na kuwa Mawakili wa Kujitegemea. Kwa bahati mbaya sana Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu haiwatambui kwani sheria inawatambua kwa ngazi ya kumaliza digrii yao ya sheria. Hali hii imeleta matatizo makubwa kwa wahitimu wa Digrri ya Sheria hasa kwa wale wote ambao hawana fedha za kulpia *Law School*. Ninashauri na kupendekeza Serikali ilete Bungeni Sheria ya Bodi ya Mikopo ili ifanyiwe mabadiliko na kuiruhusu Bodi ya Mikopo kuwakopesha wanafunzi wa *Law school*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mabaraza ya Ardhi ya Kata yapo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Wazee wa Mabaraza hawa hawana weledi wa elimu ya sheria. Maamuzi yao mengi si ya haki kutokana na kutokuwa na taaluma ya sheria. Ninapendekeza mabaraza haya yafutwe na jukumu hili lirudi Mahakama zetu za Mwanzo tu. Pia posho za hawa Wazee wa Mabaraza zinazolipwa na TAMISEMI ni ndogo na wakati mwingine zinachelewa kuwafikia na hivyo kusababisha mianya ya rushwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ajira za Mahakimu, kwa sasa nchi ina upungufu mkubwa wa watumishi wa Mahakama hasa Mahakimu wa ngazi zote. Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo ni wachache. Ombi kwa Serikali ile nia ya Jaji Mkuu Marehemu Francis Nyalali na Jaji Mkuu Mstaafu Barnabas Samatta ya kuajiri wahitimu wa Digrii ya Sheria kwenye Mahakama za Mwanzo lifanyiwe utekelezaji haraka. Kwa sasa tunao wahitimku wa Digrii ya Sheria wengi kuliko zamani. Kuajiri wahitimu wa Digrii ya Sheria kwenye Mahakama za Mwanzo kutasaidia kuitatua migogoro kwa kiwango kizuri kisheria na pia itapunguza tatizo la ajira kwa wahitimu wetu wa Digrii ya Sheria.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mahabusu za watoto, Sheria ya Mtoto namba 21 ya mwaka 2009 na kifungu namba 5 ya *Young Offender Decree, Cap. 58* inapiga marufuku kwa mtoto kufungwa au kuwekwa mahabusu moja na watu wazima. Hapa kwetu bado watoto wanawekwa mahabusu moja na watu wazima. Hali hii ipo Tanzania Bara na Visiwani. Nashauri Serikali itengete Bajeti ya kutosha kwa ajili ya kujenga mahabusu za watoto peke yao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu teknolojia (*Hansard*) ni muda mrefu sasa tumekuwa tukisisitiza umuhimu wa kutumia teknolojia katika kuendesha mashauri mahakamni. Kuendelea kutegemea Hakimu au Jaji aandike mwenendo wa shauri umepitwa na wakati na unadumaza utendaji haki kwani baadhi yao kwa bahati mbaya au kwa makusudi huacha au huandika baadhi ya maneno kwa nia ya kupotosha ukweli. Watu wengi wameumia kutokana na utaratibu huu. Nashauri Serikali itengete Bajeti maalum kwa ajili ya teknolojia hii mpya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uzalendo kwa watumishi wa mahakama, naomba nisisitize umuhimu wa uzalendo katika kutayarisha mikataba mbalimbali inayoihusu nchi. Bila uzalendo kwanza nchi yetu itapata hasara kubwa kutokana na miakataba mibovu. Naunga mkono hoja.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, mfumo wetu wa Kikatiba na kiutawala umejengwa katika misingi ya mgawanyo wa madaraka na uwajibikaji iliyowekwa na Katiba. Nchi yetu inaongozwa na mhimili yaani Mahakama, Serikali na Bunge, mihimili hii haitakiwi na haiwezi kujitenga katika utekelezaji wa majukumu yao ya Kikatiba. Pamoja na mahusiano yao vyombo hivi vinapaswa kuwa huru katika utekelezaji wa shughuli zake. Hali halisi haipo hivi kwani mara nyiningi Serikali imekuwa ikiingilia mihimili mingine. Mfano ni jinsi hoja ya hujuma dhidi ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini Ndugu Jairo Ilipoibuliwa na Bunge. Badala Bunge ileteewe taarifa ya uchunguzi wa Bwana Jairo, taarifa hiyo ilipelekwa kwa Katibu Mkuu Kiongozi na baada yake Bwana Jairo akarejeshwa kazini. Tukio hili ni la aibu na Bunge kama mhimili umedharauliwa na kuingiliwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudini kubwa ya uteuzi wa Majaji bado kesi (*cases*) nyingi zimekuwa zikichukua muda mrefu sana, hivyo ule msemo *justice delayed is justice denied*, ni vema basi ongezeko la Majaji na Mahakimu ni lazima iendane na uharakishwaji wa *cases* zilizopo.

Mheshimiwa Spika, gharama za uendeshaji wa *cases* nazo ni kubwa mno hivyo kufanya wenyewe fedha washinde *case* hata kama wao ndio wenyewe makosa. Hii ni kwa sababu gharama za Mawakili (*advocates*) ni kubwa mno. Hali hii imewafanya wasio na fedha kushindwa kabisa kusimamisha Mawakili na hivyo kupelekeea kushindwa.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kusikitisha kuona kwamba bado haki nyingi za binadamu hususan za watoto kwa mfano Zanzibar hakuna mahabusu ya watoto kwa upande wa Zanzibar, kinachofanyika ni kuwatenganisha tu wakati wa kulala usiku lakini muda wote wa mchana huchanganyika na watu wazima, kinyume cha haki za binadamu na utawala bora.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda niwapongeze kwa dhati ya moyo wangu Mheshimiwa Waziri, Mwenyekiti wa Kamati, Wajumbe wa Kamati na wadau wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya na hasa katika kipindi hiki cha mchakato wa mabadiliko ya Katiba, hongereni sana na poleni sana kwa kazi ngumu na natanguliza kusema kuwa naunga mkono hoja 100%.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu imefanya kazi kubwa sana katika kutetea haki za binadamu kwa mujibu wa Katiba ya nchi yetu. Serikali ya Chama cha Mapinduzi inasikiliza wananchi wake kwa kuwatekelezea mahitaji yake ikiwemo suala zima la badiliko la Katiba. Serikali yetu imefanya kazi kubwa sana japo palipo na mazuri basi mabaya hayakosekani. Hizo zote Serikali ichukulie kuwa ni changamoto ikazifanyie kazi kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie katika Idara ya Mahakama katika Mkoa wa Dar es Salaam. Mahakama za Mkoa wa Dar es Salaam zinazurika kesi kutokana ma migogoro isiyi na majibu kati ya wananchi na Serikali yao. Migogoro kama ya ardhi, upanuzi wa barabara, upanuzi wa miji, madai ya wafanyakazi, bomoa bomoa, uvunjwaji wa amani inasababisha mahakama zifurike.

Mheshimiwa Spika, naomba nishauri tena Serikali yangu siku ya Chama cha Mapinduzi, hivi hizi Wizara zinazosababisha migogoro hii kwa nini hawakai na wananchi kumaliza tatizo mpaka wananchi wakajazane Mahakamani? Kesi hizo nyingi Serikali inashindwa na kubeba mzigo wa madeni. Rai yangu kwa wananchi waihurumie Serikali yao kwa kutulia na kutafuta njia ya kutatua matatizo kwa amani.

Mheshimiwa Spika, niombi Mawakili wawe wanatoa elimu kwa wateja wao na hasa elimu ya kisheria maana mara nyingine kesi zinafunguliwa ambazo hazina msingi, za usumbufu tu. Sasa naomba Serikali iziangalie Mahakama ya Mwanzo Temeke, Ilala na Magomeni. Mahakama hizi ni za muda mrefu sana toka mkoloni. Naomba sasa Serikali katika kumbukumbu ya miaka 50 ya Uhuru izikarabati Mahakama hizi zenyе historia ya Uhuru.

Mheshimiwa Spika, hayo ndio mawazo yangu na ushauri wangu. Naunga mkono hoja 100%. Ahsante sana.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri kama nilivyokueleza mara mbili kuhusu tatizo la uadilifu na maadili ya Hakimu wa Mahakama hii ya Mwanzo, tatizo la Hakimu huyu ni ulevi uliopitiliza, mgongano na jamii kutokana na malalamiko ya migogoro ya ndoa za watu lakini zaidi ni matumizi mbaya ya madaraka yake kwa kuendesha vitisho kwa wananchi wa eneo hili la Nguruka.

Mheshimiwa Spika, matatizo haya yamejadiliwa na Kamati ya Maendeleo ya Kata, nimepata kumfahamisha Hakimu wa Wilaya na hata Hakimu Mkazi wa Mkoa wa Kigoma, wanayafahamu matatizo ya Hakimu huyu na Hakimu Mkazi wa Mkoa Kigoma alinieleza kuwa atafanya utaratibu wa kumhamisha kumpeleka Wilayani kwenye Mahakama ya Mwanzo karibu na Makao Makuu ya Wilaya na Mkoa kwa lengo la kuhakikisha anatazamwa kwa karibu.

Hata hivyo, tatizo limekuwa ni uwezekano wa kumhamisha kutokana na suala la Bajeti. Ni kwa msingi huo, naomba Mheshimiwa Waziri ultazame suala hili kwa ukaribu kwa heshima ya taasisi ya Mahakama na hata uhai wa Hakimu huyu kwani taarifa nilizo nazo hivi karibuni Hakimu huyu amechomewa nyumba.

Naomba kuwasilisha kwa maandishi suala hili kwako nikitumaini kuwa maoni ya Hakimu Mkazi unaweza kuyazingatia kwa heshima ya Mahakama.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Naipongeza Wizara kwa kazi nzuri inayoifanya ili kufanikisha utoaji wa haki kwa wananchi wetu, hususan katika kupanua huduma za Mahakama za Mwanzo.

Toka mwaka wa fedha 2008/2009 mpaka sasa Mahakama za Mwanzo za Ukimbu (Mgandu) na Mwamagemebe hazijakarabatiwa kama ilivyoahidiwa na Idara ya Mahakama za Mwanzo na fedha kutengwa kwa kazi hiyo. Zilitengwa shilingi milioni 70 kwa kila Mahakama hizo ziweze kukarabatiwa lakini kila mwaka hakuna kilichofanyika. Naomba kupata maelezo ni kwa nini Mahakama hizi zilizoachwa na mkoloni mwaka 1961 mpaka sasa hazijafanyiwa ukarabati kuzihuisha?

Naiomba Idara ya Mahakama za Mwanzo iongeze idadi ya Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo pale Itigi ili wasaidiane na Mahakimu wawili walipo wapanue huduma kwa Kata 11 za Jimbo. Kata ya Rungwa, Kitaraka, Ipande, Idodyandole na Aghundi zipo pembezoni sana kwa wananchi kuzifikia Kata za Mwamagemebe, Mitundu, Mgandu na Itigi ambazo zina huduma za Mahakama. Nawasilisha.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Spika, nami napenda kuchangia mada hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Tume ya Haki za Binadamu, taasisi hii imekuwa muhimu sana katika kuchunguza na kufuatilia maadili mbalimbali kwa mujibu wa Katiba na Sheria. Je, hamuoni sasa ni wakati muafaka wa kutangaza ofisi mpya nchini kote za Tume hii ili kukidhi haja ya Watanzania. Mbona *PCCB* ipo nchini kote taasisi ambayo *effect* yake kwa jamii ni ndogo sana.

Pili, mrundikano wa kesi hasa za ardhi kwa nini Kanda ya Magharibi Mahakama Kuu kesi zake zinakaa kwa muda mrefu? Kuna kesi za zaidi ya miaka 15, je, ofisi yake inafanya utaratibu gani wa kumaliza kesi hizi? Mahakama zako zimeshindwa kushughulikia matatizo ya wananchi, zimejaa rushwa na kebehi kwa wananchi maskini, huu ni udhalilishaji kwa Watanzania, ni imani yangu Bajeti hii itashughulikia kutatua kero za kesi za muda mrefu sana.

Suala la tatu ni kuhusu *law school*, hii *school of law* imekuwa ni janga la Kitaifa. Vijana wetu wamekuwa hawapati nafasi za kuendelea na masomo hayo kwa ukosefu wa ada. Vijana wakichukua fomu tu wanatakiwa watoe shilingi 1,570,000/= wananchi maskini hawawezi.

Pili walimu wao wengi ni Mawakili kada ambayo ipo *busy* sana na mambo yao binafsi, jambo linalosababisha wakose kufundishwa kinyume na lengo, hii ni hatari kwa vijana wetu.

Suala la tatu, wanafunzi wamekuwa wakikaa shulenii muda mrefu kuliko kwenda kwenye mafunzo ya vitendo, kama kusoma darasani wameshafanya hivyo pindi walipokuwa wanafanya digrii zao, kwa nini tena leo hii wanawaweka darasani muda mrefu kama vile wapo tena vyuoni wanafanya digrii zao? Tunaomba Wizara iongeze muda wa *field* au mafunzo kwa vitendo ili vijana hawa wapate uelewa mzuri na wasaidie jamii ya Watanzania!

**MHE. ABUU H. JUMAA:** Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuchangia Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria ya mwaka 2011/2012. Napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuandaa Bajeti hii kwa utaalamu mkubwa na kwa kuzingatia Ilani ya Chama cha Mapinduzi inavoyelekeza kuhusu kuendeleza na kuimarisha mikondo ya sheria katika kutoa haki sawa kwa wananchi wote. Kuendeleza sheria ya kulinda walemvu na hasa walemvu wa ngozi, sheria ya haki za watoto na sheria za makosa ya kujamiihana. Pia kuendelea kuboresha mahakama katika ngazi zote kuanzia Mahakama Kuu,

Mahakama za Mikoa, Wilaya, Mwanzo hadi Mabaraza ya Sheria ya Kata, pamoja na kusimamia haki za binadamu na utawala bora.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Katiba ya nchi yetu ipo katika mchakato wa kuboreshwa sitakuwa na mengi ya kuchangia bali kuishauri Serikali kushusha mjadala huu kwa wananchi ili washiriki kikamilifu katika kutoa mawazo yao jinsi na namna Katiba yetu inatakiwa iwe. Kwa kuwa hali ilivyo wananchi wengi hawaelewii maana ya Katiba na wala Katiba iliyopo sasa ina mambo gani na pia kwa kuwa upeo wa wananchi kuhusu mambo yanayohusu sheria ni mdogo, miongozo na elimu itolewe ili wananchi wajue wanatakiwa kufahamu na wana haki gani katika Katiba. Hii itasaidia kuwapa upeo wa kuelewa na kuchangia mawazo yao yatakayoweza kuifanya Katiba ya nchi yetu iwe na mtizamo na dira iliyoshirikisha mawazo ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, hakuna mwananchi ambaye kwa sasa hivi hafahamu msemo unaosema haki iliocheleleweshwa ni sawa na haki iliyonyimwa (*justice delayed is justice denied*). Nasema hivi kwa sababu hali ya utendaji katika Mahakama zetu kwa ngazi zote hairidhishi wala haitoi haki kwa wakati. Ni jambo la kawaida kabisa kukuta kesi ndogo inachukua muda sana kufikia hukumu kwa sababu ambazo hazieleweki. Wafungwa na mahabusu wamejazana katika magereza. Kama mkondo wa Mahakama ungekuwa na ufanisi, hukumu za kesi za wafungwa hawa zingetolewa kwa wakati. Matatizo ya msongamano na hisia za viashiria rushwa katika Mahakama zetu yasingekuwepo. Sababu zinazopelekeea Mahakama zetu zisiwe kutoa hukumu ya kesi kwa muda mfupi unachangiwa na mambo mengi katika upelelezi wa kesi kuchukua muda mrefu, ukosefu wa vitenda kazi kama majengo bora ya ofisi za Mahakama, ukosefu wa magari, pikipiki, nyumba za watumishi wa Mahakama na Mahakimu, maslahi na mishahara duni, upungufu wa watumishi wa Mahakama katika fani zote kwa maana ya Mahakimu, makarani na wasuluhihi wa migogoro ya aina zote, uhaba wa vitabu vy'a sheria pamoja na mazingira magumu ya kufanya kazi. Yote haya yanahitaji jitihada za kurekebisha kama Serikali inataki kutoa haki kwa wakati kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, japo kuna sheria inayompa haki mfungwa wa kesi ndogo ndogo kupata hukumu ya kifungo cha nje, sheria hii haitumiki ipasavyo kwani naamini kuna wafungwa ambao wapo katika magereza wakitumikia kifungo kwa makosa madogo ambayo wangeweza kuwa katika *parole* na kifungo cha nje. Kifungo cha nje kingetumika kwa uaminifu na umakini kitapunguza sana msongamano katika mahabusu na magereza. Matatizo mengine ni kuahirishwa mara kwa mara kwa kesi mahakamani. Kitendo hiki licha ya kuwakera wananchi kinawagharimu pesa nyigi sana kwa muda na kwa kuwa mashahidi wengine wanatoka mbali wanahitaji usafiri, malazi na chakula. Kuahirishwa kesi wakati mwengine sababu zinazotolewa ni za kitoto kama Hakimu kwenda kuchukua mshahara, Hakimu hayupo, Hakimu kaitwa Wizarani na kadhalika. Haya yote yanaonyesha udhaifu na uzembe wa kesi kuchukua muda mrefu bila kutolewa hukumu.

Mheshimiwa Spika, kati ya mambo ambayo yanahitaji kuboreshwa na kurekebishwa ni mfumo wa sheria uliopo ambao umepitwa na wakati. Hii inajumuisha kanuni na taratibu za mahakama za kizamani. Nashauri Srikali kuititia Tume ya Kurekebisha Sheria, iangalie namna ya kubadilisha mfumo huu kuendeana na kasi ya mabadiliko makubwa yanayotokea katika ulimwengu wa sasa katika jamii, kisiasa, kiuchumi na kiteknolojia. Mfumo ulipo sasa hautoi fursa ya kutumia mabadiliko ya maendeleo yanayoweza kufupisha muda wa kushughulikia kesi na kutoa huduma bora na haki kwa jamii.

Mheshimiwa Spika, uwezo mdogo wa wananchi kuweza kutumia vyombo vy'a kutoa haki na huduma za sheria haumpi nafasi ya kutambua namna ya kuyapa msaada wa kutetewa mahakamani. Kuna Mashirika mengi ya Mawakili ambao wanatoa huduma za kusaidia jamii katika masuali ya sheria. Mashirika haya mengi yapo mijini yakiacha wananchi waishio vijijini kutoweza kupata na kutumia fursa hii pindi wapatapo matatizo yanayohitaji ushauri na utetezi wa kisheria.

Nashauri Serikali iangalie namna ya kuwezesha wananchi wa vijijini kupata fursa ya huduma ya Mawakili. Hii itawasaidia sana kupata huduma za kisheria kwa wakati na haki kupatikana. Kuna maeneo mengine ya sheria ambayo yanahitaji kufafanuliwa na kuwekwa

bayana kwa kuwaelimisha wananchi namna ya kutumia sheria hizo bila kuleta migongano katika jamii. Mfano Sheria ya Mirathi, ni wajibu wa Serikali kupitia wakala wake *RITA*, kuhakikisha wananchi wanaelekezwa namna ya kuandika na kuhifadhi wosia. Mirathi ni tatizo kubwa sana katika jamii kwani kuna uelewa potofu kwamba anateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi ndiye aliyе na mamlaka na mali za marehemu. Kwa uelewa huu potofu umesababisha migogoro na malalamiko mengi katika jamii kwani wasimamizi wengine wanaoteuliwa hudiriki hata kuuza mali hizo na kuwanyima haki warithi na wategemezi halali wa marehemu. Hili pia ni jamob la kuelimisha wananchi kwa nguvu zote ili dhuluma ya mirathi ya mali za wafiwa zisiendelee.

Mheshimiwa Spika, mambo mengine yanayowakera wananchi katika sheria na haki ni mikataba ambayo inasimamiwa na ofisi ya Mwanasheria Mkuu inavyoleta hasara kwa Taifa. Mfano mzuri ni mkataba wa ubinafsishaji wa Shirika la Reli (*TRC*) na Kampuni ya Serikali ya India (*RITES*). Wawekezaji wabia walivyoshindwa kuendesha Shirika la Reli na kusababisha hasara kubwa kwa nchi yetu katika sekta ya uchukuzi.

Pia Mkataba wa *Dowans* na mingine mingi iliyosimamiwa katika mkondo wa sheria. Hapa umakini zaidi unatakiwa ili kuondoa dhana ya wananchi kufikiria kwamba mkataba unapokuwa na matatizo ama kuna mkuu wa mtu au viashiria vya rushwa. Sheria ya mapambano dhidi ya rushwa, watendaji wanatakiwa waendelee kutoa elimu kwa wananchi kuichukia rushwa ili wawewe kutoa taarifa za vitendo vya rushwa. Aidha, wananchi wenye mapenzi mema na nchi yetu wanapotoa taarifa za vitendo vya rushwa, kuwe na usiri wa kutowatambulisha ili waendelee kutoa taarifa. Taarifa za wanaotoa taarifa za vitendo viovu katika jamii zinapokuwa wazi zinawaweka katika hali ya kuhatarisha maisha yao na pili watu wanaogopa kutoa taarifa au ushahidi kwa jambo walilolishuhudia. Hii ni sababu mojawapo ya kesi kutomalizika mapema au watuhumiwa kuachiwa huru kwa kukosekana ushahidi kamili.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Kibaha Vijiijini kuna Mahakama nne za Mwanzo ambazo zipo katika Kata ya Mlandizi, Ruvu, Magindu na Soga. Mahakama hizi zipo katika hali mbaya sana. Hazina majengo ya ofisi na yaliyopo ni machakavu sana. Kuna upungufu mkubwa wa samani za kutosha kama meza, viti, kompyuta, kalamu na karatasi. Hakuna Ofisi za Masjala bayana zenye makabati ya kutunzia mafaili ya mienendo ya kesi na vielelezo. Kuna Hakimu mmoja ambae anazungukia Mahakama zote hizo na pia kutoa ushauri katika Mabaraza ya Kata ambazo katika Jimbo la Kibaha Vijiijini kuna Kata kumi na moja.

Mheshimiwa Spika, umbali wa kutoka Kata moja mpaka Kata nyingine inategemea na hali ya hewa lakini ni mwendo wa saa kadhaa, bila usafiri wa uhakika Hakimu huyu anapata shida sana kwani ofisi haina hata usafiri wa balskeli. Naiomba sana Serikali iangalie matatizo yaliyopo katika Mahakama na hasa za vijiijini kwani zipo katika hali mbaya na duni sana. Kwa kuwa Jimbo la Kibaha Vijiijini ni kubwa sana nashauri Mahakama ya Mwanzo iliyopo katika Kata ya Mlandizi ipandishwe daraja kuwa Mahakama ya Wilaya ili kuwasaidia wananchi wa Jimbo hili ambao hutakiwa kusafiri kwa gharama kubwa kwenda Kibaha Maili Moja kupata huduma za Mahakama ya Wilaya. Naunga mkono hoja.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, kuhusu mchakato wa Katiba mpya, kwa kuwa Watanzania wamekuwa wakililia kupata Katiba mpya mapema iwezekanavyo lakini zoezi hilo limekuwa likisusua kwani taarifa mlizotoa za mchakato wa Katiba kuanza mwaka 2014, ni mbali sana, je, Serikali ni kwa nini sasa isirudishe nyuma mchakato huo wa kuwa mwaka 2012 ili wananchi wengi wawewe kushiriki na kutoa maoni yao ili inapofika mwaka 2014 iwe ni kikomo cha kupatikana kwa Katiba hiyo mpya ambayo itatumika katika Uchaguzi Mkuu ujao. Hivyo basi tunaomba Serikali itueleze ni nini sababu za zoezi hilo kuchelewa?

Kuhusu Sheria za Mirathi, kwa kuwa ndani ya nchi zetu kumekuwa na sheria mbalimbali za mirathi, lakini pamekuwepo na sheria kuu tatu zinazotumika ambazo ni Sheria ya Mirathi ya Serikali, Sheria ya Mirathi za Kidini pamoja na Sheria za Mirathi za Kimila. Je, Serikali inawezaje kukabiliana na tofauti hizo ilhali pamekuwepo na malalamiko mengi juu ya Sheria hizo kulingana na jinsia, dini pamoja na kimaeneo maana katika maeneo ya vijiijini pamekuwepo na Sheria za Kurithiana wake

kwa lazima. Je, sasa ni kwa nini Serikali isiwe na sheria moja tu ya mirathi itakayokuwa inatumika kwa watu wa aina zote? Ninaomba ufanuzi katika hili na naomba kuwasilisha.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, Wizara ya Katiba na Sheria imepewa majukumu muhimu kwa Taifa letu kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Na. 494 la kuratibu vyombo vya kusimamia haki na uwajibikaji, masuala ambayo ni ya msingi kwa maisha ya wananchi na maendeleo ya nchi. Hivyo, Bajeti yake inapaswa kuongezwa kufikia kiwango kisichopungua bilioni 200. Aidha, kiasi kilichotengwa kwa Mfuko wa Mahakama cha shilingi bilioni 20, ukilinganisha na mahitaji izingatiwe kwamba Mfuko wa Bunge Fungu la 42 limetengewa shilingi bilioni 77.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vyombo vya Mahakama ambavyo ni vya msingi katika kusimamia sheria na kutoa haki kasi ya ushughulikaji wa madi ni ndogo sana. Kwa wastani vyombo vya kimahakama vinashughulikia kwa wastani kati ya 25 – 30% ya mashauri. Hivyo kuna haja ya kuongeza lengo kufikia asilimia 50 kwa kila chombo na ngazi ya Kimahakama kwenye mwaka wa fedha 2011/2012. Hii inahusu fungu 12, 18, 19, 40, 60, 64 na 90. Mashauri yenye kuchelewesha miradi ya maendeleo mathalani kesi ya ardhi ya wananchi wa Kwembe kwenye eneo la ujenzi wa Chuo cha Muhimbili Mloganzila ziharakishwe.

Aidha, vyombo vya Mahakama viweke mfumo wa ufuatiliaji wa utekelezaji wa hukumu zake kwa kuwa zipo hukumu za miaka mingi ambazo Serikali inapiga danadana kuzitekeleza. Mathalani za wafanyakazi wa Kiwanda cha Urafiki na kesi ya wanafunzi wa Chuo cha Ardhi (*UCLAS*) ambao mahakama imeelekeza wapewe yeti vyao. Pamoja na kuboresha maslahi ya Mahakimu na Majaji, Serikali itimize malipo ya Wazee wa Mahakama ikiwemo katika Manispaa ya Kinondoni.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Fungu 35 Divisheni ya Mashtaka, natoa wito kwa Kamati ya Haki na Jinai katika mwaka 2011/2012 kuratibu programu maalum ya kuwapangia wafungwa kazi mbadala katika Jimbo la Ubungo na Manispaa ya Kinondoni kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Fungu 16 Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, pamoja na kauli ya Wizara ya kutaka kuongeza ufanisi katika timu ya majadiliano (*GNY*) katika mikataba. Wizara ieleze hatua zilizochukuliwa dhidi ya wataalam toka walioingiza katika mikataba mibovu kwenye maeneo ya madini, mafuta, gesi asili, umeme, ardhi na sekta zingine. Aidha, mkakati thabiti wa kurithisha wataalamu na utaalamu (*succession plan*) iandaliwe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Fungu 41 la Wizara ya Katiba na Sheria Serikali itoe kauli ni kiasi gani cha fedha kimetengwa kwa ajili ya mchakato wa Katiba mpya katika mwaka wa fedha 2011/2012. Aidha, kumekuwa na mgongano wa kauli kuhusu hatua ya Muswada wa sheria ya mapitio ya Katiba kati ya kauli zilizotolewa Bungeni mwezi Aprili, 2011, kauli zilizotolewa Bungeni na Serikali pamoja na uongozi na Bunge kati ya Juni na Julai, 2011 na hotuba ya Waziri pamoja na taarifa ya Kamati zilizowasilishwa 24 Agosti, 2011. Serikali itoe kauli kuhusu mgongano huu na kuweka hadharani marekebisho ambayo imeyafanya mpaka sasa katika Muswada husika na sababu za kushindwa kuuleta katika Mkutano wa Nne kama ilivyoahidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo, Wizara itoe kauli ya kuleta marekebisho ya sheria katika mwaka huu wa fedha 2011/2012 ili kupanua wigo wa mikopo kwa wanafunzi wa sheria kwa vitendo. Izingatiwe chuo hiki kilianza toka mwaka 2008, na idadi ya udahili ni ndogo ukilinganisha na idadi ya wahitimu wa toka wakati huo ambapo wengine umaskini wa wazazi wao unawakwamisha wakati nchi ina mahitaji ya Wanasheria na Mawakili.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, Serikali haiwatendei haki Mahakimu na Majaji kikamilifu hapa nchini katika kuwapatia stahiki zao mbalimbali zilizoainishwa Kikatiba na Kisheria.

Pia Serikali ihakikishe kuanzia sasa Mahakimu Wakazi na Wafawidhi wanalipwa *uniform allowance* kama inavyotakiwa kwa kila mwaka. Leo ni zaidi ya miaka miwili hawajalipwa *uniform allowance, is that fair? No.*

Mheshimiwa Spika, Serikali haiwapatii *house allowance* Mahakimu Wakazi kama ilivyo kwa maofisa wengine wa ngazi ya mkoa na wilaya ambao hawajapata nyumba za kuishi. Leo Mahakimu hawana nyumba tena wa mkoa na wilaya halafu viongozi wengine kama vile ma-RPC, RPO, DSO, RMO na kadhalika, wana nyumba na kama hawana nyumba hulipwa *housing allowance*. Je, ndiyo haki na ndiyo namna bora ya ku-promote efficiency mionganoni mwa Mahakimu wetu kwa kuwanyima nyumba na au malipo ya nyumba? Naomba ufanuzi.

Sulala la *responsibility allowance* kutolipwa kwa Mahakimu Wakazi wa Mikoa na Wilaya ni *fair* huku tukijua kuwa watu hawa ni muhimu na wana majukumu mazito. Ni kwa nini wasipatiwe *responsibility allowance* kama ilivyo kwa maofisa wengine? Naomba ufanuzi.

Mheshimiwa Spika, *disposal case allowance* kwa Mahakimu wetu hasa Wakazi wa mikoa na Wilaya kama tunavyojuja nyakati za mchana wanaendesa kesi hawawezi kuandika hukumu huku wakiendesa kesi mchana, mara nyingi hutumia muda wa ziada hasa usiku kuandika hukumu na hivyo kucheleva kulala na hali hiyo kuchangia udhoofu wa afya zao. Ni kwa nini wasilipwe *allowance* ya kufanya kazi nje ya muda wa kazi kama ilivyo kwa watumishi wengine? Nashauri litengwe fungu maalumu kwa ajili hiyo ili kuongeza motisha kwa Mahakimu wetu na wawe wanalipwa kwa mwezi.

Mheshimiwa Spika, mishahara ya Mahakimu wa Wilaya na Mkoa ni midogo tena unakuta Hakimu Mkazi wa Mkoa anzidiwa mshahara na Hakimu wa Wilaya. Mnatumia utaratibu gani? Yaani hakuna heshima kuwa huyu ni wa Wilaya na yule ni wa Mkoa? Maajabu haya. Nawasilishia.

**MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMAR:** Mheshimiwa Spika, sina budi kumpongeza Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Celina Kombani kwa jinsi alivyowasilisha hotuba yake yenyewe kuvutia na kufahamika, tena ya kitaalamu. Pia sina budi kuwashukuru wataalam wa Wizara hiyo akiwemo Katibu Mkuu na Maafisa wote wa Wizara kwa kumsaidia Mheshimiwa Waziri ili kuweza kufanya kazi zake kwa umakini.

Mheshimiwa Spika, Mahakama zimezongwa na mrundikano wa kesi pamoja na msongamano wa mahabusu hasa magerezani na kuitia hasara Serikali kwa kutunza mahabusu. Vilevile kuwaondoshea wananchi upendo na Serikali yao kwa kuona Mahakama hazina uwezo na haraka kumaliza kesi zao, hivyo Mheshimiwa Waziri tatizo hilo la kukawia kwa kesi si ndio kutengeneza rushwa? Naomba jibu.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia walengwa wakuu utakaowakuta Mahakamani wengi wao ni vijana na hii inasababisha vijana wengi kukosa kazi za kufanya, elimu duni. Sasa tunaiomba Serikali kutafuta mbinu mbadala kuwasaidia vijana wetu.

Kuhusu TAKUKURU bado kuna utata kwani hata wanapopata kesi, inakua haina uhuru hadi jalada lipitie kwa Mkurugenzi wa Mashtaka ili ajiridhishe, je, uhalali wa kesi hiyo na TAKUKURU uko wapi? Na hapo ndio rushwa pia kuzaliwa ili kununua haki. Hata hivyo, hiyo ndio njia kuu ya kuzidisha mrundikano wa kesi mahakamani, kesi za rushwa ambazo zinashughulikiwa na TAKUKURU zingekuwa na Mahakama yake na kumaliza kesi zake mwenyewe kulingana na taratibu za sheria, huu ni udhaifu wa Serikali kwa kila kesi iende mahakamani wakati tayari kuna chombo kina uwezo wa kuifanya kazi hiyo, kimsingi TAKUKURU kujipanga na kutumia sheria za nchi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sheria zinazoletwa Bungeni zote huwa za Kiingereza. Hivyo, tunamuomba Mwanasheria na Serikali anapoleta Bungeni alete sheria za Kiingereza na za Kiswahili ili iweze kueleweka na Wabunge wote.

Kwa kuwa mikataba yote lazima ipitiwe na Serikali bado inapokea mikataba ya Kiingereza. Je, Wizara yako haloni kwamba mikataba kabla ya kufikishwa kunakohusika lazima Wizara yako kujiridhisha kuona lugha pamoja na ukweli wa lile tunalokatibiana, ili kukomesha mikataba mibovu iliyorundikana nchini. Vilevile ningiomba Serikali kuajiri Wanasheria katika kila Wizara ili kuzisaidia Wizara zetu na pia kuipunguzia mzigo mkubwa ofisi yako.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Tume hii ni ya Muungano na jambo la Muungano huwa Bara na Visiwani, ningekuomba uangalie haki za watoto na mahabusu kimtazamo Tanzania Bara zipo mahabusu za watoto lakini chache, lakini Tanzania Visiwani hakuna kabisa, je, usalama wa watoto wetu upo chini ya dhamana ya nani? Hatuoni kwamba hilo ni tatizo la kinyume na haki za binadamu na utawala bora? Pia linawadhalilisha watoto kwa mujibu wa kifungu cha 5 cha Sheria ya Watoto Sura ya 58, pamoja na Sheria ya Mtoto ya Namba 21 ya 2009;

Naomba Mheshimiwa Waziri kujibu suala hilo la mahabusu ya watoto Bara na Visiwani. Naunga mkono hoja.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, baada ya kuunga mkono hoja, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri na jinsi anavyofanya kazi zake kwa ushirikiano mkubwa na wasaidizi wake, Wabunge na jamii.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hoja zifuatazo:-

Kwanza ni kuhusu uchache wa Bajeti, nasikitika kuona kwamba Wizara hii ni nyeti na majukumu yake ni makubwa lakini kinachoshangaza ni kuona kwamba Bajeti yake ni ndogo maana itakwamisha utendaji na uamuzi wa kazi zenyewe.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kwa Bajeti ijayo ya mwaka 2012/2013, Bajeti iongezwe ili kurahisisha utendaji katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu haki za watoto, kwa kuwa watoto wana haki ya kuishi na kulindwa kutokana na sheria za nchi hii, inasikitisha kuwa watoto wa Kitanzania wengi wao wapo katika hali ya kunyanyasika na wengi wao kukosa huduma za lazima kama elimu, matunzo na kadhalika. Mfano mkubwa ni ule wa watoto ambao hupatikana na hatia mbalimbali pale ambapo wanapofungwa jela (kifungoni) wengi wao wanachanganyishwa na wafungwa watu wazima ambapo hufanyiwa vitendo visivyo vya haki kwa binadamu, mfano kubakwa na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali isiwachanganye watoto (wafungwa) pamoja na wafungwa watu wazima kwa kuwa inaathiri maisha yao, vinginevyo kujenga mahabusu za watoto katika maeneo mbalimbali katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kuna Wabunge 50 waliomba kuchangia lakini wamekosa. Kwa hiyo, nasikitika kwamba, ndiyo hivyo bila shaka walichangia kwa maandishi lakini inabidi tuendelee, muda huu tulionao haututoshi. Sasa namwita Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, achangie kwa muda wa dakika 25.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipatia nafasi hii ili nami niweze kuchangia hoja ya Mheshimiwa Celina Kombani, Mbunge na Waziri wa Katiba na Sheria na kuliomba Bunge lako kuitisha Makadirio ya Wizara yake ya Katiba na Sheria.

Pili, kabla sijakwenda mbali sana, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya ya mwili, akili na maisha na kutuwezesha kutekeleza majukumu yetu ya utumishi wa umma kwa namna tunavyofanya.

Tatu, namshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kuiongoza Wizara yetu vizuri na hasa katika masuala ya bajeti, nichukue nafasi hii kuwashukuru sana, Wabunge wote waliochangia na hasa Mheshimiwa Sadifa Khamis ambaye namfuata. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia hoja kwa kuandika, kwa kusema na kwa kusikiliza. Michango ya Waheshimiwa Wabunge inatusaidia sana, inatusaidia

kujifunza na nina hakika itatusaidia kuboresha utendaji wetu wa umma katika kuwatumikia Watanzania wenzetu.

Mheshimiwa Spika, suala la bajeti linatokana na mipango na mipango kwa asili na falsafa ya uchumi, na uongozi, inatokana na ukweli kwamba rasilimali siku zote hazitoshi, au kwa Kiswahili safi rasilimali siku zote ni tahfifu, *resources are scarce* au lugha nyingine rahisi kwamba kikombe cha rasilimali siku zote kimejaa au kinakupwa nusu. Kwa ajili hiyo, mipango itatuwezesha kutumia rasilimali hizo kukidhi mahitaji na kwa hiyo msemo wa sungura mdogo ambao unabezwa hapa, unatokana na falsafa hiyo ya kiuchumi ambayo inatumika kwa weledi na uongozi yaani viongozi wanatumiae rasilimali tahfifu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya awali, naomba sasa kujibu baadhi ya hoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Tundu Antiphas Mughwai Lissu, Waziri Kivuli wa Wizara hii ametoa hotuba ambayo kwa kweli imezua mambo mengi. Lakini kama Mheshimiwa Spika ulivyosema jambo kubwa hapa ni kuvumiliana. Kama viongozi, tukisoma Sheria yetu ya Haki za Wabunge ni kuwa waangalifu sana, maneno yanayotoka vinywani mwetu. Hata hivyo, nakiri kwamba hotuba ya Mheshimiwa Tundu Lissu, safari hii ni hotuba ambayo imekuwa *tone down* kuliko hotuba zake zilizopita, kwa hiyo, namshukuru sana.

Hata hivyo, ningependa kuweka kumbukumbu sahihi katika baadhi ya mambo. Mheshimiwa amerejea sheria ya uendeshaji wa Mahakama ambayo ilitungwa na Bunge hili akidai ni kinyume na Katiba. Sasa kwa mujibu wa Kanuni ya 53(8) ya kanuni za Bunge, Mbunge haruhusiwi kufufua jambo ambalo lilikwishaamliwa na Bunge katika Mkutano uliopo au ule uliopita. Maamuzi ya Bunge yalipitishwa kwa mujibu wa Kanuni ya 79, tulipohojwa kwa wanaokubali na wanaokataa, uamuzi ule hauwezi kutenguliwa kwa kauli ya mtu mmoja. (*Makofii*)

Hivyo, sheria hii haiwezi kuwa kinyume cha Katiba ila kama, kwa kutumia haki aliyonayo mtu kwa mujibu kifungu cha 26 cha Katiba cha kuhifadhi Katiba na Sheria za nchi, isipokuwa kama mtu atatafuta haki hiyo Mahakamani. Hadi hapo hatua hiyo itakapochukuliwa na Mahakama kutoa uamuzi, sheria hiyo lazima izingatiwe.

Kuhusu rasimu ya Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, nina hakika Mheshimiwa Waziri mwenzake atakuja kulizungumzia suala hili lakini niseme kitu kidogo, nakala ambayo Mheshimiwa Tundu Lissu amerejea siyo nakala ya rasimu iliyopo. Mheshimiwa Lissu ni mjumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na atakuwa anafahamu kwamba rasimu aliyorejea ilikuwa ni ya kitambo sana. Mheshimiwa Waziri atalizungumzia hilo, lakini ninachowaomba Waheshimiwa Wabunge tusubiri, tusiwalishishe hoja.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine alilozungumzia Mheshimiwa Tundu Lissu, ni uendeshaji wa mashauri ya jinali. Kuna maoni kwamba ofisi ya DPP imeshindwa kufungua na kuendesha mashtaka yanayohusu matukio makubwa ya kifisadi.

Mheshimiwa Spika, ili Mkurugenzi wa mashitaka aweze kufungua kesi dhidi ya mtu yeyote, narudia, ili Mkurugenzi wa Mashitaka aweze kufungua kesi dhidi ya mtu yeyote, ni lazima kisheria na kikatiba, aridhike kwamba upo ushahidi wa kutosha na kama ushahidi huo haupo hataweza kufanya hivyo na huu ndiyo msimamo wangu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, si kila tuhuma, mashtaka yanaandaliwa zile hati za mashtaka kwa ajili hiyo kesi za ujisadi 30, kubwa tumeweza kufungua mashitaka katika kesi 13 ambazo tumeona kuna ushahidi wa kutosha. Kwa hiyo, nashauri kwamba mamlaka ya kikatiba na ulinzi wa haki za watu wengi ni lazima yafuatwe.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja nyingine Mheshimiwa Tundu Lissu amesema kwamba, Mkurugenzi wa Mashtaka aondolewe madarakani kwamba ameshindwa kufungua mashtaka dhidi ya watuhumiwa wengine wa wizi wa mabilioni ya EPA. Kwa kweli, kwanza nampongeza sana Mkurugenzi wa Mashtaka, amefanya kazi nzuri, ametekeleza kazi zake kwa uwazi na uhuru

wake alionao kwa mujibu wa sheria na siwezi kumwingilia hata siku moja na sitaruhusu mtu mwagineye yeyote amwingilie. Kwa hiyo, hakuna sababu za msingi za kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, pia kulitolewa hoja hii si ya Mheshimiwa Tundu Lissu, hii ni hoja ya Mheshimiwa Angella Jasmin Kairuki, alisema vizuri sana. Nimerpongeza sana kwa kutetea Mawakili wa Serikali na tunakuomba ukimaliza kazi hii tafadhalu rudi, ofisi ipo tutumikie umma. Sasa hili alilosema la kutenganisha Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, nadhani hili ni la muundo. Ukweli ni kwamba, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ipo huru na mahusiano yake na kama Mwanasheria Mkuu wa Serikali au Naibu Katibu Mkuu wa Serikali yamebainishwa wazi katika sheria. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu masuala ya kitawala na kisera atapokea maagizo ya Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali na tunafikiri hivyo kuwa inamsaidia yeye kuwa huru katika utekelezaji wa kazi zake. Kama ambavyo nakuwa huru kwenye masuala ya sera kwamba kila ngumi ikirushwa Waziri wa Katiba na Sheria ndio anayeichukua.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la ubambikizaji wa kesi, kwamba kumekuwepo na matukio ambapo watu wengine wanabambikizwa kesi na waendesa mashtaka, hali inapungua lakini napenda kutumia nafasi hii kwa kweli kuwaonya na tayari Mkurugenzi wa Mashtaka amekuwa akichukua hatua za kufuta mashtaka hayo. Kila tukigundua Mkurugenzi wa Mashtaka analeta mashtaka hayo na baadhi yenu Waheshimiwa Wabunge, si kwa sababu ya upendeleo, mliponiletea malalamiko yenu na nikayapeleka kwa Mkurugenzi wa Mashtaka na aliposoma majalada algundua kwamba baadhi ya watu wenu walikuwa wameonewa, lakini baadhi walikuwa na tuhuma za kujibu na sikusita kuwaambia kwamba huyu ana tuhuma za kujibu. Kwa hiyo Mheshimiwa Tundu Lissu, hiyo ndio hali halisi. Mheshimiwa Nyambari Chacha Nyangwine, haya ya Tarime yatafuatiliwa, tumeshamwagiza *DPP* afanye hivyo.

Kuhusu *civilization*, Mheshimiwa Jumaa, Mbunge wa Kibaha, kwa kweli utaratibu huu wa kutenganisha mashtaka ya shughuli za upelelezi ni endelevu, tutafika kila mahali, kila ambapo tutapata nafasi pamoja na rasilimali. Kwa Wilaya ya Tunduru, tayari tumejata ofisi na tumeshaanza kushughulikia taratibu za kufanya ukarabati kutafuta vitendea kazi na kuajiri watumishi ili ofisi hiyo iweze kufunguliwa.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo naweza kulizungumzia ni suala la mikataba, iko tuhuma kwamba mikataba tunayoingia ni mikataba mibovu, naomba kulisemea kidogo hili jambo, si kwa sababu ya kulitetea lakini kwa sababu pia kuwaelimisha kinachotokea. Suala la mikataba, ni suala linalohusu sekta mbalimbali na mkataba wenye una vifungu vinavyohusu mambo mbalimbali na mambo mtambuka. Kuna vifungu vinavyohusu mambo ya fedha. Kwa mfano, riba, namna ya kulipa, ukilipa mapema inakuwaje na vitu kama hivyo. Kuna vifungu vinavyohusu masuala ya ufundi, kwa mfano, kama ni mafuta au kama ni ujenzi wa barabara au kama ni mambo ya *Uranium* na madini wako wataalam wa mambo hayo.

Mheshimiwa Spika, kuna pia masuala ya utatuzi wa migogoro, tukikosana tutatatuwa migogoro hii vipi? Tunakwenda wapi? Tutatumia sheria gani? Sasa haya ni mambo ya wataalam ambayo wanasheria wanapaswa kuyafahamu, sasa kinachotokea ni nini? Mtindo wetu wa elimu, katika nchi nyingine huwezi kuanza kusoma taaluma ya Sheria kwanza utaanza labda kusoma uchumi au utaanza kusoma kitu kingine chochote halafu ya sheria unaifanya kuwa ni ya pili.

Kwa hiyo, suala la *capacity charges*, kwa mfano, linapojitokeza si la Sheria, lakini kwa sababu wa weledi wa eneo hilo utazungumza katika mkondo mmoja na Wataalam wale. Likitokea suala la fedha utajua kwamba mtu anapokwambia *interest* yangu ni *LIBOR plus one or two plus* au kwa siku 365 au kwa siku 360 utajua maana yake kifedha.

Mheshimiwa Spika, mimi nilisoma uchumi na nilisoma Sheria za fedha. Kwa hiyo, unapokwenda ku-negotiate unajua kwamba nikikubali siku 360 napata faida gani na nikikubali siku 365 napata kitu gani, ninapokubali kuchukua riba ya *London Interbank Rate* maana yake ni nini. Pili, kuna vitu vingine ambavyo havijadiliwi katika mikataba, sasa huwezi kulaumu kwamba hapa *interest rate* ungepunguza, kuna vitu vingine havibadiliki hasa mikataba ya Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Wataalam wanawashauri juu ya mambo ya utaalal, wanashauri katika mambo hayo na wanasheria wanashauri katika mambo hayo hayo. Tunachofanya sasa hatukai tukalalamika, tulichoamua kufanya sisi ni kuwaongeza utaalal Mawakili wa Serikali wanaohusika na mambo ya mikataba. Nafahamu ni kazi kubwa inayohitaji rasilimali kubwa lakini pia tuna mpango wa kutumia *Law School* kufanya mafunzo ya muda mfupi katika maeneo maalum ya mikataba. Siyo hiyo tu hata namna ya *psychology* ya kujadiliana kwa maana kwamba unakaa vipi, mdomo wako unaufungua vipi, kama unagonga meza kama mnavyogonga Waheshimiwa Wabunge ugonge na mkono gani. Kwa hiyo, hayo mambo yote ni mambo ambayo unaweza kufikiria kama ni mambo ambayo tunayaita ni *culture* ya *negotiation*. Tupeni muda na nina hakika kwamba nina vijana weledi ambao watafanya kazi hiyo vizuri.

Mheshimiwa Spika, kuna suala lingine ambalo Mheshimiwa Tundu A.M. Lissu alilizungumzia kuhusu kifungu cha 15 cha Sheria ya Haki za Binadamu, kwamba, Kanuni hazijatungwa kuwawezesha watu kufungua kesi kwa mujibu wa Sheria hiyo. Nafikiri kama alivyosema msemajji aliyenitangulia, Mheshimiwa Tundu A.M. Lissu labda alikuwa na haraka tu, kifungu kile kinacho sema kwamba *Chief Justice* atatunga Kanuni hakiweki shurti ila kinasema anaweza yaani *may*. Sasa uksoma Sheria zetu mpaka sasa kesi hizi zinafunguliwa kwa mujibu wa Sheria za taratibu nyingine kama *Civil Procedure Act* na kama wewe ni mweledi wa *JALO* zile Sheria za Uingereza zilizokuwa zinatumika kabla ya tarehe 22/7/1922. Kwa hiyo, utaratibu wa kuwawezesha watu kufungua hizo kesi upo na nafikiri kwamba, siyo vizuri kulaumu kwamba, Jaji Mkuu hajafanya kazi hiyo, nina hakika kwamba jambo hilo halisababishi watu kutofungua kesi Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, kuna mambo mengine ambayo yamesemwa kwenye hotuba hii na nisingependa kuyarudia kwa sababu naona kama Wakili, sijui kama ni Wakili bado, Mheshimiwa Mbunge ameyasema lakini nisingependa kwenda zaidi kwa sababu nafikiri si ya kweli sana na sitaki kumnyong'onyeza mtu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa amesema kwamba, nafikiri Waziri atazungumza lakini naomba kusema kitu kimoja kwamba, Mahakama zetu za juu zimekuwa mabingwa wa kujificha katika kichaka cha masharti ya kiufundi kwa kutupilia mbali kwa sababu tu ya kuwepo makosa ya kiufundi. Sasa kwanza sikubali kwamba Mahakama zetu zinajificha kwenye kichaka cha masharti ya kiufundi, Mahakama zetu zina weledi wa kutosha na Majaji wanaokaa katika Mahakama hizo ukinitoa mimi ambaye nimeondoka kwa muda ni Majaji wenye weledi wa kutosha na wanafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, hii shughuli ya Vyama Vingi kwa kweli Mahakama ya Tanzania imefanya juhudu kubwa sana kutupa mwelekeo wa Vyama Vingi vya Siasa yaani demokrasia na kwa aina ya pekee na nimeshasema mahali pengine kwamba jambo hili namsifu sana Mchungaji Mtikila kwa sababu akiona kitu hakiendi sawasawa anakwenda Mahakamani ...

**SPIKA:** Tumesema Mtikila siyo Msigwa! (*Kicheko*)

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Nimesema Mchungaji Mtikila na siyo Msigwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nafikiri Waheshimiwa Wabunge msiwe na hofu Mahakama zetu zina weledi wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na kwamba Tume ya Haki za Binadamu haina Makamishna, nafikiri Mheshimiwa Waziri atalizungumzia hilo na uzalendo wa watumishi wa Mahakama pia Waziri atalizungumzia kwa sababu ni suala la sera.

Mheshimiwa Spika, suala la Mheshimiwa Joseph Roman Selasini kwamba kwa nini Mawakili wa Serikali wanapewa nafasi ya kwanza kuongea Mahakamani kuliko Mawakili wa Kujitegemea, je, ni wazoefu zaidi? Kwa kweli huo ndiyo utaratibu lakini pia Sheria ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imetungwa na Bunge hili Tukufu kwa lengo la kutoa na kutekeleza utaratibu wa jinsi ya kutenda kazi katika Ofisi hii, taratibu za uendeshaji wa mashauri Mahakamani na taratibu za Mawakili kuitwa Mahakamani zinasimamiwa na Sheria ya Mawakili (Sura namba 341) na Sheria hii inatambua kuwa Wakili namba moja ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye ni msimamizi wa

Mawakili wengine. Kutokana na sababu hizo za Kisheria na kwa msingi huo ndiyo maana Mawakili wa Serikali hata waliotoka masomoni punde wanakuwa wakiitwa mapema kuliko wale wa kujitegemea, ndiyo sababu yenye hiyo.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Waheshimiwa Wabunge kwamba bajeti yetu hii si bajeti ambayo itatuwezesha kufanya kila kitu, lakini kama nilivyosema kikombe kilicho nusu ni kikombe kilichojaa nusu vile vile. Kwa hiyo, tutatumia rasilimali hiyo kwa kadri tunavyoweza kufanya mambo ambayo yatatuwezesha kuvuka na kama kutakuwa na matatizo bila shaka tunaweza kurudi katika utaratibu wa kawaida kuomba nyongeza ya fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante na sasa nitamwita mtoha hoja Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kutoa hotuba yangu na Waheshimiwa Wabunge kunisikiliza na pia kuchangia katika michango yao mbalimbali. Mawazo yao ni mazuri, ni mawazo ya kujenga na naafikiana nao.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, wengi wameongelea masuala ya ufinyu wa bajeti nakubaliana nao, wengi wameongelea kuhusu ukarabati na uchakavu wa Mahakama, nakubaliana nao kwa sababu mwenye macho haambiwi tazama. Kwa hiyo, mawazo mengi tumeyapokea na mengi ni ya kujenga na siyo ya kubomoa. Kwa hiyo, nasema kwamba nawashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, kwa ajili ya umuhimu wenu naomba niwataje Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia kwa kuzungumza na baadaye niwataje wale ambao wamechangia kwa maandishi na wale ambao hawakuchangia ambao walipenda kuchangia kwa maneno watatusamehe, kwa kuwa muda wenyewe ni mdogo lakini tutajitahidi kwa kadri ya uwezo wetu kuhakikisha kwamba tunajibu mengi yale ambayo mmeyaweka kimaandishi na sisii kama hatutafanikiwa kuyajibu yote, naomba Waheshimiwa Wabunge mkubaliane nami, kama muda wa Bunge ungeongezwa mpaka Jumatatu au Jumanne, basi majibu yote yangekuwa yameshapatikana kwa sababu ninayo hapa.

Mheshimiwa Spika, naomba niwataje Waheshimiwa Wabunge hao kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Gosbert B. Blandes, yeeye alisoma kwa niaba ya Kamati; Mheshimiwa Tundu A.M. Lissu ambaye ni Mbunge Kivuli wa Wizara hii...

**SPIKA:** Ni Waziri!

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Waziri Kivuli, Waziri mwenzangu. (*Makof*)

Mheshimiwa Angellah Jasmine Kairuki, Mheshimiwa Maulidah Anna Valerian Komu, Mheshimiwa Muhammad Amour Chomboh alichangia kwa hisia kubwa, Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, Mheshimiwa Raya Ibrahim Khamis, Mheshimiwa Sadifa Juma Khamis na Mheshimiwa Jaji Frederick Mwita Werema, Mwanasheria Mkuu wa Serikali naye alichangia. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa naomba niwataje Waheshimiwa Wabunge ambao walichangia kimaandishi, lakini wengine wamechangia dakika za majeruhi, sasa hivi ndiyo wanatiletea majina yao, lakini nitawataja lakini majibu yao kwa hapa sasa hivi nikiri kwamba sina.

Mheshimiwa Spika, waliochangia kimaandishi ni Mheshimiwa Vincent Joseph Nyerere, Mheshimiwa Aggrey D.J. Mwanri, Mheshimiwa Mariam Nasoro Kisangi, Mheshimiwa Stephen Hillary Ngonyani, Mheshimiwa Jitu Vrajlal Soni, Mheshimiwa Zabein Muhaji Mhita, Mheshimiwa Hawa A. Ghasia, Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes, Mheshimiwa Benardetha Kasabago Mushashu, Mheshimiwa Jasson Samson Rwekiza, Mheshimiwa Henry Daffa Shekifu, Mheshimiwa Highness

Samson Kiwia, Mheshimiwa Engineer Salvatory Naluyaga Machemli, Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi, Mheshimiwa Meshack Jeremiah Opulukwa, Mheshimiwa Athumanji Rashid Mfutakamba, Mheshimiwa Profesa Peter Mahamudu Msolla, Mheshimiwa Ally Keissy Mohamed, Mheshimiwa Dokta Seif Seleman Rashidi, Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mheshimiwa Amos G. Makalla, Mheshimiwa Benedict Ngalamu Ole-Nangoro, Mheshimiwa Faki Haji Makame na Mheshimiwa William Augustao Mgimwa. (*Makof*)

Wengine ni Mheshimiwa Murtaza Ally Mangungu, Mheshimiwa Abdulsalaam Selemani Amer, Mheshimiwa Zarina Shamte Madabida, Mheshimiwa Gaudence Cassian Kayombo, Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, Mheshimiwa Rosweeter Faustin Kasikila, Mheshimiwa Charles John Poul Mwijage, Mheshimiwa Profesa Anna Kajumulo Tibaijuka, Mheshimiwa Joseph Roman Selasini, Mheshimiwa Anthony Gervase Mbassa, Mheshimiwa Susan Anselm Jerome Lyimo, Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mheshimiwa John J. Mnyika, Mheshimiwa Eustace Osler Katagira, Mheshimiwa Angella Jasmine Kairuki, Mheshimiwa Beatrice Matumbo Shellukindo, Mheshimiwa David Zacharia Kafulila, Mheshimiwa Abuu Hamoud Jumaa, Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, Mheshimiwa Sabreena Hamza Sungura, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomar, Mheshimiwa Agripina Zaituni Buyogera, Mheshimiwa Nyambari Chacha Mariba Nyangwine, Mheshimiwa Moses Joseph Machali, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa AnnaMaryStella John Mallac na Mheshimiwa David Ernest Silinde. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mengine pengine yatajirudia, lakini wengine ni Mheshimiwa Felix Francis Mkosamali, Mheshimiwa Ester Nicholas Matiko, Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, Mheshimiwa Vita Rashid Mfaume Kawawa, Mheshimiwa Azza Hillal Hamad, Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo, Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mheshimiwa Deogratias Aloyce Ntukamazina, Mheshimiwa Betty Eliezer Machangu, Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mheshimiwa Mohamed Hamisi Missanga, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Leticia Mageni Nyerere, Mheshimiwa Hamad Ali Hamad, Mheshimiwa David Zacharia Kafulila, Mheshimiwa Dokta Fenella Ephraim Mukangara, Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege na Mheshimiwa Lediana Mafuru Mng'ong'o. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Abdul Rajab Mteketa, Mheshimiwa Rebecca Michael Mngodo, Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, Mheshimiwa Dokta Christina Gabriel Ishengoma, Mheshimiwa Vick Paschal Kamata, Mheshimiwa Mchungaji Israel Yohana Natse, Mheshimiwa Balozi Seif Ali Idd, Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, Mheshimiwa Josephine Tabitha Chagulla, Mheshimiwa Salome Daudi Mwambu, Mheshimiwa Martha Moses Mlata, Mheshimiwa Ester Nicholas Matiko, Mheshimiwa Dokta Kebwe Stephen Kebwe na Mheshimiwa Mathias Meinrad Chikawe. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, Mheshimiwa Moza Abedi Saidy, Mheshimiwa Felister Aloyce Bura, Mheshimiwa Christowaja Gerson Mtinda, Mheshimiwa Suleiman Nassib Omar, Mheshimiwa Assumpter Nshunju Mshama, Mheshimiwa John Paul Lwanji, Freeman Aikaeli Mbowa, Mheshimiwa Rosweeter Faustin Kasikila, Mheshimiwa Neema Mgaya Hamid, Mheshimiwa Juma Sururu Juma, Mheshimiwa Catherine Valentine Magige, Mheshimiwa *Engineer Stella Martin Manyanya*, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Anthony Gervase Mbassa, Mheshimiwa Jerome Dismas Bwanausi, Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati, Mheshimiwa Pudenciana Wilfred Kikwembe na Mheshimiwa Juma Sururu Juma. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba Waheshimiwa ambao sikuwataja, natambua michango yenu na nitajitahidi kujibu kwa kadri ya uwezo wangu. Kwanza, naomba nitoe maeleo kwa masuala ya ujumla kabla sijakwenda kwenye *specific issues* ambazo zimechangiwa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, kwa wale wenye usoefu na Bunge hili, kwamba kila baada ya uchaguzi huwa mara nyangi bajeti zetu aidha, zina utata au aidha ni ndogo sana na sababu ya msingi ya kuwa na bajeti za aina hiyo ni kwamba, tumetoka kwenye uchaguzi, umepewa Wizara

mpya, uanze kujipanga, bajeti inaanza mwezi wa nne, una miezi mitatu tu, kwa hiyo ni lazima uwe mwangalifu katika kupanga vipaumbele.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo sisi kwa upande wetu wengi wamechangia kwamba, bajeti ni ndogo, nakubaliana nao. Hii nimeisema katika changamoto zangu kwamba bajeti hii ni ndogo, lakini naomba tu nitoe mtiririko wa bajeti ya Wizara hii kuanzia mwaka 2007 kama ifuatavyo:-

Kwa mfano, mwaka 2007/2008, bajeti ya Wizara hii ilikuwa shilingi bilioni 66.8/=; mwaka uliofuata wa 2008/2009/= ilikuwa shilingi bilioni 89.9/=; mwaka 2009/2010 ikapanda ikawa shilingi bilioni 107.6/=; mwaka 2010/2011 ikapanda ikawa shilingi bilioni 116.8/= na mwaka 2011/2012 imepanda imekuwa shilingi bilioni 138.7/= Kwa hiyo, kwa mwaka huu ongezeko la bajeti yetu ni shilingi bilioni 22, lakini shilingi bilioni 20 zote zinaingia kwenye Mfuko wa Mahakama ambao Waheshimiwa Wabunge walipitisha sheria yake mwezi Aprili.

Mheshimiwa Spika, sisi tulijipanga katika vipaumbele vyetu tukasema kwamba suala la kwanza tunataka kumaliza kesi, suala la pili ni ukarabati na ujenzi wa Mahakama. Sasa ili kupunguza mrundikano wa kesi ndiyo maana tumepeleka hizo shilingi bilioni 20 tukasema hizi zianzishe Mfuko wa Mahakama na kazi maalum ni kumaliza kesi. Tumeweka kabisa kwa mpangilio kwamba, kila Mahakama itapata kiasi gani, hilo tumejipangia. Kwa mfano, Mahakama ya Rufani, wao watapata shilingi milioni 720, Mahakama Kuu itapata shilingi bilioni 9.1, Mahakama za Hakimu Mkazi watapata shilingi bilioni 8.3, Mahakama za Mwanzo zitapata shilingi bilioni 2.4. Hizi tume-calculate kulingana na cases za Mahakama hizo. Kwa hiyo, *break down* tumeiweka vizuri.

Mheshimiwa Spika, niwaambie Waheshimiwa Wabunge kwamba tumejipangia vizuri, tumedhamiria na tutatekeleza kwa vitendo ili tupunguze msongamano magerezani na tupunguze mrundikano wa kesi Mahakamani. Naomba mtuamini na sisi hicho kidogo tulichopewa tutakitumia vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, suala la uchakavu wa Mahakama na Mahakama kuwa chache. Hilo halina mjadala ndugu zangu kwa sababu ninyi mmetoka huko Majimboni, mnajua hali za Mahakama zetu. Nakubaliana na ninyi kabisa kwamba, Mahakama zetu ni chache na ni chakavu. Wilaya nyingi hazina Mahakama za Wilaya, nakubaliana na ninyi kabisa, karibuni Wilaya 39 hazina Mahakama za Wilaya. Wilaya zilizoanzishwa hivi karibuni zote hazina Mahakama za Wilaya, lakini mkakati wetu ni nini! Mkakati wetu ni kwamba wakati wa kuanzishwa Wilaya mpya na hilo tumekubaliana Serikalini kwamba tutajenga majengo ya Halmashauri, ya DC, lakini pamoja na Magereza na Mahakama yatakuwa *included*. Kwa hiyo, hizo za nyuma tumejipangia tutafanya hivyo, hivyo wale Waheshimiwa wote wenye Wilaya mpya ambaeo wameniuliza swali kuhusu Mahakama katika Wilaya zao, tumejipangia jamani, zile Wilaya 11 zilizoundwa katika Awamu ya Tatoo, zote tuliziombea fedha lakini tatizo liliokuwepo pale ni kwamba, tulikuwa hatujatenga zile Mahakama 20 za nyuma.

Mheshimiwa Spika, pale kwenye Baraza tulikubaliana, wewe Mheshimiwa tumekupa fedha za mwaka jana, hujatumia na wala hujajenga hizo Mahakama 20, kwa nini tukupe fedha nyingine za *development* kwa ajili ya Mahakama hizo! Kwa hiyo, nina uhakika mwaka ujao tutapata fedha za *development* kwa ajili ya Mahakama katika Wilaya mpya na mkakati wetu katika Wilaya zetu mpya za sasa hivi ni kwamba, yakijengwa majengo ya Serikali, yatakuwepo pia na majengo ya Mahakama pamoja na Magereza.

Mheshimiwa Spika, sasa niunganishe na hizo Mahakama 20 ambazo tulizitaja kwenye bajeti iliyopita ambazo hatujajenga; Mahakama hizo tunapata ufadhili kutoka *World Bank* na mchakato wa *World Bank* mnajua ni mpaka upate *no objection*. Kwa hiyo, tumekwishapata hiyo *no objection*, tumekwishatangaza hiyo tenda na Mahakama hizo zitaanza kujengwa mwezi Septemba. Sitaki kuzitaja tena Mahakama hizo kwa sababu ziko kwenye hotuba ya mwaka jana na pia kwenye hotuba yangu katika ukurasa wa 36, aya ya 56. Naomba Waheshimiwa Wabunge msisimame kwenye vifungu na badala yake naomba msome tu katika ukurasa wa 36 na aya ya 56 hizo Mahakama zote 20 nimezitaja.

Mheshimiwa Spika, suala la ujenzi wa Mahakama ya Rufani. Hilo limechangiwa na Mheshimiwa Waziri Kivuli kwa hisia kali kabisa na Mheshimiwa Angellah Kairuki. Waheshimiwa Wabunge kama mtakumbuka Mahakama ya Rufani Tanzania, illanzishwa mwaka 1979 baada ya kuvunjika iliyokuwa Mahakama ya Rufaa ya Afrika Mashariki na ilianza na Majaji watano (5) tu. Tangu kipindi hicho Mahakama ya Rufaa Tanzania hawajawahi kuwa na jengo lao wenyewe. Mwanzoni walijibanza katika Mahakama Kuu, lakini idadi ya Majaji ilivyo zidi kuongezeka katika utawala wa awamu ya Tatu, Serikali iliama kwamba, tukarabati hoteli ya Forodhani, historia ya hoteli ya Forodhani kwa wale wenzangu wa zamani wanajua, ile ilikuwa hoteli na ilikuwa *night club*. Tukasema kwamba aah, tuikarabati kwa kuwa ni jengo la Serikali, wakae pale kwa muda ili waweze kufanya kazi zao vizuri. Pale Mahakama Kuu kwa kweli walikuwa wanajibana mno na hakukua na nafasi yoyote.

Mheshimiwa Spika, niwaambie Waheshimiwa Wabunge kwamba pale wanapokaa Mahakama ya Rufani hapana hadhi ya kukaa Majaji wetu. Kwa kweli hapana hadhi hiyo! Kwa wale ambaa wanatembelea ile Mahakama wakiangalia hata ofisi ya Mheshimiwa Jaji Mkuu, kwa kweli utamhurumia kwa kuwa lile jengo liko kihoteli hoteli kwa *background* yake. Kwa hiyo, hata mimi nawahurumia hao Majaji wa Mahakama ya Rufani. Kwa kweli kupanda na kushuka zile ngazi, ngazi zenye zimejengwa kihoteli hoteli kwa kweli nawahurumia. Tukasema jengo lile wakae kwa muda kwa sababu hawana jengo.

Mheshimiwa Spika, sasa kama Serikali tukaangalia lile na kujuliza kwamba tufanyeje ili tujenge Mahakama yetu ya Rufani yenye hadhi kama zilivyo nchi nyininge! Tukapata mwekezaji, mimi nasema mbia ambaye alisema kwamba, jamani naomba mnipatie jengo hili ili niwajengee Mahakama ya Rufani yenye hadhi.

Sisi kama Serikali tukasema ni jambo zuri na la busara tu, kama tunahamisha makaburi tunajenga maghorofa, hilo nalo ni jema. Kwa hiyo, tulichofanya ni kuongea na yule mwekezaji ili tujenge Mahakama ya Rufani katika Mtaa wa Chimala kwenye kiwanja ambacho kiko mkabala na *Ocean Road*. Mchakato huo haujafika mwisho. Waheshimiwa Wabunge bado tunakaa vikao vyta pamoja kati ya Wizara ya Ardhi, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Fedha, PPRA, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, tutaangalia *procedures* zote za utwaaji wa ardhi na uuzaaj wa mali za Serikali.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kuwaambia Waheshimiwa Wabunge ni kwamba, tutafuata sheria zote, kanuni zote na taratibu zote za utwaaji wa jengo hilo. Hatutakwenda kinyume cha hapo kwa sababu sisi ni Wizara ya Katiba na Sheria, hatuvezi kuwa wa kwanza kuvunja sheria. Kwa hiyo, wale wanaotaka kuandamana sijui kwa ajili ya ile *night club*, ni jengo la kihistoria, mimi binafsi nasikitika kwa kweli kwamba si vema kuendelea kuwaweka Majaji wetu katika jengo lile. Tutajenga jengo lenye hadhi ili Majaji wetu kama mhimili wa dola, wakae kwenye jengo zuri kama hili la Bunge. Kwa hiyo, naomba hiyo *issue* ikija, wanaosema hili limeuzwa, sijui na nini, jamani jengo halijauzwa! Bado tuko katika mazungumzo na mtuache tuendelee na mazungumzo. Nawahakikisha kwamba tutafuata kanuni na taratibu zote, Mwanasheria Mkuu yuko Wizara hii, hatuvezi tukavunja sheria.

Mheshimiwa Spika, labda tu niseme kwamba Serikali inapokuwa na mikakati fulani tusiwe tu na ile roho ya kubeza, kubeza hivi, kama tunahamisha makaburi, hivi kuna kitu kizuri sana kuliko historia ya makaburi! Kama tumehamisha lile kaburi la mtu wa Iringa pale tukapitisha barabara na ilishindikana watu wanajua historia ya lile kaburi la pale Tanangozi, la Kiyeyeu. Kama tumehamisha kaburi la mtu, hivi sembuse hili jengo ambalo ni mali ya Serikali kutwaliwa ili tupate kitu kizuri zaidi! Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge naomba kwa vitu hivi tusiwe tunakatishana tamaa. Ushauri wenu tunasema kwamba tunaupokea, wengi wamesema kwamba tufuate *procedure* na sisi tunasema hivi, tutafuata *procedure*.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni msongamano wa mashauri Mahakamani. Hilo nimekwishalisa kwamba tumeprata hizo fedha na tumejipanga vizuri tu na *bulk load* ya toka mwaka 2009 mpaka leo hii tumeitoa kama kiambatisho kwenye hotuba yangu. Kwa hiyo, tutahakikisha kwamba kesi zote hizi zinamalizika. Msifikirie shilingi bilioni 20 ndiyo bajeti pekee ya umalizaji wa kesi Mahakamani. Bajeti yake ya kawaida ipo, *on top of that* ndiyo ipo hiyo shilingi bilioni 20 kwa ajili ya kuanzisha Mfuko wa Mahakama. Nina uhakika kwamba, Mahakama zetu

zitafanya kazi vizuri na niseme tu kwamba tuwape moyo, watafanya kazi vizuri bila matatizo yoyote. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, naomba niende kwenye maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani. Sina uhakika kama maoni hayo yalikuwa ya kambi ya upinzani au ya mtu binafsi au ya nini, maana yake hapa umekwishaona watu wameanza kupingana pingana. Kwa hiyo, Waziri mwenzangu kama walivyotahadharisha wenzangu, naona mambo mengine tuwe *very careful* hasa kwa Mheshimiwa ambaye ni mwanasheria.

Mheshimiwa Spika, Wanasheria wako *very selective* na maneno yao wanayoongea. Hata Majaji wangu pale unaona hata kutembea kwao kuko tofauti na sisi, hata maneno yao yako tofauti na sisi! Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri mwenzangu namwomba tu aige mfano wa wale *learned friends*. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Sadifa alivyosema kwamba, Rais anachaguliwa kwa mujibu wa Katiba, amechaguliwa na wananchi, waliogombea ni wengi lakini ye ye kapata asilimia sitini na moja (61%), Rais kwa mujibu wa Katiba ni Mkuu wa Nchi. Rais kwa mujibu wa Katiba ni Amiri Jeshi. Kwa hiyo, Rais pale hajipachiki tu, yupo kwa ridhaa ya wananchi na kwa mujibu wa Katiba. (*Makof!*)

Mheshimiwa Waziri mwenzangu naona ana haraka kweli na ana usongo kweli na madaraka ya Rais. Namwomba tu avute subira, ameiwahisha mada, ana usongo na madaraka ya Rais. Naomba wakati wa kuchangia Katiba, kutakuwa na uwanja mpana, kwa hiyo, atajimwaga kwa mapana na marefu, kwa nguvu zote, jithada zote na yake yote ya tumboni yatatoka, lakini kwa sasa hivi naona ameiwahisha mada kujadili wakati tuko kwenye mchakato tu. Niungane tu na Mheshimiwa Muhammad Amour Chomboh na Mheshimiwa Sadifa, kwa maneno yao. Nasema kwamba, kwanza, Mheshimiwa Tundu Lissu amewasilisha mchakato wa Katiba. Naijuliza hivi ni kwa idhini ya nani! Hivi Waziri kivuli siku hizi anaruhusiwa kuwasilisha Miswada Bungeni! (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, niombe tu tuangalie kanuni zetu kama Miswada inawasilishwa na Mawaziri Vivuli! Tuelewe kwa sababu ninavyoelewa Muswada huu bado mchakato wake haujawkisha. Kwa hiyo, nasema kwamba ameiwahisha mada, tena niseme tu bila idhini yangu kwa sababu mimi ndiye Waziri wa Katiba na Sheria. (*Makof!*)

Waheshimiwa Wabunge, Muswada huo alioutoa Mheshimiwa Tundu Lissu labda ni maoni yake tu. Ndiyo maana tunabeba drafti, bado ziko katika *level* ya Kamati, unalibeba mgongoni unakuja nalo Bungeni. Jamani kanuni zinaruhusu! Muswada nilionao mimi yaani uko tofauti kabisa na bado na-*consult* wadau. Jana bahati nzuri jamani niliwaeleza kwamba tumefikia wapi! Sasa bahati nzuri au mbaya Mheshimiwa Tundu Lissu naona aliandika hiyo hotuba yake kabla hajaangalia hotuba yangu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nasema kwamba katika kujadili mambo ya Katiba Mheshimiwa Tundu Lissu kwa kweli ametoa maneno ya uchochezi na sina uhakika kwamba Kambi Rasmi ya Upinzani wote kwa ujumla wenu mlipitia hotuba yake. Nina uhakika kwamba, kama mngepitia msingeruhusu maneno ya uchochezi kama yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, mustakabali wa Taifa letu usiwekwe mikononi mwa Wazanzibari, hususan katika kura za maoni na ridhaa ya Rais wa Serikali ya Zanzibar. Hayo ni maneno ya uchochezi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, lingine ni Wajumbe wa Tume ya Katiba wasishughulikie masuala ya kikatiba, washughulikie masuala ya Kikatiba ya Muungano tu. Hayo ni maneno ya uchochezi. Wazanzibari wapige kura ya maoni kwa mambo ya Muungano tu. Haya ni maneno ya uchochezi.

Rais wa Zanzibar atoe ridhaa kwa mambo ya Muungano tu. Huu ni uchochezi. Wakati umefika kwa wananchi wa Tanzania Bara na Zanzibar kuamua kama wanataka kuendelea na Muungano, au la! Nasema hivi, hatujaanza kujadili Katiba mpya! Wakati haujafika! Sasa

nakubaliana na wale wanazuoni wanao-*argue* kwamba Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1977 imeandikwa na watu wachache na nini na nini. Sasa wamesema wananchi hawakushirikishwa, lakini naona dallii za vikundi vya watu wachache wanaotaka kuhodhi Katiba mpya. Nasema hivi kwa nini! Haya maneno haya Watanzania wa kawaida wakiyasikia wanayachukua na kuyaweka vichwani. Sasa mtu mmoja asije akawa-*drag* Watanzania wote kwa masuala yake haya. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nasema tunapokwenda kwenye kuandika Katiba, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, Katiba sio lelemama, Katiba ni Sheria Mama. Kama tunataka ku-*politicize* mambo ya Katiba, hatutafika mahali pazuri, kama tutaanza kuwapotosha Watanzania kama tulivyoanza na Muswada, watu wameubeba tu, wakaenda nao huko, wanapiga nao kelele, tukienda hivyo hatutafika. Kwa hiyo, nasema ni vema kabisa yaani upande wa Upinzani muwe mnapitia hizo hotuba kabla, asije akaja mtu mmoja tu akaandika madudu yake hapo halafu nyie wote mkaonekana wabaya. Kwa hiyo nasema kwamba ni vema jamani mambo haya yanatakiwa busara, hekima na ile karama aliyotupa Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu ametupa karama kila binadamu hapa tuzitumie vizuri hizo karama zetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Kivuli pia amesema sijasemea lolote kuhusu bajeti haitoshi hasa kwenye fungu 18. Jamani kwenye changamoto ukurasa wa 49 *paragraph* ya 72 nilisema changamoto mojawapo ni ufinyu wa bajeti. Waheshimiwa Wabunge, nafikiri mlinisikia na waliosoma hotuba yangu wameliona hilo. Sasa Mheshimiwa Tundu Lissu sijui alitaka niende barabarani nikapige kelele kwamba bajeti haitoshi, ni kwa faida ya nani. Jamani sisi tumefundishwa protokoli na mimi ni Afisa Utumishi nimekaa Serikalini, kama nimeshindwa ku-*argue* kwenye *Cabinet* siwezi nikaja hapa kupiga kelele hadharani, kwamba, jamani hiki hakitoshi, jamani hili halifanyi nini. Nawashukuru kwamba mmeliona lakini sipendi sana kukaa hadharani au kupiga kelele au sijui Mheshimiwa Tundu Lissu alitaka nilie kwamba bajeti ndogo au nini? Kwa hiyo, nasema kwamba hilo tumeliona, Wabunge mmeliona, yeze amesema tutoe kwenye fungu 98 na nimesema tukubali, fungu 98 fedha zile zitoke kwenye Jimbo lake pengine haoni huo umuhimu wa barabara.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni tuhuma nzito dhidi ya ujisadi wa Mahakama. Jamani hiyo ni tuhuma nzito. Nasema hivi ni vema tukawa na ukweli, maadamu ametwambia hilo tutalifuatilia kwa karibu na kama kuna ujisadi wowote tutachukua hatua. Lakini tuhuma hizo ni nzito zinatakiwa tufuatilie kwa uangalifu. Labda Mheshimiwa Tundu Lissu kwenye taarifa nyingi alizoandika humu, bahati nzuri taarifa nyingi tulizitoa kwenye Kamati na bahati mbaya Mheshimiwa Tundu Lissu katika vikao ambavyo tulikuwa tunawasilisha bajeti alikuwa hayupo. Kikao cha kwanza alikuwa Nyamongo, kikao cha pili alikuwa wapi sijui, sasa utayapataje hayo maendeleo na utekelezaji wa Wizara hii na wewe ukiwa Waziri Kivuli wakati uhudhuri kwenye vikao husika. Kwa hiyo, ni vema akahudhuria hata hivyo vikao, ni vema tu na ni busara tu akahudhuria hivyo vikao ili akayapata vizuri ya Waziri mwenzio katika vikao hivyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo alilisema Waziri mwenzangu ni Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora haina Mwenyekiti wala Makamishna. Tayari majina tunayo, barua zao watazipata wiki hii, majina yameshatoka, kwa hiyo, kwa ujumla masuala ambayo Mheshimiwa Mbunge aliyasema ni hayo hapo. Namshukuru sehemu nyingine ameeleza masuala *genuine*, lakini sehemu nyingine ame-overdue.

Mheshimiwa Spika, nianze kujibu maswali ya wachangiaji mmoja mmoja. Kuna suala la Mheshimiwa Mbowe ambalo amesema kwamba Mahakama ya Mwanzo ya Machame katika Wilaya ya Hai, Jimbo la Hai imehamishiwa Bomang'ombe. Wilaya hiyo ya Hai na Jimbo hilo hilo la Hai. Hao wana mgogoro, kila upande wameniletea maelezo yao lakini nitatumia busara zangu. Nitakwenda Hai kuangalia huo mgogoro njiridhishe ili nitoe maamuzi wapi Mahakama hiyo ijengwe. Kama naona itachelewa shida ya Mahakama ziko nyingi nitachukua hizo fedha nihamishie kwenye Mahakama nyingine mpaka wamalize hiyo migogoro yao.

Mheshimiwa Spika, limegusiwa kidogo suala la Mahakama ya Kadhi. Suala la Mahakama ya Kadhi Mheshimiwa Waziri Mkuu ameshaunda Kamati Ndogo. Kwa upande wa Serikali wako Wajumbe wafuatao. Bwana Mtupa na sasa hivi ni Bwana Malaba kutoka Ofisi ya Mwanasheria

Mkuu wa Serikali; Bibi Leila Mgonya, Ofisi ya Waziri Mkuu; Bwana Jacob Sarungi, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na Bwana Adam Mambi, Tume ya Kurekebisha Sheria. Kwa upande wa Waislamu ni Sheikh Suleiman Kilemle, Sheikh Abubakar Zubeir, Alhaj Said Al-Amour, Sheikh Hamad Mussa, Bwana Abdallah Matumia ambaye ni Mwanasheria Mkuu wa BAKWATA na Bwana Issa Maige Mwanasheria wa Kujitegemea. Vikao wameshakaa, mwisho tutakuja kuambiwa ni nini walichoamua. Lakini Serikali imelichukua suala hili *serious*, Waheshimiwa Wabunge naomba niwape tu taarifa hii fupi kwamba, linafanyiwa kazi bila ya matatizo yoyote. Kwa hiyo, naomba tu Mheshimiwa Mbunge patoshe tu kwa kuwa suala hili linashughulikiwa.

Mheshimiwa Spika, hoja za Wabunge ni kuhusu kutafsiri sheria, Wabunge wengi tu wameongelea hili suala la kutafsiri sheria kwa lugha ya Kiswahili. Tumejipangia *road mark*, tuna mpango kabisa *action plan* ya kutafsiri hizo sheria awamu ya kwanza, awamu ya pili na awamu ya tatu, kwa hiyo nisingependa kuzisoma awamu zote tatu hizi, kama Mheshimiwa Mbunge anahitaji tutampatia tu aone hayo mabadiliko na tulivyojipangia mpangilio wetu.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko ya Sheria ya Mirathi na Ndoa imechangiwa hasa na akinamama wenzangu wengi tu kwamba, hilo limeshafanyiwa kazi na Tume ya Kurekebisha Sheria, wameleta Ofisini kwangu, nimeshaandaa Muswada wa kupeleka kwenye Baraza la Mawaziri kwa ajili ya kuandaa *White Paper* ili kukusanya maoni ya watu wengi zaidi. Jamani Sheria za Ndoa na Mirathi ni sheria tete inahitaji kwa kweli maoni ya watu wengi zaidi kuliko sisi tukijifungia ofisini tuanze kuyazungumza hayo halafu tuje hapa muanze kutu-*challenge* kwamba hamkushirkisha wadau na kadhalika na kadhalika. Ile *White Paper* nafikiri itawasaidia wengi sana kufahamu nini maana ya Sheria ya Ndoa, vipengele gani ambavyo watu wengi wanataka virekebishwe na vipengele hivyo jamani Waheshimiwa Wabunge wengi wameandika hasa wale Wabunge wanawake.

Mheshimiwa Spika, siwezi kuzitaja zote, wao wanasesma suala la umri wa kuoau kuolewa uongezwe, utaratibu wa kufunga ndoa za dharura ufutwe, utaratibu uliopo wa kusajili ndoa za kimila ubadilishwe, kukomesha dhana inayotambua uhusiano wa mwanamke na mwanamume wanaoshi muda mrefu bila kufunga ndoa, wamekaa tu muda mrefu sasa kutambulika kuwa ni ndoa, hilo hawalitaki na mambo mengi tu, kuainisha haki za wanandoa katika mgawanyo wa mali. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wanawake wenzangu hayo tumeyachukua na tutayafanya kazi.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni mikopo kwa wanafunzi wa Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria ambalo limetolewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala Mheshimiwa William Mgimwa, Mheshimiwa Eustace Katagira, Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mheshimiwa John Mnyika, Mheshimiwa Sadifa Juma Khamis, wote hao wameongelea kuhusu suala la *Law School*. Wizara imepokeea ushauri wao na kwa sasa utaratibu maalum unaandalialiwa kwa ajili ya mikopo hiyo. Hivyo, naomba nisisitiza kwamba wanafunzi wote wanaohitaji kwa sasa hivi wanapewa mikopo hiyo. Lakini tunatafuta utaratibu wa kudumu kwa sababu huu ni utaratibu wa muda na tunaongea na wenzetu wa Bodi ya Mikopo nao walione suala hili. Pia suala la kuangalia mtaala mzima wa Shahada ya Sheria maana yake vyuo vingine miaka mitatu, vingine miaka minne. Kwa hiyo, hilo nalo tunallangalia ili huo mtaala wa sheria uwe *uniform* na uweze kukidhi mahitaji na hao wenzetu wa *Law School* waweze kupata ufumbuzi wa kudumu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Shekifu aliongelea kuhusu Chuo cha Lushoto. Tunasema kwamba chuo kile tunakiangalia vizuri tu na tunataka tujenge hosteli yenye uwezo wa kuchukua wanachuo 300, pia katika mwaka 2011/2012, ujenzi wa hosteli ya pili utaanza na shilingi milioni 500 zimetengwa na ujenzi wa hosteli nyingine mbili, nao pia uko katika mpango wetu. Jengo la Mahakama ya Rufani naona nimeshaliongelea na suala la elimu ya Katiba wakati wa mchakato wa Katiba mpya Mheshimiwa Ignas Malocha na wengine ni kweli, ni vema kabla ya kuanza kuandika Katiba mpya kutoa elimu kwa wananchi na hilo liko katika mkakati wetu na mpango kazi wetu.

Mheshimiwa Spika, masuala mengine Waheshimiwa Wabunge yaliyochangiwa Mheshimiwa Diana Chilolo ameleezea kuhusu Mahakama ya Mwanzo ya Utemi, Singida, hiyo imekamilika. Fedha za Samani ziko tayari, kwa hiyo, usiwe na wasiwasi. Mheshimiwa Ally Keissy

Mohamed ye ye ameongelea kuhusu Mahakama ya Wilaya ya Nkasi haina jengo la Mahakama. Wilaya ya Nkasi kwa kweli haina jengo la Mahakama, tumebadilisha tu sasa hiyo iko kwenye mpango mkakati wetu wa kujenga Mahakama katika Wilaya 39 na Nkasi ni mojawapo. Kwa hiyo, katika bajeti ijayo hilo naona totalitilia mkazo sana.

Mheshimiwa Profesa Msolla ucheleweshwaji wa kesi nimesema muarobaini umepatikana, hizo fedha kidogo tulizopewa za kuanzisha Mfuko wa Mahakama, hizo ndizo zitakazotuongoza na zitapunguza msongamano wa kesi. Mheshimiwa Susan Lyimo anasema pamoja na juhudu kubwa za uteuzi wa Majaji bado kesi zinachukua muda mrefu. Nimesema muarobaini ni Mfuko wa Mahakama, fedha zipo tutapunguza kwa kiasi fulani. Mheshimiwa Meshack Opulukwa ye ye ameongelea kuhusu Mahakama Kuu ya Shinyanga, tunasema mkandarasi yuko *site*. Mheshimiwa Charles Mwijage anasema upungufu wa Mahakimu, Mahakama pia watumishi na vitendea kazi. Hilo tumeliona, kwa mwaka huu tumenunua pikipiki chache tutazitawanya katika sehemu mbalimbali. Kwa upande wa ajira tutajiri kuna nafasi ambazo tumeziomba 150, nazo zitapunguza makali. Mahakama ijipange vizuri kusimamia Mfuko wa Mahakama, Mheshimiwa Ole-Nangoro, nimesema tukishatunga kanuni, tukishamteua *Chief Court Administrator* tutajipanga vizuri ili kuhakikisha kwamba fedha hizi zinagawanywa vizuri.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Job Ndugai Mahakama ya Wilaya ya Kongwa ni ndogo iongezwe. Tukipata fedha tutajitahidi kuhakikisha kwamba Mahakama hizi zinakarabatiwa na zinaongezwa na zinakuwa za kisasa zaidi. Eneo la Kibaigwa wanahitaji Mahakama ya Mwanzo, kwa kweli ni jambo jema na kweli Kibaigwa imekuwa sana na inahitaji na katika mipango yetu nafikiri hilo totalifanya kazi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Tibajuka ye ye anasema kumaliza kesi ndio tumesema muarobaini tumeshaupata. Waheshimiwa Wabunge wamepitisha Mfuko wa Mahakama na tunategemea mwaka ujao mtatupangia nydingi zaidi kama zile za Mfuko wa Bunge. Wanasheria wengi waajiriwe hilo nimeshasema. Mama Zarina Madabida ye ye ameliongelea hilo na Mheshimiwa Malocha kwamba tutajiri Mahakimu 150 na wengi tutawapanga hasa katika sehemu zile ambazo hazina Mahakimu kabisa na wale ambaa niliwaahidi kwenye maswali mbalimbali, tutahakikisha tunawapatia.

Mheshimiwa Spika, upungufu wa Mahakimu wa Mahakama, Mheshimiwa Mfutakamba hiyo ni changamoto, tukipata hao Mahakimu tutahakikisha tunaangalia mambo hayo. Mheshimiwa Machemli ye ye amesema Rais aondolewe madaraka hasa ya kuteua Majaji. Nasema hilo lingoje kwenye Katiba mpya sasa hivi anawateua kwa mujibu wa Katiba.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Mahakama ya Mvomero, ndugu yangu Mheshimiwa Makalla. Sisi tumejipanga kwamba katika bajeti ya mwaka ujao tutahakikisha kwamba hizi Mahakama 39 ambazo tumezipa kipaumbele zikiwa pamoja na hizo Wilaya tutahakikisha kwamba tunajenga. Kama tumeweza kujenga lile ghorofa la Mkuu wa Wilaya, ghorofa la Mkurugenzi sembuse Mahakama ni eneo dogo tu. Kwa hiyo hilo tumeliona na tutajitahidi kuhakikisha kwamba tunajijenga hizo Mahakama. Waheshimiwa Wabunge michango ilikuwa ni mingi na sio rahisi kuijibu yote kwa muda huu, naomba tu niwashukuru wote kwa michango yenu, michango yenu yote majibu yako hapa na tutajitahidi kwamba tunatengeneza kitabu kwa ajili ya kutoa majibu hayo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

(*Hoja ilihamuliwa na Kuafikiwa*)

## KAMATI YA MATUMIZI

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Hii Wizara inasimamia vyombo vingi sana. Sasa tutaanza kule wanakosimamia halafu Wizara tutaenda mwishoni maana nyle mnataka mshahara wa Waziri. Ngoja tumalize mafungu mengine hayo halafu mje mshahara wa Waziri, tukiishia hapo hapo basi. Katibu.

## Fungu 12 – Tume ya Utumishi wa Mahakama

Kifungu 1001 - *Administration and General*.....Sh. 492,534,100/=  
Kifungu 1002 - *Finance and Accounts*.....Sh. 100,078,000/=  
Kifungu 1003 - *Procurement Management Unit*....Sh. 42,913,700/=  
Kifungu 1004 - *Internal Audit Unit*.....Sh. 35,386,300/=  
Kifungu 1005 - *Recruitment, Appointment  
and Confirmation*.....Sh. 281,486,300/=

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 1006 - *Ethics and Discipline Section*.....Sh. 169,906,300/=

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona. Nilikuwa naulizia *sub vote 1006, item 220600*, juu ya *clothing, bedding footwear and services* kwa sababu naona imetengewa sifuri na hivi karibuni Waheshimiwa Wabunge wengi watakuwa wanajua kwamba kumekuwa kuna tatizo la Mahakimu wa Kazi pamoja na Wilaya kutokupewa fedha kwa ajili ya mavazi yao kwa maana ya *uniform*. Sasa kwa mwaka huu naona imewekewa sifuri kabisa.

Mheshimiwa Waziri naomba ufanuzi na tuna takribani hivi sasa zaidi ya miaka miwili Mahakimu wetu wanalalamika hamjawapatia fedha kwa ajili ya kununua *uniform*. Naomba ufanuzi juu ya hili kwa nini hamjawatengea fedha zozote?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni Tume ya Mahakama kwanza hilo alielewe. Fedha zao zipo katika *item 220600* kwenye Fungu la *Administration* na lingine lile alilosema kuhusu Mahakimu hawapo kwenye *vote* hii.

**MWENYEKITI:** Hili ni Fungu la Tume ya Utumishi wa Mahakama.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

## Fungu 16 – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Kifungu 1001 - *Administration and General*.....Sh. 2,153,048,000/=  
Kifungu 1002 - *Finance and Accounts*.....Sh. 511,260,000/=  
Kifungu 1003 - *Planning Division*..... Sh. 643,637,000/=

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 1004 - *Internal Audit Unit*.....Sh. 443,297,000/=

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira yangu ni kuhoji kifungu namba 230600, kinachozungumzia *routine maintenance and repair of machineries*. Ninavyoamini kifungu hiki kinahusisha na magari ambayo idara hii inatumia. Inaonyesha hapa hawajatengewa fedha je, Waziri anatuambia nini kuhusu hili?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtutura *item* hiyo inahusu *internal audit unit* nafikiri swali lako bado lipo hivyo hivyo?

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado swali langu lina hoji.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fungu hili lipo katika Fungu la Utawala na akiangalia pale kwenye *item 230400* ataona kuna ongezeko hapa. Unajua sasa hivi mambo mengi Waheshimiwa Wabunge niwaambie tunayaweka kwenye utawala kwa ajili ya *bulk purchase*.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 1005 - <i>Information, Education and Comm.</i> .....	Sh. 327,071,000/=
Kifungu 1006 - <i>Legal Registry Unit</i> .....	Sh. 319,647,000/=
Kifungu 1007 - <i>Procurement Management Unit</i> ..Sh. 345,048,000/=	
Kifungu 1008 - <i>Research and Library Service Unit</i> ..Sh. 353,063,000/=	
Kifungu 1009 - <i>Management Information System Unit</i> .....Sh. 423,572,000/=	
Kifungu 2002 - <i>Public Prosecutions Division</i> .....Sh. 0	

(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kifungu 2003 - <i>Legislative drafting</i> .....	Sh. 1,148,951,000/=
--	---------------------

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 2003, *Legislative Drafting* kasma 220100, *Office and General Supplies and Services* ambacho kinaonyesha kimekuwa kutoka shilingi milioni 108 mpaka milioni 247. Sasa kwenye hotuba ya Waziri kwenye taarifa ya utekelezaji inaonesha kwa mwaka wa fedha wote uliopita Idara hii ili *draft Miswada 12* tu ambayo ni pasi ndogo sana ya *drafting* ya Miswada. Nataka kujua kama hii *increment* ya pesa kwenye *office and general supplies and services* ina tija yoyote katika kuongeza kasi ya idara husika katika kutengeneza Miswada ama kama sivyo basi pesa hizi wazihamishie mahala kwininge ambako kutasaidia kwenye uandishi wa Miswada.

**MWENASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba kulikuwa na Miswada 12, Miswada 12 si kazi ndogo, ni kazi kubwa lakini fedha hizo zimeongezwa kwa sababu ya kununua vitu vingine vya uchapishaji vya ofisi hiyo kwa ajili ya mawasiliano kati ya Mwandishi Mkuu wa Sheria na Mpigachapa Mkuu wa Serikali.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kifungu 2004 - <i>Zone Office - Arusha</i> .....	Sh. 0
Kifungu 2005 - <i>Zone Office - Dodoma</i> .....	Sh. 0
Kifungu 2006 - <i>Zone Office - Dar es Salaam</i> .....	Sh. 0
Kifungu 2007 - <i>Zone Office - Iringa</i> .....	Sh. 0
Kifungu 2008 - <i>Zone Office - Moshi</i> .....	Sh. 0
Kifungu 2009 - <i>Zone Office - Kagera</i> .....	Sh. 0
Kifungu 2010 - <i>Zone Office - Mbeya</i> .....	Sh. 0
Kifungu 2011 - <i>Zone Office - Mtwara</i> .....	Sh. 0
Kifungu 2012 - <i>Zone Office - Mwanza</i> .....	Sh. 0
Kifungu 2013 - <i>Zone Office - Ruvuma</i> .....	Sh. 0
Kifungu 2014 - <i>Zone Office - Sumbawanga</i> .....	Sh. 0
Kifungu 2015 - <i>Zone Office - Tabora</i> .....	Sh. 0
Kifungu 2016 - <i>Zone Office - Tanga</i> .....Sh. 1,148,951,000/=	
Kifungu 3001 - <i>Civil and International Law Division</i> .....Sh. 1,609,386,000/=	

(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kifungu 4001 - <i>Constitutional Affairs and Human Rights</i> .....	Sh. 924,521,000/=
---	-------------------

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufanuzi kuhusiana hicho kifungu 4001 programu 40 Katiba.

Nimeangalia Kasma zote ambazo zimeainishwa katika kifungu na sijaona kasma yoyote inayohusu mchakato wa kwanza kutunga hii Sheria ya mapitio ya Katiba na pili mchakato wa Katiba wenye. Nilifikiri labda litakuwa kwenye fungu 41 Wizara ya Katiba na Sheria lakini vilevile huko hakuna fungu lolote ambalo limetengwa kwa ajili ya mchakato wa Katiba. Naomba ufanuzi wa Mheshimiwa Waziri. (Makof)

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizo zipo Hazina. Kwa sababu Tume haijaundwa na kitu chochote hakijafanyika kwa hiyo, ipo kwenye Mfuko wa Hazina.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninaomba maelezo ya kifungu kidogo 220800 *Training Domestic*. Ukiangalia mwaka jana na mwaka huu hakuna fedha yoyote iliyotengwa kwa ajili ya mafunzo ya ndani lakini kuna mafunzo ya nje. Nilikuwa naomba ufanuzi kutoka kwa Waziri ni kwa nini watumishi hawa hawawi-trained wakati wanazungumzia masuala mazima ya Katiba? (*Makofii*)

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *training* ipo utawala na akiliangalia fungu la utawala limeongezeka.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika maelezo ya Mheshimiwa Waziri...

**MWENYEKITI:** Tunaenda kwa vifungu!

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye fungu hili hili kuhusiana na *Constitutional Affairs and Human Right*.

**MWENYEKITI:** Kifungu gani?

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kuulizia kuhusu hii *issue* ya Katiba.

**MWENYEKITI:** Kifungu gani?

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni programu hii ya 40 kuhusiana na *Constitutional Affair and Human Right*. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ngoja kwanza Mheshimiwa, hiyo ndiyo *heading* ya programu 40. Sasa wewe unataka *item* gani katika hivi viliviyokuwa *narrated* hapa? Mheshimiwa Tundu Lissu alisema hajaona mahala popote. Sasa wewe unakwenda wapi? (*Makofii*)

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka kuhoji maelezo aliyoatua Mheshimiwa Waziri.

**MWENYEKITI:** Kwamba nini?

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Yeye ametueleza kwamba fedha zipo Hazina sasa sijui zimeelekezwa katika fungu gani kwa sababu ilipaswa kuwa hapa. Kifungu

**MWENYEKITI:** Huwezi kuuliza mara ya pili katika suala liliolizwa. Mheshimiwa Mnyika. (*Makofii*)

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *sub-vote* hiyo hiyo 4001 kuna Kasma ya 221100 *Travelling out of country* pamoja na Kasma 230700 *routine maintenance and repair* ambayo inaonyesha *ime-shoot* kutoka shilingi laki tano mpaka milioni 4.5. Maelezo yaliyotolewa na Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake ni kwamba kutokana na umuhimu wa Katiba, Wizara imeamua hii iwe ni Idara kabisa na iipe uzito kwa jambo hili la Katiba.

Lakini ukiangalia mgawanyo wa rasilimali kwenye hizo kasma hauonyeshi kama kweli Wizara imeamua kulipa kipaumbele suala la Katiba. Sasa naomba ufanuzi tu wa suala la matumizi *in line* na ambayo yamezungumzwa na Wizara. Kwa maana ya mchakato wa Katiba suala la Sheria lipo chini ya Wizara. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Sasa tusijadili, hapa hatujadili. (*Makofii*)

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Ndiyo nataka nipate uafanuzi. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Naomba sana tuelewane, tumewaachia kwenye mshahara wa Waziri mnasema lakini hapa hapana. Hapa unatikiwa kuuliza hiki kilichoandikwa ni cha kufanya nini na si zaidi ya hapo. Kule kwenye mshahawa wa Waziri utaongea. Naomba uulize tena hatujakuelewa. (*Makofii*)

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naomba kuuliza kwamba hiki kilichoandikwa hapa *routine maintenance and repair of office equipment and appliances* ambacho kimepanda mwaka wa fedha uliopita kilikuwa shilingi 500,000; mwaka huu kimepanda mpaka milioni 4.5 pamoja na safari za nje mwaka wa fedha uliopita zilikuwa shilingi milioni 146 mwaka huu zimepanda mpaka shilingi milioni 255 halafu Idara haina pesa *specific* za Katiba inategemea Hazina. Sasa je, tuna hakika kweli mchakato wa Katiba utafanyika? (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Wewe jibu hili la pili hizo hela zilizopanda ni za kitu gani. Hiyo habari ya Katiba sio. Msijifunze kuzomea, sio hapa. Tunaendelea. (*Makofii*)

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mimi nafikiri Mheshimiwa Mnyika angetusifu kwa kuongeza hela kidogo kwamba katika Bajeti zetu tukipewa *ceiling* tunaweka vipaumbele. Kwa hiyo, na hapa hilo tumeliwekea kipaumbele ndiyo maana tunaongeza fedha. (*Makofii*)

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

#### Fungu 18 – Mahakama Kuu

Kifungu 1001 - *Administration and General (RHC)*.....Sh. 5,648,632,500/=

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *Item 22100, travelling out of country.* Ukiangallia utaona kwamba kuna ongezeko la zaidi ya shilingi milioni 300 ukilinganisha na mwaka jana ninaomba uafanuzi kwa nini kumekuwa na ongezeko kubwa namna hiyo katika kifungu hicho? (*Makofii*)

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo fedha za *training inside* au *training outside* utakuta...

**MWENYEKITI:** *Traveling.*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** *Travelling*, utakuta tumezi-centralize zipo *administration* na akienda kwingine huko ataona kwamba baadhi ya sehemu hakuna fedha za aina hiyo. Kwa hiyo, zimeongezeka kwa sababu vifungu vingine vina zero kwa sababu zote zipo utawala.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 1002 - *Arusha Zone*.....Sh. 494,176,000/=  
Kifungu 1003 - *Dar es Salaam Zone*.....Sh. 2,768,884,000/=  
Kifungu 1004 - *Dodoma Zone*.....Sh. 337,423,000/=  
Kifungu 1005 - *Mbeya Zone*.....Sh. 475,837,000/=  
Kifungu 1006 - *Iringa Zone*.....Sh. 304,773,000/=  
Kifungu 1007 - *Mtvara Zone*.....Sh. 333,350,000/=  
Kifungu 1008 - *Mwanza Zone*.....Sh. 578,849,000/=  
Kifungu 1009 - *Songea Zone*.....Sh. 329,224,000/=  
Kifungu 1010 - *Tabora Zone*.....Sh. 489,634,000/=  
Kifungu 1011 - *Sumbawanga Zone*.....Sh. 360,896,000/=

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 1012 - *Bukoba Zone*.....Sh. 303,393,000/=

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uafanuzi kidogo kuhusiana na hicho kifungu cha 1012 kinachohusu Mahakama Kuu, Kanda ya Bukoba.

Mheshimiwa Waziri katika Bajeti yake aliliambia Bunge hili kwamba Jengo la Mahakama Kuu ya Kanda ya Bukoba limeshakamilika na limeshakabidhiwa na kama nilimwelewa sawasawa imefanyika mwaka huu. Lakini hata hivyo kwenye hili Fungu la 1012 zimetengwa shilingi milioni sita kwenye kasma ya 230200 *routine maintenance and repair of buildings*. Nilidhani jengo hili ni jipya na hizi fedha ni kwa ajili gani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa umeionta? Haya majibu!

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi jengo likiwa jipya, bomba likiharibika hutawenza kuli-maintain? Kwa hiyo, ni *maintenance* ya vitu vidogo vidogo; bomba, umeme na kadhalika. Hatuwezi tukajenga jengo jipya halafu tukasema tulache tu, tusipangie hela yoyote. (*Makofi*)

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 1013 – *Tanga Zone*.....Sh. 323,545,000/=

Kifungu 1014 – *Moshi Zone*.....Sh. 368,091,000/=

Kifungu 1016 – *Resident Magistrate Courts*.....Sh. 4,182,794,500/=

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

#### **Fungu 19 – Mahakama za Wilaya na za Mwanzo**

Kifungu 1001 – *Administration and General* .....Sh. 2,511,849,000/=

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nipo kifungu kidogo 220600 kinachohusiana na mavazi (*clothing, bedding, footwear and services*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia utaona kwamba kwa mwaka huu zimepungua zaidi ya shilingi milioni 120, na hapo hapo tunaambiwa kwamba Mahakimu wanaongezeka. Sasa ninataka kujua kwa Bajeti hii kuwa ndogo kuliko ya mwaka jana maana yake siyo kwamba Mawakili wetu watakosa *uniform*?

**MWENYEKITI:** Umekiona kifungu hicho? Naomba maelezo, kimepungua toka milioni 200 mpaka milioni 100. (*Makofi*)

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi zimepungua kutokana na ufinyu wa Bajeti, tusingekuwa na njia nyingine.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 1002 – *District Courts* .....Sh. 5,627,073,000/=

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 1003 – *Primary Courts* .....Sh.11,030,414,000/=

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kifungu 1003, Kasma 210300 na Kasma 210400; inaonyesha kwamba posho (*personal allowances – discretionary*) zinashuka. Mwaka wa pesa uliopita ziliikuwa milioni 497, mwaka huu zinakwenda kuwa milioni 361. Na *personal allowances – optional* zinabaki vilevile milioni 2.4 kwa miaka miwili mfululizo. Nataka uafanuzi tu, kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu ya Wazee wa Mabaraza ya Mahakama ikiwemo Mahakama za Mwanzo Jimboni kwangu Ubungo kuhusiana na posho zao. Nataka kujua kama je, huku kushuka kwa hizi posho kwenye Mahakama za Mwanzo kunaathiri vilevile

upatikanaji wao wa posho wao pamoja na watendaji wengine wa Mahakama za Mwanzo kwa kiwango ambacho kinaleta malalamiko mengi? (Makof)

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na Fungu 210300 hizo *personal allowances*, zile *statutory payments* za wafanyakazi. Sasa likizo mwaka huu mtu anapata posho, mwaka mwingine hapati posho, kwa hiyo, utakuta kwamba zinabadilika badilika hata Bajeti yake inabadilika badilika kwa sababu siyo miaka yote watu wanapata posho za aina hiyo.

Suala la pili la *personal allowances – discriptional or optional*, hizi ni za *honorarium*. Sasa sisi hatukuona sababu ya kuongeza hela kwenye *honorarium*, tukaona kwamba ibaki ile ile ya mwaka jana. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hela za Wazee wa Baraza hizo zipo kwenye *item 260500 – current subsidies to households and unincorporated business*. Kifungu hicho 260500 ndiyo zipo huko. (Makof)

**MWENYEKITI:** Zipo bilioni moja sabini na...

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Eeh, ndiyo maana umeziona zipo nyingi huko.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi naulizia kuhusiana na hii kasma namba 220800 juu ya *training domestic*. Kwa sababu tukiangalia katika mwaka wa fedha 2010/2011 ilikuwa ni takriban shilingi milioni 265. Lakini katika mwaka huu wa fedha wa 2011/2012 naona kuna sifuri. Sasa sjui Serikali inataka kutueleza kitu gani kuhusiana na Mahakimu wetu ambao pengine wanapenda kuendelea na kujiendeleza katika suala zima la kujisomea? Naomba ufanuzi Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu Mheshimiwa aangalie fungu la *Administration - 1001, item 220800 – Training Domestic* ataziona kwamba zimeongezeka nyingi sana, ni kwa sababu hiyo. (Makof)

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naangalia kasma namba 230200 – *routine maintenance and repair of buildings* ambayo imewekewa shilingi milioni 20. Na vilevile kasma 411000 – *rehabilitation and other civil works* ambayo imewekewa shilingi sifuri, zote hizi zinahusu Mahakama za Mwanzo. Naomba ufanuzi. (Makof)

Kwa uelewa wangu, kumekuwa na Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria ambayo kwayo kulikuwa na mradi mkubwa wa kujenga majengo kumi ya Mahakama na kukarabati majengo kumi chakavu ya Mahakama. Sasa kwenye *rehabilitation and civil works* ni sifuri. Huu mradi wa *ku-rehabilitate* majengo ya Mahakama za Mwanzo ambayo yamechakaa kwa nini umewekewa shilingi sifuri? Na vilevile hizi zingine *routine maintenance and repair of buildings* milioni 20 kwa Mahakama zote za Mwanzo Tanzania, hii fedha inatosha Mheshimiwa Waziri?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Tundu Lissu aende kwenye *subvote 1001, item 230200 – routine maintenance and repair of buildings*. Akiangalia kulikuwa na zero zero, sasa ikapanda ghafla ikawa milioni 106, hizo ndizo hela za ukarabati. Pia akienda kwenye *development*, iwapo tutafika, kwenye Bajeti ya mwaka jana ndiyo kulikuwa na zile Mahakama 20. Kwa hiyo, Bajeti yake ni ile ya mwaka jana.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

#### Fungu 35 – Division ya Mashitaka

Kifungu 2002 – *Public Prosecutions Division*....Sh. 1, 262,431,000/=

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kifungu 2002, Kasma 210100 – *Basic Salaries Pensionable Posts* na Kasma 210300 – *Personal Allowances Non-Discretionary*. Inaonyesha kwenye Idara hii ya uendeshaji wa mashitaka, mishahara imeshuka kutoka shilingi

milioni 968 mpaka milioni 565, wakati posho zimeongezeka kutoka shilingi milioni 97 mpaka milioni 140. Ningeomba nipewe ufanuzi, kumekuwa na malalamiko mengi ya udhaifu wa Idara hii kwenye kusimamia mashitaka.

**MWENYEKITI:** Hee, upewe ufanuzi tu! Haya!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Sasa nilitaka nipaye ufanuzi, kushuka huku kwa mishahara kwenye hii Idara na kuongezeka kwa posho kama kutasaidia kutatua hili tatizo la uwepo wa malalamiko ya mashitaka mengi yasiyofanyiwa kazi ukiwemo na ujisadi! (*Makofi*)

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naona Mheshimiwa Mnyika, ameisoma tu *subvote* 2002, lakini akiangalia huku kwenye zones, mishahara yao ipo. Kwa hiyo, asione kwamba imepungua, ila imewekwa kwenye zones husika. Suala la pili la *personal allowances non-discretionary*, kama nilivyosema hizo ni *statutory payments*. Wanavyoongezeka watumishi na *statutory payments* zinaongezeka. Kwa hiyo, ndiyo maana kuna ongezeko hilo. Kwa hiyo, ni jambo jema tu kwamba wale watumishi wanaongezeka wanaongezewa hizo *allowances* zao ambazo ni za lazima. (*Makofi*)

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu killipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 2004 – *Zonal Office Arusha*.....Sh. 487,833,000/=  
Kifungu 2005 – *Zonal Office Dodoma*.....Sh. 362,271,000/=

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 2006 – *Zonal Office Dar es Salaam*.....Sh. 969,120,000/=

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufanuzi, zone ya Dar es Salaam, 2006, hizi *basic salaries*, 210100 ambazo kuna *increment*, mwaka wa fedha uliopita ziliwa milioni 409, mwaka huu zimepanda mpaka milioni 457 ambalo ni jambo jema. Sasa kitu ambacho naomba ufanuzi, maelezo allyoyatoa Waziri kwamba fungu la mishahara kwenye *Public Prosecution* limeshuka kwa sababu mishahara imepelekwa kwenye zone halina usahihi kwa sababu mwaka wa fedha uliopita zone ziliwa zina mishahara, lakini fungu la *DPP* bado likawa na mishahara mkubwa, *Public Division for Prosecution*. Kwa hiyo, maelezo haya hayakuwa sahihi kabisa. Kwa hiyo, ningeomba ufanuzi wa lile jambo la kupungua kwa mishahara kwa kiwango kikubwa ile *total*. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mboma na wewe hapa siyo sahihi kwa sababu zinaonekana zimeongezeka kuliko mwaka jana! Hayo maelezo yako hayafanani na hii. (*Makofi*)

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nieleweke...

**MWENYEKITI:** Muda wenyewe umekwisha...

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Maelezo ambayo aliyatoa ni kwamba wame-transfer pesa kutoka *central office*, kwenye Idara wamepeleka kwenye kanda. Sasa *transfer* ya pesa ingeongeza hizi pesa za Dar es Salaam zaidi ya kiwango kilichoongezwa, kwa sababu hapa ukiangalia *gap* ni nusu. Kwa hiyo, wangeweza kuongeza zaidi pesa kwenye Dar es Salaam kama hiyo *transfer* kweli ingefanyika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika mboma maelezo yako *yana-contradict?* Hapa imeongezeka na kule imepungua!

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu killipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

(*Hapa wachezaji wa Simba Sports Club wallingia sehemu ya kukaa wageni Bungeni na kuketi*)

**MWENYEKITI:** Simba wanaingia, lakini muwaache waingie kwanza! (*Kicheko/Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Simba hao!

**MWENYEKITI:** Karibuni wageni muingie kimya kimya tu halafu tutawatambulisha baadaye! Tunaendelea! (*Makofii*)

Kifungu 2007 – *Zonal Office Iringa*.....Sh. 185,489,000/=

Kifungu 2008 – *Zonal Office Moshi* .....Sh.373,735,000/=

Kifungu 2009 – *Zonal Office Kagera* .....Sh.326,694,000/=

Kifungu 2010 – *Zonal Office Mbeya* .....Sh.391,715,000/=

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 2011 – *Zonal Office Mtwara*.....Sh. 176,298,000/=

**MWENYEKITI:** Aaa alisimama Raya! Sikukuona! (*Makofii*)

**MHE. RAYA IBRAHIM KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekeiti, ninaomba ufanuzi katika kifungu 2011, zone ya Mtwara, katika 230700 – *routine maintenance and repair of office, equipment and appliances* kwamba haikutengewa pesa kabisa na majengo yake hayaridhishi kabisa. Kwa hiyo, ninaomba kupata maelezo zaidi kutoka Waziri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, umeona? *Repair and maintenance ni vote 2011 Mtwara Zone, 230400 – routine maintenance and repair of vehicles and transport equipment*, ina hela hiyo! Ehe, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais...

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Mwenyekeiti, mpaka mwaka juzi Ofisi ya Mwanasheria Mkuu Mtwara walikuwa wanakaa kwenye jengo lao ambalo sasa limekuwa *condemned*. Kuanzia sasa wanapanga kwenye ofisi nyininge. Kwa hiyo, siyo ya kwao. Mwenye ofisi anai-maintain. (*Makofii*)

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 2012 – *Zonal Office Mwanza*.....Sh. 539,260,000/=

Kifungu 2013 – *Zonal Office Ruvuma*.....Sh. 215,383,000/=

Kifungu 2014 – *Zonal Office Sumbawanga*.....Sh. 159,226,000/=

Kifungu 2015 – *Zonal Office Tabora*.....Sh. 377,717,000/=

Kifungu 2016 – *Zonal Office Tanga*.....Sh. 396,740,000/=

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 2017 – *Zonal Office Shinyanga*.....Sh. 178,071,000/=

**MHE. JOHN M. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekeiti, kifungu hicho, Kasma 210100 – *basic salaries pensionable posts* ambayo imeshuka kutoka milioni 115 mpaka milioni 47 kwa Kanda ya Shinyanga.

Mheshimiwa Mwenyekeiti, bado sijaridhika na maelezo kabisa ya Serikali kuhusu jambo hili, kwa sababu ukiangalia pesa ambazo zilipunguzwa kule ili kugawanya kwenye Kanda ni milioni 360+.

**MWENYEKITI:** Eeh, sawa tumekuelewa, lakini hapa...

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Lakini zilizoongezwa kwenye Idara zimeshuka na nyininge zimeshuka kabisa siyo kuongezeka kama hii ya Shinyanga ambayo imeshuka badala ya kuongezeka. Kwa hiyo, naomba *explanation*. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Sawa, kwa maana hiyo *argument* yako ina msingi. Mheshimiwa Waziri, umeelewa alichokisema kwamba maelezo ya kule kwamba zimekuwa *zonalized*, hapa mbona zimepungua? (*Makofi*)

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inatokana na kuwahamisha Wanasheria wa Serikali kutoka kwenye kituo hicho kwa sababu ya *reshuffle*. Kwa hiyo, zile fedha haziwezi kubaki kwa idadi ile ile ndiyo maana zimepungua pale. (*Makofi*)

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 2018 – *Zonal Office Singida*.....Sh. 146,438,000/=  
Kifungu 2019 – *Zonal Office Lindi*.....Sh. 104,776,000/=  
Kifungu 2020 – *Zonal Office Mara*.....Sh. 145,039,000/=

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

#### Fungu 40 – Mahakama

Kifungu 1001 – *Administration and General*.....Sh. 7,197,686,000/=

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufanuzi kuhusu kasma 220700 inayohusu *rental expenses*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha ambazo zimetengwa kwa ajili ya kodi zinaelekea kushuka kutoka shilingi milioni 351 mwaka uliopita mpaka milioni 265 mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezungumza sana juu ya tatizo la madeni yasiyolipika ya Mahakama yanayohusiana na hizi kodi, hizi *rental expenses*. Naomba ufanuzi wa Mheshimiwa Waziri, kwa nini hizi fedha za kodi ya pango zimeshuka badala ya kuongezeka wakati tatizo la kutolipwa kwa kodi za pango limekuwa ni tatizo kubwa sana. Ahsante. (*Makofi*)

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii imepungua kutoptana na Serikali kujenga baadhi ya nyumba za Majaji. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Alhaj Missanga!

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni katika mshahara wa Waziri, si ndiyo?

**MWENYEKITI:** Hatujafika huko!

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Basi, naomba radhi. Ahsante sana! (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Makamba!

**MHE. JANUARY Y. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ilikuwa ni mshahara wa Waziri kwa hiyo tutasubiri. (*Kicheko*)

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 1002 - *Finance and Accounts Unit*.....Sh. 458,690,000/=

Kifungu 1003 - *Internal Audit Unit*.....Sh. 308,180,000/=

Kifungu 2002 - *Court of Appeal Dar es Salaam*.Sh. 22,006,156,000/=

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

#### Fungu 55 – Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora

Kifungu 1001 - *Admnistration and General*.....Sh.1,624,705,660/=  
Kifungu 1002 - *Finance and Accounts*.....Sh.172,734,940/=  
Kifungu 1003 - *Internal Audit Unit*.....Sh. 89,106,000/=

(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kifungu 1004 - *Legal Services*.....Sh. 206,578,000/=

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nipo kwenye kifungu hicho kipengele kidogo cha *Training Domectic* kipengele kidogo cha 220800, hapa Tume hii imetengewa shilingi milioni 1.2 tu na Tume hii ni muhimu sana na haina watalaam na haina watumishi wa kutosha na ni Tume ambayo inasaidia sana kutetea haki za wananchi vijiji. (*Makofi*)

Je, fedha hii ya milioni 1.2 itatoa *training* kwa watumishi wangapi ili kuhakikisha kwamba haki kwa wananchi inapatikana? (*Makofi*)

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kwa sababu ya *cealing*, lakini hizi hela ndogo ambazo zimetengwa ni kwa ajili ya *training* za hapa hapa ndani. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Anasema hazitoshi. (*Makofi*)

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu kwamba hazitoshi, kwanza ni sababu ya *cealing*, ambaye yupo *training* ni mtu mmoja tu ndio maana tumetenga hizo hela. (*Makofi*)

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kifungu 1005 - *Procurement Unit*.....Sh. 91,232,000/=  
Kifungu 1006 - *Management Information system Unit*.....Sh.193,114,300/=  
Kifungu 2001 - *Admnistrative Justice*.....Sh.575,492,000/=  
Kifungu 2002 - *Human Rights*.....Sh. 354,006,000/=  
Kifungu 2003 - *Research and Documentation*.....Sh.156,428,000/=  
Kifungu 2004 - *Public Education and Training*.....Sh.183,961,700/=

(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kifungu 3001 - *Zanzibar Office*.....Sh.171,314,400/=

**MWENYEKITI:** Muda wenyewe umeisha, hebu angalieni saa.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru jambo dogo tu, Kifungu hicho 3001 Kasma 229900 *operating expenses* kwa upande wa Ofisi ya Tume ya Haki za Binadamu Zanzibar, *trend* ilikuwa milioni 27 mwaka uliopita ikawa milioni 31 halafu ghafla fedha za uendeshaji kwa Ofisi ya Tume ya Haki za Binadamu zimeshuka mpaka milioni moja, sasa je, kwa hiyo milioni moja kweli hiyo Ofisi inaweza kufanya kazi ipasavyo kule Zanzibar za kuratibu masuala ya Haki za Binadamu?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ofisi yoyote ni lazima uigharamie sana, kwa hiyo miaka miwili ya nyuma ndio maana umeona hela nyingi kwa ajili ya *operating expenses* lakini mwaka huu kutoptana na *cealing* tumetengewa milioni moja hazitoshi, lakini ndio *cealing* ilivyoturuhusu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba hela nyingi kwenye haki za binadamu tuliona ni vema na busara tukatenga kwenye mambo ya *education*, ndio maana unaona *sub-vote* iliyopita hela zimeongezeka kwa kiasi kikubwa. (*Makofi*)

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nilikuwa naomba kumuuliza Waziri kuhusiana na kifungu kidogo 220400 kinachohusiana na masuala ya afya. Ukiangalia utaona kwamba kwa mwaka huu hawajatengewa kitu chochote na mimi naamini hawa ni binadamu wanaweza wakaugua wakati wowote, je, wakiugua watatibiwa katika fungu lipi? (*Makofi*)

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi *vote za medical expenses ukiangalia kwa ujumla zote tumezi-lump* kwenye utawala. Kwa hiyo, Fungu la Utawala kama ataangalia limeongezeka na fedha zake zipo katika fungu la utawala.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

**MWENYEKITI:** Kwa mujibu wa Kanuni ya 104(1) kwa hiyo tunaingia kwenye *guillotine stage*.

#### **Fungu 59 – Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania**

Kifungu 1001 - *Admnistration and General*.....Sh.1,457,633,000/=

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

#### **Fungu 60 - Mahakama ya Kazi Tanzania**

Kifungu 1001 - *Admnistration and General*.....Sh.1,186,044.000/=

Kifungu1002 - *Arusha Zone*.....Sh. 95,079,000/=

Kifungu 2002 - *Dar es Salaam Zone*.....Sh. 62,801,000/=

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

#### **Fungu 64 – Mahakama ya Biashara Tanzania**

Kifungu 1001 - *Admnistration and General*.....Sh. 1,248,872,000/=

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

#### **Fungu 90 – Mahakama ya Ardhi**

Kifungu 1001 - *Admnistration and General*.....Sh.1,217,996,000/=

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

#### **Fungu 41 - Wizara ya Katiba na Sheria**

Kifungu 1001- *Admnistration and General*.....Sh. 3,010,129,200/=

Kifungu 1002 - *Finance and Accounts*.....Sh. 240,748,800/=

Kifungu 1003 - *Policy and Information Services*.. Sh. 308,180,000/=

Kifungu 1004 - *Internal Audit*.....Sh. 85,779,300/=

Kifungu1005 - *Information Edu. and Comm*.....Sh.154,782,100/=

Kifungu 1006 - *Procurement Mgn. Unit*.....Sh.148,199,200/=

Kifungu 1007 - *Management Inf. System Unit*.....Sh.151,567,500/=

Kifungu 2004 - *Public Legal Services Unit*.....Sh. 297,939,800/=

Kifungu 2005 - *Legal Reform Unit*.....Sh. 0

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

#### **MIPANGO YA MAENDELEO**

#### **Fungu 16 – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali**

Kifungu 1001 - <i>Admnistration and HR Management</i> .....	Sh. 0
Kifungu 1002 - <i>Finance and Account</i> .....	Sh. 0
Kifungu 1003 - <i>Planning Division</i> .....	Sh. 945,000.000/=
Kifungu 1004 - <i>Internal Audit Unit</i> .....	Sh. 0
Kifungu 1005 - <i>Information Edu. and Communication</i> .....	Sh. 0
Kifungu 2002 - <i>Public Prosecutions Division</i> .....	Sh. 0
Kifungu 2003 - <i>Legislative Drafting</i> .....	Sh. 0
Kifungu 3001 - <i>Civil and International Law Divsion</i> .....	Sh. 0
Kifungu 4001 - <i>Constitution Affairs and Human Rights</i> .....	Sh. 0

(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

#### **Fungu 18 - Mahakama Kuu**

Kifungu 1001 - <i>Admnistration and General (RHC)</i> .....	Sh. 0
Kifungu 1016 - <i>Resident Magistrate Courts</i> .....	Sh. 0

(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

#### **Fungu 19 – District and Primary Courts**

Kifungu 1002 - <i>District Courts</i> .....	Sh. 0
Kifungu 1003 - <i>Primary Courts</i> .....	Sh. 0

(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

#### **Fungu 35 – Division ya Mashtaka**

Kifungu 2002 - <i>Public Proscution Division</i> .....	Sh. 5,663,957,000/=
--	---------------------

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

#### **Fungu 40 - Mahakama**

Kifungu 1001 - <i>Admnistration and General</i> .....	Sh.13,546,091,000/=
Kifungu 2002 - <i>Court of Appeal Dar es Salaam</i> .....	Sh. 0

(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

**MWENYEKITI:** Tunaomba movement zinazohusika jamani tutulie kidogo. Tuendelee.

#### **Fungu 41 – Wizara ya Katiba na Sheria**

Kifungu 1001- <i>Admnistration and General</i> .....	Sh. 200,000,000/=
Kifungu 1003 - <i>Policy and Information Services</i> .Sh.15,467,754,000/=	
Kifungu 1004 - <i>Internal Audit Unit</i> .....	Sh. 0
Kifungu 1005 - <i>Information Edu. and Communication</i> .....	Sh. 0
Kifungu 1006 - <i>Procurement Management Unit</i> .....	Sh. 0
Kifungu 1007 - <i>Management Inf. System Unit</i> .....	Sh. 0
Kifungu 2004 - <i>Public Legal Services Unit</i> .....	Sh. 0
Kifungu 2005 - <i>Legal Reform Unit</i> .....	Sh. 0

(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

#### **Fungu 55 – Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora**

Kifungu 1001 - <i>Admnistration and General</i> .....	Sh. 332,850,000/=
Kifungu 1004 - <i>Legal Services</i> .....	Sh. 22,840,000/=

Kifungu 1006 - *Management Information system Unit*.....Sh. 91,638,000/=  
Kifungu 2001 - *Administrative Justice*.....Sh. 51,410,000/=  
Kifungu 2002 - *Human Rights*.....Sh. 269,660,000/=  
Kifungu 2003 - *Research and Documentation*.....Sh. 29,520,000/=  
Kifungu 2004 - *Public Education and Training*.....Sh. 27,000,000/=

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

#### **Fungu 59 – Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania**

Kifungu 1001 - *Administration and General*.....Sh. 616,350,000/=

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

#### **Fungu 60 – Mahakama ya kazi**

Kifungu 1001 - *Administration and General*.....Sh. 1,665,200,000/=

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

#### **Fungu 64 – Mahakama ya Biashara**

Kifungu 1001 - *Administration and General*.....Sh. 1,391,340,000/=

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

#### **Fungu 90 – Mahakama ya Ardhi**

Kifungu 1001 - *Administration and General*.....Sh. 430,000,000/=

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

(*Bunge lilirudia*)

**SPIKA:** Nitatumia kifungu cha kuongeza muda mpaka tumalize kazi.

Waheshimiwa Wabunge, nina masikitiko makubwa kwamba kwa miaka mingine Wizara hii hatutaipa siku moja, maana yake imetupa usumbufu mkubwa kweli, *tuli-under estimate*, vile vitengo vyake kumbe ni vingi sana kuliko Wizara nyingine yoyote. (*Makofii*)

#### **TAARIFA**

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imeyapitia Makadirio ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka 2011/2012 Kifungu kwa Kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko, hivyo naomba kutoa hoja kwamba Makadirio hayo sasa yakubaliwe na Bunge lako Tukufu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, naafiki. (*Makofii*)

(*Hoja ilitolewa lamuliwe*)

(*Hoja illamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Makadirio ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012 yalipitishwa na Bunge*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyowaeleza kwanza niwapongeze Wizara na watu wake wote, Waheshimiwa Majaji na watalamu wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri mnayoendelea kufanya, tunatambua kwamba hela yenu ni ndogo, lakini nadhani baada ya kuanzisha ule Mfuko wa Mahakama nadhani utaratibu utaendelea vizuri zaidi kuliko ilivyo hivi sasa. (*Makofî*)

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyowaambia pia tumejifunza kwamba Wizara hii mwaka mwingine hatutaipa siku moja kwa sababu tumeionna imechanganya watu kabisa. (*Makofî*)

Hata hivyo, napenda kutangaza kwamba wale wageni wetu wa timu ya Simba tulisema wapo njiani wamefika ili muweze kuwashangilia kwa ushindi ambao waliupata katika mchezo wa Ngao ya Hisani na pia mchezo wa jana. Kwa hiyo, wapenzi wa Simba wote mnawenza kuwashangilia, naomba timu ya Simba msimame. Ahsanteni sana, karibuni na poleni na safari. (*Makofî*)

(*Hapa Wachezaji wa timu ya Simba walismama na kuonyesha Ngao ya Hisani*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kifungu cha kuongeza muda mpaka kazi ya matumizi ipite ndiyo hiyo tu hatuna kazi nyingine zaidi ya hapo, naona watu wamesimama hapa hawana nafasi hiyo. (*Makofî*)

Waheshimiwa Wabunge, lakini pia Mheshimiwa Muhammad Chomboh anaomba Wabunge Wazanizbar wote wakutane *basement* saa saba na nusu.

Waheshimiwa Wabunge, naomba nisitishe shughuli za Bunge mpaka saa kumi jioni.

(*Saa 7.18 mchana Bunge lilitfungwa mpaka saa 10.00 jioni*)

(*Saa 10.00 jioni Bunge lilitrudia*)

(*Hapa Wabunge Fulani walihoji kuhusu kutokuwepo akidi ya Mawaziri Bungeni*)

**SPIKA:** Hatufanyi maamuzi kwa hiyo, watafika, lakini tungkuwa tunafanya maamuzi tungeahirisha kikao, sasa siyo. Endelea Mheshimiwa Waziri.

#### **Hoja za Serikali**

#### **Makadirio na Matumizi ya Fedha kwa Wizara ya Fedha kwa Mwaka 2011/2012**

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea, kujadili na kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha kwa mwaka wa fedha 2011/2012. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge wote, kwa kuendesha majadiliano ya Bajeti ya mwaka 2011/2012 kwa umakini tangu yalipoanza tarehe 10 Juni, 2011 ambayo nilianzisha mimi mwenyewe hadi hii leo ninapopata fursa hii ya kuyahitimisha. (*Makofî*)

Aidha, nawashukuru Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati mbalimbali za Bunge kwa michango na ushauri waliotoa wakati wa kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara, Idara na Mikoa. Michango na ushauri wao utaendelea kuzingatiwa katika utendaji wa Serikali kwa lengo la kuboresha utoaji wa huduma kwa umma. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kuwashukuru kwa namna ya pekee Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi chini ya Mwenyekiti wao mahiri Mheshimiwa Dkt. Abdallah Omar

Kigoda, Mbunge wa Jimbo la Handeni kwa maoni, ushauri na mapendekezo waliyoyatoa. Wizara imezingatia ushauri na mapendekezo ya Kamati katika kukamilisha uandaaji wa hotuba hii. Aidha, napenda kueleza kuwa maoni hayo pamoja na yatakayotolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati wa kujadili hoja hii yataendelea kuzingatiwa wakati wa utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2011/2012. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba pia niwashukuru Naibu Mawaziri wa Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Gregory George Teu na Mheshimiwa Pereira Ame Silima kwa ushirikiano mkubwa wanaoendelea kunipa katika kutekeleza majukumu yangu na pia mchango wao mkubwa katika maandalizi ya Bajeti hii. (*Makofii*)

Namshukuru Katibu Mkuu Ndugu Alhaji Ramadhani M. Khijjah na Naibu Makatibu Wakuu Ndugu Elizabeth J. Nyambibo, Ndugu Laston T. Msongole na Dkt. Servacius B. Likweli kwa kazi nzuri wanayoifanya. Aidha, napenda kuwashukuru Profesa Benno Ndulu, Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania na Ndugu Harry Kitilya, Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania. (*Makofii*)

Hali kadhalika ninawashukuru Makamishna, Wakurugenzi, Wakuu wa Taasisi, Wakuu wa Vitengo na wafanyakazi wote wa Wizara ya Fedha na Taasisi zake kwa kazi nzuri na ushirikiano wao mkubwa wanaonipa. Ninawaomba wadumishe ushirikiano wanaonipa ili Wizara iendelee kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ili kuweza kufanikisha usimamizi wa utekelezaji majukumu kwa ufanisi, Wizara imegawanya katika mafungu manne ya Kibajeti. Mafungu hayo ni Fungu 50 - Wizara ya Fedha; Fungu 21 - Hazina; Fungu 22 - Deni la Taifa na Fungu 23 - Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali. Vilevile, Fungu 45 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ambayo inajitegemea, linaombewa fedha Bungeni na Waziri wa Fedha kwa mujibu wa Sheria. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara ilijiwekea malengo yafuatayo:-

Kwanza kuandaa na kutekeleza sera za uchumi jumla zinazolenga kukuza Pato la Taifa kwa asilimia 7.0; pili, kuhakikisha kuwa kasi ya upandaji wa bei haizidi asilimia 5 ifikapo mwezi Juni, 2011; tatu, kukusanya mapato ya ndani kufikia asilimia 17.3 ya Pato la Taifa kwa mwaka 2010/2011; nne, kusimamia Mapato na Matumizi ya Serikali yaliyokadiriwa kufikia jumla ya shilingi bilioni 11,609.6; tano, kufanya tafiti na kutoa taarifa kuhusu hali ya uchumi na kiwango kilichofikiwa katika kuondoa umaskini; sita, kufikisha huduma za mikopo na utoaji wa elimu ya ujasiriamali kwa walengwa; saba, kuendelea kusimamia utekelezaji wa miradi chini ya Mpango wa *Millenium Challenge Account (MCA-T)* na kutoa taarifa za utekelezaji; nane, kuboresha mazingira ya utendaji kazi na kuwapatia mafunzo watumishi wake kwa lengo la kuinua kiwango cha utoaji huduma kwa umma; tisa, kuboresha na kuimarisha mawasiliano ya Teknolojia ya Habari na kumi, kusimamia sekta ya fedha nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mapato na Matumizi ya Mafungu ya Wizara kwa mwaka 2010/2011 Fungu 50 – Wizara ya Fedha Wizara ililenga kukusanya mapato yasiyo ya kodi ya kiasi cha shilingi bilioni 53.49. Hadi kufikia Juni, 2011 kiasi cha shilingi bilioni 30.98 kilikusanywa ambacho ni sawa na asilimia 57.92 ya makadirio. Mapato haya yametokana na vyanzo mbalimbali vyaa mapato ya Wizara ikiwa ni pamoja na leseni za minada, gawio, malipo ya madeni na riba kutoka Mashirika ya Umma. Makusanyo pungufu yametokana na baadhi ya Taasisi na Mashirika kupata hasara, kutotoa gawio na mikopo kutolipwa kama ilivyokadiriwa.

Mheshimiwa Spika, Bajeti kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa mwaka 2010/2011, ilikuwa shilingi bilioni 95.99. Kati ya hizo mishahara ni shilingi bilioni 3.59 na matumizi mengineyo kwa ajili ya Wizara na Taasisi zilizo chini yake ni shilingi bilioni 92.40. Hadi kufikia Juni, 2011 Fungu hili lilipokea na kutumia jumla ya shilingi bilioni 72.48 kwa matumizi ya kawaida ambayo ni sawa na asilimia 75.5 ya makadirio ya mwaka 2010/2011. (*Makofii*)

Aidha, Bajeti kwa ajili ya matumizi ya maendeleo ilikuwa shilingi bilioni 278.97. Kati ya hizo, fedha za ndani ni shilingi bilioni 7.31 na fedha za nje ni shilingi bilioni 271.66 zikiwemo fedha kwa ajili

ya miradi ya *MCA-7*. Hadi kufikia Juni, 2011 Fungu hili limepokea na kutumia shilingi bilioni 201.29 kwa matumizi ya maendeleo ambayo ni sawa na asilimia 72.1 ya makadirio ya mwaka. Fedha za ndani ni shilingi bilioni 3.06 na fedha za nje ni shilingi bilioni 198.23. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Fungu 21 – Hazina, Bajeti iliyopo kwenye Fungu 21 kwa ajili ya matumizi ya kawaada inajumuisha matumizi ya Kitaifa na matumizi ya Idara na Taasisi za Hazina zilizo chini ya Fungu hili. Katika mwaka wa fedha 2010/2011 kiasi cha shilingi bilioni 962.06 kilitengwa kwa matumizi ya kawaada. Kati ya hizo, shilingi bilioni 803.25 zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya Kitaifa yanayojumuisha marekebisho ya mishahara ya watumishi wa Serikali, matumizi maalum, michango ya Serikali kwenye Mashirika na taasisi za Kimataifa, pamoja na matumizi ya dharura kwa Serikali. Shilingi bilioni 1.24 ilikuwa kwa ajili ya mishahara na shilingi 187.09 kwa ajili ya matumizi ya kawaada ya Idara na taasisi chini ya Fungu 21. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Juni, 2011 shilingi bilioni 629.45 zilihamishwa kutoka Fungu 21 kwenda mafungu mengine kwa ajili ya shughuli mbalimbali za Kitaifa. Matumizi ya kawaada kwa Idara na Taasisi chini ya Fungu 21 yalifikia jumla ya shilingi bilioni 187.09, matumizi maalum na dharura yaliyolipa kupitia Fungu hili yalikuwa shilingi bilioni 59.72. Aidha, Bajeti ya Maendeleo ilikuwa shilingi bilioni 100.02, kati ya hizo shilingi bilioni 50.83 zikiwa fedha za ndani na shilingi bilioni 49.19 fedha za nje. Matumizi ya fedha za maendeleo hadi Juni, 2011 yalifikia shilingi bilioni 24.38 ambayo ni sawa na asilimia 24 ya makadirio. Kati ya hizo, fedha za ndani ni shilingi bilioni 6.12 na shilingi bilioni 18.26 ni fedha za nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Fungu 22 linahusu Deni la Taifa, ili kuweza kutekeleza majukumu yake kikamilifu Fungu 22 liliipewa kiasi cha shilingi bilioni 1,930.86. Hadi kufikia Juni, 2011 matumizi yote yalifikia kiasi cha shilingi bilioni 1,930.86 ambayo ni sawa na asilimia 100 ya Bajeti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Fungu 23 linahusu Mhasibu Mkuu wa Serikali, Bajeti ya matumizi ya kawaada ilikuwa shilingi bilioni 94.08, kati ya hizo mishahara ni shilingi bilioni 3.7 na shilingi bilioni 90.36 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi Juni, 2011 matumizi ya kawaada yalifikia shilingi bilioni 93.05 ambayo ni sawa na asilimia 98.9 ya makadirio, Bajeti ya maendeleo ilikuwa shilingi bilioni 10.22. Kati ya hizo, shilingi bilioni 5.49 zikiwa fedha za ndani na shilingi bilioni 4.73 fedha za nje. Matumizi ya fedha za maendeleo hadi Juni, 2011 yalifikia shilingi bilioni 4.52 ambayo ni sawa na asilimia 44.2 ya Bajeti. Kati ya hizo, fedha za ndani ni shilingi bilioni 2.48 na shilingi bilioni 2.04 ni fedha za nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Fungu 45 linahusu Ofisi ya Taifa ya Ukaruzi, Bajeti ya Fungu 45 kwa matumizi ya kawaada ilikuwa shilingi bilioni 26.57. Hadi kufikia Juni, 2011 matumizi ya kawaada yalifikia shilingi bilioni 23.27 sawa na asilimia 87.6 ya Bajeti. Aidha, Bajeti ya maendeleo kwa fungu hili ilikuwa shilingi bilioni 10.07 kati ya hizo fedha za ndani ni shilingi bilioni 4.81 na fedha za nje ni shilingi bilioni 5.26. Hadi kufikia Juni, 2011 matumizi ya maendeleo yalifikia shilingi bilioni 5.11 kwa fedha za nje sawa na asilimia 97.3 ya Bajeti na shilingi bilioni 2.3 fedha za ndani sawa na asilimia 48 ya Bajeti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa majukumu kwa mwaka 2010/2011 na malengo ya mwaka 2011/2012 ukusanyaji wa mapato kwa mwaka 2010/2011 Wizara ililendelea kuchambua na kubuni sera, kuratibu na kusimamia shughuli za kiuchumi na kuandaa mikakati iliyolenga kuongeza mapato ya ndani, lengo likiwa ni kukusanya shilingi bilioni 6,176.2 ikijumuisha mapato ya Halmashauri. (*Makofi*)

Hadi kufikia Juni, 2011 Wizara ilikusanya mapato ya ndani ya shilingi bilioni 5,698.5 sawa na asilimia 92 ya lengo. Kati ya hayo, mapato yasiyo ya kodi yalikuwa shilingi bilioni 402.9 na yanayotokana na kodi yalikuwa shilingi bilioni 5,295.6 sawa na asilimia 94 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 5,638.6. Hali hii ya kutofikiwa kwa lengo ilisababishwa na changamoto mbalimbali zikiwemo, kushuka kwa uzalishaji wa bidhaa zinazotozwa ushuru wa bidhaa (*excise duty*), Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*) na pia kudorora kwa biashara kulikosababishwa na mgao wa umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2011/2012, Serikali itaendelea kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kuchukua hatua mbalimbali za kiutawala kuhusiana na maeneo ya mapato ya kodi na yasiyo ya kodi, pamoja na kupanua wigo wa mapato katika maeneo mengine ili kufikia lengo la kukusanya mapato ya ndani yasiyopungua shilingi bilioni 6,775.9. Kati ya hizo shilingi bilioni 6,228.84 ni mapato ya kodi na shilingi bilioni 547.11 ni mapato yasiyo ya kodi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu misaada na mikopo, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara ilipanga kukusanya mapato kutokana na misaada na mikopo kutoka nje yenye thamani ya shilingi bilioni 3,274.6. Hadi kufikia Juni, 2011 misaada na mikopo iliyopokelewa ilikuwa shilingi bilioni 2,701 sawa na asilimia 82 ya makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 928.38 sawa na asilimia 113 ya makadirio ya shilingi bilioni 821.6 ilikuwa misaada na mikopo ya Kibajeti na shilingi bilioni 1,772.6 sawa na asilimia 72 ya makadirio ya shilingi bilioni 2,452.9 ilikuwa misaada na mikopo ya miradi ya maendeleo na mifuko ya pamoja.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/12, Wizara imelenga kukusanya mapato ya shilingi bilioni 3,923.55 kutokana na misaada na mikopo kutoka nje. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 869.41 ni misaada na mikopo ya kibajeti na shilingi bilioni 2,366.14 ni misaada na mikopo ya miradi ya maendeleo na shilingi bilioni 688 ni misaada na mikopo ya mifuko ya pamoja. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na juhudzi za kuimarisha uhusiano na washirika wa maendeleo, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Serikali imeendelea kuimarisha uhusiano na washirika wa maendeleo katika nyanja mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutekeleza mapendekezo ya Ripoti ya Kundi Huru la Ufuatilaji wa Mahusiano kati ya Serikali na Washirika wa Maendeleo (*Independent Monitoring Group*). Mpango wa utekelezaji wa miaka minne (2011-2014) uliandaliwa ambao utaanza kutekelezwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012. (*Makof*)

Aidha, Serikali kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo ilianda mukutano wa mwaka wa mapitio ya kisera (*Annual National Policy Dialogue*) mwezi Disemba, 2010 uliokuwa na lengo la kutathmini utekelezaji wa sera, mikakati, Mapitio ya Matumizi ya Umma (*Public Expenditure Review*) na kuainisha maeneo yenye changamoto kwa lengo la kufanya maboresho zaidi katika mwaka wa fedha 2011/2012. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Serikali pia iliendelea kuimarisha uwajibikaji wa pamoja kwa kuandaa na kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Uwajibikaji wa Kanda ya Afrika uliofanyika Januari, 2011. Mkutano huu ulikuwa ni maandalizi ya mukutano wa ngazi ya juu utakaofanyika Korea Novemba, 2011. Aidha, Serikali ilishiriki katika mukutano mbalimbali ya Kimataifa yenye lengo la kuboresha ushirikiano kati yetu na washirika wa maendeleo. Baadhi ya mukutano hiyo ni mukutano ya mwaka ya Shirika la Fedha la Kimataifa, Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika na mukutano ya maandalizi ya Mkutano wa Nne wa Kimataifa Ngazi ya Mawaziri kuhusu Ufanisi wa Misaada (*4th High Level Forum on Aid Effectiveness*). (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu usimamizi wa Deni la Taifa, hadi kufikia Juni, 2011 Deni la Taifa linalojumuisha deni la Serikali na sekta binafsi lilifikia dola za Kimarekani milioni 11,376.74. Kati ya kiasi hicho, dola za Kimarekani milioni 9,439.04 ziliikuwa ni deni la Serikali na dola za Kimarekani milioni 1,937.7 ni deni la sekta binafsi. Deni la ndani hadi kufikia Juni, 2011 ziliikuwa dola za Kimarekani milioni 2,323.39.

Mheshimiwa Spika, malipo ya deni la ndani katika kipindi kilichoishia Juni, 2011 yalikuwa shilingi bilioni 1,292.7. Kati ya hizo, shilingi bilioni 1,021.1 zilitumika kulipia dhamana za Serikali zilizoiva kwa utaratibu wa kukopa na kulipia dhamana zilizoiva (*Rollover*) na shilingi bilioni 271.6 ziliikuwa ni malipo ya riba. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Serikali ilianda mukakati wa kusimamia Deni la Taifa kwa muda wa kati (*Medium Term Debt Management Strategy*) ambao ni dira ya kuiongoza Serikali katika ukopaji. Mkkati huu umeainisha na kukokotoa gharama na athari za kila aina ya mikopo ambayo Serikali inatarajia kukopa na hivyo kushauri aina bora ya mikopo ambayo Serikali inatakiwa kukopa ili Deni la Taifa liendelee kuhimiliika. Serikali imeendelea

kusimamia kwa umakini Deni la Taifa kwa kukopa zaidi kutoka vyanzo nafuu kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo na kuchambua athari zinazotokana na mikopo mipy. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa tathmini ya kuangalia uhimilivu wa deni (*Debt Sustainability Analysis*) iliyofanyika mwezi Septemba, 2010 inaonesha kwamba Tanzania ina deni linalohimilika. Aidha, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Serikali itaendelea na majadiliano na nchi za *Non Paris Club* ambazo hazijatupatia unafuu wa madeni ili ziweze kutupatia unafuu wa madeni na hatimaye kupunguza Deni la Taifa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu uandaaji, usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa Bajeti ya Serikali, katika kuandaa na kutekeleza Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2010/2011, kazi zilizofanywa na Wizara ni pamoja na kusimamia maandalizi ya mwongozo na mpango na Bajeti kwa miaka mitano (2011/2012- 2015/2016) ambao umetumika kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2011/2012; kukamilisha utoaji taarifa ya Bajeti ya Serikali kwa mfumo wa takwimu za Bajeti kulingana na majukumu ya Serikali (*Classification of the Functions of Government (CoFoG)*); kuandaa kitabu kinachotoa ufanuzi wa takwimu zilizopo kwenye vitabu vya Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2010/2011 – 2012/2013 (*Budget Background and Medium Term Framework 2010/2011 – 2012/2013*); na kukamilisha mfumo wa Kielektroniki (*Electronic Data Interface System*) utakaowezesha Halmashauri kupata taarifa za migao ya fedha mara tu baada ya fedha hizo kutolewa Hazina. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kazi nyingine zilizotekelawa ni pamoja na kuendelea kuimarisha uandaaji wa Bajeti ya Serikali kwa kuzingatia masuala ya jinsia (*Gender Responsive Budget*) ili kuhakikisha kuwa Bajeti ya Serikali inazingatia mahitaji ya makundi yote ya jamii. Aidha, Wizara iliendelea kushirikisha wadau mbalimbali katika majadiliano ya Mapitio ya Matumizi ya Umma (*Pubic Expenditure Revivew - (PER)*). Wadau hao ni pamoja na Asasi za Kiraia na Washirika wa Maendeleo kwa lengo la kutekeleza dhana nzima ya kuongeza uwazi na uwajibikaji wa mfumo wa Bajeti kwa wadau mbalimbali. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011 hadi 2011/2012, Wizara iliendelea kufuatilia na kukagua utekelezaji wa Bajeti ya Serikali, kwa lengo la kuhakikisha kuwa fedha zilizotolewa na Serikali zimetumika kama ilivyokusudiwa (*expenditure tracking*) na kwamba Serikali inapata thamani kwa matumizi ya fedha yake. (*Makof*)

Katika kutekeleza hili, Wizara ilifuatilia na kukagua matumizi mbalimbali ya fedha za umma kama ifuatavyo, kuhakiki mishahara ya watumishi katika Halmashauri 76 na Sekretarieti za Mikoa ya Tanga, Mara, Kilimanjaro, Iringa, Morogoro, Dar es Salaam, Kagera, Mwanza, Shinyanga, Ruvuma na Pwani; kuhakiki mishahara katika Vyuo Vikuu vya Umma vya Dar es Salaam, Sokoine, Mzumbe na Dodoma; kuhakiki mishahara katika Hospitali ya Taifa Muhimbili na Hospitali za Hiari na Teule za Wilaya; kukagua matumizi ya fedha zilizotolewa kwa ajili ya ununuzi wa chakula cha akiba kutoka mikoa ya Rukwa, Mbeya, Iringa na Ruvuma. (*Makof*)

Aidha, Wizara ilikagua barabara za Kitaifa na zile za Mamlaka za Serikali za Mitaa zinazohudumiwa na fedha za Mfuko wa Barabara pamoja na madaraja katika mikoa ya Dodoma, Singida, Tabora, Mwanza, Kagera, Kilimanjaro, Mara, Ruvuma, Rukwa, Manyara, Mtwara na Mbeya. Kadhalika, Wizara ilihakiki matumizi ya fedha za chakula katika Shule za Sekondari za Serikali za Bweni katika mikoa ya Mbeya, Iringa, Kigoma, Kagera na Singida. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, baadhi ya mambo yaliyobainika katika ukaguzi huo ni pamoja na baadhi ya watumishi kuendelea kulipwa mishahara licha ya utumishi wao kukoma; na baadhi ya waajiri kuendelea kulipa watumishi mishahara isyoendana na stahili zao. Aidha, masuala mengine yaliyobainika ni kutozingatiwa kikamilifu kwa sheria na taratibu za ununuzi, baadhi ya miradi ilichelewa kukamilika kutoptana na ukosefu wa fedha za ndani au za nje kwa miradi inayofadhiliwa na wahisani; udhaifu katika usimamizi wa miradi, hali iliyosababisha miradi kuchelewa kukamilika au kutoptana na viwango vya ubora unaotakiwa; ongezeko la gharama za miradi kutoptana na sababu mbalimbali kama vile kupanda kwa bei za vifaa vya ujenzi na kushuka kwa thamani ya shilingi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Wizara tayari imechukua hatua ya kuwaondoa watumishi wasiostahili kwenye mfumo wa malipo ya mishahara. Aidha, kiasi cha shilingi bilioni 2.97 ambazo zingelipwa kama malimbikizo ya mishahara kiliokolewa baada ya kugundulika walipwaji hao kuwa hawakustahili. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara itaendelea kupitia utaratibu wa uwasilishaji wa Bajeti za Wizara, Idara za Serikali, Mikoa na Halmashauri ili kuhakikisha Sera na Mipango ya Kitaifa na ya kisekta inazingatiwa kwenye Bajeti ya Serikali. Aidha, Wizara inakusudia kufanya tathmini ya Bajeti ya Serikali ili kuhakikisha kuwa inazingatia mahitaji ya makundi yote ya jamii pamoja na kutoa toleo la kitabu cha Bajeti kwa lugha rahisi (*Citizens Budget*). Kadhalika, Wizara itaendelea kufanya marekebisho ya mpangilio wa Bajeti ya Serikali kwa kuzingatia programu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kujenga uwezo wa Wizara, Idara za Serikali, Mikoa na Halmashauri katika uandaaji wa Bajeti ya muda wa katî, usimamizi wake na utoaji wa taarifa za utekelezaji kwa wakati. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara inakusudia kuendelea na ukaguzi wa miradi ya ujenzi na ukarabati wa barabara kuu na za Halmashauri. Aidha, Wizara itafuatilia matumizi ya fedha zilizotolewa na Serikali kwa ajili ya ununuzi wa pembejeo za kilimo, kulipia madeni ya askari na madai mbalimbali ya wazabuni kwa vyombo vya ulinzi na malimbikizo ya stahili za posho za wahadhiri wa Vyuo Vikuu Tanzania Bara pamoja na kufanya sensa ya watumishi wote wa Serikali na Taasisi, lengo ni kuhakikisha kwamba kunakuwa na uwiano mzuri katî ya fedha zinazotolewa na matokeo ya utekelezaji. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu usimamizi na udhibiti wa fedha za umma, katika kuimarisha usimamizi na udhibiti wa fedha za umma, Sheria ya Fedha za Umma Sura 348 imepitiwa na kurekebishesha ili kuwapatia Mlipaji Mkoo wa Serikali na Mhasibu Mkoo wa Serikali mamlaka ya kusimamia na kufuatilia usimamizi wa fedha za umma katika ngazi ya Serikali za mitaa. (*Makofî*)

Aidha, kuanzia mwaka wa fedha 2010/2011, Serikali iliunganisha mifumo ya Wizara ya Fedha na ile ya Benki Kuu na kuanza kufanya malipo kwa njia ya mtandao ambapo Wizara na Idara zinazofanya malipo yake kupitia Ofisi Kuu ya Malipo Hazina zilianza kutumia mifumo huu wa malipo kwa njia ya elektroniki (*Tanzania Inter-bank Settlement System (TISS)*). Hadi kufikia Aprili, 2011 *TRA* na Bodi ya Mapato Zanzibar ziliikuwa zimeunganishwa katika mifumo wa *TISS*. Aidha, utaratibu unaendelea ili kuiwezesha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kufanya malipo yake kupitia mifumo wa *TISS*. Mfumo wa *TISS* unasaidia kuharakisha malipo na kufanya usuluhishi wa benki kwa njia ya mtandao kwa wakati. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, katika juhudzi za kuboresha usimamizi na udhibiti wa matumizi ya fedha za Serikali, Wizara imeendelea kuwajengea uwezo wa kitaaluma watumishi wa kada za uhasibu, ukaguzi wa ndani, ugavi na uchambuzi wa mifumo ya kompyuta ambapo kwa mwaka wa fedha 2010/2011, jumla ya watumishi 307 kutoa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa wamepata udhamini wa mafunzo katika kozi mbalimbali. Vilevile, Wizara imetua mafunzo kwa watumiaji 260 wa mifumo wa *TISS*. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara itaendelea kufanya yafuatayo, kuimarisha mtandao wa kompyuta wa Mfumo wa Usimamizi wa Fedha (*IFMS*) katika ngazi zote za Serikali kwa lengo la kudhibiti matumizi na kuzuia malimbikizo ya madeni; kuimarisha kituo cha kuhifadhi kumbukumbu; kutoa mafunzo ya kuandaa hesabu katika viwango vya Kimataifa vya kiuhasibu katika sekta ya umma (*IPSAS*); kuendeleza kada za uhasibu, ukaguzi, ugavi na ununuzi, uhakikimali, maafisa mipango na wataalam wa kompyuta katika Serikali Kuu na Serikali za Mitaa; kuanza na kuendeleza matumizi ya *TISS* katika Hazina Ndogo na Sekretarieti za Mikoa yote; na kuratibu utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi. (*Makofî*)

Mheshimiwa spika, kuhusu Ukaguzi wa Ndani, katika jitihada za kuongeza ufanisi wa mifumo na ukaguzi wa ndani Serikalini, Sheria ya Fedha za Umma Sura 348 ilifanyiwa marekebishesha ili kuunda idara itakayosimamia mifumo na ukaguzi wa ndani katika Serikali Kuu, Serikali za Mitaa pamoja na Idara za Serikali. Napenda kutoa taarifa kwamba tayari Idara imeanzishwa na Mkaguzi

Mkuu wa Ndani wa Serikali na watendaji wote wa idara walioainishwa na muundo tayari wameteuliwa na kuanza kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara kupitia Idara ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali inaendelea kujipanga kiutendaji kwa kuandaa Mpango Mkakati wa Idara, miongozo mbalimbali ya ukaguzi wa ndani katika Wizara, Idara na Serikali za Mitaa; kuainisha mahitaji ya idara; na kuratibu mafunzo yanayolenga katika kuwajengea uwezo wakaguzi wa ndani hususan katika matumizi ya viwango vya Kimataifa vya ukaguzi wa ndani yaani *International Professional Practices Framework (IPPF)* ambapo Tanzania imeridhia mwezi Julai, 2011. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na ukaguzi wa hesabu za Serikali katika kutekeleza malengo ya mwaka wa fedha 2010/2011, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ilitekeleza yafuatayo, kukagua mafungu yote 49 ya Wizara na Idara za Serikali, hesabu za Mikoa yote 21 ya Tanzania Bara, Hesabu za Halmashauri 133 za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji, Balozi 31 kati ya Balozi 32, Wakala 33 za Serikali na ripoti zake kuwasilishwa Bungeni; kukagua Mashirika ya Umma 122 kati ya lengo la kukagua Mashirika 170, na ukaguzi wa hesabu za Mashirika 46 ulikuwa katika hatua mbalimbali. (*Makof*)

Pia ofisi ilifanikiwa kukamilisha ripoti mbili za ukaguzi wa ufanisi (*value for money audit*) zinazohusu huduma za mama wajawazito na watoto ambazo zilipata tuzo ya Kimataifa kutoka Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ya Sweden (*SNAO*). (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ilianzisha rasmi kitengo cha Ukaguzi wa Kiutambuzi (*Forensic Audit*). Hadi kufikia Juni, 2011 kitengo hiki kilifanya kaguzi mbili, moja ilihusu malipo ya fidia kwa wakazi wa Kipawa walioondolewa kupisha upanuzi wa uwanja wa ndege na ya pili ilihusu Idara ya Forodha ya Mamlaka ya Mapato. Aidha, Ofisi ilikagua Wizara 21 na Mikoa 21 kwa kutumia mfumo wa kompyuta. Kadhalika, ujenzi wa ofisi ya Mkoa wa Morogoro ulikamilika. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imelenga kutekeleza yafuatayo, kukagua hesabu za mafungu 49 ya Wizara na Idara za Serikali, Mikoa yote 21 ya Tanzania Bara, Halmashauri za Miji, Wilaya, Manispaa na Majiji 133, Mashirika ya Umma 170, Balozi zote 32 zilizoko nje ya nchi na Wakala 33 za Serikali; kupanua wigo wa ukaguzi katika ngazi ya Halmashauri ambapo wakaguzi watakwenda hadi vijijini kuhakiki utekelezaji wa miradi na matumizi ya fedha zinazotolewa chini ya mpango wa ugatuza (*D-by-D*); kufanya kaguzi sita za thamani ya fedha; kuimarisha Kitengo cha Ukaguzi wa Kiutambuzi na kufanya kaguzi mbili; kukamilisha ukaguzi kwa kutumia mifumo ya kompyuta katika Wizara na Mikoa yote; kuanza ujenzi wa Ofisi za Mikoa ya Dodoma na Rukwa pamoja na kukamilisha ujenzi wa majengo mawili katika Mikoa ya Kilimanjaro na Shinyanga; kuanza utekelezaji wa muundo mpya wa ofisi kama ulivyoindhinishwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kukidhi mahitaji ya Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008; kufanya ukaguzi maalum kuhusu usambazaji na matumizi ya vocha za pembejeo na kwa wakaguliwa wote wanaopata hati chafu na kufanya tafti unaohusu uboreshaji wa kukusanya mapato na pia utafiti wa utoaji wa huduma wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali. (*Makof*)

Kuhusu usimamizi wa malipo ya mishahara ya watumishi wa umma, katika kuboresha usimamizi wa malipo ya mishahara ya watumishi wa umma katika mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara kwa kushirkiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma iliendelea kuboresha mfumo wake wa mishahara ili kuongeza ufanisi wa mawasilian Wizara ya Fedha katika kushughulikia masuala ya watumishi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, aidha, mafunzo ya utumiaji wa mfumo yalitolewa kwa Maafisa Utumishi sambamba na uunganishaji wa mfumo katika Wizara, Idara zinazojitegemea, Mikoa, Halmashauri na Taasisi za Umma. Mfumo huu unawezesha waajiri kuingiza taarifa za ajira mpya, uhamisho, kupandishwa yveo, marekebisho ya mishahara pamoja na kufuta ajira wakiwa katika ofisi zao. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara itaendelea kuboresha na kusambaza mfumo wa malipo ya mishahara. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, suala la usimamizi wa mali ya Serikali, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara ilikamilisha zoezi la uthamini wa mali ya Serikali katika Wizara, Idara zinazojitegemea 12 na Mikoa minne na hivyo kufanya idadi ya Wizara, Idara na Taasisi za Serikali ambazo mpaka sasa zimefanyiwa uthamini kufikia 36. Aidha, Wizara imeendelea na uboreshaji wa daftari la mali ya Serikali kwa Wizara, Idara zinazojitegemea pamoja na mikoa yote ambayo imefanyiwa uthamini. Katika kufuatilia matumizi na kusimamia mali ya Serikali, Wizara ilihakiki Bohari 460 za Serikali na kutoa ushauri kwa Maafisa Masuuli kuhusiana na upokeaji, utunzaji, utumiaji pamoja na uondoshaji wa mali chakavu. Mali zenyenye thamani ya shilingi milioni 725.49 zilipata kibali cha kufutwa na kuondolewa kwa mujibu wa kanuni za fedha. Potevu zenyenye thamani ya shilingi milioni 226.9 zilichambuliwa kwa madhumuni ya kuwasilishwa Bungeni kwa ajili ya kufutwa. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara itaendelea na zoezi la kuhuisha Daftari la Mali ya Serikali kwa kutumia mtandao na kuhakiki mali ya Serikali katika Wizara, Idara zinazojitegemea, Halmashauri na Balozi za Tanzania nchi za nje. Aidha, Wizara itaendelea kutoa ushauri na kuhakikisha kuwa mali ya Serikali inatunzwa na kutumika kwa malengo yaliyokusudiwa.

Kuhusu usimamizi wa Mashirika na Taasisi za Umma, kufuatia marekebisho ya Sheria ya Msajili wa Hazina Sura 370 yaliyofanyika mwezi Aprili, 2010, muundo wa Ofisi ya Msajili wa Hazina nje ya Muundo wa Wizara ya Fedha umeidhinishwa. Ofisi hii, kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma itaendelea kuwa na majukumu yafuatayo; kuchambua na kuidhinisha miundo ya mashirika na taasisi, miundo ya utumishi, ikama na mifumo ya mishahara kwa mashirika yanayopata ruzuku kutoka Serikalini; kutathmini utendaji katika mashirika na taasisi za umma. (*Makof*)

Katika mwaka wa fedha 2010/2011, Ofisi ya Msajili wa Hazina ilikusudia kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 51.5 kama maduhuli. Hadi kufikia Juni, 2011 Ofisi ilikusanya maduhuli ya shilingi bilioni 28.8 sawa na asilimia 55.9 ya makadirio ya mwaka. Kati ya hizo shilingi bilioni 17.8 ni gawio, shilingi bilioni 8.7 ni michango ya Mashirika kwa mujibu wa Sheria ya Fedha Na.13 ya mwaka 2008 pamoja na Waraka wa Hazina Na. 8 wa mwaka 2008/2009 na shilingi bilioni 2.3 ni marejesho ya mikopo na riba. Lengo halikufikiwa kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na baadhi ya mashirika kupata hasara na mengine kuwa na mapato chini ya lengo liliokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Ofisi ya Msajili wa Hazina imepanga kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Fedha Na.13 ya mwaka 2008 pamoja na Waraka wa Hazina Na. 8 wa 2008/2009 ili kuongeza makusanyo ya mapato yasiyo ya kodi. Wizara itaipitia tena Sheria ya Msajili wa Hazina na zile zilizoanzisha Mashirika na Taasisi ili kuondoa ukinzani wa sheria kwa lengo la kurahisisha usimamizi wa utendaji wa mashirika na taasisi za umma.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi (*Public Private Partnership – PPP*), katika mwaka wa fedha 2010/2011, Bunge lilipitisha Sheria ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi Na. 18 ya mwaka 2010 (*Public Private Partnership Act No.18 of 2010*) ambayo imewezesha kuanzishwa kwa Kitengo katika Wizara ya Fedha (*PPP-Hazina*). Kitengo hiki kitatusika na kufanya tathmini ya miradi ya ubia na kuhakikisha kuwa miradi inayoanzishwa inaijendesha kibiaresha na kwa misingi ya ubora kulingana na thamani ya fedha. (*Makof*)

Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara imelenga kutayarisha miongozo mbalimbali ya kazi, pamoja na kuwajengea uwezo watumishi wa kitengo. Kufuatia kukamilika na kutolewa kwa Kanuni za Sheria ya Ubia, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Serikali imeziagiza Wizara, Idara na Taasisi kuwasilisha orodha ya miradi inayokusudiwa kugharimiwa kuititia utaratibu wa ubia. Aidha, Wizara itaendelea kuimarisha uhusiano na sekta binafsi ili kufanikisha utekelezaji wa miradi ya ubia. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu uratibu wa utekelezaji wa MKUKUTA, katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, Serikali ilianza kutekeleza MKUKUTA Awamu ya pili. Kazi kubwa zilizofanyika ni kukamilisha Mfumo wa Ufutiliaji wa MKUKUTA wa Pili (*MKUKUTA II Monitoring System – MMS II*) pamoja na Mkakati wake wa Mawasiliano (*MKUKUTA II Communication Strategy*) ambavyo viro katika hatua ya kuchapishwa. Kazi nyinyige ni pamoja na kukamilisha Mwongozo wa Ufutiliaji na Tathmini ya Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi;

kukamilisha rasimu ya Mfumo wa Taifa wa Kinga ya Jamii; kufanya tafiti nne za masuala ya uwezeshaji kiuchumi kuhusu stadi za ujasiriamali, mikopo ya benki kwa biashara ndogo ndogo, uainishaji wa mifuko ya mikopo inayoendeshwa kwa Bajeti ya Serikali na kuanzisha mfumo wa taarifa za uwezeshaji. Aidha, semina kwa ajili ya kuelimisha na kuhamasisha wananchi juu ya Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi zilifanyika katika kanda sita zikihusisha washiriki toka mikoa yote ya Tanzania Bara. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara iliendelea kusimamia utekelezaji wa Mradi wa kutoa Mikopo kwa Wajasiriamali Wadogo (*Small Entrepreneurs Loan Facility (SELF)*) na Programu ya Taifa ya Kuongeza Kipato (*National Income Generation Programme (NIGP)*). Mradi wa *SELF* ulitoa mikopo kwa asasi ndogo za fedha 93 yenye thamani ya shilingi bilioni 8.96 sawa na asilimia 98.6 ya lengo. Mikopo hiyo iliwafikia walengwa 9,250 ambapo wanawake ni 4,810 na wanaume 4,440. Urejeshwaji wa mikopo kwa wakati ulifikia asilimia 95. Aidha, mafunzo ya uendeshaji wa asasi ndogo za fedha yalitolewa kwa watendaji 314, sawa na asilimia 98 ya walengwa. Aidha, Programu ya *NIGP* ilitoa mafunzo ya ujasiriamali kwa vikundi vya ufugaji na vikundi vya *VICOBA*.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara itatekeleza yafuatayo, kuratibu mpango kamambe wa utekelezaji wa MKUKUTA Awamu ya Pili (*MMMP II*); kuratibu na kutekeleza Mkakati wa Mawasiliano wa MKUKUTA Awamu ya Pili; kuandaa taarifa ya mwaka ya utekelezaji wa MKUKUTA Awamu ya Pili (*MAIR*); kukusanya na kuandaa taarifa ya utekelezaji wa Malengo ya Milenia. Aidha, Wizara itaendelea kuratibu mradi wa *SELF* na programu ya *NIGP*. Katika mradi wa *SELF* imepanga kutoa mikopo kwa asasi ndogo za fedha 103 yenye thamani ya jumla ya shilingi bilioni 12.5 na kuongeza kasi ya ukusanyaji madeni; kujenga uwezo wa watendaji 300 wa asasi ndogo za fedha na wajasiriamali 3,525. Katika programu ya *NIGP*, Wizara itaboresha usimamizi wa miradi inayoendelea kwa kutoa mafunzo kwa viongozi wa asasi ndogo za fedha na wajasiriamali; na kununua vifaa mbalimbali vya miradi husika na kutoa mafunzo kwa wanachama wa miradi na vikundi vya *VICOBA*. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu huduma kwa wastaifu na warithi, katika juhudzi za kuendelea kuboresha utoaji wa huduma kwa wastaifu ambao wapo kwenye daftari la pensheni la Hazina, Wizara imeweka kumbukumbu zilizopo kwenye majalada binafsi ya wastaifu 71,000 kwenye Mfumo wa Kompyuta. Aidha, Ofisi ya Masjala Kuu ya Kumbukumbu za Wastaifu na Ofisi za Kitengo cha Pensheni zimeunganishwa na mfumo huo. Lengo ni kurahisisha upatikanaji wa kumbukumbu za wastaifu kila zinapohitajika na hivyo kuwezesha kutoa huduma kwa haraka. Kazi ya kuweka kumbukumbu kwenye mfumo kwa wastaifu wapya, pamoja na kumbukumbu zinazoongezwa na wastaifu walipo wanapowasilisha madai mbalimbali, inaendelea kufanyika na ni kazi endelevu. Vilevile, Wizara imejenga sehemu maalum ya kupokelea wastaifu ili kuboresha utoaji huduma. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kuwa wastaifu wanaostahili ndiyo wanaolipwa, Wizara kwa kushirikiana na Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma imeendelea kuboresha Daftari la Wastaifu. Aidha, Wizara imeendelea kuboresha na kudhibiti malipo ya pensheni kwa kuimarisha Mfumo wa Malipo ya Pensheni (*Government Pension Payment System - (GPPS)*). Wizara ilichukua hatua mbalimbali zenyelengo la kuondoa ucheleweshaji wa malipo ya mirathi ili kuepusha athari kwa warithi. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara itatoa mafunzo yatakayoendeshwa Kikanda kwa maafisa wote wanaoshughulikia mirathi kutoka Hazina Ndogo na Mahakama. Aidha, Wizara inatarajia kuunganisha mfumo wa malipo ya pensheni (*GPPS*) na Ofisi za Hazina ndogo ili kuwezesha baadhi ya huduma kwa wastaifu, kutolewa na Ofisi za Hazina ndogo. Kadhalika, Wizara inatarajia kufanya zoezi la kuwatambua wastaifu wote ambao wapo kwenye Daftari la Pensheni la Hazina kwa kuwalipa kuititia kaunta za benki kwa utambuzi maalum. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu ununuzi wa umma, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara imeendelea na uandaaji wa Sera ya Taifa ya Ununuzi wa Umma. Wizara imeendelea pia kuchukua hatua za kukabiliana na matatizo yanayohusu uwezo wa maafisa ununuzi na ugavi. Hatua hizo, ni pamoja na kuwaorodhesha watumishi wote wa kada ya ununuzi na ugavi wanaofanya kazi katika Wizara, Idara zinazojitegemea, Serikali za Mitaa na Wakala za Serikali. Hadi kufikia Juni, 2011 jumla ya maafisa ununuzi na ugavi 687 wameorodheshwa. Serikali

imeendelea kufanya mabadiliko na kuwapangia vituo vipyta kazi Maafisa Ununuzi na Ugavi walio katika Serikali Kuu na Idara zinazojitegemea, hadi Juni, 2011 jumla ya watumishi 106 wamehusika katika zoezi hilo. Zoezi hili endelevu linalenga kuboresha ufanisi wa utendaji kazi wa watumishi wa kada ya ununuzi na ugavi. Aidha, Serikali imekipandisha hadhi Kitengo cha Sera ya Ununuzi wa Umma na kuwa idara kamili ambayo itasimamia Sera, Sheria, Kanuni na maendeleo ya kada ya Ununuzi na Ugavi Serikalini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara imedhamiria kukamilisha Sera ya Taifa ya Ununuzi wa Umma ambayo itafafanua kwa kina malengo ya Serikali katika Ununuzi wa Umma. Sera hiyo itaweka msingi wa utekelezaji wa shughuli hii muhimu kwa Taifa. Aidha, Wizara itaendelea na jitlhada za kujenga uwezo wa Maafisa Ununuzi na Ugavi kwa kubainisha mahitaji halisi ya idadi na sifa za kitaaluma zinazohitajika; kuwapatia mafunzo watumishi waliopo kazini na kuajiri watumishi wapya wa kada hii kulingana na mahitaji na uwezo wa Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, udhibiti wa ununuzi wa umma katika mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (*PPRA*) ilitekeleza yafuatayo, kuandaa mukutano wa tatu wa ununuzi kwa Kanda ya Afrika Mashariki na kutoa mafunzo kwa watumishi wa taasisi za umma 116 ambapo watumishi 297 walipata mafunzo. Aidha, Wizara iliandaa mafunzo kwa Wakaguzi wa Ndani wa Taasisi za Umma 144 na kufanya ukaguzi wa ununuzi katika miradi 53 na taasisi 77. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kazi nyingine zilizofanyika ni kuelimisha umma kupitia jarida la ununuzi (*Tanzania Procurement Journal*); kusambaza mfumo wa upokeaji na usimamizi wa taarifa za ununuzi nchini (*Procurement Management Information System*) ambapo taasisi 285 sawa na asilimia 74 ya taasisi zote zimepatiwa mafunzo ya kutumia mfumo huo na kuunganishwa nao; kuboresha tovuti ya Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma - *PPRA* (<http://www.ppra.go.tz>); na kuandikisha watoa huduma na vifaa mbalimbali kwa vyombo vya umma wapatao 138. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma imelenga kuendelea na matayarisho ya kuanzisha mfumo wa ununuzi kwa njia ya mtandao yaani *e-procurement*; pamoja na kutekeleza mapendekezo yaliyotolewa kwenye utafiti uliofanyika mwaka 2010 yanayolenga kuboresha sheria ya ununuzi na kuandaa kanuni na mfumo mzuri wa usalama wa mtandao. Aidha, kufanya kazi kwa karibu na TAMISEMI ili kuweza kutatua matatizo yaliyopo kwenye Vitengo vya Ununuzi vya Halmashauri mbalimbali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu Rufaa za Zabuni za Umma katika mwaka fedha 2010/2011, Mamlaka ya Rufaa za Zabuni (*PPAA*) ilipokea jumla ya mashauri 33, kati ya hayo mashauri 31 yalifanyiwa mapitio na kutolewa maamuzi. Kati ya mashauri 31 yaliyotolewa maamuzi, mashauri 24 sawa na asilimia 77.4 ya walalamikaji walishinda na taasisi za ununuzi husika ziliagizwa kutekeleza maamuzi kwa kuzingatia sheria. Aidha, Mamlaka ilitoa elimu kwa umma katika mikoa ya Ruvuma na Rukwa pamoja na kuendesha warsha kwa Wabunge, wajumbe wa Bodi za Zabuni na Wakuu wa Vitengo vya Ununuzi katika Jeshi la Wananchi na JKT kuhusu Sheria ya Ununuzi wa Umma. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Mamlaka itatekeleza majukumu yafuatayo, kusikiliza na kutoa maamuzi ya migogoro ya ununuzi wa umma; kujenga uwezo wa wafanyakazi na Wajumbe wa Mamlaka; na kuelimisha umma na wadau kupitia redio na luninga. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu ununuzi Serikalini katika mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara kupitia Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (*GPSA*) ilitekeleza majukumu yafuatayo, kuendesha mafunzo kwa watumishi wa umma na wafanyakazi na kuhusu mfumo wa ununuzi wa pamoja unavyofanya kazi; kuanza kutumia *TEHAMA* katika kutekeleza kazi za ununuzi wa vifaa na huduma mtambuka; kuanza ujenzi wa ghala na kituo cha mafuta Babati na kukarabati vituo vya mafuta katika mikoa ya Shinyanga, Tabora, Lindi, Mtwara na Tanga. Aidha, Wakala uliendelea na usimamizi wa kazi ya ukarabati na upanuzi wa visima vya mafuta vya Dar es Salaam na Dodoma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wakala itaanza kutekeleza awamu ya kwanza ya mfumo wa matumizi ya *Smart Card* katika ununuzi wa mafuta ya magari ya Serikali; awamu hii itahusisha uwekaji wa mfumo wa kompyuta kwenye vituo vya mafuta vya Wakala na kuunganishwa na taasisi za Serikali ili ziweze kupata taarifa za matumizi ya mafuta kuititia mtandao. Aidha, Wakala umepanga kuimarisha mfumo wa ununuzi wa vifaa na huduma mtambuka kwa kuwajengea uwezo watumishi wake, na kutoa mafunzo kwa watumiaji wa mfumo huo wakiwa ni wafanyabiashara na watumishi wa umma kwa lengo la kuwajengea weledi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, usimamizi, ushauri na uratibu wa utekelezaji wa shughuli za Wizara, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara iliendelea na juhudzi za kuongeza ufanisi katika utendaji kazi kwa kufanya yafuatayo:-

- Kuandaa Muundo mpya wa Wizara ili kuendana na mabadiliko ya Serikali;
- Kuajiri watumishi wapya 75 katika kada mbalimbali na kuwapa Semina elekezi ya utendaji kazi;
- Kuandaa mpango wa mafunzo wa Wizara wa miaka mitatu 2010 - 2013 kwa kuzingatia mahitaji ya majukumu ya Wizara; na
- Kufanya Mikutano ya Baraza la Wafanyakazi. Aidha, watumishi 424 walihudhuria mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa lengo la kuongeza ufanisi wa utendaji kazi. Kadhalika, Wizara iliendelea kuwahudumia watumishi wanaoishi na virusi vya UKIMWI kwa kuwawezesha kupata virutubisho. Vile vile, Wizara ilitoa mafunzo ya ushauri nasaha kwa watumishi 314 na kuhamasisha upimaji wa hiari wa UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, iliandaa na kuwasilisha Bungeni Sheria ya Fedha ya Mwaka 2010 (*The Finance Act 2010*). Sheria hii ilifanya marekebisho sheria mbalimbali za kifedha kwa lengo la kuboresha usimamizi wa fedha za umma na kuboresha mfumo wa ukusanyaji kodi. Aidha, Wizara iliandaa Sheria ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2010/2011, hati mbalimbali za kisheria zikiwemo mikataba na hati za misamaha ya kodi inayotolewa kwa mujibu wa sheria. Wizara pia ilikusanya na kuititia mapendekezo kuhusu Muswada wa Sheria ya Ununuzi wa Umma (*Public Procurement Bill, 2010*). Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara itaendelea kuzipitia na kuzifanya marekebisho sheria nyingine zilizo chini ya usimamizi wake ili ziweze kwenda na wakati.

Mheshimiwa Spika, Wizara iliendelea kuratibu maandalizi ya taarifa mbalimbali za utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa kila robo mwaka ikiwa ni pamoa na kusimamia utekelezaji wa Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma – *Public Finance Management Reform Programme - PFMRP*. Wizara ipo katika maandalizi ya Awamu ya Nne ya PFMRP ambayo rasimu ya kwanza ilisambazwa kwa wadau kwa ajili ya kutoa maoni na mapendekezo na kazi hii inatarajiwu kukamilishwa katika mwaka wa fedha 2011/2012. Maeneo yanayolengwa katika awamu ya Nne ya Programu ni usimamizi wa mapato ya Serikali, upangaji na uandaaji wa bajeti ya Serikali, utekelezaji wa bajeti, uwazi na uwajibikaji, udhibiti wa bajeti ya Serikali na ufuatiliaji, na usimamizi wa programu na mabadiliko.

Mheshimiwa Spika, Wizara iliendelea kusimamia na kuhakikisha huduma na vifaa mbalimbali vinapatikana kwa Idara na Vitengo vyake. Ili kutimiza jukumu hili, Wizara iliandaa Mpango wa Ununuzi wa mwaka na kutangaza zabuni 25 kwa ajili ya kupata huduma na vifaa mbalimbali. Huduma nyingine zilipatikana kwa kutumia Mikataba Mtambuka ya Wazabuni walioteuliwa na Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (*GPSA*). Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara itaendelea kutekeleza Mpango wa Ununuzi wa mwaka ulioandaliwa ili kuhakikisha huduma na vifaa vinapatikana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa Miradi ya *Millenium Challenge Account*, katika mwaka wa fedha 2010/2011, miradi 14 kati ya 16 inayotekeliza chini ya Mpango wa

Changamoto za Milenia (*MCA-T*), ilipata wakandarsi. Ujenzi wa barabara za Pemba Vijiji unatarajiwa kuanza Oktoba, 2011. Mradi pekee uliosalia ni wa ujenzi wa kiwanja cha ndege Mafia. Uchambuzi wa zabuni za mradi huu unaendelea na ujenzi umepangwa kukamilika kabla ya mwisho wa mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, kuhusu miradi ya barabara za Namtumbo - Songea, Peramihio-Mbinga, Tunduma - Sumbawanga na Tanga - Horohoro, kazi ya kujenga matuta ya barabara inaendelea vizuri. Barabara ya Tanga - Horohoro ipo katika hatua ya uwekaji lami ya majaribio. Miradi yote ya usafirishaji inategemewa kukamilika mapema mwaka 2013. Miradi yote ya umeme inayosimamiwa na *MCA-T*imepata wakandarsi na kazi za ujenzi zimeanza. Kazi zinazoendelea ni pamoja na kufuatilia uundai wa vituo vidogo vya kupozea umeme – *substations* na utengenezaji wa *cable* kubwa ya umeme.

Aidha, kazi ya usafirishaji wa njia za umeme na kusimika nguzo kwa mradi wa upanuzi wa mtandao wa umeme katika Mikoa sita ya Tanga, Morogoro, Iringa, Mbeya, Dodoma na Mwanza imeanza. Miradi yote ya umeme inatarajiwa kukamilika mwaka 2012. Kadhalika, mradi wa umeme Kigoma katika kituo cha Igamba III utakaowezesha kuzalisha Megawati 41 za umeme unaendelea kufanyiwa upembizi yakinifu. Kwa miradi ya maji, inayohusisha ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya maji ya Morogoro na upanuzi wa mtambo wa maji wa Ruvu Chini imepata wakandarsi. Matarajio ni kuwa itakamilika mapema mwaka 2013.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, *MCA-T* itaendelea na utekelezaji wa miradi ya usafirishaji, nishati na maji kulingana na mipango kazi. Usimamizi wa karibu utaendelea kuimarishwa ili kuepuka ucheleweshaji usio wa lazima kwa kuwa miradi hii ina makubaliano maalum ya muda wa utekelezaji. Mpango huu wa changamoto za milenia utasitishwa rasmi ifikapo Septemba, 2013.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kusimamia na kuboresha mawasiliano na wadau kwa kutoa taarifa kwa wakati. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011, elimu kwa umma imetolewa kwa wananchi kuhusu majukumu, mafanikio na changamoto za Wizara kupitia machapisho na vyombo mbalimbali vya habari. Wizara pia imeendelea kutoa elimu kwa umma kupitia maonyesho ikiwa ni pamoja na Wiki ya Utumishi wa Umma, Saba Saba na Nane Nane.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara imepanga kukamilisha mkakati wa Mawasiliano, kutayarisha, kuchapisha na kusambaza majorida, vipeperushi, makala na taarifa mbalimbali zinazohusu majukumu ya Wizara kwa lengo la kuwaelimisha wananchi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Bodi ya Rufaa za Kodi – *Tax Revenue Appeals Board (TRAB)* ilipokea jumla ya rufaa 106, imesikiliza na kutolea maamuzi rufaa 85 ikiwa ni sawa na asilimia 90 ya rufaa zote. Aidha, Bodi ipo katika hatua za mwisho za uchapihaji wa Kumbukumbu ya Maamuzi ya Kesi za Kodi - *Tanzania Tax Law Reports* kwa rufaa zote zilizoamuliwa kuanzia mwaka 2005 – 2008.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Baraza la Rufaa za Kodi – *Tax Revenue Appeals Tribunal (TRAT)* ilipokea jumla ya rufaa 36. Kat i ya hizo rufaa 16 zilisikilizwa na kutolewa uamuzi na 20 bado zinaendelea kusikilizwa. Aidha, Baraza limeandaa Mpango Mkakati wake ili kuweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara kupitia Bodi na Baraza la Rufaa itaendelea kupokea, kusikiliza na kutoa maamuzi ya rufaa za kodi kwa wakati. Aidha, katika kipindi hicho, huduma zitasogezwa karibu na wananchi kwa kufungua Masjala ndogo Arusha, Mwanza na Mbeya kwa kuanzia na elimu inayohusu sheria za kodi na taratibu za kukata rufaa itaendelea kutolewa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara kupitia Kitengo cha Udhibiti wa Biashara ya Fedha Haramu ilikamilisha miongozo miwili kwa ajili ya watoa taarifa kama ifuatavyo:-

Mwongozo wa kuandaa na kuwasilisha taarifa za mashaka; Mwongozo kwa ajili ya Sekta ya Bima ambao unayaelekeza mashirika ya Bima hatua mbalimbali za kuchukua katika kudhibiti biashara ya fedha haramu ikiwa ni pamoja na namna ya kubaini na kutoa taarifa za mashaka kuhusu fedha haramu na ufadhili wa ugaidi; na mwongozo kwa ajili ya sekta ya mitaji na dhamana utakaoziwezesha taasisi zinazoshughulika na masoko ya mitaji na dhamana kuwa na mifumo ya kudhibiti biashara ya fedha haramu ikiwa ni pamoja na namna ya kubaini na kutoa taarifa za mashaka juu ya fedha haramu na ufadhili wa ugaidi upo katika hatua za mwisho. Wizara kwa kushirkiana na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma iliajiri wafanyakazi wa kitengo kulingana na mahitaji ya muundo uliopitishwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara itaendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Udhhibit wa Biashara ya Fedha Haramu na kutoa mafunzo na miongozo mbalimbali kwa wadau.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2010/2011Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maboresho wa Miaka Mitano (2008/2009 – 2012/2013) wa *TRA*, lengo kuu ikiwa ni kupanua wigo wa kodi kwa kusajili walipa kodi wapya na kuweka mazingira bora ya kulipa kodi. *TRA* ilifanya tafiti nne katika sekta za huduma za fedha, Usafirishaji, sekta isiyo rasmi na katika eneo la misamaha ya kodi ili kuainisha maeneo yanayoathiri ukusanyaji wa mapato - *risk areas*. Utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Mamlaka wa Kusimamia Kodi kwa kuzingatia mapendekezo yatokanayo na utafiti huo umeanza rasmi Julai, 2011.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, *TRA* itaendelea kusimamia kwa karibu utekelezaji wa mikakati mbalimbali ilioainishwa katika Mpango wake wa tatu unaolenga kuboresha makusanyo ya mapato yatokanayo na kodi. Maeneo ambayo yatarewa kipaumbele ni pamoja na kuendelea kuimarisha matumizi ya mifumo ya kielectroniki katika utawala wa kodi ikiwa ni pamoja na kuhimiza matumizi ya mashine za kielectroniki za kutoa stakabadhi za kodi - *Electronic Fiscal device (EFD)* kwenye ukusanyaji wa Kodi ya Ongezeko la Thamani; kuboresha mfumo wa kuwasilisha *returns* za kodi kwa njia ya elektroniki – *e'filling*, na utoaji wa leseni za udereva kwa njia ya kompyuta; Kuboresha matumizi ya mifumo mipya ya uthamini na ukadiriaji wa kodi za bidhaa zinazoingizwa nchini inayojulikana kama *Import/Export Commodity Price Database (IECDB)*, pamoja na kuboresha mfumo wa ukadiriaji wa kodi za magari yaliyotumika (*used vehicles*) unaozingatia uchakavu - *Depreciation*.

Mheshimiwa Spika, mamlaka itaendelea kushirkiana na mamlaka nydingine za mapato za nchi jirani na taasisi za kikanda kama vile Umoja wa Forodha wa Afrika Mashariki (*EAC – CU*) na Umoja wa Maendeleo wa Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*) katika kubadilishana uzoefu na kupashana habari ili kuongeza mapato na kuendelea kupambana na ukwepaji kodi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Tume ya pamoja ya Fedha, katika mwaka wa fedha 2010/11, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (*SMT*) iliandaa na kuwasilisha Waraka wa Mapendekezo ya Tume kuhusu vigezo vya kugawana Mapato na Kuchangia Gharama za Muungano na kuwasilisha katika kikao cha Baraza la Mawaziri. Baraza liliagiza Tume kuititia upya mapendekezo hayo kwa vile yalikuwa ni ya muda mrefu. Tume imetoa elimu kwa Wajumbe wa Kamati mbalimbali za Bunge na Baraza la Wawakilishi kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Tume.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Tume inakusudia kufanya uchambuzi wa mfumo wa kodi katika Jamhuri ya Muungano; na kuelimisha wadau kuhusu uhusiano wa kifedha baina ya *SMT* na *SMZ*, msisitizo ukiwekwa katika kutoa ufanuzi wa gharama za mapato ya Muungano. Aidha, Tume itaendelea kujenga uwezo wa wataalamu wake wa kufuatilia masuala ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Serikali Kuu – *Public Service Pension Fund (PSPF)* uliendelea kutekeleza jukumu lake la ulipaji mafao kwa mujibu wa sheria. Mfuko uliendelea kusajili na kuhifadhi kumbukumbu sahihi za wanachama, kukusanya michango na kuiwekeza. Katika mwaka wa fedha 2010/2011, Mfuko ulikusanya jumla ya shilingi bilioni 460.11 ambapo kati ya makusanyo hayo, michango ya wanachama ni shilingi bilioni 401.44 na mapato yatokanayo na vitega uchumi ni shilingi bilioni

58.67. Jumla ya shilingi bilioni 282.86 zilitumika kulipa mafao ikiwa ni pamoja na mafao ya kiinua mgongo na pensheni za kila mwezi kwa wanachama 3,016. Hadi kufikia Juni, 2011, Mfuko ulikuwa umefikia thamani ya shilingi bilioni 867.17. Aidha, Mfuko umefungua ofisi katika Mikoa yote ya Tanzania Bara ili kusogea huduma karibu na wananchi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Mfuko unatarajia kukusanya jumla ya shilingi bilioni 592.77. Kati ya hizo, michango ya wanachama ni shilingi bilioni 476.47 na mapato yatokanayo na vitega uchumi ni shilingi bilioni 116.30. Aidha, katika mwaka huu wa fedha, Mfuko unatarajiwa kufikia thamani ya shilingi bilioni 1,215. Mfuko pia unatarajia kulipa kiasi cha shilingi bilioni 410.68 kwa ajili ya mafao mbalimbali ikiwa ni pamoja na kiinua mgongo na pensheni za kila mwezi, ambapo jumla ya wanachama wapatao 5,945 wanatarajiwa kustaafu kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi Serikalini (*GEPF*) uliendelea kutekeleza majukumu ya kuboresha huduma kwa wanachama, kukusanya michango, kuwekeza katika vitega uchumi salama na kulipa mafao. Mfuko umeendelea kulipa mafao kwa wanachama kwa muda usiozidi siku sababu kama ilivyo katika Mkataba wa Huduma kwa Mteja. Aidha, Mpango wa Hiari wa kijiwekeea akiba ya uzeeni umeboreshwa zaidi ili kuwafikia wananchi wengi waliojajiri wenye na wote wanaopenda kutunisha zaidi malipo yao ya uzeeni. Hadi kufikia mwezi Juni, 2011 jumla ya shilingi bilioni 70.87 sawa na ongezeko la asilimia 8.16 ikilinganishwa na lengo la mwaka zilikusanya kutoka michango ya wanachama na mapato kutokana na vitega uchumi. Kati ya hizo, shilingi milioni 370.92 zilikusanya kuititia Mpango wa Hiari wa Kijiwekeea Akiba ya Uzeeni ambao wanachama wake wamefikia 6,555.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Mfuko unategemea kukusanya jumla ya shilingi bilioni 94.11 sawa na ongezeko la asilimia 32.8 ikilinganishwa na kiasi kilichokusanya mwaka 2010/2011. Makusanyo yanayotokana na michango ya wanachama yanatarajiwa kufikia shilingi bilioni 23.63 ambapo kati ya hizo shilingi bilioni 2.86 zitatokana na mpango wa hiari wa kijiwekeea akiba ya uzeeni. Chini ya Mpango huu Mfuko unategemea kusajili wanachama wapya 22,800. Aidha, katika kipindi hiki Mfuko utaendelea kutoa elimu kwa wananchi wa aina zote ikiwemo wakulima, wavuvi, wafanyabiashara wadogowadogo, madereva wa vyombo mbalimbali vya usafiri na makundi ya waajiriwa katika sekta mbalimbali ili waijunge katika utaratibu wa hiari wa kijiwekeea akiba ya uzeeni.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010, Mfuko wa Pensheni wa mashirika ya umma (*Public Pension Fund - PPF*) ulikusanya Shilingi bilioni 147.65 kutoka michango ya wanachama ambayo ni ongezeko la asilimia nane ikilinganishwa na Shilingi bilioni 136.5 zilikusanya mwaka 2009. Ongezeko hili lilitokana na waajiri kuzingatia sheria kwa kuleta michango kwa wakati na uandikishaji wa wanachama wapya. Hadi kufikia Juni, 2011, Mfuko ulikuwa umekusanya Shilingi bilioni 87.5 kutoka michango ya wanachama na Shilingi bilioni 48.9 kutokana na mapato ya uwekezaji

Mheshimiwa Spika, mwishoni mwa mwaka 2010, thamani ya Mfuko ilikuwa imeongezeka kufikia Shilingi bilioni 722.47 ikiwa ni ongezeko la asilimia 15.6 ikilinganishwa na Shilingi bilioni 624.85 mwezi Desemba, 2009. Ongezeko hilo lilitokana na ziada ya Shilingi bilioni 97.62 iliyopatikana kutokana na ukusanyaji wa michango pamoja na mapato yatokanayo na uwekezaji. Aidha, hadi kufikia Juni, 2011 thamani ya Mfuko ilikuwa imefikia Shilingi bilioni 814.8. Mfuko ulilipa mafao ya Shilingi bilioni 63.8 katika mwaka 2010 ikilinganishwa na Shilingi bilioni 47.2 zilizolipwa mwaka 2009 ikiwa ni ongezeko la asilimia 34.5. Kadhalika, katika kipindi cha Januari hadi Juni, 2011, Mfuko ulilipa mafao ya Shilingi bilioni 32.2. Kwa mwaka 2011, Mfuko unategemea kuandikisha jumla ya wanachama 45,000 kutoka katika sekta ya umma na binafsi na thamani ya Mfuko inategemewa kufikia Shilingi bilioni 863.8.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Fedha ya Benki Kuu katika mwaka wa fedha 2010/2011, ililenga katika kuweka uwiano sahihi wa kifedha utaboresha ukuaji wa uchumi. Ili kufikia malengo hayo, Benki Kuu iliazimia kutekekeza yafuatayo: kudhibiti ongezeko la ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (*M2*) usiozidi asilimia 20.7 na ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (*M3*)

usiozidi asilimia 21.0 ifikapo mwezi Juni, 2011; ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi usiozidi asilimia 21.3 kufikia Juni, 2011; kuwa na kiwango cha hazina ya fedha za kigeni cha kutosha kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje angalau kwa miezi mitano; na kuendelea kuwa makini katika kulinda utulivu katika sekta ya fedha.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Juni, 2011 mwenendo wa utekelezaji wa sera ya fedha kwa mwaka 2010/2011 ulikuwa kama ifuatavyo: ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (*M3*) ulifkia asilimia 22.0 ikilinganishwa na lengo la asilimia 21.0; Mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa asilimia 25.6 ikilinganishwa na lengo la ukuaji wa asilimia 21.3; Hazina ya Fedha za Kigeni ilifkia Dola za kimarekani milioni 3,610.2 ambayo ilikuwa inatosha kununua bidhaa na huduma kutoka nje kwa muda wa miezi 4.4, ikilinganishwa na lengo la miezi mitano. Hali hiyo ilitokana na kuongezeka kwa bei ya uagizaji wa bidhaa hususan nishati ya mafuta.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Benki Kuu inatarajia kutekeleza sera za kifedha sambamba na utekelezaji wa sera za kiuchumi zitakazohakikisha udhibiti wa mfumuko wa bei kwa kuzingatia yafuatayo: Kudhibiti ongezeko la ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (*M3*) na kuwa chini ya asilimia 19.0; kuwa na ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi usiopungua asimilia 20.8 na kudumisha kiwango cha hazina ya fedha za kigeni cha kutosha kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje angalau kwa kipindi cha miezi 4.5.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Benki Kuu itaendelea na juhudi za kuondoa vikwazo vilivyobaki kwenye urchumi ili kuhamasisha ongezeko la mikopo toka kwenye mabenki kwa ajili ya sekta binafsi ambayo ni mhimili wa urchumi wa nchi. Aidha, Benki Kuu itaendelea na sera ya kusimamia shughuli za Soko la Fedha za Kigeni ili kuimarisha akiba ya fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Serikali iliendelea na azma yake ya kuifanya Benki ya Rasilimali Tanzania (*TIB*) kuwa Benki ya Maendeleo ambapo mpango wa kuibadili benki uliidhinishwa rasmi na Baraza la Mawaziri mwezi Juni, 2010. Benki ilizinduliwa rasmi kuwa Benki ya Maendeleo mwezi Novemba, 2010. Aidha, Serikali illiongezea Benki mtaji wa Shilingi bilioni 50.0 na kufanya mtaji wa Benki kufikia shilingi bilioni 92.0. Vile vile, Benki ilizindua matawi mapya katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza na Arusha na kufanya jumla ya matawi kuwa manne.

Mheshimiwa Spika, dirisha la kilimo illiongezwa Shilingi bilioni 20 na hivyo kufanya jumla ya mtaji katika dirisha hili kufikia Shilingi bilioni 42. Mikopo yenye thamani ya Shilingi bilioni 18 imetolewa kwa makundi kama ifuatavyo: vikundi vyaya wakulima na SACROS Shilingi bilioni 6.0, wakopeshaji wadogo wadogo (*Microfinance*) Shilingi bilioni 4.0 na kampuni Shilingi bilioni 8.0. Baadhi ya waliopatiwa mikopo wameanza kurejesha ambapo hadi kufikia Juni, 2011 kiasi cha Shilingi milioni 489 zilikuwa zimerejeshwa. Aidha, maombi mengine ya mikopo yenye thamani ya Shilingi bilioni 12.0 yako katika hatua za urchambuzi.

Mheshimiwa Spika, *TIB* itaendelea kutoa mikopo ya muda mfupi, wa kati na mrefu kwa wakopaji mbalimbali. Lengo ni kuongeza mikopo hadi kufikia Shilingi bilioni 209.36 kutoka Shilingi bilioni 106.05 za mwaka 2010. Mwelekeo wa *TIB* ni kuwezesha pamoja na mambo mengine uwekezaji katika shughuli mbalimbali zikiwemo za viwanda, madini, uvuvi, mifugo, miundombinu, utalii na usindikaji. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, *TIB* itaendelea kutoa mikopo kwa ajili ya dirisha la kilimo matarajio ni kuhamishia shughuli hiyo katika Benki ya Kilimo pindi itakapoanzishwa. Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya kukamilisha muundo wa *TIB* amepatikana na anatarajiva kukamilisha kazi hiyo mwezi Desemba, 2011. Aidha, benki inategemea kufungua Ofisi Mkoani Mbeya kwa ajili ya kuhudumia Mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini inayojumisha Mikoa ya Mbeya, Iringa, Rukwa na Katavi.

Mheshimiwa Spika, Benki ya Posta Tanzania *TPB* katika kutekeleza majukumu yake ya kutoa huduma za kibenki kwa mwaka 2010, Benki ya Posta Tanzania ilitumia matawi yake 28 ambayo kati yake, nane yako Mikoa wa Dar es Salaam na Matawi mengine yako Mikooani. Aidha, Benki imeendelea kuwekeza kiasi kikubwa cha raslimali zake katika mabenki mengine, dhamana za Serikali za muda mrefu na dhamana za kampuni binafsi. Hadi kufikia Juni, 2011 thamani ya

vitega uchumi vyote ilifikia Shilingi bilioni 110.37. Kadhalika, Benki iliendelea kutoa huduma ya mikopo kwa wateja wake ambapo kwa kipindi hicho ilifikia thamani ya Shilingi bilioni 63.52.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Benki ya Posta Tanzania imepanga kutekeleza yafuatayo: kuimarisha matumizi ya mtandao wa matawi yake 28 pamoja na vituo 115 vya Shirika la Posta; kukusanya mapato ya kiasi cha shilingi bilioni 24.3; kuwahamasisha wanahisa wake kuongeza mtaji wa Benki ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake pamoja na kuiwezesha kufikia kiwango cha mtaji kinachotakiwa katika Sheria ya Benki cha Shilingi bilioni 15. Kwa sasa benki ina mtaji wa Shilingi bilioni 10.5. Aidha, Wizara itafanya mapitio ya Sheria iliyoanzisha Benki ya Posta kwa lengo la kuisajili Benki hiyo chini ya Sheria ya Makampuni.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka ulioishia Desemba, 2010 *Twiga Bancorp Limited* iliendelea kutoa huduma mbalimbali na kuweza kukusanya mapato ya Shilingi bilioni 9.6 ikilinganishwa na mapato ya Shilingi bilioni 7.9 kwa mwaka 2009 ikiwa ni ongezeko la Shilingi bilioni 1.7 sawa na asilimia 21.5. Aidha, katika kipindi hicho, taasisi ilipata faida kabla ya kodi ya Shilingi milioni 459 ikilinganishwa na faida kabla ya kodi ya Shilingi milioni 183 mwaka 2009 ikiwa ni ongezeko la Shilingi milioni 276 sawa na asilimia 150.8. Mikopo iliyotolewa ilifikia Shilingi bilioni 30.7 ikilinganishwa na Shilingi bilioni 29.4 kwa mwaka 2009, ikiwa ni ongezeko la Shilingi bilioni 1.3 sawa na asilimia 4.4. Kadhalika, Shilingi bilioni 8.6 ziliwekezwa kwenye amana na dhamana za Serikali katika Benki nyingine ikilinganishwa na Shilingi bilioni 8.5 katika mwaka 2009, ikiwa ni ongezeko la Shilingi milioni 100. Taasisi imeendelea kushirikiana na Benki Jamii (*Village Community Banks - VICOBA*). Hadi Juni, 2011 vikundi/VICOBA 134 vilikuwa vimeandikishwa vikiwa na amana/akiba zenye thamani ya Shilingi milioni 297. Vilevile, vikundi hivyo vilipewa mikopo yenye thamani ya Shilingi milioni 172.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha utakaoishia Desemba, 2011 *Twiga Bancorp Limited* imedhamiria kuendelea kuimarisha shughuli zake za kibashara, ili kupata faida zaidi, kuimarisha mtaji wake, na kuweza kumudu ushindani wa kibashara unaoendelea kukua katika sekta ya mabenki na fedha nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi kilichoishia Desemba, 2010, utendaji kazi wa Shirika Hodhi la *Consolidated Holdings Corporation - CHC* ulikuwa mzuri ambapo liliweza kupata mapato ya Shilingi bilioni 15.44 sawa na asilimia 214 ya lengo la Shilingi bilioni 7.22 wakati matumizi yalikuwa Shilingi bilioni 10.57.

Mheshimiwa Spika, Shirika Hodhi la *CHC* lilioundwa ili kukamilisha shughuli zilizokuwa zinatekelezwa na *Loans and Advances Realisation Trust (LART)*, *SIMU 2000 Ltd*, *Air Tanzania Holding Corporation (ATHCO)* na *Presidential Parastatal Sector Reform Commission (PSRC)*, lilikuwa lifikie ukomo Juni, 2011. Katika kikao hiki cha Bunge, Azimio la Serikali la kuongeza muda wa miaka mitatu wa Shirika ilipitishwa na Serikali ilishauriwa kutoa muda wa kutosha kwa *CHC* kukamilisha shughuli zilizosalia. Kwa kuzingatia ushauri huo na umuhimu wa shughuli zilizosalia, Wizara itahakikisha kuwa *CHC* inawezeshwa kikamilifu ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi katika kipindi walichopewa. Aidha, Wizara itaendelea kujengea uwezo Ofisi ya Msajili wa Hazina ili kupokea na kuendeleza shughuli zitakazosalia baada ya *CHC* kufikia ukomo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Shirika kwa kushirikiana na Wizara za kisekta limepanga kuendelea na ufuatillaji wa Makampuni yaliyouzwa 137 katи ya 336 yaliyobinafsishwa kwa lengo la kuanza kuchukua hatua kwa wote ambao hawajatekeleza makubaliano ya ubinafsishaji, pamoja na kukamilisha urekebishihi wa mashirika mbalimbali yakiwemo Kampuni ya Reli Tanzania (*TRL*), Kampuni ya Ndege Tanzania (*ATCL*), Kampuni ya Simu Tanzania (*TTCL*) na Shirika la Usafiri Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, shughuli za bima hapa nchini zilikuwa za kuridhisha. Pato kutokana na ada ya bima liliongezeka kutoka Shilingi bilioni 231.3 mwaka uliopita hadi Shilingi bilioni 283.3 ikiwa ni ongezeko la asilimia 22. Malipo ya madai ya bima nayo yaliongezeka kwa asilimia 42 hadi kufikia Shilingi bilioni 71.3 kutoka Shilingi bilioni 50.1, wakati vitega uchumi viliongezeka kutoka Shilingi bilioni 204.7 hadi Shilingi bilioni 258.7 sawa na asilimia 26.3 katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, uandaaji wa Kanuni za kusimamia Baraza la Usuluhishi wa masuala ya bima (*Regulations for Insurance Ombudsman*) uko katika hatua za mwisho kabla ya kusainiwa na Waziri wa Fedha. Aidha, kwa kushirikiana na Benki Kuu, *TIRA* inakamilisha utaratibu wa uuzaji wa bima kupitia mabenki ili kupanua soko la bima hapa nchini. Vile vile, uchambuzi wa utafiti kuhusu uanzishaji wa bima ya kilimo na wananchi maskini (*Micro – insurance*) umeanza kwa majaribio ili kuwezesha Wakulima kujipatia kinga.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Bima la Taifa (*NIC*) urekebishaji wa Shirika la Bima la Taifa umeendelea vizuri katika mwaka wa fedha 2010/2011. Kufuatia kuuzwa kwa baadhi ya majengo ya Shirika hili katika Sekta ya Umma, kiasi cha Shilingi bilioni 33 kilichopatikana kimeanza kutumika kulipa madai ya bima yaliyolimbikizwa kwa muda mrefu. Hadi sasa, kiasi cha Shilingi bilioni 13.55 kimelipwa kat i ya madai yenye thamani ya Shilingi bilioni 29.88 yaliyolimbikizwa. Kufuatia jitihada za kulipa madai ya bima, mapato ya bima za maisha yameongezeka kutoka Shilingi bilioni 9.35 hadi Shilingi bilioni 11.73 sawa na ongezeko la asilimia 22; wakati bima zisizo za maisha ziliongezekaa kutoka Shilingi bilioni 11.74 hadi Shilingi bilioni 14.58 sawa na ongezeko la asilimia 25.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, *NIC* itaendelea kuhakiki malimbikizo ya madai yote ya bima na kulipa kulingana na utaratibu na kwa wakati madai ya sasa ili kurejesha imani kwa wateja. Aidha, Wizara itaendelea kulisaidia Shirika katika juhudzi za kununua na kusimika mfumo mpya wa *TEHAMA* utakaoliwezesha kuendesha shughuli zake kwa ufanisi na kumudu ushindani katika biashara ya bima nchini. Kadhalika, Shirika limeandaa mkakati wa kujitangaza zaidi na kuongeza biashara kwa kubuni bima mpya zitakazokidhi mahitaji ya wananchi kwa kutumia teknolojia ya kisasa kupitia mitandao ya simu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (*CMSA*) iliendelea kusimamia masoko ya mitaji. Kwa kuzingatia kwamba wageni wameruhusiwa kuwekeza katika soko la Hisa, usimamizi wa masoko ya mitaji utaendelea kuimarishwa ili kukabiliana na utandawazi. Aidha, Mamlaka imeendelea kutoa elimu kwa umma kwa kushiriki katika maonyesho mbalimbali, kurekebisha sheria zake ili ziendane na za kimataifa pamoja na kuwezesha kujenga Masoko ya Mitaji katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Mamlaka itaanza taratibu za kuanzisha Soko la Hatifungani za Manispaa na Serikali za Mitaa (*Municipal Bond Market*) kwa kuzitaka Mamlaka za Serikali za Mitaa kuboresha utunzaji wa hesabu na udhibiti wa mapato kwa kushirikiana na Serikali. Aidha, Soko la Kukuza Kampuni za Wajasiriamali Iitaanzishwa baada ya kukamilika kwa taratibu zake na kuandikishwa katika Gazeti la Serikali la Novemba, 2010.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, mauzo hatifungani za Serikali katika Soko la Hisa la Dar es Salaam (*DSE*) yaliongezekaa kutoka Shilingi bilioni 264.91 kwa mwaka 2009/2010 hadi Shilingi bilioni 361.72 mwaka 2010/2011, ikiwa ni ongezeko la asilimia 36.54. Ongezeko la mauzo ya hatifungani kwenye Soko la Hisa lilitokana na ushiriki wa Taasisi za Fedha zinazohitaji kupata ongezeko la thamani ya hatifungani kwa kutumia bei ya soko. Mauzo ya hisa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam hadi kufikia Juni, 2011 yaliifikia Shilingi bilioni 48.52 ikilinganishwa na hisa zenye thamani ya Shilingi bilioni 52.91 zilizouzwa katika mwaka ulioshia Juni, 2010.

Mheshimiwa Spika, thamani ya mitaji ya makampuni yaliyoordheshwa kwenye Soko la Hisa imekua kutoka Shilingi bilioni 4,924.53 kwa makampuni 15 hadi Shilingi bilioni 5,926.60 kwa makampuni 16 ambalo ni ongezeko la asilimia 20.35. Thamani ya mitaji ya Makampuni ya kitanzania yaliyoordheshwa kwenye Soko la Hisa imeongezeka kutoka Shilingi bilioni 1,819.64 kwa mwaka 2009/2010 hadi kufikia Shilingi bilioni 2,141.69 kwa mwaka 2010/2011 ikiwa ni ongezeko la asilimia 17.70.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha mwaka 2010/2011, Kampuni ya Bia Tanzania, Benki ya *Standard Chartered* na Taasisi ya Fedha ya *Promotion of Rural Initiatives and Development Enterprises (PRIDE)* zimekopa jumla ya Shilingi bilioni 61.6 kwa kuuza hatifungani ambazo zimeordheshwa kwenye Soko la Hisa. Fedha zilizopatikana zilitumika kuongeza uzalishaji na uwezo wa kukopesha Watanzania ili kuinua zaidi ajira na pato la Taifa. Serikali imeendelea pia na juhudzi

zake za kuimarisha Soko la Hisa kwenye maeneo ya miundombinu, usimamizi wa biashara ya dhamana na utoaji wa elimu ya umma.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Serikali kwa kushirikiana na wahisani itaendelea na juhudzi za kuimarisha miundombinu, kuboresha usimamizi wa masoko ya mitaji na kuelimisha umma juu ya shughuli za Soko la Hisa. Vile vile, Mpango Mkakati wa miaka mitano wa Soko la Hisa utatayarishwa pamoja na kuendesha utafiti ili kuangalia uwezekano wa kuwekeza mitaji ya sekta binafsi kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam ili kulifanya lijiendeshe kibiashara.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Dhamana ya Uwekezaji Tanzania (*Unit Trust of Tanzania - UTT*) iliendelea kuimarisha Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja illyoanzishwa kati ya mwaka 2005 na 2008. Mifuko hiyo ni Mfuko wa Umoja, Mfuko wa Wekeza Maisha, Mfuko wa Watoto na Mfuko wa Jikimu. Aidha, *UTT* iliendelea kuboresha Ofisi zake za kanda katika Mikoa ya Mwanza, Arusha, Zanzibar, Mbeya, Dodoma na Dar es salaam kwa lengo la kuongeza idadi ya wanachama. Hadi kufikia Juni, 2011 Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja ilikuwa na wawekezaji wapatao 93,000 wakiwemo watu binafsi, taasisi, SACCOs na makampuni mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Dhamana ya Uwekezaji Tanzania inatarajia kutekeleza yafuatayo: Kuendelea kuboresha uendeshaji wa Mifuko ili kuongeza thamani ya vipande vilivewekezwa; kuhamasisha uwekezaji kupitia elimu kwa umma; kukamilisha uanzishwaji wa mifuko mipya ya uwekezaji wa pamoja ambayo ni *Real Estate Investment Trust - REIT*, Mfuko unaokusudiwa kukidhi haja ya wawekezaji wakubwa na wakati wenyewe nia ya kuwekeza kwa muda mfupi (*Liquid Fund*) na Mfuko utakaowekeza kwa kutumia Dola za Kimarekani (*Dollar Fund*) ambayo maandalizi ya kuanzishwa kwake yamekamilika.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Ofisi ya Taifa ya Takwimu iliendelea kutekeleza majukumu yake ya kukusanya, kuchambua, kutunza na kusambaza takwimu zilizohitajika katika sekta mbalimbali. Ofisi ya Taifa ya Takwimu imeendelea kutayarisha na kutoa kwa wakati takwimu za mfumko wa bei kila mwezi, Takwimu za Pato la Taifa kwa kila robo mwaka ikiwa ni pamoja na kukusanya takwimu za ajira. Aidha, kazi ya kutenga maeneo kwa ajili ya sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012 imekamilika katika Mikoa 19.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Ofisi ya Taifa ya Takwimu itaendelea na utekelezaji wa Mpango Kamambe wa Kuimarisha na Kuboresha Takwimu Tanzania (*Tanzania Statistical Master Plan - TSMP*) ambao uliridhiwa na Serikali mwezi Juni, 2010. Katika mpango huu, Serikali inakusudia kuirekebisha Sheria ya Takwimu Na. 1 ya mwaka 2002 ili kufanya Ofisi hii iweze kutekeleza kazi zake kwa ufanisi zaidi. Aidha, Ofisi ya Taifa ya Takwimu itaendelea kukusanya, kuchambua, kutunza na kuwasilisha takwimu zinazohitajika katika sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii ikiwa ni pamoja na kufanya sensa ya majaribio na kukamilisha kazi ya kutenga maeneo kwa ajili ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012 katika Mikoa yote. Kadhalika, Takwimu za Pato la Taifa kwa kila robo mwaka zitatayarishwa ikiwa ni pamoja na zoezi la ukamilishaji wa mapitio ya takwimu za Pato la Taifa kwa bei za mwaka 2007. Kazi hii inafanywa na wataalam wa Ofisi hii kwa kushirikiana na wataalamu kutoka Ofisi ya Takwimu ya *Denmark*.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, *NBAA* iliendelea na majukumu yake kwa kutekeleza yafuatayo: Kutahini wanafunzi wa taaluma ya uhasibu; kufanya mapitio ya mitaala ya taaluma ya uhasibu; kuendesha semina endelevu 11 kwa wadau wa taaluma ya uhasibu; kuendesha programu ya ukaguzi wa ubora wa kazi za Wakaguzi kwenye Kampuni za Ukaguzi 50 kati ya 140. Aidha, Bodi iliendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa kituo cha taaluma ya uhasibu eneo la Bunju Wilaya ya Kinondoni.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, *NBAA* imepanga kutekeleza yafuatayo: kuendelea kutahini wanafunzi wa uhasibu; kufanya ukaguzi na kusimamia ubora wa kazi za ukaguzi; kusimamia mradi wa maboresho ya Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu unaoendelea chini ya mshauri elekezi; na kutoa miongozo ya viwango vya uhasibu na ukaguzi. Aidha, Bodi itaendelea na ujenzi wa awamu ya pili ya kituo cha utaalamu wa uhasibu eneo la Bunju Wilayani Kinondoni.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Bodi ya wataalamu wa ununuzi na Ugavi - PSPTB iliendesa mafunzo elekezi kwa wadau 2,729 kutoka nchi nzima. Aidha, mafunzo yenye lengo la kukuza uelewa wa fani ya ununuzi na ugavi yalitolewa kwa Vyuo Vikuu na Taasisi mbalimbali za elimu nchini. Vilevile, kwa kutumia Sheria mpya Bodi iliendelea kusajili Wataalam katika ngazi mbalimbali ambapo Wataalam 247 wamesajiliwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Bodi imepanga kufanya yafuatayo: kuboresha mazingira ya mafunzo ili kuongeza kiwango cha ufaulu; kuendelea kujijengea uwezo wa utendaji kazi na usimamizi madhubuti wa taaluma ili kuweza kuendana na mahitaji; kutoa mafunzo endelevu kwa wataalamu yatakayolenga kuboresha uwezo wa utendaji unaozingatia maadili, nidhamu na miiko ya taaluma; na kufanya tafiti zitakazoibua changamoto mbalimbali zinazoikabili taaluma ili kuiwezesha Bodi kutafuta suluhisho. Aidha, Bodi imedhamiria kuendeleza uhusiano na ushirikiano na taasisi za kimataifa zinazoshughulika na fani hii ili kujijengea uwezo wa kuboresha utendaji na ukuaji wa taaluma kwa viwango vinavyokubalika kimataifa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Bodi ya Michezo ya Kubahatisha, iliendelea kusimamia Sekta ya Michezo ya Kubahatisha nchini kwa kutekeleza yafuatayo: Kutoa leseni mbalimbali kwa waendeshaji wa michezo ya kubahatisha nchini na kukagua waendeshaji wa michezo ya kubahatisha mara kwa mara ili kuhakikisha michezo inaendeshwa kwa mujibu wa sheria. Aidha, katika kipindi kilichoishia Juni, 2011 mapato ya Bodi yalifikia Shilingi bilioni 3.8 ambayo ni asilimia 105 ya lengo la Shilingi bilioni 3.6. Bodi imeweza kuchangia kiasi cha Shilingi milioni 263.7 kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali kwa mwaka 2010/2011 ikilinganishwa na Shilingi milioni 250 kwa mwaka wa fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, kodi iliyotokana na michezo ya kubahatisha ilifikia jumla ya Shilingi bilioni 12.3. Bodi ilikusanya kodi kwa maana ya *gaming tax*, inayofikia Shilingi bilioni 6.2 ikilinganishwa na lengo la Shilingi bilioni 5.8 na hivyo kuweza kuvuka lengo kwa asilimia sita. Kiasi kingine cha shilingi bilioni 4.5 kilitokana na Kodi za Ongezeko la Thamani, pamoja na ushuru wa bidhaa kutokana na uendeshaji wa bahati nasibu za simu za mikononi na illipwa moja kwa moja Serikalini kupitia Mamlaka ya Mapato.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara kwa kushirikiana na Bodi itakamilisha mapendekezo ya Sheria ya Michezo ya Kubahatisha kuititia intaneti (*Internet gaming*) na kuiwasilisha Bungeni. Kukamilika kwa Sheria hii kutaruhusu uwepo wa *internet gaming* ambazo zitachangia kuongezeka mapato ya Serikali pamoja na ajira nchini. Aidha, Bodi inatarajia kuzindua Bahati Nasibu ya Taifa mwezi Septemba, 2011. Kuanza kwa bahati Nasibu ya Taifa inatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali, kuchangia maendeleo ya michezo nchini pamoja na kuongeza ajira nchini. Bodi pia inatarajia kukusanya *gaming tax* inayofikia shilingi bilioni 7.4 katika mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Taasisi ya Uhasibu Arusha – IAA imekamilisha mikakati yake ya upanuzi kwa kupata eneo la ekari 60 Babati Mkoani Manyara ili iweze kuwafikia kwa ukaribu zaidi wananchi wa Mkoa huo na Mikoa ya jirani ikiwa ni jitihada za Serikali za kupanua elimu ya juu na kuwapunguzia wananchi gharama za kupata elimu hiyo. Taasisi imefanikiwa kukamilisha ujenzi wa Maktaba ya kisasa. Aidha, Taasisi imebadilisha uendeshaji wa mafunzo kutoka mfumo wa mafunzo kwa nadharia (*knowledge based*) kwenda mafunzo kwa vitendo (*Competence based*) katika ngazi ya cheti hadi stashahada. Hii itawajengea uwezo wahitimu kujajiri wenye. Katika mwaka wa fedha 2010/2011 taasisi imedahili jumla ya wanafunzi 3,383 ikilinganishwa na wanafunzi 3,008 mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, taasisi inatarajia kuongeza shahada za uzamili nne, ambazo ni *MSc. in Finance and Investment* kwa ushirikiano na Chuo Kikuu cha Coventry cha Uingereza. Shahada nyingine tatu za Uzamili zitatolewa kwa ushirikiano na Taasisi ya Teknolojia ya Birla kutoka India ambazo ni *MSc. in Software Engineering, MSc. in Computer Application* na *MSc. in Information Security*.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya uhasibu Tanzania – *TIA* katika mwaka wa fedha 2010/2011, iliendelea na kuboresha chuo kwa kuajiri wahadhiri wapya na kuimarisha Kitengo cha Utafiti na Ushauri wa Kibashara. Aidha, idadi ya wanafunzi wanaohudumiwa na Taasisi iliongezeka na kufikia 5,361. Hadi kufikia Juni, 2011 Taasisi ilikuwa na jumla ya kozi 14.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Taasisi inatarajia kuanza maandalizi ya kuanzisha kozi ya Uhasibu wa Sekta ya Umma (*Public Sector Accounting*) katika ngazi ya Cheti, Diploma na Shahada ili kutoa mchango mkubwa katika kutoa wahasibu wenye sifa za kufanya kazi Serikalini. Vile vile Taasisi inatarajia kukamilisha taratibu za kupata viwanja katika miji ya Mtwara na Mwanza kwa ajili ya uanzishwaji wa matawi mapya.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Usimamizi wa Fedha *IFM* katika mwaka wa fedha 2010/2011 kiliandaa na kukamilisha mitaala kwa mujibu wa taratibu za *NACTE* katika ngazi ya Shahada ya Uzamili katika fani ya Uhasibu na Usimamizi wa Fedha, Usimamizi wa Fedha na Uwekezaji, Kodi, Usimamizi wa Rasilimali Watu, Bima na Usimamizi wa Uzuaji Majanga (*Insurance and Risk Management*) na Hifadhi ya Jamii, Sera na Maendeleo (*Social Security, Policy and Development*).

Aidha, Chuo kimeendelea kutoa mafunzo ya shahada ya uzamili kwa kushirikiana na taasisi ya Biashara za kimataifa cha India, Chuo Kikuu cha *Strathclyde (Scotland)*, Chuo Kikuu cha *Avinashilingam* kilichopo India pamoja na ushirikiano wa Kitaaluma na taasisi ya Teknolojia ya Habari ya *Dublin* nchini *Ireland*. Mafunzo hayo yalitolewa kwa ajili ya shahada ya uzamili katika fani ya Biashara za Kimataifa, Teknolojia ya Habari na Uongozi, Usimamizi wa Fedha na Sayansi ya Kompyuta. Vilevile, chuo katika kipindi hicho kiliweza kudahili wanafunzi 7,234 katika Kozi za Shahada na Stashahada za Juu na Stashahada za Uzamili.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Chuo kinalenga kuanzisha kampasi ya pili huko Msata Wilayani Bagamoyo. Shughuli zitakazotekelawa ni pamoja na kuanza kulipa fidia ya eneo la chuo liliopatikana Msata. Aidha, Chuo kitaendelea kuongeza idadi ya programu za mafunzo katika ngazi za masomo ya shahada ya kwanza zikiwemo shahada za *Actuarial sciences, statistics, procurement and logistics* na *Local Government Accounting*, ifikapo mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Mipango na Maendeleo *Vijiji* – *IRD* katika mwaka wa fedha 2010/2011 kimetekeliza yafuatayo: kutoa mafunzo ya muda mrefu katika programu zake nane kwa wanafunzi wapatao 2,820; kuendelea na maandalizi ya kuanzisha mafunzo ya shahada ya uzamili katika programu za uchumi na mipango ya mazingira; kukamilisha utafiti juu ya uanzishwaji wa Kituo cha Mafunzo katika Kanda ya Ziwa Jijini Mwanza; kuendelea na ujenzi wa jengo la pili la taaluma ambalo kwa kiasi kikubwa litaondoa tatizo la upungufu wa madarasa, kumbi za mihadhara na Ofisi za Walimu; kukamilisha kazi ya kuandaa *District Socio-Economic Profiles* za Wilaya ya Bahi, Chamwino na Mpwapwa katika Mkoa wa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Chuo kitaendelea kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa kozi nane katika ngazi za Cheti, Stashahada, Shahada na Stashahada za Uzamili; Chuo kitaanza kutoa mafunzo mapya ngazi ya stashahada ya uzamili katika fani za Upangaji miradi na utawala wa kieneo na Maendeleo endelevu. Katika kusogeza huduma zake karibu na wadau wa maendeleo, Chuo kinatarajia kuanzisha mafunzo ya ngazi ya cheti katika Kanda ya Ziwa jijini Mwanza. Vile vile, Chuo kitakamilisha ujenzi wa jengo la pili la taaluma; kitaendelea kuboresha mandhari; kutayarisha michoro ya jengo la utawala; kutafuta maeneo mapya ya upanuzi wa chuo; kuendelea kujenga uwezo wa watumishi wake na kuajiri watumishi wapya ili kuimarisha ubora wa mafunzo yake na kuinua taaluma ya Mipango nchini kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha takwimu mashariki mwa Afrika – *EASTC*, katika mwaka wa fedha 2010/2011 kiliendelea kutoa mafunzo ya muda mrefu ya Stashahada na Cheti cha Takwimu. Idadi ya wanafunzi waliodahiliwa walikuwa 97 kutoka Tanzania, Afrika Kusini, Zambia, Zimbabwe, Sudani na Shelia. Kati ya wanafunzi hao, wanawake walikuwa 38 sawa na asilimia 39 ya wanafunzi waliodahiliwa. Pia katika kujenga uwezo ndani ya Serikali katika kukusanya, kuhifadhi na kutumia takwimu kwenye mipango yake, Chuo kiliingia mikataba na Wizara ya Viwanda na Biashara, ambapo Chuo kitaandaa Mfumo wa Utunzaji Takwimu za Wajasiriamali wadogo na wa

kati na pia kuendesha mafunzo kwa wafanyakazi wa Wizara kuhusu ukusanyaji na uchambuzi wa takwimu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika kitaendelea kutoa mafunzo ya muda mrefu wa cheti na Stashahada ya Takwimu kwa nchi zinazotumia huduma za Chuo, pamoja na wahitaji wengine, na kukamilisha taratibu za kuanza kutoa mafunzo ya Shahada ya Takwimu. Pia Chuo kitaendelea na kuboresha mazingira ya kusomea, Ofisi za Wafanyakazi na kuendelea na ujenzi wa jengo la utawala.

Mheshimiwa Spika, changamoto na hatua zilizochukuliwa katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Fedha, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Wizara ya Fedha ilikabiliwa na changamoto katika utekelezaji wa majukumu yake. Baadhi ya changamoto zilizojitekeza ni kama zifuatazo:-

- (i) Kuongeza mapato ya Serikali ili yaweze kuwiana na matumizi;
- (ii) Kuhakikisha Serikali na Washirika wa Maendeleo wanazingatia kanuni na taratibu zilizoainishwa kwenye Mkakati wa Pamoja wa Misaada Tanzania (*MPAMITA*);
- (iii) Kuhakikisha uandaaji wa mipango na bajeti za Wizara na Mikoa zinaendana na Sera, Mipango na rasilimali zilizopo;
- (iv) Kuhakikisha mfumo wa *TSS* unaeleweka na kusambazwa kwa Taasisi zote za Serikali na wadau mbalimbali;
- (v) Kuwianisha uandaaji wa hesabu za Serikali Kuu na uandaaji wa hesabu za Serikali za Mitaa; na
- (vi) Kuondoa/Kupunguza hoja za ukaguzi;

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto nilizotaja, hatua zifuatazo zitaendelea kuchukuliwa:-

- (i) Wizara kwa kushirikiana na *TRA* pamoja na wadau wengine inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kupanua uwigo wa kodi zikiwemo: kuingiza sekta isyo rasmi katika mfumo wa kodi pamoja na kusajili walipa kodi wapya; kurekebisha mapungufu mbalimbali katika ukusanyaji ili kuongeza mapato ikiwa ni pamoja na kupitia mfumo wa ukusanyaji kodi ya majengo; kupitia viwango vinavyobaki kama maduhuli kwa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali; kufanya mapitio ya sheria mbalimbali zinazotoa misamaha ya kodi; kuelimisha wananchi kudai stakabadhi za ununu; na kuhamasisha matumizi ya mashine za elektroniki za kutoa stakabadhi.
- (ii) Wizara inaendelea kuhamasisha Washirika wa Maendeleo ili kuzingatia kanuni na taratibu zilizoainishwa kwenye Mkakati wa Pamoja wa Misaada Tanzania. Wizara itaendelea kutoa elimu kuhusu kanuni na taratibu zilizoainishwa katika *MPAMITA*.
- (iii) Wizara itaendelea kujenga uwezo wa Wizara, Idara zinazojitegemea, Taasisi za Serikali, Mikoa na Halmashauri katika eneo la uandaaji bajeti za maoteo ya muda wa kati na kuendelea kuwakumbusha Maafisa Masuuli wasimamie uandaaji wa bajeti zao na kuhakikisha kuwa sera, mipango na vipaumbele vinaoana na kuonekana katika bajeti.
- (iv) Wizara inaendelea kutoa elimu kwa wadau wote wa mfumo wa *TSS* kupitia vyombo mbalimbali vya habari pamoja na kuusambaza kwa watumiaji ambao hawajafikiwa na mfumo huo.
- (v) Serikali imeanzisha Idara ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali kwa nia ya kuongeza udhibiti na uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali za umma. Aidha, Serikali imefanya

marekebisho ya Sheria ya Fedha za Umma (*SURA 348*) na kumwongezea uwezo Mhasibu Mkuu wa Serikali wa kusimamia na kudhibiti matumizi ya raslimali katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza majukumu ya Wizara na kufikia malengo yaliyokusudiwa katika mwaka wa fedha 2011/2012, ninaomba Bunge lako liidhinishe kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

Fungu 50:

- (a) Matumizi ya kawaida Sh. 85,794,616,000/=. Kati ya hizo, mishahara ni Sh. 4,324,549,000/= na matumizi mengineyo Sh. 81,470,067,000/=. na
- (b) Miradi ya Maendeleo Sh. 596,043,385,000/=. Kati ya hizo:
  - (i) Fedha za Ndani – Sh. 116,328,037,000/=. na
  - (ii) Fedha za Nje – Sh. 479,715,348,000/=. na

Fungu 21:

- (a) Matumizi ya kawaida Sh. 1,003,073,144,000/=. Kati ya hizo, mishahara ni Sh. 1,786,061,200/= na matumizi mengineyo ni Sh. 1,001,287,082,800/=. kati ya matumizi mengineyo, Sh. 162,408,179,400/= ni matumizi ya Idara na Taasisi zilizo chini ya fungu hili. Sh. 394,880,770,400/= ni nyongeza ya mishahara ya Watumishi wa Serikali, Sh. 129,759,950,000/= ni michango ya kisheria ya mwajiri na dharura na Sh. 314,238,183,000/= ni matumizi maalum.
- (b) Miradi ya maendeleo ni Sh. 51,489,868,000/=. Kati ya hizo:
  - (i) Fedha za Ndani- Sh. 8,492,894,000/=. na
  - (ii) Fedha za Nje - Sh. 42,996,974,000/=. na

Fungu 22:

Deni la Taifa Sh. 1,901,850,995,000/=. Kati ya hizo:

- (i) Mishahara ni Sh. 4,755,956,000/=. na
- (ii) Matumizi Mengineyo ni Sh. 1,897,095,039,000/=. na

Fungu 23:

- (a) Matumizi ya kawaida, Sh. 83,096,505,000/=. Kati ya hizo:
  - (i) Mishahara Sh. 3,388,248,000/=. na
  - (ii) Matumizi mengineyo Sh. 79,708,257,000/=. na
- (b) Miradi ya Maendeleo, Sh. 6,858,846,000/=. Kati ya hizo:
  - (i) Fedha za ndani, Sh. 4,185,752,000/=. na
  - (ii) Fedha za Nje, Sh. 2,673,096,000/=. na

Fungu 45:

- (a) Matumizi ya kawaida Sh. 32,710,903,000/=, Kati ya hizo,  
mishahara ni Sh. 6,859,847,763/= na matumizi mengineyo Sh. 27,998,721,000/=.
- (b) Miradi ya maendeleo Sh. 13,407,903,000/=, kati ya hizo:  
(i) Fedha za ndani Sh. 4,812,494,000/=; na  
(ii) Fedha za nje Sh. 8,595,409,000.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. ABDALLAH O. KIGODA – MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA FEDHA NA UCHUMI:**

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 99(7) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Fedha na Uchumi, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Fedha kwa mwaka wa fedha 2010/2011 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Fungu 50 – Wizara ya Fedha, Fungu 21 – Hazina, Fungu 22 – Deni la Taifa, Fungu 23 – Mhasibu Mkuu wa Serikali na Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, ambalo linaombewa fedha Bungeni na Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikutana tarehe 3 Juni, 2011 na kupokea maelezo ya muhtasari wa Bajeti ya Wizara ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012. Aidha, Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hiyo na mafungu yake kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha imeweza kutekeleza vyema malengo yake kwa mwaka wa fedha uliopita 2010/2011, ikiwa ni pamoja na kujivekaa mipango mizuri kwa mwaka huu wa fedha na hivyo kuhakikisha usimamizi thabitii wa fedha za umma na uwajibikaji pamoja na kukua kwa uchumi mkubwa kwa kiwango cha juu ambapo ukujaji huu sasa unahitajika kutoa matokeo yatakayonufaisha wananchi walio wengi hususan vijiji (*Micro level*). Kamati inaipongeza Wizara kwa umakini kutekeleza jukumu lake la kutafuta na kusimamia matumizi ya fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeendelea kutoa michango, ushauri na maelekezo ambayo Wizara ya Fedha imeendelea kuyazingatia katika kuboresha utekelezaji wa majukumu yake ya kubuni na kusimamia utekelezaji wa sera za uchumi jumla; kusimamia ukusanyaji wa mapato ya ndani na nje, na matumizi ya Serikali; utekelezaji wa *MKUKUTA*, Sera ya Uwezesheji Wananchi Kiuchumi na kupanga mipango ya maendeleo; kusimamia sheria, kanuni na taratibu za uhasibu, ukaguzi wa ndani Serikalini, ununuzi wa umma na usimamizi wa mali ya Serikali pamoja na kushirikiana na Tume ya Mipango ili kutekeleza mipango ya maendeleo iliyoinishwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto katika kutekeleza Mpango wa Bajeti ya mwaka wa fedha wa 2011/2012, katika kipindi cha mwaka wa Fedha 2010/2011, Kamati ilitoa maoni na ushauri juu ya utekelezaji katika maeneo mbalimbali ya kukuza uchumi hasa yale yaliyohusu ukusanyaji wa mapato ya ndani; uchakachuaaji wa mafuta; utekelezaji wa *MKURABITA*; manunuzi ya umma; urasimu wa utekelezaji wa miradi ya wahisani; masuala ya ubia baina ya sekta ya umma na sekta binafsi (*Public Private Partnership*); misamaha ya kodi pamoja na Soko la Pamoja la Afrika Mashariki. Katika kuititia Taarifa ya Wizara, Kamati iliridhika na utekelezaji wa baadhi ya ushauri iliyoutoa kwa Wizara na hivyo kuliomba Bunge lako Tukufu lipitishe makadirio ya Wizara hii. Hata hivyo, bado yapo maeneo yanayohitaji kuangaliwa ili kuendeleza ufanisi na tija katika utekelezaji wa kuinua Uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Spika, mwanzoni mwa Mkutano huu wa Bunge, Kamati yangu iliwasilisha taarifa kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2010 na malengo ya Uchumi katika kipindi cha muda wa kati (2011/2012 -2015/2016). Kamati ilitoa maoni ya kuishauri Serikali kupunguza kwa kiasi fulani makali ya maisha, hasa kwa kurekebisha na kudhibiti ongezeko la bei ya mafuta na ongezeko la bei za bidhaa na huduma. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua iliyocheukua ya kupunguza mzigo wa bei ya mafuta hususan dizeli na petroli kuititia kupunguza kodi na tozo mbalimbali zilizokuwa zinaingizwa katika bei ya mafuta.

Hata hivyo, Serikali ilitakiwa ifanye mkakati wa makusudi wa kutoa elimu kwa wananchi juu ya taratibu ya bei za mafuta katika Soko la Dunia ambazo Tanzania hatuzipangi. Licha ya Serikali kupunguza kodi na tozo mbalimbali, hali hii itategemea sana na viwango vya bei za mafuta katika soko la Dunia. Hata kama Serikali itapunguza kodi na tozo ikiwa bei ya mafuta itapanda huko Duniani, nchi zetu hazitaweza kupata unafuu tuliotarajia. Unafuu utapatikana tu bei za mafuta za Soko la Dunia zitakaposhuka. Kutokopanga kwetu kwa bei ya Soko la Dunia kunatufanya tuwe wahanga wa bei hizo kupanda au kupungua.

Mheshimiwa Spika, hali hii inaisisitizia Serikali kujipanga na kujizatiti katika zoezi zima la kuagiza mafuta kwa wingi (*Bulk Procurement*) kama ilivoamua kuititia kampuni ya COPEC. Hii itasaidia sana kupooza bei za mafuta. Ukosefu wa miundombini kwa upande wa COPEC ni changamoto inayohitaji kufanyiwa kazi kwa juhudu kubwa, maarifa na uadilifu. Hivi karibuni bei ya petroli imepanda kwa Sh. 100.34 sawa na asilimia 5.51, dizeli kwa Sh. 120.47 sawa na asilimia 6.30 na mafuta ya taa kwa Sh. 100.87 sawa na asilimia 5.30. Hali hii inatokana na kupanda kwa bei ya mafuta katika Soko la Dunia ambayo hatuna uwezo wa kuipanga na kuendelea kushuka kwa thamani ya Shilingi ya Tanzania, ikilinganishwa na Dola ya Marekani. Kamati inashauri Serikali kuangalia namna bora ya kuweka mipaka ya bei za bidhaa ya petroli baada ya kukokotoa, hasa ikizingatiwa kuwa bei za mafuta zinabadilika mara kwa mara katika Soko la Dunia, na nchi yetu kutokuwa na uwezo wala mamlaka ya kupanga bei hizo.

Mheshimiwa Spika, zoezi la kuhamisha chakula kutoka kwenye maeneo yenye ziada (*surplus area*) kwenda kwenye maeneo yenye uhaba (*deficit area*) litabidi liende kwa umakini. Hili linahitaji maandalizi mazuri pamoja na bei nzuri kwa wakulima wanaozalisha ziada. Aidha, mikakati ya kuboresha uchumi kuititia uuzaaji nje ni muhimu ili kuimarisha thamani ya sarafu yetu inayoendelea kushuka.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Wizara ya Fedha kuwa umefika wakati sasa wa kuchukua hatua madhubuti za kusimamia ukusanyaji wa mapato na kuibua vyanzo vipyta ili kuongeza mapato yatakayokidhi matumizi. Nini kifanyike?

- (i) Sekta isiyorasmi iingizwe katika mfumo wa kodi pamoja na kuondoa vikwazo katika shughuli wanazofanya wajasiliamali wadogo (*SMEs*) na kuwajengea ujuzi na uwezo;
- (ii) Serikali iimarishe ufuatiliaji wa kodi za majengo (*Property Tax*), eneo linalokua kwa kasi kubwa hivi sasa;
- (iii) Serikali iamue sasa kutekeleza haraka na kikamilifu mapendekezo na ushauri uliotolewa na Tume ya Bomani ya Sekta ya Madini unaogusa mfumo wa utozaji kodi na uhuishaji wa baadhi ya vipengele vya Sheria ya Madini;
- (iv) Kuangalia mfumo wa umiliki wa gesi yetu ya asili pamoja na ukokotoaji wa mapato yatokanayo na gesi;
- (v) Kutathmini mapato ya njia za mawasiliano na mitandao ya simu ili Serikali ipate kodi zinazohusika;
- (vi) Serikali ijikite kwa nguvu zote katika kukusanya mapato yatokanayo na uvuvi na bidhaa za misitu. Aidha, ni mantiki kuwawezesha wavuvi wadogo hasa katika upatikanaji wa vifaa na zana bora za uvuvi;

- (vii) Serikali ifikirie tena na ikiwezekana ihishe uamuzi wake wa kuanzisha wakala lukuki (*executive agencies*) na kuona ni vipi mapato yapatikanayo yanatumika kutunisha fedha za Serikali;
- (viii) Misamaha ya kodi iwe asilimia moja ya Pato la Taifa kama Kamati ilivyopendekeza awali. Aidha, ukubwa wa deni la Serikali na ufutaji wa madeni yasiyolipika viangaliwe kwa umakini;
- (ix) Kasi ya kukamilisha mradi wa vitambulisho vya kitaifa iongezwe, chanzo kizuri cha kukusanya kodi; na
- (x) Matumizi yasiyo ya lazima yadhibitiwe pamoja na kujenga mkakati ya kuongeza zaidi mapato kuliko matumizi zaidi.

Mheshimiwa Spika, ni ushauri wa Kamati kuwa maeneo haya yafanyiwe kazi haraka ili kuongeza kipato kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kuwa katika kipindi hiki cha Bunge la Bajeti, maoni na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge wengi yalihoji umakini na uwezo wa Watendaji wa Serikali katika kusimamia na kutekeleza majukumu yao hususan katika kusimamia fedha za Serikali katika ngazi zote za utawala Taifa, Mikoa, Wilaya na hata Vijiini. Madai ya uwajibikaji dhaifu, rushwa, matumizi mabaya, ubadhirifu na maamuzi yenye utata au ucheleweshaji wa kutoa maamuzi yamekuwa yaktolewa na Waheshimiwa Wabunge kuhusiana na utendaji wa Serikali. Hali hii inagusa hisia za utekelezaji duni wa kujenga uchumi wa nchi yetu. Eneo hili lifanyiwe kazi haraka hasa ikieleweka kuwa vyanzo vya mapato ya fedha za Serikali havijakidhi mahitaji ya kuibua zile sekta ambazo zinatoa fursa ya kukuza uchumi wa nchi. Eneo hili ni changamoto kwa Serikali hususan Wizara ya Fedha. Ushahidi unaonekana kwenye ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali wa upotevu wa fedha za Serikali za matumizi yasiyothibitika kwa mfano kiasi cha Shilingi bilioni moja kilitumika kuwalipa watumishi hewa.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba, katika Mkutano Tatu wa Bunge uliopita, Kamati yangu ilipewa kazi ya kuupitia na kuujadili Muswada wa Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2010, ambao unafuta Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004 kwa dhamira ya kuweka utaratibu mzuri zaidi katika kusimamia ununuzi wa umma. Mnamo tarehe 13 Aprili, 2011, Kamati ilikutana mara tatu Mjini Dodoma kujadili Jedwali la Marekebisho la Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2010 pamoja na majibu ya Serikali kuhusu ushauri uliotolewa na Kamati ikiwemo kufuta kifungu Na. 63 (3) na (4) cha Muswada kuhusu ununuzi wa mitambo na mashine zilizotumika.

Aidha, wakati majadiliano yakiendelea ndani ya Kamati, Serikali liliamua kuuondoa Muswada huu ili kuufanya marekebisho na kuendelea na mashauriano ndani ya Serikali. Manunuzi ya Umma yanagusa maeneo ya uchumi, jamii na siasa na yanagusa pia uwazi na uwajibikaji katika kuendesha na kusimamia raslimali za umma.

Kamati inasisitiza kuwa marekebisho ya Muswada huu yazingatie maoni ya Kamati iliyotoa hasa kwa upande wa ununuzi wa mitambo na mashine zilizotumika, sera za ununuzi wa umma, ununuzi wa dharura, muda wa kushughulikia ununuzi, mashirikiano kati ya sekta binafsi na sekta ya umma (*PPP*) pamoja na uidhinishaji wa zabuni na kadhalika. Kimsingi, Mpango wa Manunuzi unatakiwa uandaliwe pamoja na Mpango wa Bajeti ya Taifa. Hili halikufanyika. Kamati inaishauri Serikali kukamilisha Muswada huu haraka hasa ikizingatiwa kuwa ni nyenzo muhimu ya kudhibiti matumizi ya fedha za Serikali. Karibu asilimia 90 ya fedha za maendeleo zinatumika kwa manunuzi.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilizindua Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/2012 - 2015/2016) ikiwa ni awamu ya kwanza ya Mpango Elekezi (*Roadmap*) wa kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo, 2025 kwa kipindi cha miaka 15 iliyobaki. Mpango huu ni mwongozo wa kutekeleza vipaumbele vichache vitakavyoharakisha ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini, hasa katika maeneo ya miundombinu, kilimo, viwanda, maji na maendeleo ya raslimali watu. Kamati imeona kutokana na uzoefu tunaoendelea nao mpaka sasa ili tuwe na Mpango

madhubuti ambayo inatekelezeka. Ni vyema tuwe sambamba na bajeti inayopangwa na kutolewa; Kamati inaishauri Wizara ya Fedha kuhakikisha maeneo yaliyopewa kipaumbele kwenye mapendekezo ya Mpango wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali yanapatiwa fedha za kutosha na kwa wakati ili kuhakikisha kuwa malengo yaliyowekwa na Tume ya Mipango yanafikiwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati kuititia Wizara ya Fedha na Tume ya Mipango, inatoa angalizo katika eneo hili, kwa Serikali ili kuepusha maswali yafuatayo:-

- (a) Ni nani hasa anamiliki Dira ya Taifa 2025 au Dira hii ni ya nani?
- (b) Je, ipo ratiba inayoelewaka ya utekelezaji wa Dira?
- (c) Je, upo Mpango wa usimamizi, utendaji na utekelezaji wa Dira unaoelewaka na Wizara zote za Serikali kufuatana na maeleo maalum ya Dira hii (*implementation and action plans*)?
- (d) Je, utayarishaji wa Mipango na Bajeti pamoja na ugawaji wa raslimali za nchi, ki-Wizara unalenga katika kujengwa na kuitekeleza Dira ya mwaka 2025 kufuatana na malengo na matokeo yaliyowekwa?

Mheshimiwa Spika, kutokuwa na majibu sahihi ya vipengele hivyo hapo juu, kutaifanya Dira 2025 kutokuwa na mmiliki au Mwenyewe, na hivyo kutofikia malengo.

Mheshimiwa Spika, hali hii italeta changamoto kubwa hasa ikizingatiwa kuwa kuanzia mwaka 2011/2012, Serikali itanza utekelezaji wa Mpango wa Miaka Mitano, ambao vile vile una changamoto kiutekelezaji wa raslimali, nidhamu, uadilifu, tija na ufanisi. Kamati inaishauri Serikali kuititia Wizara ya Fedha na Tume ya Mipango kujipanga na kuijandaan kikamilifu katika kukabiliana na eneo hili.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1992, Serikali ilipitisha Sera ya Taifa ya Idadi ya Watu. Serikali inategemea kufanya Sensa ya watu 2012 kulingana na Sheria ya Takwimu Na.1 ya mwaka 2002 na inakadiriwa kuwa Sensa hii itagharimu kiasi cha Shilingi bilioni 113.8. Kamati inaishauri Serikali ijpange vizuri kuhakikisha kuwa sensa hii inafanya kwa ufanisi ili kupata takwimu sahihi za idadi ya watu ambazo zitaiwezesha Serikali kupanga mipango yake ya maendeleo pamoja na kutathmini hali ya utekelezaji wa Malengo ya Milenia ifikapo mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Wizara ya Fedha kufanya marekebisho ya Sheria mbalimbali zinazosimamia maslahi ya umma na yale ya wananchi. Mfano mzuri ni kuangalia kisheria maslahi ya umma (*Managing Government Interest*) katika Kampuni na Mashirika ambayo Serikali ina hisa chini ya asilimia 50. Hivi sasa mashirika yenye mfumo huu wa hisa hayana usimamizi mzuri wa Serikali na hivyo kuwa kichocheo cha matumizi mabaya ya raslimali za umma. Aidha, Ofisi ya Msajili wa Hazina inahitaji kuimarishwa katika usimamizi wa Mashirika yote ya Umma, hivyo Kamati inaikumbusha Serikali kuharakisha kuifanya marekebisho ya kimundo na kisheria ili iwe na meno katika kusimamia mali za Serikali.

Mheshimiwa Spika, uchumi wa nchi yetu unaendelea kukua wakati maisha ya wananchi wa kawaida bado hayajanufaika kikamilifu na ukuaji wa uchumi mkubwa. Serikali pamoja na juhudi zake za kupambana na umaskini kuititia MKUKUTA na programu mbalimbali kama vile programu ya Taifa ya kuongeza kipato (NIGP), mpango wa uwezeshaji wananchi kiuchumi na kuongeza ajira, mifuko ya kutoa mikopo (SELF), SACCOS na VICOBA bado Takwimu zinaonyesha kuwa juhudi zote hizi zinawafikia wananchi wachache hasa katika maeneo ya mijini. Kiasi cha asilimia 73.7 (millioni 31) ya Watanzania wanaishi vijijini. Hali hii inaonyesha kuwa bado Serikali ina safari ndefu katika kuhakikisha kuwa inawawezesha wananchi wake kiuchumi ili kuwakwamua kutoka katika dimbwi kubwa la umaskini. Zoezi la kufikia walengwa hasa vijana na akina mama linahitaji kupewa kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Wizara kwa kuboresha huduma kwa wastaifu ikiwemo kuwapokea wastaifu, kuweka majalada katika mfumo wa kompyuta na kufanya mfumo mzima wa pensheni kuwa wa kompyuta pamoja na kuunganisha katika masjala kuu. Huduma zote hizi zinasaidia kupunguza msongamano na usumbufu kwa wastaifu. Ni vyema Serikali ikalipa deni la PSPF ili iweze kuhudumia malipo ya wastaifu kama ilivyoainishwa kwenye mabadiliko yaliyotolewa kuititia GN. No. 209 ya mwaka 2009 ya kurekebisha pensheni zao za kila mwezi.

Mheshimiwa Spika, Mwaka 2008, Bunge lako Tukufu lilipitisha Muswada wa Sheria ya Kurekebisha sheria mbalimbali kuwezesha ardhi kutumika kupata mikopo ya kibenki kuititia (*Mortgage Finance Act, 2008*) na Muswada wa Sheria ya Miliki za Sehemu za Majengo (*The Unit Titles Act, 2008*) ambao umeweka utaratibu kisheria wa kutoa miliki za sehemu za majengo. Lengo kuu la sheria hizi ni kuwawezesha Watanzania hasa wenyewe kipato cha chini kukopa kuititia ardhi au kupata nyumba au fedha za kujenga nyumba na kumilikishwa sehemu ya jengo husika.

Tatizo kubwa la sheria hizi pamoja na ile ya *lease financing* bado hazijaeleweka vizuri kwa wananchi na pia Benki zetu bado hazijapewa msukumo wa kutosha na Serikali wa kuwakopesha wananchi wenyewe kipato cha chini ili waweze kufaidika na huduma hizi. Serikali inatakiwa kuboresha mazingira na kuweka mfumo wa upatikanaji wa mikopo hii kwa urahisi na uwazi, kwa ajili ya ujenzi na ununuzi wa nyumba kwa kumlinda mkopaj na mkopeshaji na kuweka haki na wajibu kwa wote. Ingawaje Benki Kuu inaendelea na utekelezaji wa Hatua ya Pili ya Mageuzi ya Kifedha, athari yake bado haijaonekana na hivyo kufanya zoezi zima kuonekana ni la kinadharia tu badala ya kuwa la kiutendaji. Kwa njia hii itachukua muda mrefu wa kusukuma ajenda ya kupunguza umaskini baina ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuiongezea fedha Tanzania *Investment Bank (TIB)* na *Tanzania Agricultural Bank (TAB)*. Hata hivyo, Benki ya Posta ya Tanzania pamoja na Benki ya *Twiga Bancorp* ambazo Serikali ina hisa asilimia 100 bado hazijapata hadhi ya kuwa benki kamili kutokana na kupungua kwa mtaji wa msingi (*core capital*) ya Shilingi bilioni 15 zilizowekwa kama kigezo na Benki Kuu. Hali hii inazipunguzia sifa za ushindani katika sekta ya fedha inayokua kwa kasi hapa nchini.

Serikali kwa uamuzi wa makusudi iziongezee mtaji wa msingi Benki hizi ili zisaidie katika azma nzima ya Kilimo Kwanza. Kamati bado ina wasiwasi mkubwa wa utendaji wa *TIB* na *TAB* jinsi itakavyohudumia walengwa waliokusudiwa. Upo wasiwasi kuwa wakulima wenyewe vipato vidogo watashindwa kufaidika na huduma hizi kutokana na masharti magumu yaliyowekwa ya kupata mikopo husika.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Fedha na Uchumi inaelewa kuwa Serikali imetambua umuhimu wa kupunguza kero ya upatikanaji wa maji katika maeneo mengi ya nchi. Maji ni uhai na mahitaji yake sasa, kwa maana ya nyumbani na yale ya viwandani, vijiji na mijini yamekuwa makubwa. Kamati inaishauri Serikali kubuni mkakati wa makusudi wa kutatua tatizo la maji kama ilivyoofanya kwenye Sekta ya Barabara na nyinginezo. Serikali iona njia ya kuachana na programu za maji ambazo zimeleta matumizi yasiyo na matokeo kwa wananchi kwa mfano *quick win*. Ipo haja ya kuongeza uwezo (*capacity*) wa Wizara ya Maji kifedha, ili kero ya maji ipatiwe ufumbuzi. Ushauri wa Kamati kwa Serikali ni kufanya maamuzi ya makusudi ya kupunguza kero ya maji kwa kutenga fedha nyingi hata kama siyo katika bajeti hii, lakini kwa ulazima wake katika bajeti ijayo. Maoni ya Wabunge wote katika mjadala wa bajeti ya maji iwe ni kigezo kwa Wizara ya Fedha kuthibitisha hoja hii.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapenda kumshukuru Waziri wa Fedha - Mheshimiwa Mustafa Mkullo, Manaibu Mawaziri wa Fedha - Mheshimiwa Gregory G. Teu na Mheshimiwa Pereira A. Silima, Katibu Mkuu, Manaibu Katibu Wakuu pamoja na wataalamu wao kwa kuwa tayari kutoa ufanuzi na kupokea maoni na ushauri wa Wajumbe wa Kamati yangu wakati wote wa mjadala wa makadirio haya. Aidha, Kamati inatoa shukurani kwa Taasisi na Idara zote zilizo chini ya Wizara hii kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati katika kipindi chote cha mwaka wa fedha ultiotangulia. Ni matarajio ya Kamati kuwa ushirikiano huu utaendelea katika mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee kabisa, napenda kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi ambao wameweza kutoa maoni na michango ya mawazo yao mbalimbali katika kuboresha makadirio haya ili hatimaye yaletwe mbele ya Bunge hili Tukufu. Naomba nitumie nafasi hii kuwatambua wajumbe wote kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Dkt. Abdallah Omari Kigoda - Mwenyekiti, Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Josephine J. Genzabuke, Mheshimiwa Eustas O. Katagira, Mheshimiwa Maulidah A. V. Komu, Mheshimiwa Dkt. Binilith S. Mahenge, Mheshimiwa Devotha M. Likokola, Mheshimiwa Martha J. Umbulla, Mheshimiwa Christina L. Mughwai, Mheshimiwa Mwigulu L. N. Madelu, Mheshimiwa Abdul-Aziz M. Abood, Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mheshimiwa Dunstan L. Kitandula, Mheshimiwa Dkt. William A. Mgimwa, Mheshimiwa Richard M. Ndassa, Mheshimiwa Rosemary K. Kirigini, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Freeman A. Mbewe, Mheshimiwa Leticia M. Nyerere, Mheshimiwa Amina Abdullah Amour, Mheshimiwa Alhaj. Mohamed H. Missanga, Mheshimiwa Andrew J. Chenge na Mheshimiwa Luaga J. Mpina. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kukushukuru wewe binafsi na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kutupatia maelekezo mbalimbali kwa Kamati yetu ambayo wakati wote yamefanikisha kazi za Kamati. Aidha, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashilillah pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake. Pia napenda kumshukuru Ndg. Michael Kadebe - Katibu wa Kamati ya Fedha na Uchumi kwa kukamilisha maandalizi ya Makadirio haya kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, napenda tena niwashukuru wapigakura wangu wa Jimbo la Handeni, kwa *support* kubwa wanayonipa katika kutekeleza majukumu yangu. Kauli mbiu yangu ni ile ile, "mambo mazuri hayataki haraka." (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha pamoja na Taasisi zilizo chini yake kwa mwaka wa fedha 2011/2012 kama alivyowasilisha mtoa hoja Waziri wa Fedha na Uchumi muda mfupi uliopita.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makof*)

**MHE. KABWE Z. ZITTO - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya na uzima na kuweza kusimama mbele ya Bunge hili kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kwa Wizara ya Fedha, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kanuni ya 99 (7), toleo la mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, natoa pongezi na shukrani zangu za dhati kwako wewe binafsi, Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kulongoza Bunge letu, licha ya changamoto nyingi. Tukiwa tunakaribia mwisho wa Mkutano wa Nne wa Bunge la Kumi, nawapongeza Wabunge wote wa pande zote mbili za Bunge na wa vyama vyote kwa michango yao na changamoto mbalimbali walizotoa ndani ya Bunge. Naamini Serikali itafanya kazi hoja mbalimbali ambazo Wabunge wamezitoa na pia Wabunge watafanya kazi majibu mbalimbali ambayo Serikali imeyatoa.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, natoa shukrani zangu za dhati kwa Kiongozi wa Upinzani Bungeni pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote wa Kambi ya Upinzani kwa ushirikiano walioonyesha katika uwasilishaji wa hotuba zote mbadala katika kipindi chote cha Mkutano huu. Kwa uzito wa pekee, nitambue ushiriki mkubwa wa Naibu Waziri Kivuli wangu Mheshimiwa Christina Mughwai kwa kujituma kwake katika kazi za Wizara hii tunayoismamia. Busara na hekima zake, ucheshi na uchapakazi wake ni nguzo muhimu kwangu kama Kiongozi wake. Nakushukuru sana Mheshimiwa Christina Mughwai. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kipekee, naomba kutoa pongezi na shukrani kwa Mawaziri vivuli wote kwa kazi kubwa waliyoifanya katika Mkutano Huu. Kwa niaba ya uongozi mzima wa Kambi ya Upinzani nawaahidi wananchi wote kuwa hotuba zote za Mawaziri Vivuli zitahaririwa na

kuchapishwa katika kitabu kimoja kwa ajili ya wananchi kufanya rejea na kujionea kazi iliyofanywa na Waheshimiwa Wabunge wa CHADEMA katika Mkutano huu na kipindi hiki cha Bajeti ya mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, Mkutano huu wa Bunge ulikuwa na changamoto nyingi sana. Hata hivyo, Mkutano huu umeweka rekodi kadhaa. Bunge limejjengea heshima zaidi kwa kuhakikisha Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini imeongezwa ili kutatua tatizo la umeme, Bajeti ya Wizara ya Usafiri iliongezwa ili kufufua reli na usafiri wa anga na hasa Shirika la ATCL na Azimio la Bunge la kuongeza muda wa Shirika la CHC liliboreshwa na kuwezesha shughuli ya kufuatilia zoezi la ubinafsishaji kuwa na ufanisi.

Mheshimiwa Spika, nakupongeza sana kwa uongozi wako mahiri. Ninaamini wale waliokuwa wanahojihoji uwezo wako sasa watafikiri mara mbili. Mungu akupe nguvu zaidi ili uendelee kuwa na msimamo wa kulinda hadhi na heshima ya Bunge letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwapongeza Wabunge wote kwa mafanikio hayo, napenda kutoa pongezi maalum kwa Wabunge wafuatao:-

Mheshimiwa Januari Makamba na Mheshimiwa Peter Serukamba kama Wenyeviti wa Kamati zilizopelekea uboreshaji huu na Mheshimiwa John Mnyika na Mheshimiwa Muhonga Ruhwanya kama Mawaziri Vivuli ambao changamoto zao zilizaa matunda na kuwezesha bajeti za Wizara zile kuweza kuwa bora. Napenda kurudia, linalosemwa kila siku, Vijana ni hazina kubwa kwa Taifa letu. Bila kujali itikadi za vyama vyetu, vijana hawa wamelitendea haki Taifa letu. Napenda kuwapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa nипитie baadhi ya maeneo yaliyo chini ya Wizara ya Fedha na Uchumi na kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha na Uchumi kuititia Shirika la CHC inasimamia Sera ya Ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma ilioanza kutekelezwa mwanzoni mwa miaka ya tisini pamoja na kuleta baadhi ya manufaa imekuwa ikilalamikiwa sana siku hadi siku na wananchi. Malalamiko mengi ni kwamba nchi yetu imetekeleza zoezi la ubinafsishaji vibaya, zoezi liliogubikwa na rushwa (*briberization as termed by Joseph Stiglitz*) na uuza ji holela wa mali za yaliyokuwa Mashirika ya Umma kama majengo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Mashirika ya Umma 360 yalibainishwa (*specified*), yaliorodheshwa kwa ajili ya ubinafsishaji mpaka Desemba, 2009. Kati ya Mashirika hayo, 331 yamebinafsishwa tayari na 29 yalikuwa katika hatua mbalimbali za kubinafsishwa. Mpaka muda huo, pato la Serikali kutokana na ubinafsishaji huo yalikuwa Shilingi bilioni 482. Hii maana yake ni wastani wa shilingi bilioni 1.5 kwa kila Shirika lillouzwa.

Mheshimiwa Spika, ni takribani miaka 20 sasa toka tuenze kutekeleza sera hiyo na mashirika mengi yakiwa yamebinafsishwa, na hivyo ni wakati muafaka wa kufanya tathmini ya kina juu ya sera ya utekelezaji wa Sera ya Ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma (*Public Inquiry on Privatisation*). Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuanza mchakato wa kufanya uchunguzi huu ili tuone mafanikio na matatizo ya sera hii kwa ajili ya kujifunza na pale inapowezekana kurekebisha makosa ambayo yatakuwa yametokea. Wananchi washirikishwe vya kutosha katika mchakato huu.

Mheshimiwa Spika, utafiti uliofanywa mwaka 2007 na asasi ya AFRODAD (*African Forum and Network on Debt and Development*) ukitolea mfano wa Tanzania katika sera ya ubinafsishaji, uligundua kuwa pamoja na matarajio ya Serikali kuhusu ubinafsishaji, bado haukuwashirikisha wananchi hata katika hatua ya kuwapa taarifa na kuwaelimisha kuhusu sera hiyo na pia wananchi wamekuwa na malalamiko ya mara kwa mara kuwa hawanufaiki na mafanikio ambayo Serikali imekuwa ikiyatoa.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hayo, ubinafsishaji pamoja na uwekezaji kwa ujumla haujawenza kutatua tatizo la ajira ambalo linawakumba vijana wengi huku kukiwa na malalamiko

kuwa wabia hao wa maendeleo huwaajiri wageni wengi zaidi kinyume na sheria kama ambavyo ilijadiliwa katika hotuba ya bajeti ya Wizara ya Kazi na Ajira.

Mheshimiwa Spika, pia mashirika mengi ya umma yaliyobinafishwa wawekezaji wameshindwa kutekeleza mambo/masharti waliyokubaliana na Serikali hii ikiwa ni pamoja na wao kufanya mambo mengine kinyume na makubaliano. Kwa mfano, Kiwanda cha Urafiki Dar es Salaam ambapo mwekezaji kutoka China amekuwa akiuza baadhi ya mashine kama vyuma chakavu, Kiwanda cha kuzalisha mbao cha *Tembo Chipboard* cha Mkumbara Mkoani Tanga ambapo mwekezaji alianza kwa kuuza miti ya msitu bila kuendesha kiwanda na hivyo kusababisha mgogoro na wananchi baada ya kuvamia maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, hiyo ni baadhi ya mifano ambayo inaonyesha kushindwa kwa mashirika/taasisi zilizobinafishwa, hii ikiwa ni pamoja na baadhi ya wawekezaji/wabia kutoa taarifa za uongo/zisizo sahihi juu ya uwezo wao kufufua na kuendesha taasisi zilizobinafishwa kwao mathalan kiwanda cha kusindika nyama kilichopo Kawe Dar es Salaam cha *Tanganyika Packers*.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani Bungeni inapendekeza, kama ilivyoelezwa hapo juu, kufanyika kwa uchunguzi maalum kuhusu utekelezaji wa sera ya ubinafishaji (*Public Inquiry on Privatisation*).

Mheshimiwa Spika, mwezi Juni mwaka huu 2011 na katika Mkutano huu wa Nne, Bunge lako Tukufu lilijadili na kuitisha azimio la kuongeza muda wa Shirika la *CHC* baada ya kufanya marekebisho azimio lilioletwa Serikali ambapo awali kulikuwa na nia ya kuunganisha Shirika hili na Ofisi ya Msajili wa Hazina. Uamuzi huu wa Bunge haukuwfurahisha baadhi ya Watendaji wa Serikali.

Hivi sasa Mkurugenzi Mkuu aliyejewa anakaimu wa Shirika la *CHC* (Kaimu) Ndugu Mathusela Mbajo amesimamishwa kazi kwa tuhuma ambazo zilitokana majungu yaliyotokana na hoja ambazo zilitoka hapa Bungeni na Wabunge ambazo walichangia. Tuhuma hizo ziliwasilishwa kwangu kwa barua na kunakiliwa kwa Waziri Mkuu na Waziri wa Fedha. Kufuatia maagizo ya Waziri wa Fedha kwa Bodi ya Wakurugenzi wa *CHC*, Mtanzania huyu kasimamishwa kazi na kwamba CAG ameombwa eti achunguze majungu haya ambayo yalitokea.

Mheshimiwa Spika, nilikuandikia barua kukuomba hatua muafaka zichukuliwe kwani suala hili bado lipo katika mamlaka ya Bunge na kwa mujibu wa Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge, Sheria Na. 3 ya mwaka 1988. Maamuzi haya ya Waziri wa Fedha ni sawa na *contempt of Parliament*. Barua ya wanaojiita wafanyakazi wa *CHC* (niliyoandikiwa tarehe 24 Juni, 2011, siku mbili tangu kuitishwa kwa Azimio la Bunge na kutuhumu Mawaziri kuwa walishawishiwa), Barua ya maelekezo ya Serikali (iliyosainiwa na ndugu Mmbaga, Msaidizi wa Waziri Mkuu ya tarehe 10 Agosti, 2011) na Barua yangu ya majibu (18 Agosti, 2011) niliyowapa zimewasilishwa mezani kwako kama vithhibitsho na kwa hatua zaidi utakazoona inafaa.

Mheshimiwa Spika, Bunge hili linapaswa kusimama imara kuzuia kuingiliwa kwa mamlaka yake na tawi la Utendaji. Mijadala ndani ya Bunge inalindwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tusipokuwa makini, Bunge litaendelea kudharauliwa na hivyo kushindwa kufanya kazi yake ya kuwawakilisha wananchi, kutunga sheria na kuisimamia Serikali ipasavyo. Nataka maelezo ya kina ya Waziri wa Fedha, kwa nini alichukua hatua nilizoleza hapo juu ilhali akijua jambo hili lipo mezani kwa Spika wa Bunge? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, usimamizi wa mashirika ya umma, ukiangalia katika Fungu la 50, kasma 229900 (*Other operating expenses*) katika kasma ndogo ya 229931 (*contingent liabilities*) Serikali imetenga Shilingi bilioni 35.7 zikiwa ni fedha za kulipia madeni na mahitaji ya dharura kwa Mashirika ya Umma. Vile vile katika fungu 21, kasma 229929, Serikali imetenga Shilingi bilioni 26.4 kwa ajili ya kulipa fidia kwa mikataba mbalimbali ambayo Serikali imeingia. Kwa vyovyyote vile mionganoni mwa mikataba hiyo ni pamoja ule wa Shirika la Reli na mingineyo. Hii inaonyesha kuwa Serikali inatumia fedha nyingi sana kwa ajili ya Mashirika ya Umma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo basi, usimamizi thabiti unatakiwa ili kulinda fedha hizi za umma zinazotumika kwenye Mashirika ya Umma. Kinyume chake kumekuwa na usimamizi mbovu sana na unaopelekea Taifa kupoteza fedha nyingi sana kutokana na ubadhifuru katika Mashirika ya Umma. Hii ni kweli kwa Mashirika ambayo Serikali ina hisa nyingi (*majority share holding*) na hata kule ambapo Serikali ina hisa chache, yaani *minority share holding*.

Mheshimiwa Spika, liko tatizo la Serikali kushindwa kusimamia vizuri hisa zake kwenye Taasisi/Mashirika ambayo Serikali ina hisa chini ya asilimia 51. Hisa hizi zinasimamiwa kwa niaba ya Taifa na Ofisi ya Msajili wa Hazina. Muundo wa Ofisi hii ulikuwa unakwaza kazi ya kusimamia Mashirika ya Umma na hivyo Bunge ilifanya mabadiliko ya Sheria mwaka 2010 kuimarisha Ofisi ya Msajili wa Hazina. Mpaka leo mapendekezo ya muundo wa Utumishi hayajapata kibali ili Ofisi ifanye kazi ipasavyo. Tunaitaka Serikali ieleteze ni lini kibali hiki kitatoka ili kuwezesha usimamizi bora wa Mashirika ya Umma?

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Msajili wa Hazina (*TR*) imekuwa dhaifu mno katika kusimamia mali za Serikali Katika Mashirika. Mifano miwili ya namna hisa za Serikali zilivyouzwa itasaidia kuonyesha hali hii. Kampuni ya *Oryx* ilikuwa inamiliikiwa na Serikali kwa asilimia 50 mpaka mwaka 2004. Mwaka 2004, kuititia Ofisi ya *TR*, Serikali iliuza hisa zake ambazo ni asilimia 50 kwa bei ya kutupa kwa thamani ya Dola milioni 2.5. Hivi sasa *Oryx* ni moja ya Kampuni inayofanya vizuri sana katika Sekta ya Mafuta, lakini hatuna umiliki tena na pesa kiduchu tulizopata zimekwishatumika.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali ilikuwa na hisa katika kampuni ya simu za mkononi ya *Mobitel* ambayo kwa sasa inajulikana kama *Tigo*. Katika hatua ya kushangaza na haina maeleo kabisa, Serikali imeuza hisa zake asilimia 16 kwa thamani ya dola 1.3 milioni mwaka 2006 na kwa sasa kampuni hiyo ni ya kigeni kwa asilimia mia moja jambo ambalo ni kunyume na sheria. Kampuni za Simu zinatakiwa kumiliikiwa na Watanzania sio chini ya asilimia 35 kwa mujibu wa Sheria za Simu. Asilimia 16 ya hisa *Tigo* leo thamani yake ni zaidi ya kumi ya bei tulivyouza mwaka 2006.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Msajili wa Hazina inashikilia hisa '*minority*' za Serikali kwenye Kampuni zaidi ya 24 hapa nchini. Baadhi ya Kampuni hizi wala hazina wajumbe wa Bodi wanaowakilisha Serikali au Wajumbe ni maafisa wale wale wa Ofisi ya Msajili wa Hazina ambao hufikia hata kuhudhuria Bodi tatu mpaka tano kwa siku. Matokeo yake hawawezi kutoa maamuzi ya kibiaresha na hivyo kutolinda Mali za Taifa vizuri. Mfano wa hivi majuzi ni sakata la uuzwaji wa Shirika la *UDA* ambapo Msajili wa Hazina hakuwahi kuteua Mjumbe wa Bodi wa *UDA* kwa zaidi ya miaka mitatu na ndio chanzo cha mgogoro wote wa Shirika la *UDA* unaoendelea hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, baada ya tathmini hiyo fupi, Kambi ya Upinzani tunapendekeza mambo yafuatayo ambayo tunaitaka Serikali kuzingatia ili kuboresha usimamizi wa Mashirika ya Umma ili kuleta tija zaidi kama ifuatavyo:

Ofisi ya Msajili wa hazina (*TR*) ifumuliwe na ianzishwe Ofisi ya Mashirika ya Umma ambayo itakuwa ni kama Wakala wa Serikali chini ya Wilaya ya Fedha ikiwa ni chombo huru chenye kusimamia Mashirika yote ya Umma (*Office of Public Enterprises – OPE*). Ofisi hii itasimamia Mashirika yote ya Umma ambayo Serikali ina hisa zaidi ya asilimia 51 (*majority*). Mashirika ambayo Serikali inamiliiki hisa chini ya asilimia 51 (*minority*) yaundiwe Kampuni Hodhi (*holding company*) ambayo itasimamiwa na *OPE* ambayo sasa ni Ofisi ya Msajili wa Hazina. Hata hivyo, ili kupunguza mlolongo wa Mashirika, Shirika la *CHC* laweza kuongezewa majukumu na kuwa *National Holding Company* na hivyo kumilikishwa hisa hizi na kuzifanyia biashara kwa tija.

Mashirika yaliyo katika Sekta nyeti kwa umma yasibinafsishwe tena na badala yake yaendelee kumilikiiwa na Serikali kwa kuweka Menejimenti mahiri na kuwa na lengo la kuorodhesha hisa zao katika Soko la Hisa la Dar es Salaam ili kumilikisha wananchi na kuweka uwazi katika uendeshaji. Lazima kufikiria upya zoezi la kubinafsisha Mashirika yaliyo katika sekta nyeti kwa wananchi kama *TANESCO*. Sekeseka la juzi la Mafuta liwe fundisho kwetu katika kuangalia sera za Uliberali zilizokuwa zinapigiwa debe na Mashirika ya Fedha ya kimataifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, chombo rasmi kinachojihusisha na kutafuta, kuandaa na kusambaza takwimu hapa Tanzania ni Ofisi ya Taifa ya Takwimu (*Nation Bureau of Statistics*). Ofisi ya Taifa ya Takwimu ni Wakala wa Serikali chini ya Wizara ya Fedha, na iliundwa kupitia Sheria ya Wakala wa Serikali Na. 30 ya mwaka 1997.

Mheshimiwa Spika, katika kupanga mipango ya maendeleo na kuandaa sera mbalimbali za nchi husika, upatikanaji wa takwimu rasmi zinazotokana na Kanuni na Mbinu za Kitaalamu iliyowekwa na Ofisi ya Takwimu ya Umoja wa Mataifa (*United Nations Statistical Division*) ni muhimu. Takwimu zote zilizo rasmi duniani hutolewa na Ofisi za Takwimu za nchi husika kupitia Sheria za Takwimu za nchi mbali mbali.

Mheshimiwa Spika, Mapendekezo ya kuboresha utendaji wa Ofisi ya Takwimu. Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza yafuatayo ili kuboresha utendaji wa Ofisi hii ya Takwimu ya Taifa:-

- (i) Taarifa mbali mbali za takwimu zitolewe kwa uwazi ikiwahusisha wanahabari na wataalamu wa kada mbalimbali kama vile wachumi na kuwepo mjadala wa wazi kuhusiana na taarifa hiyo. Kwa mfano, taarifa za robo mwaka kuhusu ukuaji wa uchumi ziwe zinatolewa mbele ya Waandishi wa Habari na kurushwa 'live' na Televisheni ya Taifa. Hii itasaidia sana kupasha habari za kiuchumi, lakini pia kuwezesha wataalamu na Wanahabari za Uchumi kuwahoji maswali Maafisa wa *NBS*. Hii hufanyika katika nchi kama za Uingereza na husaidia sana katika kutunga sera.
- (ii) Kuwa na uhisiano wa moja kwa moja wa Ofisi ya Takwimu ya Taifa na ngazi za Mikoa, Halmashauri za Wilaya, Kata na Vijiji kurahisisha upatikanaji wa takwimu ili zisaidie katika kupanga mipango ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani tunasikitishwa na upungufu wa makusanyo madogo ya kodi na hii ni kutokana na Serikali kushindwa kusikiliza maoni ya Kambi ya Upinzani tunayotoa kila mwaka ambapo tumekuwa tukitoa vyanzo mbadala vya kuongeza mapato.

Mheshimiwa Spika, bei ya dhahabu katika Soko la Dunia imeongezeka mara dufu. Hadi kufikia tarehe 23 Agosti, 2011 bei ya dhahabu kwa mujibu wa mtandao wa *gold-alert* ilikuwa Dola za Kimarekani 1902.61 (kutokana na taarifa ya gazeti la *Financial Times* (ft.com) la leo 25 Agosti, 2011, bei imeshuka mpaka Dola 1760 kwa wakia moja). Hili ni ongezeko kubwa sana na hivyo kuna kila haja ya kuangalia namna ya kurekebisha kodi kwenye raslimali hiyo muhimu hapa nchini ili Taifa lifaldike na kupanda kwa bei ya dhahabu.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani tunaitaka Mamlaka ya Mapato Tanzania kuanza mara moja kufanya utafiti wa namna bora ya kutoza kodi ya faida kwenye dhahabu (*windfall tax*) ili kuongeza mapato ya Serikali kwa sababu wawekezaji wanapata faida mara dufu kwa sasa kwa sababu ya ongezeko hilo la bei. Matokeo ya tafiti hii yaletwe Bungeni kama Muswada wa Sheria ili kurekebisha sheria za kodi na kutoza aina hii mpya ya kodi.

Mheshimiwa Spika, tunapendekeza, kwa kuwa gharama ya kuzalisha wakia moja ya dhahabu hapa nchini, ni wastani wa Dola za Marekani 650, basi bei ya dhahabu ikiwa ya katni ya Dola 1000 – 1300, mrahaba uwe mara mbili ya unaotozwa sasa, ikiwa katni ya Dola 1301 – 1600 mrahaba uwe mara tatu ya unaotozwa sasa na ikiwa zaidi ya 1,601 mrahaba uwe mara tano ya ule unaotozwa sasa. Kwa mfumo huu, Taifa litafaidika na kupanda kwa bei ya dhahabu katika Soko la Dunia na pale ambapo bei zitashuka, wawekezaji watalipa mrahaba wa kawaida kwa hiyo, hapatakuwa na mtu yejote ambaye anapata hasara.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, iwapo mfumo huu wa kodi katika madini ungekuwa unatumika sasa na ambapo bei ya dhahabu imefikia zaidi ya Dola 1,900 kwa wakia, na Taifa letu linazalisha takribani tani 60 ya dhahabu kwa mwaka. Serikali ingekusanya takribani shilingi 450 bilioni kama mrahaba. Mrahaba unaokusanya sasa kwa mujibu wa *revenue book* ni Shilingi bilioni 99 tu lakini kwa mabadiliko haya ambayo tungeyafanya kwa *uniform tax*, tungeweza kukusanya mpaka shilingi bilioni 450. Hii ingetuwezesha hata kutokopa, kwa mfano kwa ajili ya

mpango wa ule wa dharura wa umeme na tungeweza kutumia fedha za ndani kwa ajili ya kuendesha jambo hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya upinzani tunatambua kuwa ni lazima nchi zikope, na nchi nyingi duniani zinakopa ili kuboresha huduma na miradi mbalimbali ya kimaendeleo na pia kuendesha shughuli za Serikali pia, lakini tatizo letu ni ukuaji wa kasi sana wa deni la Taifa. Katika hali isiyokuwa ya kawaida, deni la Taifa limeongezeka kwa kasi sana na hali hii siyo kuachwa hivi hivi tu kwa sababu watakaoumia ni Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Mdhhibit na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali, deni la Taifa liliongezekwa asilimia 38 kutoka trillioni 7.6 mwaka 2008 mpaka Shilingi trillioni 10.5 mwaka 2009/2010, hadi kufikia mwisho wa mwezi Aprili, 2011 kwa mujibu wa tamko la hali ya kifedha la Benki Kuu ya Tanzania la Juni, 2011, deni la Taifa lilikuwa Dola za Kimarekani milioni 11,455.4 sawa na shilingi trillioni 17.1 ambapo asilimia 80 ya deni hilo ni deni la nje.

Mheshimiwa Spika, pamoja na umuhimu wa kukopa kama ambavyo mataifa mengine hufanya hivyo, kwetu sisi hii ni kasi kubwa mno ukilinganisha na ukuaji wa uchumi wa nchi yetu kwa sababu ukopaji unategemea uwezo wa kulipa pia. Hii itasababisha mzigo huu wa madeni kubebwa na kizazi cha sasa na kijacho. Ukilinganisha na nchi nyingine za Afrika Mashariki, Tanzania bado ina viwango vidogo vya mikopo kama sehemu ya pato la Taifa (*debt/GDP ratio*). Hata hivyo, wakati wenzetu wanakopa ili kuongeza uzalishaji (*capital investments*), sisi tunakopa kwa matumizi ya kawaida. Kambi ya Upinzani inapendekeza kuwepo kwa namna bora zaidi ya kuamua kuhusu mikopo ambayo Taifa linaingia ili kuhakikisha inaelekezwa katika uzalishaji mali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Bunge lilipitisha sheria ya Mamlaka ya Kudhibiti Mifuko yote ya hifadhi za jamii mwaka 2008 kwa lengo la kuangalia ni kwa namna gani mifuko hiyo inavyofanya kwa kuratibiwa vizuri na pia uwekezaji kwa kutumia fedha za wanachama wake unafanyika kwa vigezo vilivyowekwa. Kambi ya Upinzani inapongeza juhudzi zinazoendelea za kuimarisha taasisi ya SSRA ili kuweza kusimamia Mifuko hii ya Umma vizuri na kuweka mazingira ya mifuko binafsi ya pensheni kuanzhishwa.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa kuna mifuko mitano ya hifadhi ya jamii nchini yenyenye jumla ya wanachama 1,073,441. Kati ya hao, Shirika la NSSF lina wanachama 506,218 (47%), Shirika la PSPF lina wanachama 289,046 (27%), Shirika la PPF lina wanachama 160,068 (15%), Shirika la LAPF lina wanachama 73,833 (7%) na Shirika la GEPF ambalo lina wanachama 35,279 (4%). Idadi hii ya wanachama katika Mifuko yote ni sawa na asilimia 2.5 ya idadi ya watu waliopo nchini na ni asilimia 4.7 ya nguvu kazi yote iliyo katika sekta rasmi ya ajira. Hii inaonyesha kwamba watu wengi sana hawana mfumo wa hifadhi ya jamii (*social security*) licha ya kukua kwa kasi kwa watu wa daraja la katii, yaani the *middle class*. Inakadiriwa kuwa, asilimia 12 ya Watanzania ni daraja la katii kwa kipato.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuwa na uendeshwaji tofauti wa mifuko hiyo, kila mfuko umewekeza katika miradi mbalimbali kulingana na sera za uendeshaji wake. Mifuko hii imewekeza katika vitega uchumi vyenye thamani ya Shilingi trillioni 2.8, ambayo ni takribani asilimia 8.7 ya Pato la Taifa kwa bei za sasa. *NSSF* inaongoza kwa kuwa na uwekezaji wenye thamani ya Shilingi trillioni 1.03 (38%), *PSPF* inafuatiwa kwa kufanya uwekezaji wenye thamani ya Shilingi bilioni 751 (27%), *PPF* uwekezaji wenye thamani ya Shilingi bilioni 670 (24%), *LAPF* Shilingi bilioni 206 (7%) na *GEPF* Shilingi bilioni 82 (3%).

Mheshimiwa Spika, huu ni uwekezaji mkubwa sana na hii inadhihirisha ni kwa kiasi gani Tanzania ina mitaji ya kuweza kujiletea maendeleo yake. Narejea kuipongeza mifuko yote kwa uwekezaji wao katika ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma, Chuo Kikuu cha Nelson Mandela Arusha na hivi karibuni kwa mfuko wa *NSSF* kuamua kuwezeka katika kuzalisha umeme na hivyo kuelekea kuliokoa Taifa na mgawo wa umeme, kulinda ajira za viwandani, kuongeza uzalishaji na hivyo ajira mpya na wanachama wengi zaidi wa mifuko kuweza kupatikana.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inapendekeza kwa Mifuko ya *PSPF* na *PPF* kuangalia namna ya kuwekeza katika maeneo yanayochochea ukuaji wa uchumi na hivyo kuzalisha ajira na kupata wanachama zaidi. Maeneo kama uwekezaji kwenye Bandari na Reli yanapaswa kuangaliwa kwani kutokana na Jiografia ya nchi yetu ni maeneo yanayoweza kuzalisha faida kubwa sana. Tunaitaka Serikali illeleze Bunge, kuna mipango gani katika Mashirika haya (*PSPF* na *PPF*) kuangalia maeneo mapya ya uwekezaji katika miundombinu na hasa Bandari?

Mheshimiwa Spika, mifuko ya hifadhi ya jamii imewekeza katika miradi ya ujenzi wa nyumba nafuu kwa ajili ya wanachama wao na pia wanachi kwa ujumla. Tunasisitiza kwamba miradi hii isiwe Dar es Salaam na Mwanza tu, bali ienee nchi nzima kama ambavyo mfuko wa *PSPF* umeanza.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani Bungeni bado inasisitiza ushauri wake kuwa Mifuko yote ya Hifadhi ya Jamii ihamishiwe Wizara ya Kazi na Ajira kama Wizara inayohusika na *social security*. Hata Mdhibiti wa Mifuko (*SSRA*) yupo chini ya Wizara ya Kazi.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika, hakuna sababu ya kuwa na uitiri wa mifuko mingi kama ilivyo sasa. Ipunguzwe na kubakia na mifuko miwili tu, mmoja wa wafanyakazi walio katika sekta binafsi na sekta isiyo rasmi na mwingine kwa wafanyakazi wa sekta ya umma. *NSSF* na *PPF* iunganishwe kuwa mfuko mmoja kwa ajili ya sekta binafsi na isiyo rasmi na *PSPF*, *LAPF* na *GEPF* iunganishwe na kushughulika na wafanyakazi wa Sekta ya Umma.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa mifuko ya hifadhi ya jamii inawekeza katika teknolojia mbalimbali ili kuboresha utoaji wa huduma, bado kuna changamoto. Inafahamika kuwa malipo bado yanachelewa kwa sababu mbalimbali katika ule mlolongo wa kutoa huduma hii. Kwa mfano, hata pale hundi za mirathi zinapokuwa tayari na kufikishwa Mahakamani kwa ajili ya kuwakabidhi warithi, wapo watendaji ambao huzifungia kabatini au kutafuta visingizio vyovoyote vile ilimradi uwepo ugumu kwa mhusika kuzipata hundi hizo. Hii ni kero na ni chanzo cha rushwa.

Mheshimiwa Spika, tatizo la kumbukumbu na michango ya watumishi nalo bado ni kero, japo juhudzi za mapema kwa waajiri na mtumishi mmoja zinaweza kabisa kumaliza tatizo hili kama kutakuwa na mawasiliano kati ya mtumishi/mwanachama, mwajiri na mfuko husika. Wananchi na wanachama kwa ujumla wawe karibu na mifuko ili wapate taarifa zao mara kwa mara ili kama kuna mapungufu yoyote yarekebishwe mapema kabla ya muda wa kustaafu. Hii itapelekea malipo kufanyika haraka mara tu mwanachama anapostaafu.

Mheshimiwa Spika, watumishi wa umma wanaolipwa na Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (*PSPF*) wanapostaafu hulipwa mafao yao tangu kipindi walipoanza kazi, japo wao wameanza kuchangia kuanzia Julai, 1999. Kipindi cha Julai, 1999 kurudi nyuma ni deni ambalo Serikali inapaswa kuulipa Mfuko huu wa *PSPF*. Kwa bahati mbaya deni hili liliikuwa halilipwi kwa kipindi chote tangu Mfuko uanzishwe hiyo Julai, 1999, na limeendelea kukua na kuwa deni kubwa sana sasa, takriban Shilingi bilioni 3,380.

Mheshimiwa Spika, Wizara ipongezwe kwanza kwa kukubali kuwepo kwa deni hili na pili kwa kuanza kulipa sehemu ya deni husika (Shilingi bilioni 716.6). Jambo la msingi, Wizara iharakishe uhakiki wa sehemu kubwa ya deni lillosalia (Shilingi bilioni 2,663.48) ili ianzo kulipa na kuuwezesha Mfuko kuwekeza katika maeneo yenye tija kwa nchi na wanachama. Serikali ione suala hili kama suala nyeti maana tayari *acturials* wameonyesha katika hesabu za Mfuko wa *PSPF* kuwa mfuko huu ni *technically insolvent*.

Mheshimiwa Spika, Shirika la *PPF* limekuwa likifanya vizuri katika uwekezaji wake licha ya kuhudumia wastaafu wengi kuliko Mashirika mengine. Tunapenda kutoa pongezi za dhati kwa Shirika hili kwa kubuni na kutekeleza fao la elimu. *PPF* ni mfuko pekee unaotoa fao la ellimu kwa watoto wasiozidi miaka minne. Fao hili hutolewa endapo mwanachama atafariki dunia na amechangia miaka isiyopungua mitatu. Hadi kufikia mwishoni mwa mwaka 2010 *PPF* ilikuwa imelipia zaidi ya watoto 1,105 kiasi cha Sh. 505,212,000/=. Ni vizuri mifuko mingine iangalie

uwezekano wa kuanzisha fao hili ili kusaidia watoto wa nchi yetu ambao wazazi wao wameondoka duniani.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani Bungeni inapenda kupata taarifa kuhusu agizo la kufanya ukaguzi maalumu kwa Shirika hili kuhusiana na malipo ya mafao kwa kada ya watumishi wa mikataba. Vile vile tumeypata taarifa kuwa kuna wafanyakazi wa mfuko huu wamesimamishwa kazi kutokana na kutoa taarifa kuhusu malipo haya. Kambi ya Upinzani Bungeni inapenda kupata taarifa ya Serikali kuhusu suala hili.

Mheshimiwa Spika, Shirika la *GEPF* limeanza kuandikisha wanachama katika sekta isio rasmi. Zoezi hili limefikia wananchi wa kada ya chini kabisa na hivyo kuongeza idadi ya Watanzania walio katika mfumo wa Hifadhi ya Jamii. Hatua hii ni ya kupongeza sana. Kambi ya Upinzani inawataka *GEPF* wafike katika maeneo ya wavuvi ili waweze kuchangia na kufaidika na mafao ya aina mbalimbali yanayotolewa.

Mheshimiwa Spika, Serikali iliongeza viwango vya pensheni ilipwayo kwa wastaifu na kiwango cha chini kilipanda na kuwa Sh. 50,000/. Wastaifu wanalalamika kuwa sasa unaanza mwaka wa tatu bado hawaioni nyongeza hiyo. Wakienda Wizarani wanaambiwa nendeni *PSPF*, wakienda *PSPF* wanaambiwa Wizara hajatoa hizo pesa ili *PSPF* iwaongezee/kuwalipa wastaifu hawa. Serikali itamke kuwa ni lini wastaifu hawa watalipwa? Kwa mujibu wa sheria iliyopo, nyongeza yoyote ya pensheni italipwa kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali. Kwa hiyo, Wizara itoe majibu ni lini itamaliza kero hii, vinginevyo hili nalo ni deni ambalo litaendelea kukua na pengine kupelekeea/kuanzisha mgogoro kama wa wastaifu wa iliyokuwa Jumuia ya Afrika Mashariki ambao kila kukicha wazee wetu hawa wanaandama kwenda Hazina na Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani imepata taarifa kwamba wanajesi wastaifu na hasa waliofikia ngazi ya Brigedia Jenerali wanalipwa pensheni ndogo sana. Inasemekana mwanajesi aliyestaifu katika cheo cha Brigedia na kuendelea anapata pensheni ya Sh. 58,000/= tu. Hiki ni kiasi kidogo sana kwa watu walitolitumia Jeshi na Taifa letu. Ninashauri kiwango hiki kiongezeke maradufu ili angalau wanajesi wetu waishi maisha yenyen staha katika ustaifu.

Mheshimiwa Spika, kasma 229,900 - Shilingi bilioni 100 zimetengwa kwa ajili ya dharura za kitaifa. Ni kweli kwamba kunaweza kuwa na dharura wakati wowote. Hata hivyo, Shilingi bilioni 100 za dharura zimefikiwa kwa vigezo gani? Katika vitabu vya bajeti havionyesi mwaka jana zilitengwa kiasi gani kwa dharura. Kambi ya Upinzani inataka maelezo ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, ni vyema sasa tuanze utaratibu wa kupata takwimu ya jumla ya ruzuku ambazo Serikali inatoa kwa Mashirika na Taasisi za Umma. Takwimu zinakuwa ngumu kupatikana na hivyo kutoweza kudhibiti kikamilifu ruzuku hizi. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ieleze, kwa mfano, kwa mwaka huu wa fedha 2011/2012 Serikali inatoa ruzuku kiasi gani kwa taasisi na Mashirika ya Umma? Ni Ofisi gani Hazina inayohusika na kugawa ruzuku hizi? Inawezekana Ofisi ya Msajili wa Hazina badala ya kurekebishwa ikapewa jukumu hili la kugawa ruzuku.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na miundo kandamizi ya Wahasibu wa Serikali kwa muda mrefu, hivyo kusababisha wastaifu wakiwa mafukara kwa sababu ya mishahara midogo wanayolipwa. Muundo huo unaweka kigezo cha Mhasibu kupanda ngazi moja tu baada ya kuajiriwa katika maisha yake ya kazi iwapo hatapata shahada ya taaluma ya uhasibu (*CPA*). Huu ni unyanyasaji ambao hauwezi kuvumiliwa, iwapo mhitimu wa shahada nyingine yoyote ile anapandishwa kila muda unapofika bila matatizo. Hiki ni kilio cha muda mrefu kwa Wahasibu wote nchini. Taarifa zinazoletwa hapa Bungeni, zinaandalialiwa na Wahasibu hawa ambao hawajatunukiwa shahada ya *CPA*: Je, inakuwaje taarifa hizo tunazikubali, lakini waandaaji tunawawekea miundombinu kandamizi? Kambi ya Upinzani inamtaka Waziri alieleze Bunge ni Wahasibu wangapi wana shahada ya *CPA* kwa sasa? Ni vyema utaratibu huu ukaangaliwa upya na kada hii ya uhasibu ikajiona kuwa mchango wake ni muhimu sana katika kulitumikia Taifa hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Wizara ya fedha ni makubwa na muhimu kwa nchi yetu. Majukumu haya yakisimamiwa vizuri tutaweza kupeleka mbele nchi yetu. Ninawataka watumishi wote wa Wizara ya Fedha na Taasisi zake wafanye kazi kwa bidii katika kusimamia uchumi wa nchi

yetu. Uwajibikaji ndio suluhisho kubwa kwa matatizo ya rushwa, hongo, ubadhifuru na ufisadi. Kambi ya Upinzani na Waziri kivuli wa Fedha na Uchumi atatupia jicho kali kuhakikisha kunakuwepo na uwajibikaji na kila mtumishi anajibu kwa matendo yake.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha kwamba Taifa letu limepoteza miaka mitano ya mwanzo ya utawala wa awamu ya nne kutokana na kelele nyingi za kisiasa. Kuna hatari kubwa sana kwamba miaka mitano ijayo inaweza pia kupotea. Ni lazima sote kwa pamoja bila kujali itikadi za vyama vyetu kuhakikisha tunafanya kazi kwa pamoja ili kuendeleza nchi yetu. Watawala watekeleze wajibu wao ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu sasa sote kama Taifa kuweka nguvu zetu zote na kuweka mazingira yanayochocha uwekezaji katika gesi asilia na mafuta ufanikiwe. Tusipoteze muda huu, kwani uwekezaji mkubwa katika gesi asilia utasaidia sana kupata umeme nafuu na wadau kwenye sekta, wanasema pato la Taifa litapanda kwa asilimia 40. Vile vile uwekezaji katika Mradi wa Mchuchuma na Liganga utaongeza pato la Taifa kwa asilimia 25. Wizara ya Fedha na Uchumi iwe Wizara kiongozi kuhakikisha miradi hii haipotei, kwani ikitekelezwa nchi yetu itakuwa na uchumi mkubwa zaidi kuliko nchi zote za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani tutaendelea kuwa jicho la Watanzania dhidi ya watawala. Ninawataka Mawaziri Vivuli wote wafuatilie kwa karibu sana utendaji wa Mawaziri katika maeneo yao ili kuhakikisha kuwa bajeti hii inatekelezwa kwa faida ya mwananchi wa kawaada. Uwaziri kivuli usiishie Bungeni wakati wa Mikutano ya Bunge, bali siku zote. Kila kauli inayotolewa na Waziri wa Serikali lazima Waziri Kivuli aitolee jibu na pale pa kupongeza papongezwe, lakini pale pa kukosoa tukosoe kwa nguvu zetu zote. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inasema, ni lazima kuhakikisha Mawaziri wawe macho muda wote ili wale Mawaziri goigoi na wanaosinzia kila kukicha wapishe utumishi wa umma na hivyo kuondoa vikwazo vya maendeleo ya nchi yetu. Pale ambapo Serikali hii ikianguka Mawaziri vivuli wawe tayari mara moja kuchukua majukumu ya Mawaziri wa Serikali na kuanza kazi bila kuchelewa.

Mheshimiwa Spika, nawatakia wote sikuu njema ya Eid El Fitr. Kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Moja tu kubwa ulilolisema hapa ni kwamba tuache kelele za kisiasa, tufanye kazi. Nadhani hilo ni muhimu sana. Kabla sjatoa nafasi kwa wachangiaji wengine, naomba niwatambue wageni waliopo katika Ukumbi wetu waliokuja rasmi kwa Wizara hii. Kwa hiyo, ni wageni wa Wizara ya Fedha. Yupo Dkt. Likwelile, yeye ni Naibu Katibu Mkuu, kwa sasa anakaimu nafasi ya katibu Mkuu, nadhani yuko kwenye sehemu ya kazi. Yuko Laston Msongole, ni Naibu Katibu Mkuu, Bi. Elizabeth Nyambibo, ni Naibu Katibu Mkuu, yupo Ndugu Mwanaidi Mtanda - Mhasibu Mkuu wa Serikali. Yuko Athanas Pius ambaye ni Msaidizi wa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, yupo...

(*Hapa Umeme Ulikatika*)

**SPIKA:** Aah! Hii yote Ngeleja! Si ndiyo inaitwa hivyo? (*Kicheko/Makof*)

Yupo pia Ndugu Harry Kitilya - Kamishna Mkuu wa TRA, yupo Prof. Beno Ndullu Gavana wa Benki Kuu, yupo Ndugu Veronica Lyapa, Mhasibu Mkuu wa Wizara, yupo Ndugu Sayi Msungi - Mhasibu Mkuu wa Fungu 21, maana yake ni Hazina. Nadhani wako kwenye shughuli za kazi.

Halafu yupo Israel Kamuzora - Kamishna wa Bima, yupo Ndugu Irene Kisaka - Mkurugenzi Mkuu wa *Social Security Regulatory Authority*, yupo Ndugu William Erio -Mkurugenzi Mkuu wa *PPF*, yupo Ndugu Adam Maingu - Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa *Public Service Pension Fund*, yupo Ndugu Khamis Ame - Katibu Tume ya Pamoja ya Fedha, yuko Mwenyekiti mwenyewe - Mheshimiwa William Shellukindo ndiye Mwenyekiti wa Tume hiyo na Mheshimiwa Mbunge mstaafu. Alifanya kazi

kubwa sana katika kulifanya Bunge letu liwe kama liliyo leo hii. Kwa hiyo, tunakukaribisha sana na tunakupongeza sana, *of course* ni mume wake na Beatrice Shellukindo. (*Makofi*)

Pia yuko Ndugu Peter Noni, yeye ni Mkurugenzi Mkuu wa *Tanzania Investment Bank*. Halafu pia kuna wageni wengine wa Mheshimiwa Mustapha Mkulo - Waziri wa Fedha ambao ni Wakurugenzi Wakuu, Wakuu wa Idara, Wakuu wa Vitendo, Wenyeviti wa Bodii, Wakuu wa Taasisi zilizopo chini ya Wizara yake na Watumishi wa Wizara hiyo. Karibuni sana. (*Makofi*)

Vile vile wapo wageni wa Naibu Waziri wa Fedha - Mheshimiwa Gregory Teu, ni mke wake na watoto wake. Karibuni sana. Halafu yupo pia Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mpwapwa na Madiwani 17 kutoka Mpwapwa, karibuni sana. (*Makofi*)

Basi nashukuru na tunaendelea. Sasa kama mtakavyoona jana, tuna tatizo kabisa na hii Wizara, tumeipa siku moja lakini wachangiaji wako wengi. Kwa hiyo, tutaanza na wachangiaji ambaao hawajachangia hata mara moja nao ni Mheshimiwa Devotha Likokola, atafuatiwa na Mheshimiwa ambaye amechangia mara moja naye ni Mheshimiwa Khatib Said Haji. Kwa hiyo, kwa leo ni hao tu tutakaowenza kuwafikia. Sasa namwita Mheshimiwa Devotha Likokola.

**MHE. DEVOTHA M. LIKOKOLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kuunga mkono hoja hii ya Wizara ya Fedha na ninaunga mkono kwa sababu ya jitihada kubwa zinazofanywa na Watendaji wa Wizara hii wakiongozwa na Mheshimiwa Waziri na Manaiwu Waziri. Kwa kweli wanafanya jitihada kubwa, lakini bado tunaona kuna changamoto nyingi ambazo zinatukabili.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa leo nitajielekeza katika maeneo makubwa mawili, lakini eneo la kwanza ni suala zima la uwezo wa Serikali kukusanya mapato yake. Lakini pia nitachangia katika eneo la pili la uwezo wa wananchi kupata mitaji na kupata fedha za kuweza kuzalisha. Sasa naomba nianze kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha pamoja na majukumu mengi ambayo inafanya lakini ina taasisi kubwa mbili ambazo zinajitahidi sana kufanya majukumu yake, na ni taasisi kubwa. Taasisi ya kwanza ni *TRA*. Waheshimiwa Wabunge wote tumekuwa tukitoa pongezi kubwa kwa *TRA* kwa kazi wanazofanya. Mkurugenzi Kitilya anajitahidi sana kukusanya mapato, lakini bado changamoto ni kubwa, mapato hayatoshi na Waheshimiwa Wabunge wote wanassema habari ya sungura. Sasa hivi tunaomba mapato yaongezeke ili tuweze kuwa na tembo na Wizara zote ziweze kupata fedha za kutosha kutekeleza majukumu yake. Kwa hiyo, bado tunashauri kwenye Wizara hii suala la kuongeza wigo wa mapato, ni suala muhimu, bado kuna biashara nyingi sana ambazo haziko rasmi na bado hazitozi kodi.

Mheshimiwa Spika, kama biashara nyingi zitaendelea kutotoza kodi, maana yake walipa kodi watakuwa ni wachache na Sungura ataendelea kuwa mdogo na malalamiko yataendelea. Kwa hiyo, tutajigeuza kuwa Taifa la malalamiko. Tunachoomba, wenzetu wa *TRA* watusaidie kuongeza wigo wa kodi.

Mheshimiwa Spika, bado kuna changamoto kubwa. Katika Halmashauri zetu kuna mapato mengi sana, lakini naomba watu wa *TRA* wasaidie kuelimisha watu wa Halmashauri ili waweze kukusanya kodi za kutosha. Tuna miradi mingi, tuna changamoto nyingi, lakini bado kulingana na uwezo wa fedha ambazo zinapatikana kutoptana na mapato ya Serikali, miradi hii haiwezi kutekelezeka vizuri. Naomba pia elimu iendelee kutolewa ili Watanzania tuone fahari ya kulipa kodi. Watanzania wote tuone kwamba kodi ndiyo inayoendesha maendeleo ya nchi hii. Wananchi wakielimishwa kwa wingi wataelewa umuhimu wa kodi na watalipa kodi kwa wingi na Serikali itakuwa na mapato ya kutosha na kuweza kutekeleza miradi mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, bado tuna changamoto kubwa hii ya kulipa kodi ambayo inatokana na uwezo wa wananchi kufanya biashara ambaao unaambatana na vikwazo mbalimbali vikiwemo vikwazo vya kupata mitaji.

Mheshimiwa Spika, sasa nihamie upande wa Benki Kuu (*BoT*). Benki Kuu wanatusaidia sana kusimamia sera za fedha na mifumo mizima ya fedha katika nchi yetu, lakini kama wananchi bado watakuwa wana uwezo mdogo wa kupata mitaji, hata kama wanajua kufanya biashara, bado hawataweza kufanya biashara na bado hawataweza kulipa kodi. Kwa hiyo, ninaomba sana Mheshimiwa Gavana aangalie uwiano uliopo kati ya Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) na kwa upande wa *BoT* ili muone kwamba kama mtafanya kazi kwa kushirikiana vizuri, maana yake watu wengi wataweza kupata mitaji, watafanya biashara na watalipa kodi nyingi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na yote, Mheshimiwa Gavana anajitahidi sana na tumeona nchi yetu inapata sifa kubwa ya kukuza uchumi, lakini changamoto kubwa ni ya kuondoa umasikini kwani nchi hii inashindwa kuondoa umasikini. Umasikini umekithiri mpaka vijiji, watu wanalamika maisha yamekuwa ni ya shida. Kwa hiyo, tunaomba tuangalie kwa kina jukumu hili la kuondoa umasikini wa nchi yetu ili tuweze kulifanya vizuri. Haina maana nchi kukuza uchumi kama itashindwa kuondoa umasikini. Wananchi kama wanazidi kulalamika, maana yake ni kwamba bado hawajaridhi, na mapato yanayopatikana kwa Serikali yetu hayajaweza kwenda mpaka ngazi za chini na kuonyesha kwamba nchi yetu inakuza uchumi.

Mheshimiwa Spika, ingawa bado tuna mapato mengi yanayopatikana, lakini vilevile kuna mifumo mingi ambayo inaweza kusaidia katika kupunguza umaskini. Ninaomba kitengo chetu cha kuondoa umaskini kijitahidi kushirikiana na wadau mbalimbali ili waweze kuongeza kasi ya kuondoa umaskini katika nchi yetu. Wananchi wengi sana wanaweza kufurahia kama watakuwa siyo maskini.

Mheshimiwa Spika, ninapongeza sana Serikali, Mheshimiwa Waziri pamoja na Gavana kwa *ku-commission study* maalum kuangalia mfumo mzima wa *VICOBA*.

Mheshimiwa Spika, wana-*VICOBA* wamenitura kumshukuru Gavana ambaye amefanya *study* katika Mikoa ya Ruvuma, Njombe, Iringa na Morogoro kuangalia utendaji wa shughuli nzima za *VICOBA* na hivyo kuangalia ni namna gani Serikali itajikita katika kusaidia mfumo huu. Ninatoa pongezi katika suala hilo na kwa sababu Waheshimiwa Wabunge wengi wamekuwa wakihangaika kusaidia mfumo wa *VICOBA* katika majimbo yao, na sasa Serikali inataka kuanza kusaidia *VICOBA*, basi ninapongeza sana jitihada hizi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika Serikali yetu tuna benki ambazo zinamilikiwa na Serikali kwa asilimia mia moja. Benki hizi ni pamoja na Benki ya Twiga pamoja na Benki ya Posta. Wote ni mashahidi kwamba Benki ya Posta mtandao wake umefika mpaka vijiji. Pia Benki ya Twiga imekuwa ikijitahidi sana kufanya shughuli mbalimbali za Serikali hii na za kibashara. Lakini ninaomba kutamka kwa masikitiko makubwa kwamba mitaji ya Benki hizi ni midogo sana. Mitaji ni midogo kiasi kwamba ni huruma kwa Watendaji wa Benki hizi, kwani wanahangaika sana, ni kama vile tunawachanganya. Kwa kweli ninamhurumia sana *Chief Executive Officer (CEO)* wa Benki ya Twiga, Bwana Mbululo, anahangaika. Ana uwezo mkubwa wa kukusanya *deposits* za wateja, lakini haruhusiwi kukopesha kulingana na ukomo wa mtaji wake.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ombi langu ni kwamba Mheshimiwa Waziri kwa dhati atoe maamuzi magumu, awape Benki ya Twiga angalau Shilingi bilioni kumi waongeze mtaji wao. Awape Benki ya Posta angalau Shilingi bilioni kumi waongeze mtaji wao, ili wafanye kazi kwa raha jamani. Tunawachanganya hawa Watendaji wetu katika hizi Benki mbili na wanashindwa sasa kuongeza huduma zao katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa namna pekee nampongeza mtendaji Mkuu wa Twiga kwa maana ye ye ndiye *CEO* pekee aliyeweza kuthubutu kujaribu kukopesha vikundi vya *VICOBA* na ameweza kuona mafanikio yake.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Samahani Mheshimiwa Likokola. Mheshimiwa Tundu Lissu nawaombeni sana, dakika zetu ni ndogo, ukisimama wewe basi mtu mwingine ni lazima aache kusema. Naomba sana tumalize kwanza hii kazi. Mheshimiwa Likokola endelea!

**MHE. DEVOTHA M. LIKOKOLA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na hizo changamoto mbalimbali, lakini naomba pia Serikali ijaribu kuangalia suala zima la kuwezesha mifuko mbalimbali kama vile ya *SELF, NIGP* na mifuko mingine ili iweze kuendelea kuwawezesha wananchi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kumsifia Gavana, lakini tuna tatizo la msingi la kupanda kwa dola. Wananchi wengi wanalamika dola inapanda kila siku. TunamWomba Mheshimiwa Gavana, kwa utaalami wake ajaribu kuangalia hili suala la dola kupanda thamani. Wananchi wa nchi hii wanatumia dola kama ndiyo shilingi. Maduka mbalimbali wanaweza kununua kwa kutumia dola, hoteli mbalimbali wanalipa kwa kutumia dola.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri tukaithamini shilingi yetu. Hata ushuru wa Serikali kuna maeneo mengine yanatozwa kwa kutumia dola. Mimi naomba kwa kweli tuithamini shilingi yetu na hivi itazidi kukua. Lakini kama tutaichia shilingi itazidi kuperomoka na hatimaye tutaendelea kuthamini fedha za kigeni. Ninaomba sana kwa utaalami wa Gavana, ninaamini atajitahidi kushirikiana na watendaji wenzake ili kuhakikisha kwamba shilingi yetu ya Tanzania inapanda thamani. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa mchango huo, ninaomba pia kuwashukuru sana viongozi wote na watendaji wa Wizara hii, lakini vilevile ninaomba kuwashukuru sana na kuwatachia kila la kheri wanawake wa Mkoa wa Ruvuma. Wanawake wa Mkoa wa Ruvuma wamejipanga vizuri na tunaomba kwa ushirikiano ambao tumeanza na Benki ya Wanawake, ninaamini kwamba tawi la kwanza la Benki ya Wanawake litakuwa Mkoa wa Ruvuma kwa sababu wanawake wale wamejipanga vizuri. Mheshimiwa Jenista Mhagama alianzisha *SACCOS* za kutosha, mimi nimeanzisha *VICOBA* ya kutosha, kwa hiyo sasa tunaomba Wizara itusaidie ili Benki ya Wanawake tawi la kwanza liende Mkoa wa Ruvuma. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na ushiriki mkubwa wa Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, katika kuendeleza Wajasiri amali, tunaamini kwamba Benki ile tutaweza. Kwa sababu muda ni mchache na ninaona ni busara niwaacie wenzangu wapate nafasi ya kuchangia hotuba ya Wizara hii, naunga mkono hoja. Nasema ahsante. (*Makof*)

**SPIKA:** Kabla hujakaa, useme juu ya uhusiano wako na *VICOBA*, hukusema mwanzo!

**MHE. DEVOTHA M. LIKOKOLA:** Mheshimiwa Spika, na-declare interest kwenye *VICOBA*.

**SPIKA:** Wewe ni nani? Ndiyo hiki Mheshimiwa Tundu Lissu alikuwa anataka kusimama ili akuulize. Una *interest* gani kwenye *VICOBA*?

**MHE. DEVOTHA M. LIKOKOLA:** Mheshimiwa Spika, mimi naendesha taasisi inayoitwa *VICOBA Sustainable Development Agency*, kwa hiyo ni Mkurugenzi wa ile taasisi.

**SPIKA:** Kwa hiyo, una *interest!* Tunaendelea na Mheshimiwa Khatib Said Haji, na naona kwa jioni hii ndiye atakuwa msemaji wetu wa mwisho.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nashukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Kwanza, kabla ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuwa katika hali ya afya kamili katika siku ya leo na kuweza kufikia mfungo wa mwezi ishirini na tano wa Ramadhani. Ni imani yetu kwamba tutazimaliza tano, inshallah tutakula Sikukuu ya Idd El Fitri. Waheshimiwa Wabunge, karibuni Konde sote tule Idd El Fitri. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa dhati kabisa, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa jinsi ambavyo unaliendesha Bunge letu. Kwa sisi Wabunge wapya tumefarijika sana na jinsi ambavyo

unatuelekeza hata pale tunapokosea na unatulinda na yale mambo mengine ambayo ni mapya na tunakutana nayo hapa. Endelea kutulinda na mimi naamini hakukuwa na makosa kwa sisi kukuchagua wewe kuwa Spika wetu. Wanawake wanaweza na ni zaidi ya kuweza. (*Makofi/Kicheko*)

**MBUNGE FULANI:** Kweli ni zaidi ya kuweza!

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Spika, mimi leo mchango wangu katika hoja hii, kwanza nitoe masikitiko yangu juu ya usumbufu wanaoupata wafanyabiashara wa Zanzibar. Kwanza, samahani napenda ku- *declare interest* ...

**SPIKA:** Sawasawa!

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mimi ni mfanyabiashara au mjasiriamali ndogo ndogo na ninamiliki Kampuni ya *Clearing and Forwarding*, na pia namiliki kampuni ya biashara inayojihusisha na uagizaji wa bidhaa kutoka nje.

**SPIKA:** Ahsante!

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Spika, wafanyabishara kutoka Zanzibar wamekuwa na kilio cha muda mrefu juu ya hali wanayokutana nayo hasa wanapoingia katika Bandari ya Dar es Salaam. Hili siyo jipya na hapa limeshakuja sana na hata mimi leo naona haja ya kulizungumza.

Mheshimiwa Spika, pale Zanzibar au Tanzania kwa ujumla Mamlaka ya Mapato Tanzania ni moja. Wafanyakazi wa *TRA* ninavyojuua mimi wanateuliwa na Kamishina Mkuu aliyeo hapa Dar es Salaam, lakini la kushangaza wale wale, maamuzi yao yanayofanyika Zanzibar yanapofika Dar es Salaam yanakuwa kama hayafanyi kazi. Hili jambo limejitekeza na linaendelea kujitekeza na hata tunaposema inaonekana kama ni wimbo.

Mheshimiwa Spika, imekuwa ni kawaida kwa wafanyabiashara wanapofika na bidhaa zao pale inaonekana kile walichokifanya Zanzibar hakitambuliki au ushuru wallolipia Zanzibar siyo ushuru halali, na badala yake inakuwa ni matatizo makubwa ya bidhaa zao kuwekwa muda mrefu pale, kitu ambacho kinarudisha nyuma maendeleo ya biashara zao.

Mheshimiwa Spika, mfano hai wakati tunaanza kikao hiki cha Bunge kulikuwa na msongamano wa magari zaidi ya 300 pale katika Bandari ya Dar es Salaam ambayo yalishalipiwa kodi Zanzibar na yalipofika pale kwa sintofahamu yalizuiwa muda mrefu na mengine nadhani mpaka sasa yako pale. Tatizo halieleweki ni lipi! Mfumo wa kodi ni mmoja, chombo kinachosimamia kodi ni kimoja Tanzania Zanzibar na Tanzania Bara, lakini maamuzi ya Zanzibar yanaonekana sivyo.

Mheshimiwa Spika, wafanyakazi wale wengine wanaotoka huku Bara wako pale Zanzibar. Sasa mimi namwambia Waziri na leo, Watendaji Wakuu wa *TRA* wapo hapa, kama wale wanaopelekwa pale kusimamia mambo yale hawaaminiki, basi wapelekwe hao malaika basi, kwa sababu limekuwa ni tatizo, tena kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo katika nchi ambazo zina muungano kama huu au zinashirikiana katika hali kama hii, mfano, pale katika Falme za Kiarabu kuna muungano wa nchi saba zile kuanzia Dubai, Abudhabi, Ajmani, Sharjah na kadhalika, lakini katika sehemu zile unaponunua gari au unapotoka na gari pale unaweza ukaingia nalo katika nchi yoyote kati ya zile pasipokuwa na vikwazo.

Mheshimiwa Spika, tukiacha hilo la kodi, hata Mzanzibari leo akitamani kutoka na gari lake Zanzibar kuja huku kwa matumizi ya kawaida hawezi kupita kwa urahisi pale na akalitumia gari lake. Hata kama hana nia ya kufanyabiashara Bara, nia yake anakuja Dar es Salaam au Tanzania Bara, ana safari yake labda anataka kukaa miezi miwili au mitatu hawezi kuingia na gari lile pale akaweza kufanya shughuli zake. Atakumbana na vikwazo tele! Ataambiwa badilisha kwanza namba. Sitaki kukaa na gari hili Bara, nimekuja kwa shughuli zangu binafsi na baada ya muda

nitarejea na gari hili Zanzibar. Kwanini viwepo vikwazo ambavyo siyo vyatia? Kwanini Mzanzibari huyu asiachiwe kutumia gari lake huku?

Haya mambo naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa ayaeleze vizuri kabisa, ayatolee ufanuzi kiasi ambacho kitatuwezesha na sisi tujihisi kwamba tuko huru kama Wa-Bara walivyo huru kuingia na magari yao. Mtu wa Bara akiingia nusu saa, tayari yuko Darajani na gari lake, hakuna kero. Hapa pia hali hiyo iondoke. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, leo ni ajabu kwamba mtu kutoka Congo au Kenya hachukui dakika 15 kuingia na gari lake. Basi uwewe utaratibu kama uliyowekwa kule mpakanii! Haichukui hata dakika 15 mtu tayari ameingia na gari, anatanua ndani ya ardhi ya Tanzania Bara, lakini kwa Mzanzibari hawezi kusema gari hili nataka kulitumia Dar es Salaam likaisha, atachukua labda wiki mbili au miezi miwili pale katika Bandari ya Dar es Salaam, bado anasumbuka kuingia na gari lake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri kama kuna utaratibu, uwewe ili Mzanzibari ambaye hataki kuja kuuza gari lake katika nchi ya Tanzania Bara aweze kuruhusiwa kuingia na gari lake alitumie kwa mujibu wa mfumo ambaa utawekwa na atakapomaliza shughuli zake aweze kulirejesha gari lake Zanzibar. Lakini ile hali ya sasa kwa kweli haturidhiki, haturidhiki, haturidhiki! Tena hayo siyo mazuri japo mwatufanyia tu. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nataka kuzungumzia suala dogo la wafanyabiashara wakubwa. Mamlaka ya Mapato imeweka mpango ili wafanyabiashara wakubwa sana ambaa wana jina wamewabatiza kwamba wao mizigo yao inapoingia bandarini siyo muhimu kukaguliwa pale, watakaguliwa pengine kama itatokea haja huko katika maghala yao ya kuhifadhiya mizigo. Mimi hili silifahamu vizuri, hivyo ni vyema Mheshimiwa Waziri alitolee ufanuzi. Hata hivyo, mimi naona hii ni hatari kubwa. Ni hatari kwa usalama wa Taifa, na ni hatari pia kwa pato la Taifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wafanyabiashara ni sisi, na mmojawapo ni mimi ambaye nimejitambulisha hapa. Mfanyabiashara siku zote anaangalia maslahi yake kwanza na mambo mengine yanafuata baadaye.

Leo mfanyabiashara mkubwa akija na makontena yake yawe ni 20 au 30 anaambiwa aiingize tu, utaratibu huu naona siyo mzuri hata kidogo. Lakini wajasiriamali wadogo wadogo tukileta pale kikontena kimoja ambacho tumechangia watu 20, kitatolewa darubini zote hapo. Hii vipi? Hajatulia hata kidogo! Naomba iangaliwe. Wafanyabiashara wakubwa na wao wakaguliwe, kwani kuna kuna hatari wakaingiza vitu tuvitakavyo na tusivyonitaka. Tafadhali hili liangaliwe, kwani ni suala zito sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuzungumzia habari ya kutokuaminiwa kwa wafanyabiashara. Lipo tatizo tena kubwa ambapo Mamlaka ya Mapato leo hii imeweka utaratibu wa kuwa na bei zao. Mfano, kwa upande wa magari, ukinunua gari ukija nalo pale wao wana viwango vyatia kodi ambavyo wameviweka na tatizo siyo kiwango cha kodi ambacho wamekiweka, tunakubaliana kwa hilo, lakini kukubaliana na mnunuzi kuhusiana na bei aliyonunula gari lake, hilo kwao halipo. Gari umenunua wewe, bei wanakupangia wao, sasa haya mambo yanatoka wapi?

Mheshimiwa Spika, leo kuna vile vigari vinaitwa *Vitz*, kile kigari sana sana utakuta ni Dola 1000 Japan, lakini ukija nacho hapa ukifika Dar es Salaam unaambiwa hiki tunaki-value Dola 4000, utake usitake ni Dola 4000. Sasa jamani kama chombo cha Serikali tunachokitegemea kitoe haki ndiyo hicho kinachokandamiza haki, nyie mlisema kwamba ushuru tutatoza asilimia sitini (60%) na asilimia kumi na nane (18%) kulingana na bei ya gari. Leo ninapokuja nikasema gari hili nimelinunua Dola 1000 mnasema ni Dola 4000, nimenunua mimi au mmenunua ninyi! (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri sasa hivi dunia hii ya utandawazi hii gari nilioleta pale documents zinaonyesha kwamba nimenunua Dola 1000, waki-search kwa sababu mpaka duka

wanalijua, watapata *data* zote kama lile gari nimelinunua kwa Dola 1000, lakini hawakubali kabisa! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nasema hawa wanafundisha samaki kuogelea wakati anazaliwa kwenye maji. Ndiyo kwa sababu mfanyabiashara siku zote kadri wao wanavyokazana kupanga mbinu za kudhibiti wizi wa mapato na mfanyabiashara ndivyo anavyojitahidi kutafuta mbinu za kukwepa mapato. Sasa wewe unapomwonyesha kwamba unataka kumwibia, na yeye akiiba dhambi iko wapi? Mwizi akimwibia mwizi kuna kosa? Ndiyo! Kwa hiyo, tukubaliane na ukweli ulivyo. Gari linauzwa Dola 1000, mkubali! Nchi zinazotoa magari ambayo yanaletwa zaidi Tanzania ni Japan, Uarabuni na Uingereza, basi. *TRA* wekeni mawakala wenu pale kwa ajili ya ukaguzi ili mnunuzi anaponunua gari anakwenda pale anaonyesha kwamba, hii gari jamani nimeshanunua, nendeni tu pale mkathibitishe. Siyo magari ya watu, walalahoi yanafika hapa na yanaganda bandarini kwa bei za ajabu ajabu. Jamani, tunawaonea watu wetu, hata aibu hatuoni! Hebu tufike mahali tukubaliane na ukweli ulivyo. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuzungumzia hotuba ya Mheshimiwa Waziri hususan katika ukurasa wa 51 kifungu cha 92 ambapo amezungumzia habari ya *Tanzania Investment Bank (TIB)*. Pamoja na malengo mazuri ya *TIB*, lakini ningetaka nimwulize tu Mheshimiwa Waziri kwamba sisi Zanzibar hatumo! Kwenye *TIB* Zanzibar hawamo na sisi hatuli! Ndiyo! Kwa sababu hapa pana matawi zaidi ya nane ambayo wameshafungua, lakini sikusikia Zanzibar ikitajwa hapa. Naomba tu na hili nalo litolewe ufanuzi ili tujue kama na sisi tunahusika au ni kama kawaida yetu, sisi baadaye pia tujue.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kwa ruhusa yako, naomba niseme jambo moja ambalo kama muda utaniruhusu naomba univumilie kidogo na hili. Siku ya tarehe 18 nilipochangia kwenye hotuba ya Afrika Mashariki nilizungumzia jambo moja ambalo kiasi fulani nahisi lilinikwaza baadaye.

Mheshimiwa Spika, nilizungumzia suala la maslahi ya Wabunge, lakini kwa bahati mbaya suala hili limezua *soo* kubwa sana. Kuna gazeti moja ambalo kila siku linatoa taarifa ile kana kwamba mimi nilifanya jambo la ajabu sana hapa Bungeni. Gazeti la Tanzania Daima, makala zao zote na mpaka toleo la jana, wameandika taarifa kwenye ukurasa mmoja kwamba, Bungeni kuna Wabunge na Mbua kumbe Bungeni kuna Wabunge na Mbua. Sasa hili neno mbua katika Kiswahili cha Kipemba mimi sikulipata, nimelitafuta sikulipata lakini kwa tafsiri zisizo rasmi nimesikia kama ni wa njaa.

Mheshimiwa Spika, lile suala la sisi Wabunge maslahi kwa jamii, mimi nasema Wabunge maslahi kwa jamii, kuzungumzia hapa suala la kuboreshewa maslahi yetu kwa ajili ya ajili ya kusaidia wananchi wetu, mimi suaona kama ni dhambi. Wale wanaotumia gazeti lao uchwara la Tanzania Daima nawaonya hapa, limekuwa likitoa makala toka siku ile mpaka jana, juu ya kwamba mimi nilifanya dhambi kubwa sana. Ninachosema ni kwamba, kile kidogo inachotupa Serikali, sisi tunasaidia wananchi wetu. Tunasaidia na ndiyo maana Mheshimiwa Shibuda akatuita Wabunge Jamii. Sisi ni Wabunge Jamii.

Mheshimiwa Spika, nikupe mfano mdogo tu, mimi katika jimbo langu la Konde tayari wananchi wangu wanafaidika na huduma za Mbunge kwa kusaidia huduma ya kuwasafirisha wagonjwa kwenda hospitali, na bima nimewawekea mfano wake kwa sababu mgonjwa yeoyote hasumbuki kupelekwa hospitali pale anapoumwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu ya Zanzibar ilifanikiwa kuendesha kampeni ya uzazi salama na uzazi wa mpango. Wapemba tumesoma zaidi uzazi salama, lakini wa uzazi wa mpango hatukuujuu. Mpemba mmoja anaweza kuwa na wanawake wanenye, na wakabahati kujifungua kwa mara moja, hilo linatokea. Maskini, hawana uwezo, leo gari za Mbunge ziko pale zinawapeleka wagonjwa hospitali. Hilo dogo! (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, leo hii kama ninachosema ni cha utani, hebu waruhusu hawa wahudumu humu ndani wakukusanyie simu za Wabunge 50 tu uweke kwenye ukumbi wako, ndani

ya dakika kumi usome matatizo ya wananchi wetu yaliyomo, uone kama hutaletewa *ambulance* hapa ndani. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, uone na uyasikie yaliyoko huko. Hii Idd El Fitri wengine tunajishauri turudi au rusirudi! Lakini leo hao hao wanaosema kwamba wao posho hii haina maana hawajaiacha hata siku moja, ni wa mwanzo kuipokea. Hao hao! Mengine bora tunyamaze tusiyaseme maana tukiyasema hapa yataleta mengine. (*Makof!*)

**MBUNGE FULANI:** Sema!

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Spika, lakini msiwasikilize! Waheshimiwa Wabunge wanaposaidia jamii, jamii inashukuru kwa Serikali yao. Wanasema alihamdulillah. Serikali hii msiwasikilize sana hao wengine kwani nia yao ni kuifanya Serikali ioneke mbaya mbele ya wananchi. Sisi tuna lengo la kuifanya Serikali ioneke nzuri mbele ya wananchi. Kwa hiyo, ninachosema tusisikilize kila wanadolisema. Tena bayaa zaidi ni kwamba ni hao hao waliotangaza kwamba Mbunge analipwa Shilingi milioni 12, sasa leo wananchi wanashangaa wewe Shilingi milioni 12 bado unataka uongezwe! Uongo! Ni uongo, hakuna milioni 12! Tena ni aibu kwa mtu anayegombea uongozi wa Taifa, anataka awe Rais wa nchi hii, anakwenda anasema uongo kwa malengo yake ya kisiasa. Ni aibu! Hafai! Wananchi jichungeni na watu hawa! Hawa watu ni hatari kabisa! Mtu unakuwa muongo mpaka kwa Taifa zima! (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, mimi nilipokuja hapa nikuwa natamani kwamba nitaziona hizo Shilingi milioni 12, lakini sijazona! Ziko wapi! Semeni kama sisi waongo tuliwadanganya wananchi, msione aibu muungwana hukubali makosa yake. Kwa hayo, machache nasema ahsante sana! (*Makof!*)

**SPIKA:** Mshahara wa Mbunge ni Sh. 2,300,000/= kabla ya kodi, na kodi yenye inakuja karibu Sh. 700,000/= halafu amekopeshwa hilo gari ambalo ni wajibu wake kuwa na gari, kwani atatembeaje katika Jimbo la milima kama lile la kwangu bila kuwa na gari, na analipa zile kodi? Sasa hivi kwa sababu tulipata tukiwa tumechelewa kidogo, hivyo inakuja kwenye Sh. 864,000/. Kwa hiyo, katika Sh. 2,3000,000/= ulipe kodi ya Serikali ya Sh. 864,000/= haifiki hata milioni.

Hizi habari za simu na kuandikiwa *messages* ni kawaada. Sisi sote mpaka sasa inabidi wakati mwingine usifungue simu. Hiyo ni ukweli kabisa! Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tuwe wakweli tu. Hivi sasa naambiwa mwachangie watu, nimebana na kukaa kimya maana yake nikisema hivyo mtnanimaliza sasa hivi. Nikisema kila Mbunge achangie sijui ombi gani walloleta watu hapa, nitashambuliwa na ninyi wenye. Hata mimi najua kwamba wengine wanaogopa hata kurudi nyumbani, kwa sababu fedha walizopokea hapa walikuwa wanalala hotelini, wanakula hotelini, wanasafiri, wanarudi nyumbani kwao hawana hata senti moja. Huu ndiyo ukweli wenye na wala siyo kuwatetea. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, tunakushukuru Mheshimiwa Khatib kwa kuweza kusema huo ukweli. Wanaoandika wanapenda kuandika, lakini ukweli uko pale pale. (*Makof!*)

Waheshimiwa Wabunge, kesho kama ilivyokuwa leo, tutakuwa na bahati mbaya kweli kwani hatuwezi kuwapa nafasi Wabunge wengi, itabidi kipindi cha asubuhi tuweze kumaliza hota ya hii Wizara. Kwa hiyo, wataokuwepo kwenye orodha yangu ya uchangiaji ni Mheshimiwa Esther Midimu, Mheshimiwa Abdulkarim Shah, Mheshimiwa Anastazia Wambura, na kama tukifanikiwa sana attachangia na Mheshimiwa Dkt. Charles Tizeba.

Waheshimiwa Wabunge, sina tangazo lingine kwa hiyo, naomba niahirishe shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(*Saa 12.27 jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Ijumaa,  
Tarehe 26 Agosti, 2011 Saa Tatoo Asubuhi*)

